


Mwongozo wa Tatu

# Mafunzo Ya Omega

***Mafunzo ya Vitendo Kwa  
wapanda Kanisa***



*Na Muungano wa Kueneza Upandaji kanisa Wakishirikiana na Huduma ya  
Peter Dayneka wa Urusi*

**Kozi ya Omega:  
Mafunzo ya Vitendo Kwa Wapanda kanisa  
Mwongozo wa Tatu**

Tafsiri ya asili ilichapishwa na  
The Bible League, P.O. Box 28000, Chicago, IL 60625 USA  
Tel: (800) 334-7017 E-mail: [info@BibleLeague.org](mailto:info@BibleLeague.org) [www.bibleleague.org](http://www.bibleleague.org)

Copyright © 2000,2006 United World Mission.  
Machapishwo haya kwa asili yalinukuliwa na *The Alliance for saturation Church Planting* na  
yaliandaliwa na ushirika huo kwa kushirikiana na huduma ya Peter Deyneka  
wa Urusi, mradi 250.

Unaruhusiwa na Unashauriwa kuzalisha na kusambaza zana hii katika mfumo wowote endapo kama:  
(1) Unampa sifa mwandishi, (2) unaonyesha kama marekebisho yamefanyika, (3) Hulipishi zaidi  
ya gharama ya kuzalishia tena, na (4) hutengenezi kopi zaidi ya 1000.  
Kama utapenda kuweka nakala za nyenzo hii kwenye internet au kama matarajio yako ya matumizi ni  
tofauti na vichwa vya habari hapo juu tafadhali wasiliana na  
United World Mission: Jay Weaver/Omega, 9401-B Southern Pines Blvd.  
Charlotte, NC 28273-5596, or [omega\\_course@alliancescp.org](mailto:omega_course@alliancescp.org)

Kutafsiri na kurithi katika lugha yako pia kunashauriwa. Tena, tafadhali wasiliana na  
[omega\\_course@alliancescp.org](mailto:omega_course@alliancescp.org) ili kwamba tuweze kutia moyo na kuwajulisha wengine wanaoweza  
pia kuwa wamevutiwa katika lugha yako au matumizi yaliyokusudiwa.

Kwa taarifa zaidi juu ya huduma zao za kuheshimika, tafadhali wasiliana na :



(tovoti/rasilimali zinapatikana ila kwa sasa ushirikiano huo haupo tena)  
[http://www.alliancescp.org/resources/interchanges/2005\\_aug.html](http://www.alliancescp.org/resources/interchanges/2005_aug.html)



P.O. Box 496  
Wheaton, IL , USA 60189  
Tel: (630) 462-1739 Fax: (630) 690-2976  
[info@russian-ministries.org](mailto:info@russian-ministries.org)  
[www.russian-ministries.org](http://www.russian-ministries.org)

Kwa asili yalipigwa chapa au yalichapishwa katika nchi ya Marekani (USA).

## **SHUKURANI**

Tunatoa shukurani zetu kwa moyo wa dhati na za pekee kwa wote waliochangia katika matayarisho ya miongozo hii ya mafunzo. Wafuataa ni watu waliojitoa sana kwa kiwango kikubwa kwenye hatua ya kuandika na kutengeneza miongozo hii. Bwana, panda kanisa lako...mpaka miisho ya dunia.

Jay Weaver, Mtengenezaji, Timu ya Ulimwengu

Richard Beckham	<i>Greater Europe Mission</i>
David & Lisa Bromlow	<i>Christ For Russia</i>
Ron Brunson	<i>World Witness and United World Mission</i>
Don Crane	<i>Greater Europe Mission</i>
Bea Crane	<i>Greater Europe Mission</i>
Hunter Dockery	<i>World Harvest Mission</i>
Mike Elwood	<i>Greater Europe Mission</i>
Jeff Geske	<i>United World Mission</i>
Dave Henderson	<i>C B International</i> —Project 250 of Peter Deyneka Russian Ministries
Bob Mackey	<i>United World Mission</i>
Bob Martin	<i>United World Mission</i>
Paul Michaels	<i>Grace Brethren Intl. Mission</i>
Norie Roeder	<i>United World Mission</i>
Ki Sanders	<i>World Team</i>
Larry Sallee	<i>UFM International</i> —Project 250 of Peter Deyneka Russian Ministries
Eric Villanueva	<i>United World Mission</i>
David Westrum	<i>Interlink Ministries</i> —Project 250 of Peter Deyneka Russian Ministries

## **SHUKRANI ZA PEKEE KWA AJILI YA MSAADA WAO WA KIUONGOZI NA UTALAAM**

Edith Bond	<i>The Alliance Regional Resource Team</i>
David Gál	<i>The Alliance Regional Resource Team</i>
Nell Harden	<i>Retired English Professor</i>

## MWONGOZO WA TATU

### Yaliyomo

DIIBAJI .....	8
KUHUSU MUUNGANO.....	10
MZUNGUKO WA UPANDAJI KANISA.....	11
MTAALA .....	12
MTAZAMO WA UTARATIBU .....	14
MAONO YA KUM .....	19
SOMO LA 8: Kusonga Mbele kwa Mara ya Kwanza.....	20
I. Kuzaliwa kwa Kanisa la Agano Jipya .....	20
II. Mateso .....	21
III. Safari za Paul za Kimishenari.....	21
IV. Baraza Huko Yerusalem (Matendo 15) .....	23
V. Kanuni Nyuma ya Shughuli za Kimkakati za Kimishenari.....	24
SOMO LA 9: Asili ya Harakati za Upandaji Kanisa .....	28
I. Mapana ya Kimsingi ya Harakati za Kueneza Upandaji Kanisa .....	28
II. Matofari ya Kujenga ya Kueneza Harakati za Upandaji Kanisa .....	29
III. Matokeo: Harakati za Upandaji Kanisa.....	32
KANISA .....	35
SOMO LA 9, 10: Kanisa na Vipawa Vya Kiroho .....	36
I. Kwa nini Tunahitaji Vipawa Vya Kiroho? .....	36
II. Viongozi... Wanaotolewa na Yesu... Kuandaa Mwili.....	37
III. Uwezo... Unatolewa na Roho Mtakatifu... Kuujenga Mwili.....	37
IV. Vifungu Vya Mafunzo ya Biblia kwa Kufata Neno juu ya Vipawa Vya Kiroho.....	39
V. Vipingamizi Katika Kugundua Vipawa .....	41
VI. Kuhamasisha Kanisa Kulingana na Kujaliwa Vipawa Vya Kiroho .....	42
VII. Vipawa Vya Kiroho na Upandaji Kanisa .....	42
SOMO LA 11: Nguvu za Kijamii za Kanisa .....	44
I. Kanuni za Kibiblia.....	45
II. Kanisa la Agano Jipya na Utamaduni.....	46
III. Kutoka Agano Jipya Mpaka Sasa .....	49
IV. Utamaduni wa Wakati Huo na Kanisa .....	50
TABIA YA KIROHO .....	53
SOMO LA 8, 9: Sheria na Injili.....	54
I. Kusudi la Mungu kwenye Sheria .....	55
II. Upungufu wa Sheria.....	56
III. Kuishi kwa Sheria.....	58
IV. Roho Anatufungua Kutoka Kwenye Sheria .....	58
V. Maisha Ndani ya Roho na Imani katika Injili .....	59

<b>SOMO LA 10: Toba Kama Njia ya Maisha .....</b>	<b>64</b>
I. Tabia za Toba ya Kweli .....	65
II. Toba ya Kweli Kama Njia ya Maisha .....	67
III. Baraka za Toba ya Kweli.....	68
<i>Ziada: Nafasi ya Wenye Dhambi .....</i>	<i>70</i>
 <b>MAOMBI .....</b>	 <b>73</b>
<b>SOMO LA 5: Maombi na Kufunga .....</b>	<b>74</b>
I. Umuhimu Asili wa Maombi .....	74
II. Jukumu la Kufunga .....	75
 <b>SOMO LA 6,7: Kongamano la Maombi .....</b>	 <b>78</b>
I. Mshukuru Baba--Wakolosai 1:3-5 .....	78
II. Omba Kwa Ajili ya Injili Kusikika Ulimwenguni Kote--Wakolosai 1:6-7 .....	79
III. Omba Mungu Aweze Kukujaza na Ufahamu wa Mapenzi Yake--Wakolosai 1:9-11 .....	80
IV. Toa Shukurani Kwa Baba--Wakolosai 1:12-14 .....	80
 <b>UONGOZI .....</b>	 <b>81</b>
<b>SOMO LA 3: Mizunguko ya Uongozi.....</b>	<b>82</b>
I. Mifano ya Yesu .....	82
II. Mizunguko ya Upandaji Kanisa ya Uongozi .....	84
III. Mizunguko Yako ya Uongozi.....	85
 <b>SOMO LA 4: Utangulizi Kwa Kazi ya Timu .....</b>	 <b>87</b>
I. Nini Maana ya Kazi ya Timu?.....	87
II. Misingi ya Kibiblia kwa Kazi ya Timu .....	88
III. Tabia za Kazi ya Timu ya Ufanisi .....	89
 <b>SOMO LA 5: Maendeleo ya Timu .....</b>	 <b>93</b>
I. Kuunda Timu Yako.....	93
II. Kuongoza Timu Yako .....	95
III. Kuilewala Timu Yako.....	96
 <b>VIKUNDI KINI .....</b>	 <b>99</b>
<b>SOMO LA 7: Nguvu ya Majadiliano ya Kikundi Kiini .....</b>	<b>100</b>
I. Kuongoza Majadiliano Katika Kikundi Kiini.....	100
II. Kuanzisha Maswali Mazuri .....	102
III. Matatizo ya Majadiliano.....	103
<i>Ziada: Vikundi Kiini: Mfano wa Maswali ya Majadiliano .....</i>	<i>107</i>
 <b>SOMO LA 8: Kuwajali Watu Kwenye Kikundi Kiini.....</b>	 <b>109</b>
I. Kujenga Mahusiano .....	109
II. Utambuzi wa Mahaitaji ya Watu .....	111
III. Kutunza Mahitaji Kwenye Kikundi Kiini Chako .....	111

<b>SOMO LA 9: Kuwafunza Viongozi Wapya wa Kikundi Kiini.....</b>	<b>114</b>
I. Chagua Kiongozi Mwanafunzi.....	114
II. Mwandae Kiongozi Wako Mwanafunzi.....	116
III. Mtoe Mwanafunzi Wako Kwenye Huduma .....	118
<b>UINJILISTI .....</b>	<b>121</b>
<b>SOMO LA 8: Uinjilisti wa Kimahusiano .....</b>	<b>122</b>
I. Fanya Urafiki na Wasio Wakristo .....	122
II. Kumfata Kristo Katika Urafiki.....	124
III. Kuhesabu Gharama .....	124
IV. Uzoefu wa Maisha Kuhusiana na Uinjilisti wa Kirafiki .....	125
<b>KUFUASA .....</b>	<b>127</b>
<b>SOMO LA 1: Utangulizi Katika Kufuasa .....</b>	<b>128</b>
I. Msingi wa Kibiblia.....	128
II. Tafsiri ya Wanafunzi na Kufanya Wanafunzi au Kufuasa .....	130
III. Wito wa Mungu wa Kufuasa .....	130
IV. Jinsi Ufuasishaji Unavyochangia Kwenye Upandaji Kanisa.....	131
V. Kuanza Ukiwa na Mwisho Akilini .....	131
<b>SOMO LA 2: Jukumu Lako Katika Kufuasa .....</b>	<b>133</b>
I. Ukuaji Kiroho.....	133
II. Eleleza Upendo wa Kristo kwa Wafiasi Wako .....	134
III. Kuzania katika Mahitaji Halisi ya watu, Na Siyo Vipindi.....	135
IV. Dhamiria Kuzaliana na Kuzidisha.....	136
V. Kila Mara Tathimini Huduma Yako na Uwe Tayari Kufanya Mabadiliko Yanayohitajika .....	136
VI. Jifunze, Jifunze, Jifunze! .....	136
<b>Ziada: Tabia Za Upendo wa Kikristo.....</b>	<b>138</b>
<b>SOMO LA 3: Jua Lengo Lako, Jua Watu Wako.....</b>	<b>140</b>
I. Jua Lengo Lako la Kufuasa.....	140
II. Elewa Hali Iliyopo ya Kiroho ya Watu Wako .....	141
III. Mipaka ya Kivitendo Katika Kufuasa .....	143
<b>Ziada: Imani, Tumaini na Upendo .....</b>	<b>145</b>
<b>SOMO LA 4: Kuwasaidia Wafiasi Kukua Kiroho.....</b>	<b>147</b>
I. Gundua chanzo cha Kawaida cha Mahangaika ya Kiroho.....	147
II. Onyesha Msaada Wanaohitaji Waumini Kushinda Vipingamizi Vya Kiroho.....	150
<b>Ziada: Ukuaji Kiroho Unahitaji Tathimini.....</b>	<b>152</b>
<b>SOMO LA 5: Mifumo ya Kufuasa .....</b>	<b>154</b>
I. Mfumo 1: Kukua wa Binafsi.....	155
II. Mfumo 2: Kufuasa Kwa Mmoja Kwa Mmoja .....	155
III. Mfumo 3: Huduma ya Kikundi Kidogo .....	156
IV. IMfumo 4: Huduma ya Kikundi Kikubwa .....	157
V. Ukumbusho .....	158
<b>Ziada: Azimio la Kufuasa.....</b>	<b>159</b>

---

<b>VITA VYA KIROHO .....</b>	<b>165</b>
<b>SOMO LA 1: Kuelewa Mtazamo wa Kidunia.....</b>	<b>166</b>
I. Mitazamo ya Kawaida ya Dunia .....	166
II. Mtazamo wa Kibiblia wa Dunia.....	167
III. Mtazamo wa Dunia na Upandaji Kanisa.....	169
<b>SOMO LA 2: Nguvu za Vita Vya Kiroho .....</b>	<b>171</b>
I. Anga la Mungu .....	172
II. Anga la Mwanadamu.....	173
III. Anga la Roho Hai .....	174
IV. Anga la Mashambulizi .....	174
<i>Ziada: Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno Waefeso 4:17-5:21 .....</i>	<i>177</i>
<b>SOMO LA 3: Mashambulizi ya Kiroho .....</b>	<b>179</b>
I. Viwanja vya Mashambulizi ya Kishetani .....	180
II. Jinsi ya Kujua Kama Tatizo Linatokana na Sababu za Asili au Mashambulizi ya Kishetani .....	181
III. Jinsi ya Kujilinda Mwenyewe Dhidi ya Mashambulizi ya Kishetani .....	181
IV. Mipaka Katika Kushughulika na Mateso ya Mapepo .....	182
<i>Ziada: Kujifunza Biblia.....</i>	<i>186</i>
<i>Ziada: Michanganuo Kutoka Ulimwenguni.....</i>	<i>188</i>

## DIBAJI

### KUSUDI LA NYENZO HII

Wapanda kanisa mara nyingi wanafunzwa na kupelekwa nje wakiwa na mafunzo kidogo au bila mafunzo kwa ajili ya kazi iliyo mbele yao. Viongozi wa kanisa ambao wamezidiwa na matatizo ya huduma mara nyingi wanakosa maono wazi ya kile Mungu anachotaka kukamilisha kuitia wao. Wote wapanda kanisa na viongozi wa kanisa wanahitaji mafunzo na maono, lakini shule za Biblia na seminari siyo uchaguzi unaofahamika kwa wengi.

Nyenko hii imeandaliwa siyo kutoa maono tu kwa wapanda kanisa na viongozi wa kanisa, lakini pia msingi wa kibiblia na ujuzi wa vitendo wa huduma ili kuona maono hayo yanakuwa kitu halisi. Siyo kielimisho cha "maazimio." Badala yake, inatoa misingi muhimu ya kibiblia na kielimu, vilevile na ujuzi wa vitendo wa huduma, unaohitajika kwa upandaji kanisa. Ingawa kozi ya Omega iliandaliwa kwa ajili ya Ulaya ya mashariki na Kati na Muungano wa Urusi ya zamani, tumetiwa moyo na taarifa ambazo zimeshapatikana kuwa za msaada zinaporithiwa katika mandhali zingine.

Kozi yote hii imeandaliwa kukamilisha malengo mawili:

1. Kutoa mafunzo muhimu kwa makanisa kuweza kupandwa.
2. Kutia moyo uhamasishaji katika mwili mzima wa Kristo kuelekea harakati za upandaji kanisa.

Leo tunaona harakati za upandaji kanisa zikitokea katika nchi nyingi ulimwenguni kote, ikiwemo, Brazil, Roma, Ufilipino, Nigeria, na kwengine. Tunaamini kwamba kanisa la mtaa ni chombo cha msingi cha kuinjilisha ulimwengu, na kwamba upandaji wa kanisa unaotokana na kanuni ya kuongezeka mara dufu ni njia yenye mafanikio zaidi ya kutumia kuelekea kwenye kukamilisha utume mkuu. Makanisa mapya lazima yapandwe kwa maono ya kuongezeka mara dufu na uwezo wa kupanda makanisa mengine mapya. Hili linapotoka, kuna uwezekano wa harakati za makanisa zinazoweza kupangusa kuzunguka taifa na kubadilisha maisha ya watu katika nchi yote.

Harakati za upandaji kanisa zinahitaji watu waliohusika katika ngazi zote za kazi ya upandaji kanisa, kutokea kwa waumini wachanga walio na shauku ya imani yao mpya, hadi kwa viongozi wa madhehebu. Wapanda kanisa peke yao hawawezi kuwa kiungo cha harakati za upandaji kanisa. Nyenko hii inafaa na ina manufaa makubwa katika ngazi zote za wafanya kazi wa kanisa na viongozi wa kanisa ambao wanawea kuunga mkono juhudhi za wapanda kanisa moja kwa moja au kwa namna nyingine wanapokuwa wanajitahidi kutimiza huduma aliyowaitia Bwana.

### MTAZAMO WA TARATIBU

Mwomngozo huu ni moja ya miongozo mitano, ambayo kila mmoja una wastani wa masomo 26 ya saa moja. Ili kukamilisha malengo yaliyoelezewa hapo juu, kozi yote inatosheleza mapana mbalimbali ya masomo ambayo ni muhimu kwa kazi ya upandaji kanisa. Haya ni pamoja na maono ya KUM, huduma ya kikundi kiini, ufuasishaji, kanisa, uinjilisti, mafunzo ya Biblia kwa kufata neno, uongozi, maombi, tabia ya kiroho na mengine mengi.

Taratibu zilingawanywa katika miongozo mitano ili kutoa njia inayozidi kupanuka kwenye kozi ya mafunzo. Wakati kila mshiriki anapomaliza mwongozo, anatumia mda kabla ya mwongozo unaofuata akiziweka katika matendo kanuni alizojifunza. Kwa hiyo vipindi vingi vya baadaye vinajengwa juu ya kanuni na ujuzi uliojifunza na kufanyiwa mazoezi katika masomo ya mwanzoni.

Kwa maneno mengine, taratibu zimeandaliwa kujifunzwa na kutumiwa sambamba na upandaji halisi wa makanisa. Washiriki wanapofanya kazi kwa juhudhi kwa ajili ya kuanzisha kanisa jipy, watahitaji kiwango fulani cha ujuzi na ufahamu, na watakutana na matatizo mbalimbali wanapoendelea. Ujuzi na ufahamu unaohitajika mwanzoni mwa upandaji kanisa unatolewa katika mwongozo wa kwanza, wakati shughuli na kanuni zinazohitajika baadaye katika upandaji kanisa zinatolewa katika miongozo ya mbele. Kila mwongozo umeandaliwa kutoa ujuzi, kujibu maswali, na kujadili matatizo nyeti ambayo yanahusiana na hatua sambamba ya upandaji kanisa ambapo washiriki wanafanya kwa juhudhi. Baada ya dibaji hii uthaona orodha ya shughuli muhimu za maendeleo au "mapito" ambayo wafunzwa wameandaliwa na kutarajiwa kuutumia wakati wa mafunzo ya semina.

Masomo yamegawanywa kwa mada, na kila moja ya miongozo mitano ina masomo kutoka baadhi ya mada. Baadhi ya visa, kama vile "maono" na "kanisa" yote yamo katika miongozo yote mitano. Mengine, kama vile "kufuasa" kunatokea baadaye kwenye kozi, wakati mshiriki anapokuwa kwenye

hatua katika huduma yake ambapo visa hivi ni muhimu. Mtazamo wa kozi yote ulio na orodha ya mada ya somo kwa kila moja ya miongozo mitano imehusishwa baadaye katika hatua hii.

## **UTUMIAJI WA NYENZO**

### **Ushauri Kwa Washiriki**

Mda wa kutosha, maombi na juhudu yamewezesha utayarishaji wa miongozo yote hii mitano katika kozi yote. Kila mwongozo umeandaliwa kugusia ujuzi maalumu wa huduma na ufahamu unaohitajika wakati wa utaratibu wa kuanzisha kanisa jipya. Kwa hiyo inashauriwa kabisa kwamba unaanza na mwongozo wa kwanza, siyo mwongozo mmojawapo wa baadaye. Kwa heshima hiyo hiyo, kila somo limechaguliwa kwa uangalifu na kufanyiwa ufundi ili lifae, kutumika na la lazima katika kazi ya upandaji kanisa. Ni kwa manufaa yako pia kutovuka somo.

Tambua kuwa kusoma halisi kunatokea unapoyatumia mawazo yaliyotolewa katika masaomo haya katika maisha yako binafsi na katika huduma yako. Masomo mengi yana utekelezaji wa azimio mwishoni. Utekelezaji huu wa azimio umeandaliwa kukusaidia wewe kutumia mawazo katika somo na unatakiwa umalizike kabla hujaanza kufanya kazi mwongozo unaofata. Inaweza kuwa msaada wa hali ya juu kuwa na mshauri wa kukutia moyo na kukushauri unapofanya mwenyewe upandaji kanisa. Mshauri pia anaweza kusaidia hitaji lako la uwajibikaji unapokuwa unayatumia mawzo yaliyofunzwa katika maisha yako na huduma. Kuwa na mtu anayekuwa nawe bega kwa bega siyo tu maandalizi ua ufanisi, lakini wapanda kanisa wengi wanashuhudia msaada ambao hili linatoa katika maisha yao na katika huduma yao. Kwa hiyo, tunakutia moyo kabisa kwa maombi kutafuta aina fulani ya ushauri kuwezesha na kudumisha huduma yako ya upandaji kanisa.

### **Ushauri kwa Wakufunzi**

Nyenko hii inaweza kutumika kwa aina mbalimbali ya maandalizi kama vile shule ya Biblia, semimari au semina ya kikanisa. Kwa jinsi hiyo hii siyo tu kama nyenko ya kuanzia ya kuelimishia. Ni nyenko ya kufundishia. Elimu inayokazia katika ufahamu na habari. Kusudi la nyenko siyo tu kukuwezesha kupata ujuzi, lakini pia ni kuchochea kuelekeea kufikia kuweka huduma inayofanana na ya kibiblia. Mwongozo huu ni kwa ajili ya 'watendaji'.

Ingawa njia unayochagua kufundishia masomo kwa kila mwongozo itategemeana na mandhali yako, kila mwongozo unaweza kufundishwa katika semina ya wiki nzima. Kutohana na maelekezo haya, vituo mbalimbali vya mafunzo vimefanikiwa kwa kutumia mpangilio tofauti unaendana na mtiririko wa maisha na huduma zilizopo. Wakati mwingine wamechagua siku mbili mfululizo za mapumziko ama vipindi vya kila wiki. Inashauriwa kwamba utekelezaji wa azimio mwishoni mwa kila somo usisitizwe ili kwamba uwe umemalizika kabula ya semina nyingine. Kipindi cha kati ya miezi minne hadi sita ni kipindi kinachofaa kujatarajia kati ya semina na semina. Faida ya njia hii ya ufundishaji ni kwamba inaunganisha kanunu ulizojifunza kwenye semina na ushiriki kwenye semina.

Wakati wa semina siyo lazima kufundisha kila kiini kilichopo kwenye mwongozo kwa sababu washiriki wanaweza kusoma nyenko wenyewe. Wakati mwingine kufanya wafunzwa kusoma soma na kujadiliana jinsi linavyogusa uzoefu wao ni njia nzuri. Na wakati mwingine, maelezo kutoka kwa mtu ambaye ana uzoefu wa somo lililomalizika inaweza kuwa njia nzuri ya kujenge mawazo. LAKINI USIKALIE NJIA YA MAELEZO. Uwe mbunifu wakati ukijaribu njia mablimbali kujenga kanuni na ujuzi uliomo kwenye masomo. Wakufunzi wengine wamepata mchanganyiko kama vile kujadiliana kwenye makundi, karakana, na inaonekana kufanya kazi na kuwfurahisha.

Umetengwa kwa kutumainiwa, Mungu wa makanisa anahitaji mataifa yafuasishwe, na viongozi wanahitajika.

Una uwezo wa ajabu kusaidia kuandaa wengi watakaoendeza harakati za upandaji kanisa na kuwezesha wengine katika huduma za kuzaliana kwa kanisa

### **Msaada Zaidi**

Usisite kuwasiliana nasi kama tunaweza kuwa msaada zaidi kwako katika kueneza maono ya kueneza upandaji kanisa au kwa vitendo kuandaa wapanda kanisa.

Jay Weaver, General Editor  
Budapest, Hungary, January 2000  
[JayWeaver@compuserve.com](mailto:JayWeaver@compuserve.com)

## KUHUSU MUUNGANO

Taratibu hii imetayarishwa na *Muungano wa Kueneza Upandaji Kanisa* wakishirikiana na huduma ya Peter Deyneka wa Urusi, mradi 250. *Muungano* ni ushirikiano wa makanisa na mawakala wa umishenari waliojitoa kuwahamasisha waumini kuenea katka kila nchi zilizopo kati na mashariki ya Ulaya na ushirika wa makanisa ya kiinjili ya Urusi ya zamani. Kueneza upandaji kanisa ni mbini ambayo inakusudia kuanzisha makanisa katika kila mji, vijiji, na maeneo unayopakana nayo ili kwamba kila atakayemwamini Yesu apate kuwa na kanisa jirani atakaloweza kushiriki na kukua ndani ya Yesu na kujengwa au kuandaliwa kwa huduma. *Muungano* umejengwa juu ya msingi amba o kuunganisha nguvu kutaongeza ufanisi, kupunguza marudio na kuonyesha umoja kati kati ya mwili wa Kristo.

### TUNACHOAMINI

- Kanisa la mtaa ni zana ya msingi ya Mungu anayoitumia kueneza injili na ufuashishaji
- Ushirikiano na makanisa pamoja na mashirika ya kimishenari ni madhubuti kwa ongezeko la makanisa ya mtaa na maendeleo ya harakati za kueneza upandaji kanisa.
- Kuelimisha viongozi ni mhimu kwa upandaji kanisa na ukuuaji wa kanisa.
- Maagano ya Lausanne ni maelezo ya imani ya Muungano (Alliance)

### TUNACHOFANYA

#### **Kuelimisha na Kushauri Wapanda Kanisa**

*Muungano* unatoa ujuzi unaotokana na mafundisho katika mtindo wa semina pamoja na mazoezi ya huduma yanayolenga kwenye kuanzisha makanisa yanayozaliana.

#### **Ukusanyaji Bayana wa Taarifa.**

Taarifa makini zinapelekea uamuzi mzuri katika kazi za upandaji kanisa. *Muungano* unaweza kuhusika katika kufundisha na kushauri katika hitaji la kukusanya taarifa zinazohitajika katika eneo la upandaji kanisa na kukua kwa kanisa.

#### **Harakati za Kuhusisha Maombi**

Harakati za upandaji kanisa zinaanza na maono, ambayo yanagundiwa na kuandaliwa kwa kutafuta moyo wa Mungu kwa maombi. *Muungano* unaweza kukusaidia kuelewa zaidi nafasi ya harakati za maombi katika kazi ya upandaji kanisa, na namna unavyoweza kuwezesha harakati za maombi katika eneo au sehemu yako.

#### **Utupaji Maono**

Ni kitu gani Mungu anataka kwa nchi yako? Anataka makanisa kila mahali! *Muungano* unaweza kusaidia kuendeleza maono ya makanisa mapya kwa zana ya semina katika kanuni ya kuendeleza upandaji kanisa.

#### **KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**

*The Alliance For Saturation Church Planning (Muungano wa Kueneza Upandaji wa Kanisa)*

Regional Resource Team

H-1111 Budapest


Budafoki ut 34/B III/2, Hungary

Tel: + (36-1) 466-5978 or 385-8199

Fax: (36-1) 365-4606

E-mail: [KUMAAlliance@compuserve.com](mailto:KUMAAlliance@compuserve.com)

## MZUNGUKO WA KUPANDA KANISA



Kupanda kanisa siyo mfuatano wa matukio na shughulu zilizounganishwa bila utaratibu; Ni utaratibu wenyewe msukumo wa lengo. Utaratibu huu unahitaji ulinganifu wa shughuli, mchanganyiko wa ujuzi, falsafa ya kawaida na ujasili katika uongozi. Maendeleo katika maeneo haya nyeti ndilo lengo la kufundisha wapanda kanisa. "mzunguko wa kupanda kanisa" ni mchoro wa utaratibu wa kupanda kanisa ambao kwa macho unaonyesha, kutoka katika wazo fulani la mtazamo, mwingiliano wa kanuni za ufunguo na kufanya mazoezi ya kazi katika utaratibu huo. Hii inawakilisha 'ramani ya barabara' kwa mpanda kanisa, kuruhusu watu kuonyesha ni wapi wametoka na wapi wanaelekea.

## MITAALA

### Ya Utaratibu wa Upandaji Kanisa kwa Kozi ya Omega

**Mitaala** (vianzio) ni msingi mugumu wa shughuli za huduma ambazo zimeshirikishwa katika utaratibu huu. Kila mtaala unaweza kufikiriwa kama jiwe la kuvukia la mtu binafsi katikati ya utaratibu mkubwa wa kuanzisha kusanyiko jipya. Mitaala inatoa hatua ya utekelezaji imara ambao unaweza kusaidia wafunzwa kuweza kwa vitendo kutumia mawazo yaliyomo kwenye Kozi ya Omega. Zote ni mawe ya mbali ambato yanaonyesha maendeleo, vile vile ubao wa alama ambao unasaidia kutoa mwelekeo zaidi. Zifuatazo ni orodha za mitaala na msisitizo katika Kozi ya Omega

#### **MWONGOZO WA Msisitizo juu ya Maono ya KUM, Kusudi la Kanisa, Kujifunza Biblia kwa KWANZA: Kufata Neno na Utafiti**

##### Vitu Maalumu vya Kutekeleza

- Kuchunguza kusudi la Kanisa katika mwanga wa Utume Mkuu
- Kuanzisha mkakati wa jumla wa huduma ukizingatia maono ya “Z-kufikiri”
- Kuchunguza “mfumo na kazi” katika Kanisa la kwanza na Kanisa la sasa
- Kujifunza na kufanya majaribio ya Kujifunza Biblia kwa kufata neno
- Kuandika na kushirikisha ushuhuda binafsi
- Kuanzisha vikundi vya kusaidia maombi kwenye uinjilisti na upandaji kanisa
- Kukamilisha mradi wenye mambo mengi wa utafiti katika eneo linalolengwa

#### **MWONGOZO WA PIL: Msisitizo Juu ya Uinjilisti na Vikundi Kiini**

##### Vitu Maalumu vya Kutekeleza

- Kushirikishana yaliyopatikana katika mradi wa utafiti na wengine katika eneo linalolengwa
- Kuandika maelezo ya kusudi la kanisa
- Kuanzisha falsafa ya huduma ya upandaji kanisa
- Kuanzisha mkakati wa binafsi wa uinjilisti, ikiwemo uinjilisti wa mmoja kwa mmoja
- Kuanzisha vikundi kiini kwa msisitiza juu ya uinjilisti
- Kutumia njia ya kujifunza neno kwa kulifuata binafisi na kwenye vikundi kiini

#### **MWONGOZO WA Msisitizo juu ya Ufuasishaji, Vita Vya kiroho, Vikundi na Kufanya Kazi TATU: Kwa Timu**

##### Vitu Maalumu vya Kutekeleza

- Kuwatambua na kuwaelimisha viongozi nyeti wa vikundi kiini
- Kutumia muda katika maombi na kufunga
- Kutathimini mtazamo wa dunia wa wapanda kanisa ukilinganishwa na mtazamo wa dunia kibiblia
- Kutumia ukweli wa maandiko kupinga vipingamizi vya kiroho katika maisha na katika huduma ya wapanda kanisa
- Kuunda mpango binafsi wa kufanya ufuasishaji kwa watu wanaojihusisha katka huduma ya upandaji kanisa
- Kufanya maendeleo ya timu na shughuli za kutathimini
- Kuchanganua vipawa vya kiroho vya wapanda kanisa na vya timu ya upandaji kanisa

**MONGOZO WA Msisitizo Juu ya Uongozi na Uwakili Mwema  
NNE:**

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kutathimini uwezo na udhaifu wa mtindo wa uongozi wa huduma ya mpanda kanisa, kwa msisitizo juu ya njia za mwingiliano wa mtu binafisi na wengine
- Kushirikisha kanuni za kiongozi mtumishi kwenye maisha na huduma ya mpanda kanisa
- Kufuatilia matumizi ya muda katika maisha na huduma ya mpanda kanisa, kuweka vipao mbele, na kutengeneza ratiba
- Kutathimini utoaji fedha wa mpanda kanisa, vilevile na wa kanisa lenyewe lililopandwa
- Kutazama kwa upya nafasi ya mke na mme kibiblia na wajibu ambao wapanda kanisa wanao kwenye familia zao
- Kuongoza vikundi kiini vilivyopo katika utaratibu wa kuongezeka mara difu
- Kuandaa mpango wenye mkakati utakaoelekeza kwenye huduma ya kueneza upandaji kanisa

**MWONGOZO WA Msisitizo Juu ya Kuongezeka Mara Difu, Kuhamasisha Wengine, na  
TANO: Kuchochea Harakati za KUM**

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kuanzisha Ushirikiano wa huduma na vikundi vingine vya kiinjili katika eneo linalolengwa
- Kupanga na kuweka muundo wa usimamizi kwa vikundi kiini ambao utachochea kukua kunakoendelea na kuongezeka mara difu
- Kuwafundisha watu kuomba kwa ajili ya Ongezeko la upandaji kanisa; kuhamasisha maombi katika mji, mkoa na hata katika ngazi ya Taifa
- Kuanzisha na kuweka mpango kwa mkufundisha na kushauri wapanda kanisa wapya
- Kuwezesha na kutoa viongozi wapya kwa ajili ya huduma ya upandaji kanisa
- Kuchochea maono katika makanisa mapya kwa wamisionari kujihusisha siyo tu katka eneo lao wanadolenga, bali pia mpaka "miisho ya dunia"

## Kimsingi Inagusia Awamu ya MISINGI ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

### MTAZAMO WA MWONGOZO WA KWANZA

Maono ya KUM (MO)	Kanisa (KA)	Tabia ya Kiroho (TK)	Maombi (MB)	Njia za Kujifunza Biblia (NKB)	Uinjilisti (UI)
<b>Somo la 1:</b> “Z” Kufikiri	<b>Somo la 1:</b> Misingi ya Kibiblia kwa Ajili ya Kanisa	<b>Somo la 1 (1A)</b> Kuhesabiwa Haki Kwa Imani	<b>Somo la 1, 2:</b> Kongamano la Maombi: Kucombea Uamsho	<b>Somo la 1 (1A):</b> Utangulizi wa Njia za Kujifunza Biblia Kwa Kufata Neno 1A: <i>Jinsi Tulivyopata Biblia</i>	<b>Somo la 1:</b> Utangulizi Juu ya Uinjilisti
<b>Somo la 2:</b> Utume Mkuu na Upandaji Kanisa	<b>Somo la 2 (2A):</b> Kusudi la Kanisa 2A: <i>Karatsasi ya Mazoezi Kwa Utume Mkuu</i>	<b>Somo la 2:</b> Kuishi Kufuatana na Injili	<b>Somo la 3:</b> Ukuaji wa Mkristo	<b>Somo la 2 (2A):</b> Kulichunguza Neno la Mungu 2A: <i>Lugha ya Biblia</i>	<b>Somo la 2,3:</b> Kutayarisha Ushuhuda Binafsi
<b>Somo la 3(3A):</b> Mzunguko wa Upandaji Kanisa 3A: <i>Vielezo vya Upandaji Kanisa</i>	<b>Somo la 3 (3A):</b> Mfumo na Kazi 3A: <i>Mfumo na Kazi Iliyotumika</i>	<b>Somo la 4:</b> Nguvu ya Injili Inayobadilisha	<b>Somo la 3 (3A):</b> Jinsi ya Kuwezesha Maombi 3A: <i>Maombi ya Utatu</i>	<b>Somo la 3:</b> Warsha ya Uchunguzi	
<b>Somo la 4 (4A, 4B)</b> Kanuni za Utafiti 4A: <i>Kulifahamu Eneo unalolenga</i> 4B: <i>Mifano ya Maswali ya Utafiti</i>	<b>Somo la 4:</b> Kutafsiri Maana ya Kanisa la Mtaa	<b>Somo la 5:</b> Kutunza Kumbukumbu za Maisha ya Kiroho		<b>Somo la 4 (4A):</b> Kufafanua Neno la Mungu 4A: <i>Majedwali ya Biblia</i>	
4	4	5	3	<b>Somo la 5:</b> Warsha ya Ufafanuzi	
				<b>Somo la 6:</b> Kulitumia Neno la Mungu	
				<b>Somo la 7 (7A):</b> Warsha ya Kulitumia Neno la Mungu 7A Waefeso-an 1.B.S.	
				7	3

Namba katika mabano (26) zina maanisha mwishoni

## Kimsingi Inagusia Awamu ya KULETA ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

### MTAZAMO WA MWONGOZO WA PILI

Maono ya KUM (MO)	Kanisa (KA)	Tabia ya Kiroho (TK)	Maombi (MB)	Uongozi (UO)	Vikundi Kiini (VK)	Njia za Kujifunza Biblia (NKB)	Uinjilisti (UI)
<b>Somo la 5:</b> Misingi ya Kibiblia ya Kueneza Upandaji Kanisa	<b>Somo la 5:</b> Asili ya Kanisa	<b>Somo la 6:</b> Kuishi Kama Wana Badala ya Mayatima	<b>Somo la 4:</b> Kongamano la Maombi: Kuabudu na Kuritafakari neno	<b>Somo la 1 (1A):</b> Misingi ya Kibiblia ya Uongozi 1A: <i>Mchanganuo wa Uongozi</i>	<b>Somo la 1:</b> Kazi na Faida za Vikundi Kiini	<b>Somo la 8 (8A):</b> Njia Tofauti Tofauti za Kutumia Njia ya Kujifunza Biblia Kwa Kulifata Neno	<b>Somo la 4 (4A):</b> Uinjilisti na Upandaji wa Kanisa 4A: <i>Kutathimini Mikakati ya Uinjilisti</i>
<b>Somo la 6:</b> Warsha ya Utafiti	<b>Somo la 6 (6A):</b> Kazi za Umoja za kanisa 6A: <i>Ubatizo Katika Agano Jpya</i>	<b>Somo la 7 (7A):</b> Kujifunza Kuwa Wana 7A: <i>Yatima Dhidi ya Wana</i>		<b>Somo la 2 (2A):</b> <i>Sura ya kiongozi</i> 2A: <i>Hadhi ya Kiongozi</i>	<b>Somo la 2 (2A, B):</b> Kanuni za Uongozi wa vikundi Kiini 2A: <i>Vikundi Kiini Vivunja Barafu</i>	<b>Somo la 9 (9A,9B)</b> Kuongoza Mafunzo ya Biblia Kwa Kulifuata Neno 9A: Mafunzo ya Mathayo 20:17-28 9B: Kujifunza Juu ya LK 15:1-7	<b>Somo la 5 (5A.5B):</b> Vizuizi dhidi ya Mafanikio ya Injili 5A: "Kanisa kwa Watu Wote" 5B: <i>Kujibu Juu ya Kupinga kwa Kawaida</i>
<b>Somo la 7:</b> Kuhamasisha Rasilimali Kupitia Utafiti	<b>Somo la 7:</b> Kuandaa Maelezo ya Kusudi la Kanisa			<b>Somo la 3 (3A):</b> Kuanzisha Vikundi Kiini 3A: <i>Karatasi ya Upangaji</i>	<b>Somo la 4 (4A):</b> Uinjilisti wa Vikundi Kiini 4A: <i>Kuhusu "Oikos"</i>	<b>Somo la 10, 11 (10A):</b> Warsha ya Kuongoza Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno 10A: <i>Vfungu Kwa Ajili ya IBS</i>	<b>Somo la 6;7 (6A,6B,6C)</b> Utaratibu wa kukata Shauri 6A: <i>Sura ya Mtu katika Kuinjilisha</i> 6B: <i>Kanuni Tatoo</i> 6C: <i>Kuchunguza Njia Aliyotumia Yesu</i>
3	4	2	1	2	6	4	4

Namba katika mabano (27) zina maanisha mwishoni

## Kimsingi inagusia **Awamu ya UANZILISHI** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

### MTAZAMO WA MEONGOZO WA TATU

Maono ya KUM (MO)	Kanisa (KA)	Tabia ya Kiroho (TK)	Maombi (MB)	Uongozi (UO)	Vikundi Kiini (VK)	Uinjilisti (UI)	Kufuasa (KS)	Vita Vya Kiroho (VK)
<b>Somo la 8:</b> Kusonga Mbele kwa Kwanza	<b>Somo la 9,10:</b> Kanisa na Vipawa Vya Kiroho	<b>Somo la 8,9:</b> Sheria na Injili	<b>Somo la 5:</b> Maombi na Kufunga	<b>Somo la 3:</b> Mzunguko wa Uongozi	<b>Somo la 7 (7A):</b> Nguvu ya Majadiliano	<b>Somo la 8:</b> Injili ya Mahusiano	<b>Somo la 1:</b> Utangulizi katika kufuasa	<b>Somo la 1:</b> Kuelewa Mtazamo wa Kidunia
<b>Somo la 9:</b> Asili ya Harakati za Upandaji kanisa	<b>Somo la 11:</b> Nguvu Za Kijamii za Kanisani	<b>Somo la 10 (10A):</b> Toba Kama Njia ya Maisha	<b>Somo la 6,7:</b> Kongamano la Maombi: Kuombea Kuenea kwa injili	<b>Somo la 4:</b> Utangulizi kwa Kazi ya Timu	<b>Somo la 5:</b> Maendeleo ya Timu	<b>Somo la 8:</b> Kutunza Watu Walio Kwenye Vikundi Kiini	<b>Somo la 2 (2A):</b> Jukumu lako Katika Kufanya Wanafunzi	<b>Somo la 2:</b> Nguvu za Vita vya Kiroho
		<i>10A: Sehemu ya Wenye Dhambi</i>				<b>Somo la 9:</b> Kufundisha Viongozi Wapya wa Vikundi Kiini	<i>2A: Tabia ya Upendo wa Kikiristo</i>	<i>2A: Mafunzo ya Waefeso 4:17-5:21</i>
2	3	3	3	3	3	1	5	3

Namba katika mabano (26) zina maanisha mwishoni

## Kimsingi Inagusia Awamu ya KUFUNDISHA ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

### MTZAMO WA MWNGOZO WA NNE

Maono ya KUM (MO)	Kanisa (KA)	Tabia ya Kiroho (TK)	Maombi (MB)	Uongozi (UO)	Vikundi Kiini (VK)	Kufuasa (KS)	Uwakili Mwema (UM)	Familia (FA)
<b>Somo la 10 (10A, 10B):</b> Vipengele vya Mkakati kwa Harakati za Upandaji Kanisa <i>10A: Imani</i> <i>na Utii dhidi ya Hofu na</i> <i>Kutokuamini</i> <i>10B: Vitu</i> <i>Vinavyoamsha</i> <i>Ukuaji wa Asili</i>	<b>Somo la 12:</b> Nguvu ya Makanisa yanayoibuka	<b>Somo la 11:</b> Upendo Kama Msingi kwa Huduma	<b>Somo la 8, 9:</b> Kongamano la Maombi Kuomba Kibiblia	<b>Somo la 6 (6A):</b> Uongozi wa Kitumishi 6A: Orodha ya Viongozi	<b>Somo la 10:</b> Majadi- liano ya Maswali na Matatizo ya Vikundi Kiini	<b>Somo la 1:</b> Warsha ya Kufuasa	<b>Somo la 6:</b> Utangulizi juu ya Uwakili Mwema	<b>Somo la 1:</b> Majukumu ya Kibiblia Katika Familia
<b>Somo la 11:</b> Dalili za Harakati	<b>Somo la 13:</b> Tabia ya Makanisa Yanayokua	<b>Somo la 12:</b> Kuuelewa Moyo wa Baba	<b>Somo la 13:</b> Neema ni Kwa Wanyenye kevu	<b>Somo la 7:</b> Nguvu za Uongozi <b>Somo la 8:</b> Mitindo ya Mwingiliano	<b>Somo la 11:</b> Kuzidisha Kwa Kikundi Kiini		<b>Somola 2:</b> Uwakili mwema Kwenye Fedha	<b>Somo la 2:</b> Kulea
<b>Somo la 12:</b> Ungalizi Kati Kati ya Harakati	<b>Somo la 14:</b> Serikali ya Kanisa na Ofisi za Kanisa:			<b>Somo la 9:</b> Mahitaji ya Uongozi <b>Somo la 10 (10A):</b> Kufunza Viongozi Wapya <i>10A: Hadhi za Kutia</i> <i>katika Uongozi</i> <i>Mpya</i>			<b>Somo la 3:</b> Matumizi ya Muda	
3	3	3	2	5	2	1		

Namba katika mabano (25) zina maanisha mwishoni

## Kimsingi Inagusia Awamu ya KUZIDISHA NA HARAKATI Katika Mzunguko wa Upandaji Kanisa

### MTAZAMO WA MWONGOZO WA TANO

Maono ya KUM (MO)	Kanisa (KA)	Tabia ya Kiroho (TK)	Maombi (MB)	Uongozi (UO)	Vikundi Kiini (VK)	Kuhubiri (KR)	Familia (FA)
<b>Somo la 13:</b> Maono na Kupiga Darubini	<b>Somo la 15:</b> Malezi ya Kanisa	<b>Somo la 15:</b> Huduma ya Upatanishi	<b>Somo la 10:</b> Maombi ya Kuwezesha kwa Harakati za Upandaji Kanisa	<b>Somo la 11:</b> Kutoa Viongozi	<b>Somo la 12:</b> Viini Vinavyoenea Kupitia Makanisa ya Mtaa	<b>Somo la 1:</b> Mahubiri ya Kibiblia 1: Kuelewa Ujumbe	<b>Somo la 3:</b> Huduma Kwa Famila
<b>Somo la 14:</b> Kuhamasisha	<b>Somo la 16:</b> Ibada ya Umoja katika Kanisa la Mtaa	<b>Somo la 16:</b> Unyoofu wa Maadili Kwa Wapanda Kanisa	<b>Somo la 11,12:</b> Kongamano la Maombi: Kumshukuru Mungu Kwa Ajili ya Uaminifu wake	<b>Somo la 12:</b> Uongozi wa Harakati 12A: Viongozi wa Harakati	<b>Somo la 13 (13A):</b> Kusimamia vikundi Kiini 12A: Hatua ya Mwisho	<b>Somo la 2:</b> Mahubiri ya kibiblia 11: Kuelewa Wasikilizaji	
<b>Somo la 15:</b> Hatua Inayofuata	<b>Somo la 17:</b> Jinsi ya Kuongoza Ibada ya Pamoja Katika Kanisa la Mtaa					<b>Somo la 3:</b> Mahubiri ya kibiblia 111: Kujielewa Mwenyewe	
<b>Somo la 16:</b> Mafunzo Kama Sehemu ya Harakati za Upandaji Kanisa	<b>Somo la 18:</b> Kanisa la Mtaa na Mwili Mkubwa wa Kristo						
<b>Somo la 17:</b> Kuhamasisha Viongozi Kupitia Uanzilishi wa Kitaifa	<b>Somo la 19:</b> Mguso wa Kihistoria wa Kanisa — (Historia ya Kanisa Katika Mandhali ya Nchi)						
5	5	5	3	2	2	3	1

Namba katika mabano (23) zina maanisha mwishoni

JUMLA YA MASAA YA KOZI YOTE: 127

---

---

## **MAONO YA KUM**

---

---

MAONO YA KUM

8

SOMO LA

# Hatua ya Kwanza ya Kusonga Mbele

## HARAKATI ZA UPANDAJI KANISA KATIKA MATENDO

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wafunzwa kuelewa harakati za zamani za upandaji kanisa kwa kuangalia kwenye kupanuka kwa kanisa kama ilivyoandikwa katika Matendo.

### ☞ Wazo Kuu

- Kuenea kwa kanisa la karne ya kwanza kulikuwa kwa haraka na kwa nguvu.
- Matukio fulani na matumizi ya kanuni ya huduma maalumu yalichangia kuenea kwa kanisa.

### ☞ Matokeo Yanayotarajija

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoelewaka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujuu kanuni kutoka kwenye kuenea kwa injili kwa nguvu kwenye Agano Jipya ambako kuliwagusa timu ya upandaji kanisa kufikia kwenye harakati za upandaji kanisa.
- Kushiriki katika harakati za upandaji kanisa kwa makanisa yanayokua ambayo yanaongezeka kwa kupanda makanisa mengine yanayokua na kuzaliana.
- Kuweza kuweka mkakati wa kuinjilisha eneo kwa upandaji kanisa

### ☞ Ushauri kwa Wapanda Kanisa

#### A. *Uwe na ramani ya Ulimwengu wa Mediterenia-\* tayari kuonyesha maeneo yaliyoenezwa kwa huduma ya Paulo.*

### UTANGULIZI

Katika siku za nyuma kufuatia mpao wa Yesu, injili ilikuwa haijagusa ulimwenguni nje ya Yudea, Samaria, na Galilaya. Mwanzoni, ukristo ulionekana kuwa mdogo na usio na nguvu ukilinganisha na uwezo wa kisiasa siku hizo. Hata hivyo, uliviringika kama maporomoko ya theluji kuzunguka ngome ya Urumi kiasi kwamba kati kati ya kizazi kimoja jamii zinazoabudu zilikuwa zimeanzishwa kila mahali kutoka Yerusalemu mpaka Urumi na zaidi. Wanahistoria wa sasa wanastaajabu, wakishangaa kuona jinsi gani ukristo ungeweza kuenea kwa upana kiasi hicho katika kipindi kifupi (Berkhof, p. 21). Huu ulikuwa tu upanukaji wa bahati? Je wamishenari wa kwanza walitanga tanga kiupofu ulimwenguni kueneza injili? Siyo sawa. Mafunzo ya uangalifu ya Matendo yanadhihirisha kwamba kupanuka kwa kanisa kulitokana na mpango wa kuongozwa na Roho ukizingatia kanuni ya huduma ambayo tunaweza tukaendelea kuitumia leo.

Mafunzo ya uangalifu ya Matendo yanadhihirisha kwamba kupanuka kwa kanisa kulitokana na mpango wa kuongozwa na Roho ukizingatia kanuni ya huduma ambayo tunaweza tukaendelea kuitumia leo.

Wakati wa somo hili tutajifunza maandiko, kitabu bora katika upandaji wa kanisa mahali popote. Tutaangalia vipengele ambavyo vilichangia kupanuka kwa haraka kwa kanisa tukiamini kwamba inawezekana kuzindua kanuni za huduma za kuziendeza na kueneza kila eneo kwa injili.

### I. KUZALIWA KWA KANISA LA AGANO JIPYA

Siku ya pentekosti, wakati kanisa la Agano Jipya lilipokuwa limezaliwa, lilisimama katika nafasi kubwa ya kuenea kwa haraka kwa ukristo. Upendekosti ultokea wakati wa kipindi kikuu cha kusherehekeea

wakati maelfu ya Wayahudi na waongofu walipokuja Yerusalem kutoka ulimwenguni kote. Luka anaandika watu kutoka katika mikoa 13 tofauti ikiwemo Pathia, Midia, Elamu, Mesopotamia, Yudea, Kapodisia, Pontias, Asia, Perigia, Pamphilia, Misri, Sirini, Krete, na Urumi. Wengi wa pentekosti wahiji walichukua imani zao mpya nyumbani kwao lakini baada ya kupokea maelekezo na kupata uzoefu wa kanisa uliotokea baada ya kusherehekea pentekosti (Mdo 2:42-47). Mwanzo huu wa mafunzo ungeweza kuelezea jinsi kanisa Urumi ilivyoanzishwa vizuri kabla ya mtume yeyote kufika pale.

## II. MATESO

Katika Matendo 8 mateso makuu yaliibuka ambayo yalisababisha kanisa kutawanyika (Mdo 8:1; 11:19-21). Hii pia ilichangia kuenea kwa injili. Waumini walipotawanyika walieneza injili karibu kwa Wayahudi wenzao wengi. Huko Antioki na Siria, kwa jinsi hiyo, Wayunani wengi walilengwa na kuleta kwa Kristo na kupelekeea kuanzishwa kwa kanisa la kwanza lililojengwa na watu wengi wa Mataifa kama ilivyoandikwa kwenye maandiko. Hii ilionekana kuwa ya tofauti kwamba viongozi katika kanisa la Yerusalem walimtuma Barnabas kuchunguza hali (Mdo 11:26).


Barnabas alivutiwa na waumini mataifa huko Antiokia kiasi kwamba alitumia angalau mda wa mwaka akihudumu huko. Hata alimwandaa Paulo mbali kutoka Tarso kuungana naye (Mdo 11:25-26). Na wengine kutoka maeneo mengine waliunda timu ya uongozi wenye nguvu (Mdo 13:1). Ilikuwa hapo Antiokia ambapo wanafunzi kwa mara ya kwanza waliitwa "Wakristo" (Mdo 11:26).

## III. SAFARI ZA KIMISHENARI ZA PAULO

"Hivyo, kutoka kote Yerusalem mpaka Iliriko, nimekwisha kuihubiri injili ya Kristo" St. Paulo(Rum 15:19).

Paulo alikuwa wa mambo mengi: mtume, mwanatheolojia na mwalimu. Lakini katika mambo yote haya jukumu lake kama mmishenari mpanda kanisa lilikuwa wazi. Wengine wamepokea waliokata shauri wengi kuliko Paulo, wengine wamehubiri kwa wasikilizaji wengi, lakini pengine hakuna mmoja wao amefanikiwa katika upandaji makanisa (Allen 1962:3). Kwa kuiangalia safari ya Paulo ya kimishenari tunajifunza funguo za mafanikio ya Paulo.

Kilelezo 8.1 Kuenea kwa Injili



### A. Safari ya Kwanza (mdo 13-14)—Ikipanuka mpaka Kipro na Galatia

Paulo na Barnabas walipelekwa kama wamishenari mara ya kwanza kwenye visiwa vya kipro, nyumbani kwa Barnabas. Walianza kwa kuhubiri kwenye masinagogi kwenye mji mkubwa zaidi wa Salami kisiwani. Baadaye walikwenda kwenye mji wa Pafo mji wa uongozi

wa kisiwa. Kukata shauri kwa Sergio Paulo (liwali) angewapatia upendeleo kwenye mji (Mdo 13:1-12).

Kufuatia huduma ya Kipro walielekea Galatia ambayo siku hizi ni Uturuki. Huko Pisidia ya Antioquia, mji mkuu wa Galatia kusini, Paulo alihubiri kwenye sinagogi na kuwaona Mataifa wengi waliokata shauri. Ukiwa mji wa kimikakati Antioquia katika pisidia ilikuwa, matokeo ya mguso wa huduma ya Paulo na Barnabas ambayo haikuzuiliwa kwenye kairi "Neno la Mungu *lilivyoenea kwenye eneo lote*" (Mdo 13:49). Bila kujali mafanikio haya mateso yaliyochochewa na Wayahudi yalikuwa makali kiasi kwamba Paulo na Barnabas walilazimika kuondoka (Mdo 13:14-52).

Baada ya hapo Paulo na Barnas walisafiri mpaka Ikonio, sehemu mashuhuri ya Biashara pia huko Galatia. Wengi waliitikia mahubiri yao ndani ya Sinagogi, lakini mara walikutana na mtego kutoka kwa Mataifa na Wayahudi (Mdo 14:1-7). Wakiwa wametolewa, walikimbilia Listra, mji wa kijeshi wenyе asili ya Kirumi. Inaonekana kwamba Paulo alipitishwa na wenyeji wa miji kwenye jimbo kama Mithia na Vasada (Allen 1962:13). Kama raia wa Urumi, Paulo alijisikia uhuru zaidi kwenye miji na uwepo wa nguvu ya Rumi. Baada ya kupona kwa kiwete huko Listra, watu walitoa ushauri kumwabudu Paulo na Barnabas, wakiwachanganya na mingi ya Zeu na Herme. Wayahudi walianzisha upinzani na Paulo akapigwa mawe. Pasipo hofu, Paulo na Barnabas wakakimbilia Derbe (Mdo 14:8-20).

Huko Derbe walihubiri injili na kuwafundisha wengi. Kutoka Derbe, Paulo ngeweza kurudi kwa urahisi Antioquia kupitia myumbani kwake, Taasisi. Lakini aliona ni muhimu kuwatia moyo waumini wapya na kuteua viongozi kwenye makanisa manne aliyopanda Pisidia Antioquia, Ikonio, Listra na Derbe bila kujali hatari ambayo angekutana nayo tena (Mdo 14:20-23).

#### **B. Safari ya Pili (15:36-18-22)—Ikipanuka Huko Makedonia na Akia**

Matokeo ya kutoibaliana kuhusu nafasi ya Yohana Marko kwenye timu, Paulo na Barnabas walianza kuhudumu tofauti. Barnabas na Yohana Marko walirudi Kipro. Silasi alichaguliwa kwenda na Paulo kwenye safari yake ya pili ya kimishenari. Waliweka lengo la "kuimarisha makanisa" (Mdo 15:36-41).

Timu mpya ilirudi Derbe na Listra na pengine kwenye miji mingine ya Galatia (16:1-6). Wakiwa Listra, Paulo alimwandaa Timotheo kuungana nao kwenye huduma. Paulo alitaka kwenda Asia lakini Roho akamwongoza pengine. Akiwa Troa Paulo akapata maono ya mtu wa Makadonia (Mdo 16:7-11). Luka akaungana nao na hivyo timu ikakua wakiwemo wanne (Paulo, Sila, Timotheo, Luka). Na kwa pamoja wakahamia Filipi. Filipi ulikuwa mji mashuhuri kwenye "njia kuu," njia panda ya Urumi inayounganisha Makedonia na Asia (Mdo 16:12-40). Huko Filipi, Lidia akaokoka na nyumba yake ikageuka kuwa nyumba ya kutendea. Sila na Paulo walipigwa na kufungwa baada ya kumfungua msichana aliyejikuwa amefungwa na pepo ambako kulitokea kwenye malalamiko ya kiofisi ya mabwana wa watumwa. Mlizni wa geleza na "nyumba yake yote" wakaokoka (Mdo 16:16-40).

Wakishakupita kati ya Amfipoli na Apolonia Paulo, Sila na Timotheo walifika Thesalonike mji mkuu wa wilaya na bandari kuu ya Makedonia. Kisha tena, walianzia kwenye sinagogi ambako Paulo alihubiri kwa sabato tatu. Kulikuwa na mwitikio mzuri wa wengi wa Wayahudi na Mataifa waliomuogopa Mungu. Lakini kwa wivu wa baadhi ya Wayahudi katika sehemu hiyo wakaanzisha ghasia (mdo 17:1-9). Kisha Paulo akahamia Beroya, ambako walikuwa tayari kusikiliza. Wakati Wathesalonike watesaji walipowafata wamishenari mpaka Beroya, Paulo akalazimika kukimbilia akiwaacha Timotheo na Sila Beroya (Mdo 17:1-15).

Paulo akawasubiri Timotheo na Sila kuungana naye katika mji wa Athene uliojaa sanamu. Akiwa hapo alihubiri injili yenye nguvu ambapo alianzisha msingi na wasikilizaji na akisha akatangaza tofauti za imani. Wachache wakaokoka (17:15-34).

Baada ya haya Paulo akafika Korintho, mji mkuu wa Akaya, mji mashuhuri kwa usafirishaji na kitovu cha mawasiliano katika eneo (Mdo 18:1-16). Paulo akaungana na Akila na Prisila watengenezaji wa mahema kutoka Urumi. Sasa wakawa Paulo, Sila Timotheo, Akila na Prisila. Kama zilivyo sehemu zingine, huduma ya Paulo huko Korintho ikawa na nguvu kubwa katika jimbo hilo la Akaya (2Kor 1:1).

Baada ya miezi 18 Paulo akatweka mpaka Antioquia huko Siria akiwaacha nyuma Sila na Timotheo kuendeleza kazi huko Korintho. Njiani Paulo alipitia Efeso, Bandari ya sasa ya magharibi mwa Uturuki. Paulo alipokelewa vizuri kwenye sinagogi na Wayahudi wakamkaribisha kukaa. Akiwa mwanzoni amekatazwa na Roho kuhubiri Asia, aliahidi kurudi tena, "kama ni mapenzi ya Mungu." Paulo akawaacha Akila na Prisila hapo kuendeleza kazi (Mdo 18:19-21).

#### C. Safari ya Tatu (Mdo 18:23-21-15)-Ikipanuka kwenye Jimbo la Asia

Paulo akaanza safari yake ya tatu ya kimishenari kwa kuyatembelea makanisa aliopanda huko Galatia kwa kipindi cha nne kilichoandikwa (Mdo 18:23). Akafika Efeso kupitia nchi za juu (Mdo 19:1). Efeso ulikuwa bandari kwenye njia kuu ya msafara na urahisi wa kufika jimbo la Urumi la Asia, ambalo Paulo alikuwa na mzigo nalo kwa mda mrefu. Km 150 tu kwenda mashariki mpaka kwenye bonde la Likusi kuliko na miji ya Laodikia, Colosai, na Hirepolisi. Efeso ulikuwa umekandamizwa kwa uchawi na ukahaba. Katika wakati huo ulikuwa ni moja ya miji mitatu mikubwa ya mashariki mwa ulimwengu wa mediteraniani (miji mingine mikubwa ni Alexandria na Antioquia huko Siria). Hii ilikuwa sehemu ya kimikakati katika kuhudumu.

Kama iliyokuwa sehemu yake, Paulo alihubiri katika sinagogi na kukataliwa baada ya miezi mitatu. Kukataliwa huku kilitokana pengine na kilichokuwa kikomo cha huduma yake, kupanuka kwa hali ya juu kwa injili kwenye jimbo la Asia: "...akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa la mtu mmoja jina lake Tirano. Mambo haya yakaendelea kwa mda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana, Wayahudi kwa Wayunani" (Mdo 19:9-10).

Ilikuwaje kwamba kila mmoja katika jimbo la Asia asikie neno la Bwana? Vifungu vingine kwenye Agano Jipyä vinadhihirisha kuchipuka kwa makanisa hayo katika miji ya Kolosai (Col 1:2), Laodikia (Col 4:16), Hierapoli (4:13), Smirna (Uf 2:8), Thiatira (Uf 2:18), Sardi (Uf 3:1), Filadefia (Uf 3:7), na mahali pote (pengine) Maginesia, Troa, Militusi n.k.). Makanisa haya katika jimbo la Asia yanadhihirisha harakati za upandaji wa makanisa na kuthibitisha maelezo ya Paulo kwamba Asia yote ilisikia neno la Bwana. Kwa kuongeza, vitabu vya Waefeso, Wakolosai, Timotheo ya kwanza na ya pili, Filemoni, Yohana ya Kwanza, ya Pili na ya Tat, Ufunuo na sehemu ya Matendo vyote ni juu ya makanisa na viongozi wa makanisa Asia waliotokana na kuendelea kwa injili huko.

Baada ya miaka mitatu huko Efeso Paulo aliamua kurudi Makedonia na Akaya kutembelea makanisa manne aliopanda katika safari yake ya pili huko Filipi, Thesalonike, Borea na Korintho. Aliwatuma Timotheo na Erasto mbele yake (Mdo 19:21) na kukaa Efeso kwa mda mrefu kidogo. Baada ya ghasia kuchochewa na waliokuwa wakipata kipato kwa njia ya ukahaba Efeso, Paulo aliondoka kwenda Makedonia. Paulo alikuwa akisafiri na Sepatro (kutoka Beroya), Aristariko na Sekundo (kutoka Thesalonike), Gayo (kutoka Derbe) Timotheo (kutoka Listra), Tikiko na Trofimo (Mdo 20:3-6). Baadhi ya hawa walikuwa wenzake Paulo aliokuwa akiwafundisha kwenye kituo cha mafunzo alichoanzisha kwenye ukumbi wa Tiranusi Efeso.

Paulo aliwatia moyo ndugu huko Makedonia na Akaya waliokaa Korintho kwa miezi mitatu (Mdo 20:1-2). Njiani akielekeea Yerusalem Paulo alipita Mileto alikokutana na wazee wa kanisa wa Efeso kuwaelekeza katika uongozi wao (Mdo 20:17-38).

#### IV. BARAZA LA YERUSALEMU

Katikati ya tukio lilioleezwa, mara tu baada ya safari ya kwanza, mukutano muhimu ulifanyika Yerusalem ambaa ulikuwa na mguso mkubwa katika kuenea kwa kanisa mionganini mwa Mataifa. Matukio yaliyopelekea kwenye baraza ni pamoja na tukio la mvutano wa Wayahudi na Mataifa. Tukio la kwanza la mfarakano lilitokea wakati mwanamke mijane wa Yerusalem alipoanchwa kuhudumiwa. Stefano, mmoja wao wa waliochaguliwa kuamua tatizo kisha akapondwa mawe. Wasiwasi unaonekana tena katika uzoefu binafsi wa Petro. Alikuwa ameambiwa na Mungu kuvunja sheria iliyokuwa imeshatolewa ya kula "chakula kinajisi." Mara baada ya hili tu Petro alishuhudia kukata shauri kwa mtu wa kwanza wa Mataifa, (Kornelio) (Mdo 10). Tukio la tatu lilihusu kanisa la Antioquia ambalo lilihusisha wakata shauri wengi Mataifa. Ilionekana kitu cha ajabu kwa Wayahudi Yerusalem ya kwamba Mataifa wa Antioquia watakuwa wanamfata masiya wa Wayahudi. Hivyo, walilichunguza wenywewe wakamtuma Barnabas kwenda kupeleleza (Mdo 11:19-24). Safari ya kwanza ya kimishenari ilikuwa kipande cha mwisho kwenye hatua ya tukio la

Matendo 15. Paulo na Barnabas waliona na kutafuta Mataifa waliokata shauri katika miji mingi ya Galatia. Mara baadhi ya Wayahudi wakristo kutoka Yerusalem walikuwa Antiochia, kituo cha harakati za Mataifa wakristo, wakifundisha kwamba kila mkristo anatakiwa kutunza amri za Musa (Mdo 15:1)

Hili lilipelekea mukutano wa Yerusalem. Swala muhimu ilikuwa kama Mataifa walitakiwa kuzifata sheria za Musa. Au weka kwa njia nyingine, je injili ilikuwa wazi hata kwa mataifa au walitarajiwa kuwa wa imani ya Yuda kwanza? Kwa kuongozwa na Mungu, halmashauri ilifanya uamzi wake bila usumbufu mwangi. Uhuru ulikuwa umetolewa kwa Mataifa ili kwamba wasitarajiwe kufata sheria za Musa. “*Kwa maana ilimpendeza Roho Mtakatifu na sisi, tusiwatwike mzigo ila hayo yaliyo lazima, yaani mjiepushe na vitu viliviyotolewa sadaka kwa sanamu, na damu na nyama zilizosongolewa, na uasharati, mkijizua na hayo mtafanya vema*”(Mdo 15:28-29).

Matukio katika Matendo 15 yana ukweli wa kimishenari na kitheolojia. Harakati za upandaji kanisa zinatokea wakati injili, katika utimilifu wake, inapokumbatiwa na kanisa . Wakati injili inapofichwa au kubadilishwa kwa mapokeo, sheria au “mifumo” iliyotengenezwa na-mwanadamu, nguvu yake ya kubadilisha maisha inakwisha. Tunajaribu kuweka msisitizo kwenye “mifumo.” Ilikuwa kitu cha asili kwa wakata shauri Wayahudi wa kwanza kuwatarajia Mataifa kuonyesha imani yao sawasawa na “mifumo” yao waliyokuwa wamezoea. Lakini Mungu alikuwa akifanya mambo mapya! Kama Halmashauri ya Yerusalem ingefanya uamzi wa kimakosa ukristo ungebakia kuwa tawi dogo la Kiyahudi badala ya kuieneza mionganoni mwa “mataifa yote” kama ilivyokusudiwa.

Harakati za upandaji kanisa zinatokea wakati injili, katika utimilifu wake, inapokumbatiwa na kanisa . Injili inapofichwa au kubadilishwa, nguvu yake inakwisha.

## V. KANUNI NYUMA YA SHUGHULI ZA KIMISHENARI ZA KIMIKAKATI

Maandiko yanatupa kwa upana shughuli za Paulo. Hatujui sana juu ya mitume wengine. Kwa jinsi hiyo, mapokeo yanasema kwamba mtume Mathayo alipanda makanisa huko Mesapotamia, Tomasi huko India, Petro huko Urumi, na Marko huko Misri wakati Anderea alichukua injili mpaka Sithia kaskazini mwa bahari nyeusi (Shenk, Uk. 157 na Foster, Uk. 40). Katika tukio lolote kanisa liliendelea kupanuka kwa kuendelea hata baada ya kipindi cha utume. Tambua uchunguzi ufuata:

- “Kristo amepanda taifa letu mpya la **wakristo katika kila taifa**.” Bardaisani, mkristo-mwenye sifa nzuri wa Edessa kasikazini mwa Mesopotamia karibu mwaka 200 Bk.
- “Lakini hao unaowaita ‘taifa la tatu’ wanaweza kuwa wa kwanza, kwa kuwa **hakuna taifa lisilo na wakristo**.” Tertulian wa Carthage karibu 200 BK.
- “**Kuna makanisa sasa kwenye mipaka ya ulimwengu**, na ulimwengu wote unapiga yowe kwa furaha kwa Mungu wa Israeli.” Origen 240 BK (Foster 1972, P. 35).

Hii inatokeaje? Ilikuwa ni kubahatisha? Mafunzo ya uangalifu katika Matendo yanadhihirisha kuwa kupanuka kwa kanisa kulitokana na mpango ulioongozwa na Roho ukizingatia kanuni ambazo tunaweza kutumia leo. Na sasa tumejifunza Matendo kwa uangalifu, zifuatazo ni badhi ya kanuni.

### A. Kujitoa Kuongozwa na Roho Mtakatifu

Kazi nyingi za kimishenari siyo tu matokeo ya mikakati ya kibiblia au kufanya uamzi mzuri , lakini ni uongozi wa kimungu. Roho alimpeleka Paulo kwa toashi Muethiopia; Bwana alimwambia Petro kwenda nyumbani kwa Koroneli; Roho Mtakatifu akasema na viongozi huko Antiochia akiwaambia kumtuma Barnabas na Paulo kama wamishenari. Roho alimwongoza Paulo kwenda Makedonia badala ya Asia (Mdo 16:6ff). Yesu alimtokea Paulo huko Korintho akimwambia kukaa pale. Roho Mtakatifu na nabii Agabas alidhihirisha kwamba Yesu alimwambia Paulo katika mazungumzo yake, kwamba “imempasa kuteseka kwa ajili ya jina langu.” (Mdo 9:16). Unabii huu ulimpeleka mpaka Yerusalem.

Hatuwezi kuziweza njia za Mungu kikamilifu, lakini tunaweza kuwa na uhakika kwamba kulikuwa na sababu kwa hayo yote yaliyozungumziwa hapo juu. Pengine Mungu alimzuia Paulo kufanya kazi Asia wakati wa safari ya pili kwa sababu mda haukuwa muafaka na kwa sababu Mungu alijua kwamba sehemu hasa ya kimikakati ya kuifikia Asia ilikuwa kutokea Efeso na siyo Bethania na Masia. Inashangaza kuona kwamba Paulo alipokwenda

Makedonia mtu wa kwanza kukutana naye ni Lidia anayetoka mji wa Thiatira katika jimbo la Asia. Pia tambua jinsi Mungu alivyoandaa njia ya barua yake kufika Efeso kwa kumtuma Prisila, Akila na Apolo huku kabla yake.

Wakiwa wameshahusika katika kazi, Paulo na wenzake walipata maelekezo wakiwa "njiani." Hakuna sababu ya kibiblia kwa mtu yejote kubakia amekaa mpaka hapo atakapopokea wito maalumu. Hao waliohusika katika upandajii kanisa lazima wafanye kazi katika maandalizi mazuri na mkakati lakini wakihitaji kufahamu kuwa Mungu ataingilia hata kubadili mipango yao—kuwaongoza kufanya kusudio lao la upandaji kanisa.

#### B. Kuhama kwa Haraka

Paulo alikaa wastani wa miezi michache tu katika miji mingi alikopanda makanisa. Kwa mfano alikaa wiki tatu tu huko Thesalonike. Jinsi gani Paulo aliweza kupanda makanisa kwa haraka kiasi hicho? Pengine Paulo alifahamu kanuni kuu ya upandaji kanisa na kujua lini alihitajika kuondoka. Alijua kuwa kulikuwa na kitu fulani kuhusu uwepo wake kama mwalimu mkuu ambacho kilizua maendeleo ya wengine. Mda mfupi Paulo aliokaa katika kila sehemu uliwalazimisha wengine kutambua kwamba wasingetakiwa kumtegemea katika kila jambo. Walitakiwa kutafuta rasilimali zao wenyewe. Paulo aliwafundisha viongozi na kumtumaini Roho Mtakatifu kuwaongoza waumini wapya. Kama anavyoelezea Roland Allen:

"Ni mafundisho ya waumini wapya yanayoandaa aina ya wakati ujao. Kama muumini wa kwanza amefundishwa kumtegemea mmishenari, katika kazi zote, kiuinjilisti, kielimu, jamii inakazia mikononi mwake, jumuia ya watoto wachanga inajifunza kujisikia uhuru wa kutendewa kwa mtu waliyepata ufahamu wao wa kwanza kwenye injili" (Allen 1962:81, 930).

Paulo alielewaa pia alikuwa ameitwa kuwa mtume. Kwa Paulo hili lilimaanisha kuwa "mwanzilishi", "mweka msingi" (Rum 15:20; 1Kor3:6-8). Paulo aliwatumaini wengine waliokuwa wamejaliwa kama wachungaji kuongoza makanisa aliyoanzisha.

#### C. Kuwawezesha Wengine Kwenye Huduma

Kama tulivyosema Paulo alihama kwa haraka, lakini kuna hali ya pekee inayoonekana katika utendaji huu. Paulo alikaa miezi 18 Korintho na miaka mitatu huko Efeso. Lakini katika matukio haya, wakati Paulo alipokuwa hahami, alifanya kazi katika njia ambayo injili ilikuwa inaendelea.

Kujifunza safari za Paulo kunadhihirisha mabadiliko ya taratibu katika kusisitiza wakati wa huduma yake. Wakati wa safari yake ya kwanza, alipanda angalau makanisa manne na kufanya ufuutiliaji kwa kila moja. Msisitizo wake ulikuwa uinjilisti wa mpakani na upandaji kanisa. Lakini wakati wa safari yake ya mwisho anaonekana kutokuwa na malengo yaleyle. Badala ya kuhama kwa haraka, alitumia mda wake mwingsi wa safari hii Efeso. Efeso kilikuwa kitovu cha kutosha kiasi kwamba alipanda kanisa moja tu (Efeso) wakati wa safari hii lakini aliwekeza mda wake wa safari katika kutembelea angalau miji tisa alikopanda makanisa kabla. Mkazo wake ulibadilika kutoka mipaka/uinjilisti kwenda kwenye ufuasishaji/ufundishaji. Wakati wa safari hii Paulo alikuwa na wanafunzi aliokuwa akisafiri nao (Mdo 20:1-2). Tunasoma pia juu ya huduma yake ya kufundisho kutoka kwenye ukumbi wa Tirano ambayo ilipelekea kuinjilisha jimbo la Asia (Mdo 19:9-10).

#### D. Kuhubiri Kwa Wanaoitikia

Miji yote aliyotembelea Paulo ilionekana kuwa na kiasi cha jumuia ya Wayahudi isipokuwa Filipi. Paulo kawaada aliingia kwenye sinagogi kuhubiri ujumbe wake. Hii ni sehemu ya kwamba yeze mwenyewe alikuwa Myahudi, na sehemu kwa sababu ya kuja kwa Masia kuna maana ya kipekee sana kwa Wayahudi (Rum 1:16), na sehemu kwa sababu watu kwenye sinagogi "wangehubiriwa-kwanza." Wangeelewa na kuipokea injili, ambayo ina mizizi ya Wayahudi, na kiasi kidogo cha mfarakano wa utamaduni.

Wakati Paulo akianzia katika sinagogi kama mtume kwa Mataifa, lengo lake hasa ilikuwa kwa Mataifa wanaomuogopa Mungu. Waliomuogopa-Mungu walikuwa Mataifa walioamini katika Mungu mmoja tu na wangeweza kukata shauri kwenye imani ya uyahudi kama kusingekuwa na sheria kali walizohitajika kutii, hasa za kutahiriwa. Waliomuogopa Mungu walihudhuria mikutano kwenye Sinagogi na wangekuwa wamejifunza maandiko ya Agano la Kale. Injili ilipokuwa imehubiriwa na mfarisayo, Paulo, kwenye Sinagogi, kutahiri hakukuhitajika, na

wengi waliomuogopa Mungu wangejisikia kwamba hii ilikuwa imani yenye maana kwao. Ujumbe wa Paulo ulikuwa wa Mungu mmoja ambao uliwavutia kwenye Sinagogi bila kulazimishwa ambako kuliwafanya kutokubadilika kuwa kwenye imani ya kiyahudi.


#### E. Kufanya Kazi Kutokea Kwenye Msingi wa Kimkakati kwa Ajili ya Harakati za Eneo

Paulo alijaribu kuinjilisha eneo lote, lakini siyo kwa kuhubiri kila sehemu. Badala yake, alianzisha maeneo ya kimkakati ya kanisa ambako injili ingeweza kuenea na kujaza eneo lote. (tazama Kielelezo 8.2).

Karibu vitovu vyote ambako Paulo alihudumu vilikuwa ni vitovu vinavyofaa sana kwa ajili ya biashara. Vilikuwa ni njia panda muhimu kwa siku hizo. Kwa hakika hata leo, kama mwanatheolojia aliyesafiri eneo nilichunguza, miji yote Paulo alikofanya kazi inaweza kufikiwa kwa treni au kwa boti au kwa zote. Hii inathibisha umuhimu wa maeneo haya. Paulo kwa uongozi na nguvu za Mungu, aliweza njia panda ya magari ya biashara kwa kueneza injili kutoka Yerusalem kote mpaka kwenye mji mkuu wa Urumi (Berkhof, Uk. 40).

Kwa kuanzisha maeneo ya kimkakati ya kanisa ambako injili ingeweza kuenea na kujaza eneo lote zima.

#### Kielelezo 8.2 Harakati za Eneo za Upandaji Kanisa



##### 1. Galatia kutoka Pisidia Antiokia

Kimikakati katika uchaguzi wa Pisidia Antiokia "Neno la Mungu likaenea katika eneo lote (Galatia)" (Mdo 13:49).

##### 2. Makedonia, Akaya, na kila mahali kutoka Thesalonike

Utume Mkuu kama ilivyoandikwa katika Matendo 1:8 ilikuwa imeelezewa katika kanisa la Thesalonike kile ambacho Paulo anasema "Maana kutoka kwenu neno la Bwana limevuma, si katika Makedonia na Akaya tu, ila na kila mahali imani yenu mliyonayo kwa Mungu imeenea kila mahali" (1The 1:8)

##### 3. Jimbo la Asia kutoka Efeso

Matokeo ya huduma ya Paulo ya kufundisha huko Efeso "Wayahudi wote na Wayunani katika jimbo la Asia wakalisikia neno la Bwana" (Mdo 19:10).

#### SULUHU

Je kupanuka kwa kanisa kulikuwa kumetolewa hivi hivi tu? Kupanuka kwa kanisa kulitokana na mipango ilioongozwa na Roho ikizingatia kanuni za huduma ambazo tunaweza tukaendelea kuzitumia leo. Kwa ufupisho, mpango wa Paulo ilikuwa kuinjilisha watu waliotayari kusikia katika vitovu vyta kimikakati, akiwezesha harakati za eneo za upandaji kanisa (hasa Galatia, Makedonia na Asia) chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Wanachohitaji wapanda kanisa zaidi ya kitu kingine chochote ni kurudi nyuma njia za wamishenari wa kanisa la kwanza.

#### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ilikuwaje siku ya pentekosti katika Matendo 2 siku kuu ya kuenea kwa injili?

- Kwa nini baraza la Yerusalemu lilikuwa muhimu sana?
- Jinsi gani mateso yalivyoathiri kuenea kwa injili? Mateso yamepelekea kupanuka kwa kanisa katika kizazi cha hivi karibuni?
- Kulingana na mafunzo yako ya Agano Jipya, ni makanisa mangapi Paulo aliyopanda moja kwa moja?
- Elezea mabadiliko katika msisitizo kati ya safari ya kwanza na ya tatu ya Paulo.
- Ni kwa jinsi gani utafiti uligusa kukua kwa kanisa katika kitabu cha Matendo?

### **VYANZO**

- Allen, Roland. *Missionary Method – St. Paul's or Ours?* Grand Rapids, MI: Wm. B. Eerdmans, 1962.
- Berkhof, Louis. *Paul the Missionary*. Grand Rapids, Mi: Eerdmans-Sevensma, n.d.
- Foster, John. *Church History: The First Advance*. London: Society for the Promoting Christian Knowledge, 1972.
- Shenk, David W., and Ervin R. Stutzman. *Creating Communities of the Kingdom, New Testament Models of Church Planting*. Scottsdale, PA: Herald Press, 1988.

MAONO YA KUM

9

SOMO LA

## Asili ya Harakati za Upandaji Kanisa

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kutoa asili zinazochocha harakati za upandaji kanisa. Wapanda kanisa wanatakiwa kujiona wenyewe kama sehemu ya harakazi za upandaji kanisa ambazo ni kubwa kuliko wazo la kusanyiko moja kwa mda.

### ☞ Wazo Kuu

- Harakati za upandaji kanisa lazima ziundwe kwenye mwamba mugumu wa neno la Mungu.
- Njia mpya ya kufikiria juu ya maono, kanisa, na uongozi ni msingi kwa harakati za upandaji kanisa.
- Matofari ya kujengea ya maombi, utafiti, uhamasishaji, mafunzo, uinjilisti na utupaji wa maono vinachangia katika mafanikio ya harakati za upandaji kanisa.
- Mungu ni msanifu wa harakati za upandaji kanisa.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

- Wakati yaliyoma katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .
- Kwa imani kuweza kuweka mkakati wa kuinjilisha eneo kwa njia ya upandaji kanisa.
  - Kushiriki katika harakati za upandaji kanisa za makanisa yanayokua ambayo yanaongezeka kwa kupanda makanisa mengine yanayokua na kuzaa makanisa.

## UTANGULIZI

Lengo la harakati za KUM ni ushirika wa waumini wa ushuhudiaji wa kwenye eneo hilo hilo la kijografia na kiutamaduni kumfikia kila mtu ili kwamba kila mtu atawea kusikia injili ikiwa imetolewa katika namna inayoendana na namna ya kiutamaduni katika matukio kadhaa na kuona jamiia ikiishi maisha ya Kristo.


Unapokuwa unasoma somo hili, harakati za kueneza upandaji kanisa zinakua katika jozи za mataifa ulimwenguni. Kila harakati zina vipengele vya kipekee, kutegemeana na utamaduni wake; lakini kwenye kiini zote zina lengo kama lilliolezewa hapo juu. Zote pia katika njia zingine zina sura au mfumo, asili iliyoelezewa hapo chini.

Kama tukifikiria harakati za kueneza upandaji kanisa kwa kutumia mfano wa nyumba (tazama kielelezo 9.1), **mwamba mugumu ni neno la Mungu**. Iliyojengwa kwenye mwamba huo mugumu ni mifumo mitatu ya kimsingi inayoweka uzio wa maenedeleo ya harakati za upandaji kanisa. Katika msingi huu, matofali ya kujengea ya maombi, utafiti, uinjilisti, mafunzo/ushauri, rasilimali na kutupa maono.

### I. MAPANA YA KIMSINGI KATIKA KUENEZA HARAKATI ZA UPANDAJI KANISA

Mfumo wa kwanza ni MAONO ambao hauzuili kuanzisha makanisa machache, isipokuwa mmoja unaoona taifa limejazwa makanisa yanayozaliana yaktumiza Utume Mkuu. Mfumo wa pili ni KANISA ambalo ni mkusanyiko wa watu wote wa Mungu, waliojaliwa na waliojawa na Roho Mtakatifu, wanaofanya kazi pamoa kutumiza Utume Mkuu. Mfumo wa tatu ni UONGOZI unaofundisha na kutoa watu wa Mungu kufanya kazi ya huduma. Kwa sababu haya ni muhimu, mkondo pekee katika taratibu hizi za upandaji kanisa umejitoa kwa kila mmoja.

### 9.1 Vipengele vya Harakati za Kueneza Upandaji Kanisa



## II. MATOFALI YA KUJENGEA YA KUENEZA HARAKATI ZA UPANDAJI KANISA

### A. Maombi: Yakitangaza Utetegemezi kwa Mungu

Sehemu ya harakati za upandaji kanisa ni kujenga matofari ya maombi, yote ya hiari na yaliyoandalisha. Maombi ni lazima katika yote kazi ya upandaji kanisa na kutunza kuendelea kwa harakati za upandaji kanisa katika mwelekeo sahihi.

#### 1. Maombi ya Kuombea

Maombi yanahitajika kwa niaba ya wamishenari, wapanda kanisa na wachungaji. Watu hawa wako kwene nafasi ya kiroho nyeti na wanahitaji maombi ya watu wa Mungu. Paulo anaeleza umuhimu wa kuombea siasa na viongozi wengine kama kipao mbewe katika maisha ya muumini (1Tim 2:1-3). Kujitoa huku kuwaombea watu katika mamlaka ni ili kwamba kuwe na hali ya kuridhisha kwenye kueneza injili.

#### 2. Kuombea Umoja

Yesu aliomba kwamba wafiasi wake wawe na umoja (Yoh 17:22-23). Paulo anawatia moyo waumini kuomba katika roho ya umoja mmoja kwa mwengine (1Tim 2:8). Pengine hakuna kinachotia moyo kama maombi ya ushirika. Maombi mara nyingi yanatumiwa na Mungu kuwaleta waumini pamoja, ambapo wangegawanyika kwa maswala mengine.

#### 3. Maombi ya Vita vya Kiroho

Kupanuka kwa kanisa ni vita vya kiroho. Shetani hataki harakati za upandaji kanisa katika eneo lako na atahamasisha mapepo dhidi yake. Vita vya kiroho vyenye nguvu dhidi ya Shetani, utawala wa kimapepo, mamlaka, nguvu za ulimwengu wa giza na msukumo wa nguvu za uovu zinahitaji kuishi maisha ya ukristo vyenye nguvu na maombi (Efe 6:10-20).

### B. Utafiti: Kuionna Picha Kubwa

Utafiti unawezesha watu wa Mungu kuona jinsi Mungu anavyofanya kazi kwa kufanya wazi picha kubwa ya kile Mungu anachotaka kufanya katika taifa lao au kikundi cha watu. Utafiti pia unatoa taarifa ambazo zinawasaidia wakristo wafanya kazi kufanya uamzi mzuri kuhusu juhudzi za huduma na mkakati. Zaidi hasa, inwasaidia mawakala na makanisa kujua wapi makanisa yanahitajika kupandwa na njia ya aina gani ya uinjilisti ni ya ufanisi mionganoni mwa makundi mbali mbali ya watu.

Harakati za upandaji kanisa mara nyingi ni pamoja na utafiti kwa sababu watu waliohusika wanataka kujua wapi na jinsi gani Mungu anafanya kazi. Wakati mwingine utafiti ni moja ya kitu cha kwanza kinachofanyika na matokeo yake ni kuhamasisha wengine, kutoa harakati.

Kuna sehemu mbili maalumu ambazo utafiti unafanyika:

#### 1. Kanisa Maalumu liliopandwa

Kwa kudhihirisha mtazamo wa dunia na mahitaji yaliyopo ya watu wanaoishi katika eneo linalolengwa, utafiti unawenza kusaidia kuonyesha aina gani ya uinjilisti na mkakati wa upandaji kanisa unaopaswa kutumika. Utafiti pia utadhihirisha raslimali zilizopo za upandaji makanisa ambazo zinaweza kuhamasishwa kusaidia juhudzi za upandaji kanisa.

#### 2. Eneo – Taifa/jimbo/tarafa/mji

Kutafiti nchi nzima kunaweza kutoa picha kwa ujumla ya kiwango cha ukristo ndani yake. Taarifa hizi kwa hiyo zinaweza kutia changamoto viongozi wa kanisa na hitaji la kuhamasisha makanisa kwa ajili ya uinjilisti kulijaza eneo hilo kwa makanisa.

Ni utafiti wa aina gani unahitaji kufanyika katika eneo lako?

### C. Kuhamasisha Raslimali

Moja ya kipengele kinachoonekana cha uhamasishaji ni raslimali. Kanisa linapokua katika Agano Jipy, waumini walihamasisha raslimali zilizohitajika kwa ukuaji wake. Watu wa kanisa la Yerusalem walitoa kwa kujitoa kusaidia wengine walio na mahitaji (Mdo 4:32-37). Wakristo waliwasihhi wakristo kusaidia waumini wengine amba hawakuwa na njia nyingine inayoonekana ya kuwasaidia, kama vile wajane wanaompenda Mungu (1Tim 5:9-16). Waliokuwa na mali walishauriwa kutoa zaidi, kuwasaidia waliokuwa na vichache (1Tim 6:18-19).

Kwenye moyo wa swala la raslimali ni ukweli wa kimsingi kwamba watu wa Mungu wenye wanatoa njia ya msingi kwa ajili ya kazi ya injili. Utimizaji wa Utume Mkuu katika taifa unatakiwa kufanyika kimsingi kwa raslimali zilizohamasishwa za waumini wa nchi hiyo. Sehemu yao ya kumi na matoleo yanatakiwa yatumike kusaidia kazi yao. Niki Nedelchev ni kiongozi wa taifa kutoka Bulgaria. Niki ana uzoefu mkubwa katika uhamasishaji wa raslimali kwa ajili ya huduma ya upandaji kanisa. Niki anaandika:

“Kama makanisa ya Bulgaria yanahitaji kuendelea kukua na kuongezeka, rasilimali, yote wanadamu na fedha, kimsingi lazima vitoke Bulgaria... Tunakaribisha uwekezaji Bulgaria na watu wa Mungu kutoka nchi zingine. Kwa jinsi hiyo, uwekezaji huo unatakiwa ufanywe katika mfumo wa ushirika wa kimkakati na huduma za Bulgaria. Hao washiriki wanatakiwa wawe na matarajio wazi na wawe wamebuni mda maalumu, kuepuka kujengeka kwa utegemezi wa mda-mrefu.”

### D. Kufundisha/kushauri: Kuwaandaa Wengine Kwenye Huduma

Kuwafundisha wainjilisti, viongozi wa kikundi kiini, wapanda kanisa, na wachungaji katika mtindo wa ongezeko kunachochea harakati za upandaji kanisa. Kila mmoja wa wafanya kazi hapo juu anahitaji aina tofauti ya mafunzo, na kwa hiyo mchanganyiko kadhaa wa njia za kufundisha zinahitajika kuwepo kusaidia harakati za upandaji kanisa.

Kuwafundisha wainjilisti, viongozi wa kikundi kiini, wapanda kanisa, na wachungaji katika mtindo wa ongezeko kunachochea harakati za upandaji kanisa.

Matendo 20, wakati Paulo alipowasalimia wazee wa Efeso, inatoa baadhi ya ushauri mzuri wa mafunzo ya viongozi wa kanisa mahali popote. Matendo 20:20, 31, na 35 inaonyesha kwamba Paulo “alifanya kazi sana,” “mchana na usiku,” na wazi wazi na kutoka nyumba kwa

nyumba.” Upandaji kanisa na kuwfundisha viongozi wa kanisa inachukua kazi ngumu. Matendo 20:20 na 27 inaonyesha kwamba aliwfundisha kwa uthabiti. Alifundisha kilichokuwa “msaada” kwenye kazi yao. Matendo 20:33-34 inaonyesha kwamba aliishi kwa ukamilifu. Kulikuwa hakuna swali kuhusu nia binafsi ya Paulo. Hakuna mmoja ambaye angetoa mashaka yoyote juu ya alivyoshughulikia pesa. Matendo 20:35 inaonyesha kwamba Paulo alifundisha na kuwa kielelezo cha utoaji na uaminifu. Matendo 20:31 na 36 inaonyesha kwamba Paulo alimwaga hisia zake kwenye uhusiano wake na viongozi hawa walitoa machozi kwa pamoja. Huduma inatoka katika uhusiano. Mafunzo bora ni pamoja na kushauriana mmoja kwa mwngine na siyo tu elimu ya kawaida.

Kanuni zifuatazo zinahusu kuwfundisha viongozi katika mandhali ya Upandaji kanisa.

1. *Mafunzo Yanatakiwa Kwenzie Uongozi*

Mafunzo ambayo viongozi wanapokea yanatakiwa yawawezeshe kuwaandaa wengine kwa ajili ya harakati zinazozalisha makanisa na kueneza injili kwenye eneo lote. Tambua katika Matendo 20:15-38 kwamba Paulo anawakumbusha viongozi wa Efeso jinsi alivyofanya kazi nao wakati akiwfundisha uongozi. Kutoka Efeso, Paulo aliwaandaa waumini kuendesha harakati za kiroho ambazo zilifunika eneo lote.

Kitabu cha Matendo kinaonyesha Paulo akielezea jinsi alivyowafundisha viongozi na kumwambia Timotheo jinsi ya kuwachagua. Timotheo ya kwanza 3:1ff inaonyesha vitu vya lazima kwa mmoja kuwa kiongozi. Kwa mfano, tabia inachukua kipao mbele dhidi ya upendeleo (2Tim 3:2-10). Mafunzo ya uhusiano ya Paulo na Timotheo yalikuwa ya Baba na Mwana (2Tim 2:1).

2. *Mfunzo Yanatakiwa Yawe Yanayozaliana*

Harakati za uandaji kanisa zinahitaji mafunzo yanayoweza kuongezeka (i.e. yanayoweza kufundishwa tena kwa wengine). Mafunzo ya Paulo yaliendelea kwa vizazi vine. Yalianza na Paulo akipitisha mafunzo kutoka moyoni mwake (2Tim 2:2). Kisha Timotheo aliwfundisha watu waliokuwa “wakiweza kuwfundisha wengine pia.” Mafunzo na mafundisho tunayoyatoa tunapokuwa tunasaidia watu kukua ndani ya Kristo na kuandaa viongozi wapya yanapaswa yafanyike ili kwamba waweze kuyazalisha.

Kielelezo hiki cha vizazi-vinne ni njia ya kimkakati ya kupanga mafundisho. Hii inahitaji urahisi ili kwamba wengine waweze kuyatoa bila vyombo vyenye gharama, ufahamu wa hali ya juu, au elimu ya kawaida. Mafunzo yanayozaliana yanaweza kuwa changamoto kwa sababu nyenzo tunayofundisha inahitaji siyo tu kuwa rahisi lakini ya undani na yenye thamani ya juu ili kwamba yapekee makanisa yenye nguvu ambayo yanagusa maisha ya watu na jumuia.

Mafunzo yanatakiwa yawe na yote maneno na mifano. Tunapofundisha na kufunza, kile tunachofundisha kinachoweza kuzalishwa katika ngazi nne? Ni rahisi vya kutosha? Ni kwa undani vya kutosha? Inaweza kuendelezwa kwa mfano uleule na maneno?

3. *Mafunzo Yanatakiwa Yawe Yanapatikana*

Ni kazi ya makanisa ya mtaa kuwafunza wafanya kazi kukamilisha Utume Mkuu. Watu wanapofikiria juu ya vipindi vya mafundisho, kawaida wanafikiria vyuo vya seminari na Biblia au vipindi vingine vya makazi. Hii ni ya kujutia, kwa kuwa baadhi ya vipindi vya mafundisho yenye ufanisi siyo vya makazi na vinavyotokana-na kanisa. Kwa kudhani kuwa wafanya kazi wa kanisa wanahitaji kwenda mbali shulenii kufundishwa kunaweza kukakwamisha harakati za upandaji kanisa. Wakati, mara nyingine, makanisa ya mtaa yanachukulia bila mzaha majukumu yao ya kufundisha wafanya kazi, kisha mafunzo yanapatikana kwa watu zaidi.

4. *Mafunzo Yanatakiwa Yakue Kutoka Kwenye Msingi wa Kimkakati*

Wakati wa safari ya tatu ya Paulo ya kimishenari, alitumia karibu mda wake mwngi Efeso (Mdo 19:9-10). Alichagua mkakati wa kufanya kazi kuanzia kwenye msingi wa kimkakati kuwfundisha viongozi ambao wangeweza kuliflikia eneo lote (tazama pia Mdo 2:18ff.). Kutoka kwenye kipindi cha mafunzo ya Paulo, viongozi hawa walikwenda nje na kufikia jimbo la Asia kwa neno la Bwana. Makanisa yaliyoorodheshwa katika ufunuo sura ya 2 na ya 3 yote yako katika eneo hili na yanaweza kuwa yamepandwa na watu waliojifunza kuto kwa Paulo wakati wa kipindi chake Efeso. Kwa kuwaandikia waumini huko Kolosai

(katika jimbo la Asia), Paulo hata anataja makanisa “ambayo hayajaniona uso kwa uso” (Kol 2:1).

Umeshapata msingi wa kimkakati kwa ajili ya kufundishia wapanda kanisa ambao watasaidia harakati zako kuenea kwenye eneo lako lote katika hali ya mafanikio zaidi?

#### E. Uinjilisti: Mashamba ni Meupe

Mungu anafanya kazi ulimwenguni kuwaleta watu kwake. Ametupatia huduma ya upatanisho (2Kor 5:18). Ni wajibu wa kanisa kuieneza injili kwenye jumuia yake na kupita. Kwa harakati za kueneza upandaji kanisa kutokea, injili lazima itangazwe kila mahali.

Yesu aliwaonesha wanafunzi wake kwamba hawakuweza “kuona” watu kama Mungu alivyowaona—aliwuwa ameshaaandaa kwa ajili ya (nyeupe) mavuno (Mt 9:35-38). Watu wanahitaji kabisa uhusiano na Mungu. Waliopotea wanaishi huku ndani yao Mungu akiwamefagiwa nje ya nafsi zao, na wanatafuta kitu cha kujalizia sehemu hii tupu. Matunda ya kiinjilisti ni ya chini siyo ya kutosha kwa sababu watu hawamtafuti Mungu, lakini kwa sababu wanakataa mifumo na kuonyeshwa kwa imani ambayo makanisa ya mapokeo yanatumia. Mifumo mipya na kuonyesho kusikopitwa na wakati kunahitajika kufikia kizazi kipyä.

Uinjilisti ni kazi isiyo ya wataalamu, lakini kwa kila muumini ambaye amekutana na upendo wa Mungu. Kueneza upandaji kanisa kuweza kutokea, waumini wengi lazima wafunzwe iwezekanavyo, wahamasishwe, na kutiwa changamoto kushirikisha imani zao majumbani kwao, sehemu ya kazi, sehemu za starehe au—kila mahali.

#### F. Utupaji Maono

Harakati za uandaji kanisa zinaanza na maono. Maono yanaleta bayana kwenye kazi, yanavuta ushirikiano miongoni mwa vikundi vya waumini, na kuhamasisha watu wa Mungu kujaribu mambo makubwa kwa ajili yake. Maono au ‘Z’ ni kuona makanisa yameanzishwa kila mahali ili kwamba kila mwanaume, mwanimke, na mtoto wanapanata nafasi ya kusikia na kukubali injili

Lengo ni ushirika wa waumini wanaoshuhudia kwa kila mtu wanayeweza kumfikia ili kwamba kila mmoja aweze kusikiliza injili ikitolewa na kuona wakiishi maisha ya Kristo katika jumuia.

Baadhi ya maeneo yanakosa harakati kwa sababu mwili wa Kristo unakosa maono kwa ajili yake. Jinsi gani watu wanaweza kukazania kile ambacho hawakiwazii? Kwa kutofautisha, katika sehemu za ulimwengu ambako kuna harakati za upandaji kanisa, kuna maono makuu.

Maono yanachochewa kwa maombi, utafiti na kwa kuuliza “nini Mungu anataka?” Hili ni swali lenye nguvu. Maono yanaweza kuulizwa kwa mmoja kwa mwingine, katika vikundi au katika semina ya maono ya-kurusha. Hao ambao wanafikiria kwa undani wanakuja kugundua kuwa Mungu anataka watu wote wapate nafasi ya kusikia injili katika lugha yao, na zaidi ya haya kwamba Mungu anataka kukua katika namna kwamba kila mmoja ana nafasi ya kuwa mfuasi wa Yesu. Haya ni maono ya KUM ambayo lazima yaendelezwe kwa wengine katika nafasi ya utupaji wa maono mbali mbali.

### III. MATOKEO: HARAKATI ZA UPANDAJI KANISA

Dari, au msonge wa nyumba zetu, ni harakati za upandaji kanisa. Lengo ni ushirika wa waumini kushuhudia kati kati ya eneo la kijografia na utamaduni kwa kila mtu wanayeweza kumfikia ili kwamba kila mmoja atawea kusikiliza injili ikitolewa na kuona wakiishi maisha ya Kristo katika jumuia. Kuona Utume Mkuu umekamilishwa, ni lazima tuwe na mitindo inayozaliana majumbani na hata kwenye tamaduni zote.

#### A. Upandaji Makanisa Yanayozaliana.

Upandaji makanisa yanayozaa yenye ni njia bora ya kuinjilisha eneo. Upandaji makanisa kwa mtindo wa nyongeza hautapelekea harakati. Moja kujumlisha moja kujumlisha moja sawaswa na tatu. Moja mara mbili mara mbili sawasawa na nne.

Ni vigumu kuona tofauti mwanzoni, lakini kwa kulinganisha vipande hivi kwenye shimo refu inaleta tofauti KUBWA. Mtindo wa kuzidisha ni mtindo ambao unawajibika kueneza upandaji kanisa. Hii ina maana kwamba wakati kanisa jipya linapandwa, linatakiwa liwe na maono ya kuzaa hata kuanzia kwenye mwanzo wake.

Waenezaji upandaji kanisa wanaangalia mtindo wa kuzaliana usio na mwisho. Wanataka kupanda kanisa linaloweza kuzalishwa kiurahisi ili kwamba harakati ziweze kutokea. Waenezaji upandaji kanisa hawamalizi wanapokuwa wamepanda kanisa—wanatarajia kanisa hilo kuzaliana na hivyo tu wanakaribia kwenye ukamilishaji wa kusudi la Mungu.

#### B. Upandaji Kanisa Katika Tamaduni Zinazoingiliana

Mara makanisa yanapoongezeka mara dufu kawaida yanazaa ‘aina yake.’ Hii ina maanisha katika hatua fulani mvumbuzi na upandaji kanisa katika tamaduni zinazoingiliana inaweza kuwa lazima kufikia kikundi kipy Cha watu kwenye eneo.

Uamsho huko Asia ulifikia kwenye mipaka yote ya kiutamaduni kwa wote “Wayahudi na Wayunani” (Mdo 19:10). Waefeso 3:6 inaeleza kwamba injili kuvuka mipaka yote ya tamaduni ni maajabu ambayo yametimizwa na kanisa. Watu wa Mungu siyo kikundi kimoja cha kiutamaduni isipokuwa kutoka katika mataifa ya ulimwengu (Uf 7:9-10). Upandaji kanisa katika utamaduni unoingiliana ni moja ya shughuli za kanisa zonazotimiza maajabu haya.

#### MWISHO: “BWANA HUINJENGA NYUMBA”

Mungu ni msanifu wa harakati za kujenga makanisa. Harakati kuu za kiroho zinamtegemea Yeye na mda wake muafaka. Hakuna anayeweza kumlazimisha Mungu kwenda. Mungu ni mwenyezi na anakwenda anapotaka. Katika kitabu cha Matendo, tunaona haya yakiwa yameonyeshwa katika maisha ya Paulo. Paulo alikuwa na haja ya kuifikia Asia kwa injili na alikuwa akipanga kwenda huko mpaka Roho Mtakatifu alipoingilia. Alipokuwa akisonga mbele, Mungu alimpa mwelekeo mpya. Baadaye, katika Matendo 19, wakati Mungu alipofungua mlango kwa Paulo kufanya kazi katika jimbo la Asia, alionyesha nguvu zake kipekee na kwa njia za ajabu (Mdo 19:1-12). Asia yote ikalisikia neno la Bwana! Baadhi ya dalili za nguvu za Mungu (kama uponyaji kwa njia ya vitambaa) haikuwahi kutokea katika hesabu nyingine ya kimaandiko. Ilikuwa wazi kwa watu wa Asia kwamba Mungu alikuwa akifanya kazi nao katika tabia isiyo ya kawaada. Wazo kwa kifupi ni kwamba huko Efeso wakati huo, Mungu katika ukuu wake alichagua kufanya kazi kwa njia ya kipekee.

Kuanzisha harakati za kueneza upandaji kanisa haiwezekani kama siyo mda muafaka wa Mungu. Jinsi gani tunaweza kujua wapi na lini anafanya kazi au anatamani kufanya kazi?

Kujua mapenzi ya Mungu lazima kwanza tumjue Mungu. Kumjua lazima tuanzishe uhusiano naye kwa maombi. Tuanapokutana katika maombi na pengine katika kufunga, atatuonyesha mapenzi yake. Pengine sababu hafanyi kazi ni kwa sababu kuna dhambi ambayo haijashughulikiwa. Pengine ataidhihirisha hiyo sasa mda wa kupanda mbegu, au wa kumwagilia kwa maombi mbegu ambayo imepandwa. Pengine atatuonyesha njia tofauti ambayo itakuwa ufunguo wa kufungua miyo ya watu, kuendelea kutafuta uso wake kwa maombi.

Kujua mapenzi ya Mungu lazima kwanza tumjue Mungu.

#### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni nini maono yako?
- Harakati za maombi ni sehemu ya mpango wako wa upandaji kanisa?
- Jinsi gani tunafanya kazi na mwili wa Kristo uliopo kabla ya upandaji kanisa?
- Una mpango wa kieneo wa upandaji makanisa katika miji inayozunguka?
- Ni wapi hasa Mungu anafanya kazi katika maisha yako?
- Ni asili zipi za harakati za upandaji kanisa zilizopo katika eneo lako?



---

## KANISA

---



# Kanisa na Vipawa Vya Kiroho

## UWEZESHAJI WA MUNGU KWA AJILI YA HUDUMA

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kusaidia timu ya upandaji kanisa kutambua vipawa vya kila mmoja ili kwamba wote waweze kumtumikia Bwana katika namna aliyowajalia.

### ☞ Wazo Kuu

- Vipawa vya kiroho vinatolewa na Roho Mtakatifu kuuwezesha mwili wa Kristo
- Vipawa vya kiroho havifanani kama kawaida au uelekevu na uwezo unaojifunzwa.
- Vipawa vya kiroho vinaweza kugunduliwa kwa kupitia huduma na kisha kuendelezwa.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoelewaka, kila mshiriki anatakiwa:

- Ajue kugundua kipawa chake na kuwasaidia wengine kugundua vipawa vyao vya kiroho.
- Kuwa tayari kufanya mabadiliko yoyote ya lazima kufanya kazi na wengine kulingana na vipawa vya kiroho.
- Kushiriki katika juhudi za timu za upandaji kanisa ambapo kila mjambe anaweza kuwa wa ufanisi zaidi kulingana na kipawa cha kiroho Mungu alichompa kila mmoja.

### ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Tambua kuwa hili ni somo la masaa-mawili. Kama kutulia kunahitajika, inawezekana kupumzika kati kati ya hatua ya 111, "Uwezo... Uliotolewa na Roho Mtakatifu...", na hatua ya 1V, "Uchunguzi kutoka kwenye orodha ya Vipawa Vya Kiroho."

## I. KWA NINI TUNAHITAJI VIPAWA VYA KIROHO?

Kanisa ni umilele wa kiroho. Tunaamini kwamba katika nguvu za asili za ufalme wa Mungu , malaika na mapepo wapo. Tunaamini pia kwamba Mwanadamu hakujiteza peke yake tu, isipokuwa aliumbwaa na kujaliwa kimwili na kiroho. Tu zaidi ya mwili, damu na chembechembe. Tunatamani kuishi maisha yenye nguvu ya asili, kuishi katika roho badala ya mwili. Paulo alieleza:

"Maana inagawa tunaishi katika ulimwengu, hatufanyi vita kwa jinsi ya ulimwengu. Maana silaha za vita vyetu si za ulimwengu, bali zina uweza katika Mungu hata kuangusha ngome (2Kor 10:3-4).

Kanisa lazima litumie nguvu ya asili. Kilazima, kuna aina mbili zinazopatikana kwetu—*maombi* na *vipawa vya kiroho*. Zote zinifikia nguvu za Mungu kwa niaba ya watu wake na kazi yake. Zote zinifikia nguvu ya Mungu kwa niaba ya watu wake na kazi yake. Zote ni muhimu kukamilisha huduma ambayo ni ngumu sana kwa juhudi za kibinadamu. Mungu hakukusudia kwamba tunahudumu kwa uwezo wetu. Anakusudia kutusaidia. Yesu aliwaagiza wanafunzi wasiondoke Yerusalem au kuazisha huduma yao mpaka watakopokuwa wamepokea nguvu kutoka kwa Roho Mtakatifu (Mdo 1:4-5).

Bwana ametoa aina kadhaa ya vipawa kwenye mwili wake kuuwezesha kufanya kazi sawasawa. Moja ya kitengo cha **vipawa** "kuwaandaa watu wa Mungu kwa ajili ya kazi za huduma" (Efe 4:12). Kitengo kingine cha **vipawa** kinahusika na uwezo maalumu kwa ajili ya huduma unaotolewa kwa mchanganyiko tofauti kwa kila muumini. Tunachojua juu ya kila moja ya vitengo hivi tunajifunza kutoka kwenye maandiko.

## II. VIONGOZI: WALIOTOLEWA NA YESU KUUANDAA MWILI

Kitengo hiki cha kwanza cha vipawa ni pamoja na viongozi walioelezewa katika Waefeso 4:11-16. Hizi siyo nafasi au ofisi ambazo watu wamechaguliwa. Hawa kwa kifupi ni watu waliotolewa na Mungu kwenye mwili wa Kristo kumwandaa kila mmoja kufanya sehemu yake. Watu hawa siyo wataalamu kufanya kazi kwa ajili yetu; ufanisi wao unapimwa kwa ufanisi wetu tunapofanya kazi ya huduma.

Somo linaorodhesha mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji/walimu. Hao wenye nafasi ya utume ni hao ambao wametumwa nje kuwa msingi katika kuanzisha huduma mpya. Hao walio na nafasi ya unabii wanalitangaza neno la Mungu kwenye mwili wakati wainjilisti wanalitanganza neno kwa waliopotea. Wachungaji/walimu wanalinda na kuwafundisha watu wa Mungu. Kuelewa nafasi ya kiongozi kwenye mwili, fikiria mwinjilisti: hawezu kufanya tu uinjilisti; lazima pia awaandae wakristo wengine kufanya uinjilisti.

## III. UWEZO: UNATOLEWA NA ROHO MTAKATIFU KUWEZESHA MWILI

### A. Tafsiri

Kitengo kingine cha vipawa ni uwezo unaotolewa kwa waumini na Roho Mtakatifu. Uwezo wa asili au ulisomewa na vipaji vinatakiwa vitumike katika huduma ya Mungu. Kwa jinsi hiyo, Roho pia anawapa waumini uwezo wa kuchangia kwa namna ya kipekee katika kuujenga mwili wa Kristo. Hivi vinaitwa **vipawa vya kiroho**. Ukweli fulani unaosimama kwenye vipawa hivi ni:

- Kila muumini ana angalau kimoja (1Kor 12:7; 1Pet 4:10)
- Vinatolewa kwa kutaka kwa Roho badala ya kuhitaji kwetu wenyewe (1Kor 12:11)
- Vipo kwa ajili ya faida ya wote badala ya faida ya mmoja (1Kor 12:7; 12-27 Rum 12:4-5)
- Kipawa (vipawa) tulivyonyavyo ni kazi ya Roho (1Kor 12:4). Huduma ambayo tunavitumia inaunganika na Kristo (1Kor 12:5), na ufanisi wake ni kazi ya Mungu (1Kor 12:6). Wajibu wetu kwa kifupi ni utiifu.

### B. Vipawa vya Kiroho na Mwili wa Kristo

Mungu amegawa vipawa hivi kwa kusudi la kujenga mwili

#### 1. *Umuhimu wa kila Mjumbe*

Maelezo ya mwili katika 1Wakorontho 12 yanaonyesha hitaji kwa kila mjumbe kutimiza nafasi yake kwenye mwili. Kama vile mwili unavyouguia mjumbe mmoja anapoumwa, mwili wa Kristo unaumia wakati mijumbe mmoja anaposhindwa kutumia kipawa chake. Kila muumini ana “kazi njema” (Efe 2:10) za kutimiza. Kazi hizi haziwezi kutimizwa katika nguvu za kibinadamu. Tunahitaji nguvu ya asili ya Roho Mtakatifu kufanya kazi ndani yetu kuweza kuvikamilisha.

#### 2. *Kazi ya Watu “Waliojaliwa”*

Mungu ametoa watu waliojaliwa kwenye kanisa kuongoza na kuwafundisha waumini. Kila kanisa la mtaa lina mtu binafsi aliye na kipawa cha kipekee katika maeneo haya. Kwa jinsi hiyo, hivi havijakusudiwa kuwa kwa kikundi cha wa hali ya juu wanaofanya huduma ya kanisa. Badala, Efe 4:11-13 inaweka wazi kwamba wanatakiwa kuwaandaa watu wa Mungu ili kwamba waumini hao waweze kuchukua kazi ya huduma. Ni muhimu kwamba kila muumuni anagundua na kutumia kipawa chake kwenye huduma.

#### 3. *Kuhudumu Neema ya Mungu*

Tunapotumia vipawa vyetu, hasa tunakuwa tunahudumu neema ya Mungu (Pet 4:10-11). Neema ya Mungu na nguvu inamiminika kupitia sisi kwenda kwa wengine tunapohudumu. Mungu anataka kuhudumia watu, na amechagua kufanya kupitia sisi—hasa kwa kutumia vipawa vyetu vya kiroho. Ameshaamua jinsi anavyotaka kutumia kila mmoja wetu, na ametupatia vipawa vinavyoafikiana. Kazi yetu ni kuvitumia, na kuzaa matunda kwa ajili yake.

### C. Muonyesho wa Kipawa (vi) cha Mtu

Kuonyesha vipawa yetu ni vipi kunahitaji mda na uzoefu. Kama hujui vipawa vyako ni vipi, unaweza kujifunza kwa kujua vipawa ni nini kwa ujumla, kuhusika katika huduma ya mwili, na kutathimini Mungu anachofanya kupertia wewe kwa njia ya vipawa vyako na uwezo wa asili. Katika hisia vipawa vyako vitakuwa dhahiri kwako na wengine unapohudumu.

Hakuna jaribio la vipawa vya kiroho kwenye Biblia. Havitegemei juu ya uwezo wa kawaida au uliojifunzwa. Mganga siyo lazima kwamba ana kipawa cha rehema, au mwalimu kuwa na kipawa cha kufundisha. Vitu hivyo lazima yawepo mafunzo na uzoefu kwenye utalamu huo, lakini hii siyo sawa na kupewa vipawa vya kiroho. Vipawa vyao hasa vinaweza kuwa uinjilisti, utawala au aina nyingine. Kutathimini cheo chako siyo njia ya kugundua vipawa vya kiroho.


Kipawa kinagunduliwa kwa ufanisi wake kinapokuwa kimetumika. Tunapot wahudumia wengine, neema ya Mungu, nguvu na baraka zinazominika kutoka katika vipawa yetu kwa kiwango kinachopita uwezo wetu wa kibinadamu. Njia pekee ya kugundua vipawa yetu ni kuhusika katika mifumo mbali mbali ya huduma na kuangalia kuona Mungu anachotumia. Utaratibu ni wa lazima "kujaribu na kukosea." Kwa kuwa nguvu ya Mungu itamiminika kupertia kwetu kwenda kwa wengine, ni muhimu kusikiliza kwenye ushauri wao. Tuanaweza tusigundue jinsi Bwana anavyotutumia, lakini wengine wataona.

Kipawa kinagunduliwa kwa ufanisi wake kinapokuwa kimetumika.

Kuna vipawa vingi vya kiroho vilivyo orodheshwa kwenye Agano Jipy (tazama fungu la D hapo chini). Kwa kuwa kila orodha ina vilivyo tofauti, inaonekana yamkini kwamba hakuna orodha iliyo kamili. Inawezekana kukawa na aina nyingine ya vipawa vya kutumikia. Pia, ni wazi kwamba kila muumini ana kipawa. Lakini si wazi kama kila mmoja wetu ana kimoja. Wengine wanaweza kuwa na viwili au zaidi. Ni vigumu kusema. Kwa sababu ya upana huu, ni lazima kwamba waumini wajihishe katika huduma za aina nyingi.

Ingawa vipaji vya asili au vya kusomea si sawa na vipawa vya kiroho, mafunzo au vipaji vinaweza kwa hakika kuongeza ufanisi wa kipawa. Labda, kama mtu ana kipawa cha kufundisha, hii ina maana Mungu anataka kumbariki katika huduma hiyo. Lakini kipawa si badala ya kujifunza ili kwamba viweze kupata cha kusema. Mungu anaweza kubariki kidogo tulicho nacho. Anapenda vilevile kubariki kingi tulichonacho. Kuwa na kipawa siyo kibari cha kutokuwa mvivu. Hii inahusu kipawa chochote. Mara tunapotambua vipawa tulivyonavyo, tunatakiwa kufanya kila linalowezekana kuviendeleza ili kwamba tuweze kuongezeka kuwa zana bora kwa huduma ya kanisani.

#### Kielelezo 9.1 Mungu Anazidisha Juhudi Zetu



#### D. Maelezo ya Vipawa Vya Kiroho

Marejeo makuu mawili ambayo kuelewa kwetu kunatokana ni Warumi 12 na 1Wakorintho 12:14. Kwa kujua asili ya jaribu letu la kuruhusu somo hili kuwa la kugawanyika, Roho Mtakatifu anaweka ukurasa mkuu juu ya upendo, 1Wakorintho 13, katikati ya mafundisho yake ya vipawa. Kufata mpango wa alfabeti badala ya orodha ya vipao mbele

#### E. Tahadhari Mbili

Kwanza kumbuka, kama ilivyoelezwa nyuma, kwamba ufahamu wetu wa kipawa kimoja au wa vipawa vyote hivi ni kutoka kwenye Biblia. Pili, kuwepo kwa baadhi ya vipawa hivi ni jambo la kutokubaliana katika mwili wa Kristo. Mabishano kawaida yanaingilia kama endapo baadhi ya vipawa viro au havipo kwenye kanisa leo, tangu Agano Jipyä lilipoandikwa. Baadhi wanaamini kwamba, kwa kumalizika kwa ufunuo wa Mungu ulioandikwa, baadhi ya vipawa, hasa katika mfumo wa kimiujiza, vimekoma. Wengine wanaamini kwamba Biblia inachofundisha kuhusu vipawa vya kiroho kwenye kanisa la Agano Jipyä bado vinatumika kwa ajili ya kanisa leo. Bila mzaha, Kwa unyofu, na wasomi waliosomea wanakubaliana na pande zote. Kwa hiyo nini tufanye? Ufumbuzi rahisi ni kupima na kuonaisha utii wetu na usoefu kwenye matumizi kamili na rahisi ya kile Biblia inachosema.

### IV. VIFUNGU VYA MAFUNZO YA BIBLIA KWA KUFATA NENO JUU YA VIPAWA VYA KIROHO

#### A. Uchunguzi

Chini kuna orodha ya mistari inayozungumzia vipawa vya kiroho. Kwenye safu ya pili andika uchunguzi kwa jumla juu ya vipawa vyote; kwenye safu ya tatu orodhesha vipawa. Baadhi ya kazi za kuanzia zimeshafanyika kwa ajili yako.

#### B. Ufanuzi

Kwenye safu ya nne andika kile ambacho kila fungu linasema juu ya kila kipawa.

Maandiko	Uchunguzi kwa Ujumla	Vipawa	Ufanuzi
Rum 12:6-8	Tuna vipawa tofauti kulingana na neema	Unabii	
	Tumia kulingana na imani	Utumishi	
1Kor 12:4-11	tofauti...sawasawa kila mtu ana angalau kipawa kimoja		

<b>Maandiko</b>	<b>Uchunguzi kwa Ujumla</b>	<b>Vipawa</b>	<b>Ufafanuzi</b>
1Kor 12:27-29			
Efe 4:11			

Sasa linganisha orodha. Kutokana na ufaahamu wako wa maandiko, tunga tafsiri inayofanya kazi kwa kila moja ya kipawa:

### **C. Matumizi**

Buni orodha ya vipawa unavyodhani unavyo. Kando ya kila kimoja, sema kwa nini unaamini kwamba Mungu anataka utumie vipawa kuhudumia kwenye mwili:

## **V. VIZUIZI KATIKA UGUNDUZI WA VIPAWA**

### **A. Sababu za mtu**

- Kuogopa baadhi ya kuonewa au kutumiwa vibaya na wengine
- Kukosa kuelewa kunakofanya kazi kwa nguvu ya asili inayofanya kazi katika ulimwengu wa mwili. Hili ni tatizo la mtazamo wa kidunia.
- Kuhifadhi tatizo la dhambi ambayo hajashughulikiwa na/kukosa imani.
- Kukosa kujitoa kuhudumu na kuhudumia wengine.
- Kujaribu kuiga wengine katika kuvitendea kazi vipawa
- Kukazana sana “kupata vipawa” badala ya kumtafuta mtoaji wa vipawa.
- kurithi tabia ya“kusubiri kipawa kabla ya kuanza kuhudumu” , badala ya kuendelea kwa utii kuhudumu na kuhudumia wengine, ukiamini kwamba Bwana atakamilisha kusudi lake kupitia kwetu. Kwa hakika, tunaweza tukawa hatufahamu kabisa matokeo ya matumizi ya vipawa vyetu tunapokuwa tunatafuta kuwapenda na kuwashudumia wenginme.

### B. Tatizo la Kichama

- Kuona aibu ya kimafundisho: Baadhi wanaondoa vingine; wengine wazidisha –msisitizo wa baadhi ya vipawa
- Kusitiza zaidi kwa baadhi ya vipawa kama “alama ya kiroho” badala ya kama huduma kwa wengine.
- Hakuna mafundisho ya kibiblia juu ya vipawa wala uhuru wa kuvitumia.
- Kuweka vipawa kama mwishio wao badala ya kama zana ya huduma.

## VI. KUHAMASISHA KANISA KULINGANA NA KUJALIWA VIPAWA

Moja ya funguo za mafanikio katika ukomavu na ukuaji katika juhudzi za upandaji kanisa ni kutafuta njia za kuwafundisha wajumbe wote kugundua, kuendeleza na kufanya mazoezi katika shughuli za huduma. Hakuna mpaka katika ukuaji wa kanisa ambalo linatoa watu kuhudumu kwa nguvu za Roho Mtakatifu, kisha na kuwazuia kwa ajili ya kushikilia nafasi katika huduma.

Mpanda kanisa siyo tu “kufanya kazi ya huduma” lakini badala yake ni kuwafundisha waumini wapya kufanya huduma.

### A. Jinsi ya Kuwasaidia Wengine Kugundua na Kutumia Vipawa Vyao

Kitu cha kwanza tunachotakiwa kufanya kuwasaidia wengine kugundua vipawa vyao ni kuwatia moyo na kuwawezesha kuhusika katika huduma. Watakapokuwa wanahudumu ndipo tutaweza kuona Mungu akiwatumia kwa ufanisi. Ni muhimu kwamba tunawafundisha wengine juu ya

- Hitaji la Vipawa
- Asili ya Vipawa
- Ugunduzi wa vipawa vyetu
- Wajibu wa kuvitumia vipawa vyetu

Kisha, kwenye huduma, tunahitaji kuchunguza matokeo ya huduma kuonyesha jinsi Bwana anavyobariki au ambavyo habariki. Kama tunaona uwepo wa kipawa, tunahitaji kumtia moyo muumini kukiendeleza na kuongeza huduma yao katika eneo hilo (1Pet 4:10). Kama hatuoni uwepo wa kipawa, tunahitaji kuwa waaminifu kuwashauri makaka na madada juu ya kujaribu eneo jingine la huduma, badala ya kuwaruhusu kuchanganyikiwa kutokana na kukosa matokeo.

Ni muhimu pia kukumbuka kwamba waumini wote, *kama sehemu ya mwili wa Kristo*, wana vipawa nya kiroho. Angalia kwenye matokeo ya juhudzi za kiuinjilisti za mwanamke msamaria (Yoh 4:28-30). Alikuwa ameamini kwa mda wa chini ya saa moja Mungu alipomtumia kuleta umati kwa Yesu. Waumini wapya wanatakiwa watiwe moyo kuhudumu na kugundua vipawa vyao.

Kuna nakala moja ya tahadhari kuhusu waumini wapya kwenye huduma. *Wanatakiwa wahudumu*. Lakini hawatakiwi wamiliki ofisi (1Tim 3:6). Kuwahudumia wengine siyo sawa na kuwaelekeza wengine. Ofisi ya uongozi inatakiwa kukomaa na kudhihirisha uaminifu. Lakini wakristo wote wanahitaji kujishghulisha kwenye kuwahudumia wengine na katika kiuinjilishi waliopotea.

### B. Mafunzo Yanasaidia Kuendeleza Vipawa

Ingawa vipawa nya kiroho ni zawadi za neema kutoka kwa Mungu, bado kuna nafasi ya mafunzo na kuendeleza matumizi yake katika shughuli za huduma. Mafunzo ni kiwango cha ujuzi wa kibinadamu, wakati utoaji wa vipawa ni kiwango cha kuwezesha kiroho. Yote yanatakiwa yaungane kwenye shughuli za huduma.

## VII. VIPAWA VYA KIROHO NA UPANDAJI KANISA

Ili kuwa na ufanisi katika huduma ya upandaji kanisa, mpanda kanisa lazima afahamu kipawa (vi) chake. Matokeo yake, anaweza kuzakania katika huduma ambayo Mungu anaibariki katika maisha yake. Kuna njia nyngi za upandaji kanisa. Watu wanawenza kuleta kwa Mungu kupitia mafundisho ya mpanda kanisa, uinjilisti, huruma, au kipawa kingine. Ni muhimu kwamba mpanda

kanisa mwenye kipawa cha uinjilisti anatumia mda wake pamoja na waliopotea kuliko mda wote kuandaa mafunzo ya Biblia. Lakini mpanda kanisa mwenye kipawa cha kufundisha anatakiwa akazanie kwenye mafundisho ya Biblia. Kama ana kipawa cha rehema, anatakiwa awe na wagonjwa na wanaoumia.

Kwa kuwa hakuna hata mmoja aliye na vipawa vyote, ni muhimu kwamba mpanda kanisa anaunda timu na wengine walio na vipawa vya kukamilisha chake. Kwa njia hii tu kutakuwa na uwiano katika huduma. Mpanda kanisa asiye na kipawa cha uinjilisti anaweza kupanda kanisa, lakini atakuta ni vigumu sana labda atafute mwana kikundi mwenzake aliye na kipawa hicho. Kipawa chochote anachopungukiwa mpanda kanisa kitakuwepo kwa wajumbe wa timu. Vinginevyo, kazi nyingi zitategemea nguvu, na juhudzi za kibinadamu.

Timu inaweza kutoa  
vipawa vya ukamilishaji.

Mpango wa Mungu ni kwamba mwili wa kanisa la mtaa kufanya kazi kwa pamoja na kila mjumbe akitumia kipawa (vi) chake. Kwa jinsi hiyo, katika kanisa jipya lillipopandwa, kunaweza kukawa na waumini wachache mwanzoni. Katika hali hii, hata ina maana zaidi kwamba vipawa vya kila muumini vigunduliwe, viendelezwe na kutumika kwa haraka na kwa ufanisi.

Yesu ametoa watu walio bora kwenye mwili kuwaandaa kila mtu kufanya sehemu yake. Kwa nyongeza, Roho Mtakatifu anawezesha kila muumini na uwezo maalumu kafanya kazi yake ya kipekee, na kwa hiyo, kuufanya mwili wote kufanya kazi. Viongozi wametolewa kwenye mwili kuandaa kila muumini kufanya huduma.

#### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Fanya mafunzo ya kufata neno kwenye sehemu ya 1V.
- Tafsiri hitaji ambalo unaamini Mungu anataka kundi lako litimize. Orodhesha nafasi za huduma ambazo Mungu ameonyesha kwenye kikundi.
- Uwe na mda wa kujitoa kwa Bwana ukimuuiliza kukuwezesha na kutoa vipawa vinavyohitajika kutimiza mahitaji mliyonayo. Usikazanie kwenye vipawa isipokuwa kwa mtoaji wa vipawa.
- Ruhusu kila mtu kuanza kutimiza mahitaji wanayojisikia kuwa tayari kuyatimiza. Tia mkazo na msisitizo kwenye kutimiza mahitaji badala ya kwenye kipawa.
- Wafundishe watu kulingana na kipawa cha huduma wanachojisikia kuwa tayari kutumia katika kutimiza mahitaji.
- Ruhusu wengine kutathimini na kushauri kwa uthibitisho wa vipawa ulivyokuwa ukitumia.



# Nguvu ya Kijamii ya Kanisa

## JINSI UTAMADUNI WETU UNAVYOATHIRI KANISA LETU

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kueleza jinsi utamaduni—yote kidini na kijamii —ambavyo vimeathiri kanisa katika historia yote. Pia itachora sambamba kati ya kanisa leo katika Ulaya ya kati/mashariki na Urusi ya zamanii na kanisa la kwanza la kitume.

### ☞ Wazo Kuu

- Kanisa litaathiriwa na utamaduni lakini lazima lisivuke mstari kwenda kwenye dhambi.
- Utamaduni unaweza kuwa na mguso bayana, si bayana, au kati kati kwenye kanisa.
- Kanisa lazima lirithi mifumo yake kwenye utamaduni unaobadilika ili kuweza kuendana.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa...

- Afahamu mguso mkubwa wa utamaduni kwenye kanisa wakati wa nyuma.
- Ashawishike kwamba mifumo ya kanisa lazima ibadilike kadiri utamaduni na mahitaji yanavyobadilika.
- Kutathimini kanisa lake kuona kama linarithi kuweza kuwapata waliopotea au kutarajia waliopotea kubadilika kuendana na kanisa.

### ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

- Katika kijiandaa kufundisha somo hili, kwa kifupi fanya marudio ya mawazo makuu ya historia ya dini katika nchi yako. Fikiria kuandaa historia fupi ya mandhalii yako
- Fikiria kutengeneza uangavu wa kielelezo 11.1, au kichore kwenye ubao. Jadili kama tamaduni tatu zilizoonyeshwa zina haki ya kutofautiana na kila moja—au ziwe sawa wakati wote kama ni za kibiblia.

## UTANGULIZI

Tamaduni mara zote zinasimama katika nafasi muhimu katika kuonyesha jinsi tunavyofikiri na kutenda. Tumeundwa na tamaduni zetu, tukizungukwa nazo, na kuathiriwa nazo. Hii mara kwa mara inatokea bila sisi kufahamu. Hata tunapokutana na mtu mwagine kutoka kwenye utamaduni mwagine, ambao ni tofauti na wetu, tunaweza tukaamua kwamba hayuko kawaida, na sisi tuko “kawaida.”

Tamaduni zinazunguka na kuathiri kanisa.

Tamaduni pia zinaathiri kanisa. Makanisa katika kila nchi yako tofauti. Baadhi ya tofauti zinatokana na mafundisho ya imani, lakini tofauti zaidi zinatokana na utamaduni. Kwa mfano, jengo la kanisa Africa litakuwa tofauti sana na la Urusi. Tabia ya nchi ni tofauti, na hivyo hata utamaduni. Muziki wa kanisa la Amerika ya Kusini utakuwa tofauti na mziki katika kanisa la Korea. Tofauti hizi zinatokana na tamaduni na siyo katika mafundisho.

Zaidi ya hayo, hakuna nchi ambayo ni kundi la utamaduni wa jinsi moja. Kila nchi ni pamoja na watu kutoka nchi zingine wenye matukio ya nyuma. Utamaduni unaweza kutofautiana mionganii mwa kundi la wenyepi kwenye nchi hiyo. Tofauti za hali ya kiuchumi, kiwango cha elimu, na umri vinaweza kusababisha mtazamo tofauti sana wa kidunia. Hata tofauti za utamaduni kati ya maeneo ya mjini na vijijini inaweza kuwa kubwa.

Baadhi ya mivuto hii ya kiutamaduni ni dhahiri. Inasaidia kanisa kujihusisha kwenye na kuwapata watu wake. Mfano wa aina hii ya mivuto inaweza kuwa matumizi ya mashairi. Kama huu ni mfumo wa sanaa zinazothaminiwa sana kwenye utamaduni inaweza kutumika kwa ufanisi katika kuonyesha ukweli wa kiroho. Miguso mingine ya kiutamaduni ni ya katikati na siyo ya maana sana; kwa kifupi inaashiria njia ambayo kanisa fulani linachagua kufanya kitu fulani. Mfano wa mivuto ya katikati ni ukusanyaji wa matoleo: yakusanywe wakati wa ibada tu, mwanzoni, katikati au mwishoni au kikapu kiachwe nyuma ya chumba ambapo watu wataweka sadaka zao? Hata hivyo, kuna miguso pia isiyo bayana ambayo inaweza kugusa maisha ya kanisa. Hii inaweza kuwa ni pamoja na ubaguzi au hali ya kupatanisha pande mbili zinazotofautiana ambazo zinamwajika kanisani kutoka kwenye utamaduni.

Tofauti za kiutamaduni zinaweza kuwa dhahiri, kinyume au za katikati.

## I. KANUNI ZA KIBIBLIA

### A. Kuweka Uwiano

Kuendana na utamaduni bila kukabili dhambi iliyoko kwenye utamaduni inaweza ikawa vigumu. Hili ni swala muhimu kwa wapanda kanisa. Anapokuwa anafanya kazi kuandaa kanisa jipya, anahitaji kufanya maamzi juu ya mifumo na miundo ipi ya kutumia. Kuna vifungu viwili nya maana juu ya swala hili kwenye Agano Jipya.

#### 1. Matendo 14:11-18

Katika fungu hili, Paulo alikuwa ndio amemponya mtu kwete katika mji wa Listra. Watu walipoona muujiza, waliendelea kutoa sadaka kwa Paulo na Sila. Nia yao ilikuwa nzuri, lakin Paulo alitambua katika utendaji wa kiutamaduni kwamba hiyo ilikuwa kinyume na maandiko.

#### 2. Wakorintho 9:19-23

Paulo waziwazi anaeleza kwamba yuko tayari kuwa kama Myahudi, Mmataifa, au mtu mwingine yeoyote ili kuweza kuwaleta kwa Kristo. Alifikiria wokovu wa waliopotea kuwa wa muhimu zaidi kuliko upendeleo wa utamaduni. Kwa jinsi hiyo, pia anaelezea kuwa kuna kikomo kwenye kiwango anachowenza kuwa kama utamaduni mwingine. Paulo wakati wote yuko chini ya sheria ya Kristo (V.21). Hawezi kukubaliana na dhambi, lakini yuko tayari kujitoa kutoa sehemu nyingine yote ya utamaduni kwa ajili ya waliopotea.

### B. Mfumo na Kazi

Wazo la mfumo na kazi vimeshajiliwa tayari kwenye masomo yaliyopita. Ni ufunguo katika kutafuta uwiano kwenye kanisa wa kukabili utamaduni. Ni muhimu kukumbuka maana ya maneno haya

#### 1. kazi—Nini Lazima Tufanye

Vitu ambavyo kanisa limeamriwa kufanya ni kazi. Kazi kuu ni pamoja na kufundisha, kuhubiri, kuinjilisha, kubatiza, kuabudu, kuomba na kutunza meza ya Bwana. Kuna kazi nyingine nyingi, kama vile kutiana moyo, kupendana, kuimba nyimbo za sifa na nyimbo za kiroho, na kumtolea Bwana na kwa wahitaji. Kanisa lazima lifanye mambo haya.

#### 2. Mfumo—Jinsi Tunavyochagua Kufanya Kazi

Mifumo ya kanisa ni njia ambazo kanisa linatumia kufanya kazi zake. Kanisa lina uhuru mkubwa katika eneno hili ili mradi tu halichagui mfumo uliokatazwa na maandiko. Kwa mfano, kanisa limeamriwa kuomba. Jinsi gani, wapi, lini, na mara ngapi kanisa linatakiwa kuomba hajaelezwa. Nafasi ambayo mtu anadhani (kusimama, kupiga magoti, kukaa n.k.) inatofautiana kutoka utamaduni hadi utamaduni. Kuna uhuru katika maamzi haya. Kama, kwa jinsi hiyo, kanisa limeamua kuomba kwa Budha, hiyo inaweza kuwa dhambi. Hatuna uhuru kiasi hicho.

Tuna uhuru wa kuchagua jinsi ya kuabudu na kuhudumu ili mradi tu hatuvuki mstari kwenye dhambi ambao umekatazwa kiuthabiti kwenye Biblia.


Kutofautisha mifumo na kazi ni hatua ya kwanza katika kuanzisha kanisa ambalo linaendana na kila kikundi cha kiutamaduni. Lazima tuelewe kuwa tuna uhuru kuchagua jinsi ya kuabudu na kuhudumu ili mradi tu hatuvuki mstari kwenye dhambi ambao

umekatazwa kiuthabiti kwenye Biblia. Mifumo inaweza na itakuwa tofauti kutoka katika kila utamaduni. Hii ni nzuri na ya kawaida ili mradi dhambi imeepukwa.

Kielelezo 11.1 kinasaidia kueleza jinsi gani upana wa uhuru wetu unaruhusu mapana katika kuabudu kwetu na maisha ya Kikristo.

Tambua katika kielelezo kwamba kuna sura tatu tofauti katikati zinazowakilisha mifumo ya kanisa inayofaa kwa tamaduni pana. Mlengo wowote katikati kwenye weupe unakubalika kwa Bwana. Kwa jinsi hiyo, tamaduni tofauti zinapendelea mifumo tofauti kwenye eneo hili linalokubalika. Utamaduni A, B na C unaweza kila mmoja kuchagua njia tofauti ya kufanya kazi zake za kibiblia. Hii ni nzuri na ya kawaida. Eneo la rangi ya kijivu linawakilisha dhambi. Kila mfumo wa kiutamaduni unalingana kisheria endapo tu hauvuki mstari wenyewe deshi kwenye eneo la dhambi ambazo Biblia inakataza.

#### Kielelezo 11.1 Upana wa Uhuru wa Utamaduni wa Kanisa na Maisha ya Kikristo



## II. KANISA LA AGANO JIPYA NA UTAMADUNI

Mvuto wa utamaduni unaonekana waziwazi kwenye masimulizi ya kanisa la Agano Jipy. Ilianza kimsingi na kikundi cha Wayahudi, na ghafla ikaenea kwa Mataifa. Hatimaye, Kanisa katika eneo la Mataifa lilizidi kwa mbali kanisa la Yerusalem kwa ukubwa na umuhimu. Na katika 70 BK, uharibifu wa Warumi wa mji wa Yerusalem kiudanganyifu ulimaliza umuhimu wa kanisa hilo.

Tunaposoma katika kitabu chote cha Matendo na nyaraka, tunaona mifumo ya kuabudu, miundo ya kanisa na taratibu zilizoanzishwa *zilipohitajika*, mara nyingi kwa matokeo ya maswala ya utamaduni. Huu ulikuwa utaratibu unaoendelea kadiri changamoto mpya na tamaduni mpya zilipokabiri kanisa linalokua.

Mifumo ya kuabudu, muundo wa kanisa na taratibu zilianoanzishwa *zilipohitajika*—Mara nyingi kwa matokeo ya maswala ya utamaduni.

### A. Kanisa la Yerusalem

Kanisa la Yerusalem lilikuwa mfano wa kushangaza wa kanisa la mtaa lilokuwa linashamili. Bado linasaidia kama mtindo wa upendo, kujali, mwili unaoshirikishana. Lilikuwa na kasoro moja kubwa. Kusanyiko ilikamilisha sehemu ya kwanza tu ya amri ya Cristo ya kushuhudiwa "Yerusalem, na Yudea yote na Samaria, na mwisho wa dunia." Ni lazima tuijwa upendo wa waumini hawa wa mmoja kwa mwagine, lakini si kukosekana kwao kwa kuhusika na ulimwengu uliobakia.

Kanisa la kwanza Yerusalem lilikuwa kiasilia ni mkusanyiko wa Wayahudi waliokuwa kwa kiasi kikubwa wameathiriwa na utamaduni wao wa Kiyahudi. Mitume kawaida walihitaji kuamua jinsi ya kuingiza mapokeo yao ya kiyahudi na mifumo ya kuabudu na imani yao mpya ya ukristo.

#### 1. Maombi kwenye Hekalu

Mitume waliendelea kukutana, kuomba na kuabudu katika hekalu la Wayahudi hata baada ya kukata shauri kwao (Mdo 2:46; 3:1). Walikuwa wameshazoea mtindo huu wa kuabudu, na walikuwa wameridhishwa kuendelea nao. Kadiri idadi ya waumini ilivyokua na kuwa maelfu, kulikuwa hakuna sehemu nyininge kubwa ya kutosha kukutania. Kulikuwa hakuna wazo la kujenga jengo "kanisa". Waumini walikuwa ndiyo kanisa. Sehemu hii ya utamaduni wa dini yao ya Kiyahudi ilikuwa inakubalika. Kwa jinsi hiyo, hawakuwa wanajihusisha katika kutoa sadaka. Walielewa kwamba Kristo, mwana kondoo wa Mungu, ameshakamilisha kazi ya kutjoaji (Ebr 7:27). Waliikataa barabara desturi, bila kujali kina chake cha mizizi kwenye utamaduni wao.

#### 2. Makanisa ya Nyumba

Kwa nyongea ya kukutana kwenye hekalu, waumini walikutana pamoja kutoka nyumba kwa nyumba (Mdo 2:46). Mtindo huu ulianza hata kabla ya pentekosti. Wanafunzi walikuwa pamoja mara nyingi wakati wakiwa wanamsubiri Roho Mtakatifu (Mdo 1:12-14), na kwa miaka mitatu mwanzoni wamekuwa pamoja kila siku na Yesu. Desturi hii kwa hiyo ilibuka siyo kutoka kwenye utamaduni wao wa Kiyahudi, lakini kutoka kwenye uzoefu wao na Kristo.

#### 3. Uinjilisti

Utamaduni wa Wayahudi ulikuwa na matokeo ya kinyume kwenye uinjilisti. Walikuwa na tatizo katika kuamini kwamba Mungu angeweza kuwaokoa Mataifa "mbwa" bila kujali kukubaliwa kwa watu wote kwa Kristo (Yoh 4). Bwana alisahihisha udhaifu huu kwa kutuma mateso ya kuwatoa nje ya Yerusalem kushuhudia ulimwenguni. Pia aliongea kwa wote Petro na Paulo kupitia maono ya kimaigizo ili kuwashawishi kwenda kwa mataifa (Mdo 9,10).

Mtazamo wa kiutamaduni wa wayahudi kwa mataifa ulikuwa na matokeo ya kinyume kwenye uinjilisti wa ulimwengu.

#### 4. Maendeleo ya Wahudumu

Ofisi za msingi za kanisa walikuwa ni mitume na manabii (Efe 2:20). Ofisi iliyo fata ilione kana kuwa hiyo ya mashemasi, ingawa haikuitwa hasa kama katika Matendo 6:1-7. Matukio ya maendeleo ya ofisi hii yalikuwa matatizo ya kiutamaduni. Ilione kana kwamba kanisa lilifanya matunzo bora kwa Wayahudi wajane "halisi" walioongea Kiyahudi kuliko walivyofanya kwa hao walioongea Kiyunani.

Uamzi huu wa mitume ilikuwa ni kusanyiko kuchagua wanaume saba wa kutunza kazi hii. Kwa kuwa wote walikuwa na majina ya Kiyunani, inaonekana kwamba kanisa lilifanya uamzi wao kulingana na utamaduni. Waliamua wajane wanaoongea Kiyunani walikuwa muhimu kama wajane walioongea Kiyahudi. Waliamua pia wanaume walioongea Kiyunani wangeweza kuhudumu vizuri kwenye kikundi cha utamaduni wake. Lakini waliwachagua katika mtindo wa hadharani ulioonyesha hawakuwa na "daraja la pili" la utamaduni katikati ya kanisa.

### B. Kanisa Miiongoni Mwa Mataifa

Pamoja na mateso ya Matendo 8:1-3, wanafunzi hatimaye walienteza injili Samaria na "sehemu za mwisho wa dunia." Wengi wa Mataifa kwa utayari waliamini ujumbe, hasa walipoona miujiza ikifanywa na mitume. Mungu pia alimchagua mitume Paulo kuhudumu kwa kundi hili hasa (Mdo 9:15). Matokeo ya huduma yake, kanisa likalipuka katika kukua bila kujali vipingamizi.

Hata makanisa katika maeneo ya Mataifa wa Asia ndogo yalikuwa na idadi ya kutosha ya Wayahudi. Njia ya Paulo ya kawaida ya kupata miji mpya ilikuwa ni kwenda kwa Wayahudi kwanza na kwa Mataifa wakati tu Wayahudi wanapokataa ujumbe wa injili. Paulo alijua kwamba Wayahudi Walikuwa wateule wa Mungu na kwamba wameshapata ufahamu wa msingi wa Mungu na Agano la Kale. Wakati mwininge alikuta mcha Mungu mwanaume na

mwanamke waliomwezesha kwa haraka kutoka kwenye kiini cha kanisa jipya. Lakini pia walikuja na yote tofauti za utamaduni wa serikali na kidini ambazo mara nydingi zilirudisha nyuma ufikiaji kwa Mataifa.

Kisa kikuu katika Agano Jipya ni jinsi ya kuunganisha waumini hawa Wayahudi kwenye mwili wa kristo. Kristo amevunja mgawanyiko na kuunda mwili mmoja mpya—kanisa—kutoka kwa wote Mataifa na Wayahudi (Efe 2:14-16). Kwa jinsi hiyo, hawakuweza kuelewana mara zote. Kawaida migogoro iliibuka wakati wakristo Wayahudi walipositisiza juu ya kupidishwa kwa tamaduni zao za kidini kwa Mataifa wakristo. Nyaraka mara zote zilikemea tabia hii.

Migogoro mara nydingi iliibuka kwenye kanisa la kwanza wakati wakristo Wayahudi walipositisiza juu ya kupidishwa kwa tamaduni zao za kidini kwa Mataifa wakristo.

### 1. Baraza la Yerusalem

Matendo 15:1-21inaandika kuhusu uamzi wa mpaka wa kiasi gani cha utamaduni wa kidini uweze kuletwa kanisani. Waumini Wayahudi walisisitiza kwamba kutahili kulikuwa lazima kwenye wokovu. Kuna uamzi wa aina mbili uliofanywa na baraza.

#### A. Kutahiriwa

Kutahiriwa kulikuwa moja ya ibada wakfu ya Kiyahudi. Kwa jinsi hiyo, baraza liliikataa. Hawakuwa tayari kuweka mzigo mwingine kwa hao waliookoka (Mdo 15:10-11, 19). Wokovu kwa neema kwa njia ya imani uliondoa hitaji la kufanya kazi yoyote ya kidini. Kitabu cha Wagalatia kimeandika kilazima kugusia swala hilo hilo. Harakati za kuwalazimisha waumini wapya kujitoa kwa mapokeo ya Kiyahudi na tamaduni za kidini zilikataliwa kiudanganyifu.

#### B. Kuliwa kwa Nyama

Wakati wakikataa hasa kutahiriwa, baraza lilitoa idhini nydingine (Mdo 15:19-21). Waliwaomba waumini Mataifa kuepukana na yafuatayo:

- Chakula kilichochafuila kwa miungu
- Zinaa ya uzinzi
- Nyama ya mnyama aliyenyonwa na damu

Mstari wa 21 unatoa sababu kwa hili. Kulikuwa na Wayahudi wasioamini katika kila mji, ambao kanisa lilipenda kuwaleta kwa Bwana. Zinaa ya uzinzi, nyama iliyotolewa sadaka kwa miungu na nyama yenye damu ndani yake kiutamaduni ilikuwa ni machukizo kwao ambayo yangezuia kuwafikia kwa ajili ya Kristo.

Zinaa ya uzinzi imezuiliwa hasa kwenye Biblia kama dhambi. Kuzuiliwa kwake kunaeleweka. Lakini vipi kula nyama yenye damu na nyama iliyotolewa sadaka? Paulo baadaye aliongeza majadiliano muhimu kwenye somo hili. Katika 1Wakorintho 6 anahuishisha kanuni zifuatazo:

- Miungu si kitu
- Chakula tunachokula hakigusi uhusiano wetu na Mungu

Analaumu pia kuchukua kutoka kwenye chakula Katika 1Timotheo 4:3-5. Waziwazi, kula chakula siyo dhambi. Hata hivyo anaamua kutokula nyama ambayo imetolewa sadaka kwa miungu ili kuepuka kuwakwaza "ndugu wadhaifu." Paulo anarejeza kwa wakristo wachanga ambaobado ni dhaifu kwenye imani zao na hawajaweza kuelewa uhuru wao mpya ndani ya Kristo. Paulo anaachilia nyama kama hiyo ili kutokuwa kikwazo kwa waumini dhaifu. Hii kwa karibu inaelekeana na hali katika Matendo 15. Tunaona kwa hiyo wanafunzi walitakiwa kutoa idhini ya makundi mawili

Waumini lazima warekebishe mifumo yao ya kidini kuwa isiyokwaza kidogo kwenye utamaduni wa wasioamini na wakristo "dhaifu".

- Wayahudi wasiookoka
- "Wakristo dhaifu"

Mafundisho muhimu ni kwamba *waumini lazima warekebishe mifumo yao ya kidini ili kuwa kidogo isiyokwaza kwenye utamaduni wa wasioamini wakristo "wadhaifu"*. Hii kisha inakuwa mandhalii kwenye maelezo ya Paulo juu ya kuwa (nimekuwa hali zote kwa watu wote" ili kuweza kuwapate (1Kor 9:19-23).

## 2. Tika Matendo

shoni kwenye mwanzo wa ajabu wa Yerusalem kufanya mabadiliko ya lazima kwenye mifumo yao ya kuabudu ambayo Misheni Huko Antioquia. Mungu kwa uweza alilitumia kanisa la Antioquia kama chanzo cha kuwatuma nje Paulo na Barnabas, na baadaye Sila, kuinjilisha ulimwengu wa Mataifa. Tunajua kidogo juu ya maisha ya ndani ya kanisa ikilinganishwa na kanisa la Yerusalem, ambalo mengi juu yake yameandikwa. Kipengele Kipywa ambacho Bwana anatuonyesha kupitia Antioquia ni ulazima wa kuchukua injili kwa watu wote . Utamaduni wa kidini wa Wayahudi waumini uliwazuia kutoamilisha kazi hii. Hawakuweza, na wasingeweza, kufanya mabadiliko ya lazima kwenye mifumo yao ya kuabudu ambayo ilikuwa muhimu kuwafikia nchi za Mataifa. Mungu aliwatenga pembeni na badala yake kutumia kanisa la Antioquia. Inavunja moyo mwishoni kwenye mwanzo wa ajabu wa kanisa la Yerusalem katika Matendo 2.

Muundo wa kansia umebadirika, umekua, na ulilainishwa ilivyotakiwa.

## 3. Maendeleo ya Ofisi za Kanisa

Kadiri kanisa lilivyoenea Asia yote, na eneo la Mediteraniani, ofisi mpya zilongezwa kwenye utamaduni wa kanisa.Tunaona wazee wa kanisa wameongezwa kwenye 1Timotheo 3:1-11 na Tito 1:5. wahudumu wanaendelea, lakini kuhitajika kwao, kama wazee wa kanisa kunatolewa kwa kina katika 1Timotheo3:1-11 na Tito 1:5-9. Katika vitabu hivi tunaona pia uwezekano wa marejeo ya uhudumu na marejeo kwenye misaada maalumu kwa wajane wa kanisa, ukimalizia kwa orodha ya uhitaji wao. Ni wazi kwamba muundo wa kanisa umebadilika, kukua na ulilainishwa kama ilivyohitajika katika mda unaobadilika na mahitaji. Na huduma ya kanisa ilirekebishwa kulingana na hitaji la utamaduni maalumu na tofauti ya kila kikundi (1Tim 1:12-14).

Huduma ya kanisa ilirekebishwa kulingana na hitaji la utamaduni maalumu na tofauti za kila kikundi.

## 4. Mateso ya Urumi

Mwanzoni mwa Matendo 8, kanisa la kwanza lilikuwa limeteswa sana na Warumi. Mateso na vifo nya wakristo wakati wa kipindi hiki yanajulikana vizuri, kwa ajili ya imani yao na upendo wao. Sehemu kubwa ya Agano Jipywa iliandikwa wakati huu, na kuitisha kubakia waaminifu ni jambo la kawaida. Kwa ujumla, waumini walibakia wakweli kwenye imani na kuwa mfano mzuri kwetu. Wakiwa wamezuiliwa kukutana hadharani, walikutana majumbani, mistuni na mapangoni. Lakini kukaza mwendo kwenye uaminifu ilikuwa vigumu. Waliendelea kuhangaika katika kuacha mifumo yao na desturi. Mateso yaliyoyokuwa makali zaidi, ilikuwa jaribu lenye nguvu kwa Wayahudi waumini kurudi kwenye imani ya Kiyahudi na usalama wa hali yake ya kiofisi. Ukweli kwamba hawakuweza kuvunja kabisa yaliyopita na mifumo yao ya zamani ya kuabudu ambayo baadaye ilikuwa kama mtego kwo. Kitabu cha Waebania wameandikiwa kundi hili kuionyesha ujinga wa ubadilishaji nguvu ya Kristo kwa mifumo hii ya zamani.

## III. KUTOKA AGANO JIPYA MPAKA SASA

Mda wa kutosha umepita kutoka Agano Jipywa mpaka kwenye kipindi chetu, na kanisa la kikristo pia limebadilika. Baadhi ya mabadiliko haya yamekuwa ya hakika na mengine yamekuwa kinyume. Mengi kati yake yameathiriwa na tamaduni badala ya mafundisho.

### A. Maendeleo ya Hali ya Kanisa

Sala za watakatifu hatimaye zilifanikiwa—hata mfalme Constantine aliamini, na ukristo ukaitwa eneo la kidini. Tendo hilo lilibadirisha picha ya kidini ya ulimwengu. Badala ya kikundi kidogo cha waumini waliojitoa wanaokutana majumbani kwa kujihatarisha kwa hali ya juu, jengo kubwa

Kadiri nguvu ya kisiasa na uonekanaji wa kanisa kuongezeka, mifumo ya kuabudu iligeuka kuongezeka umuhimu zaidi kuliko kazi zake.

sana la kanisa la eneo lilionekana likiwa na sifa zilizowavutia hata wasioamini kwenye nguvu zao, uzuri na utajili. Kulikuwa na waumini wa kweli—"masilio." Lakini kadiri nguvu ya kisasa na kuonekana kwa kanisa kuongezeka, ukiroho wake ulididimia. Mifumo ya kuabudu iligeuka kuongezeka umuhimu zaidi kuliko kazi zake.

#### B. Kugawanyika kwa Mashariki-Maghribi

Hatimaye katoliki na Othodox ziligawanyika. Swala lilikuwa mafunzo ya sehemu ("filioque") lakini pia lilikuwa limeathiriwa kwa ukubwa na tofauti za kiutamaduni kati ya Mashariki na Magharibi, na mahangaiko ya madaraka mionganoni mwa viongozi wa makundi mawili.

Kanisa la Kiprotstanti polepole lilitirithi mingi ya mifumo sawa ambayo Othodox na Katoliki walitumia.

Yote ya makanisa ya mashariki na ya magharibi yaliegemea zaidi kwenye mifumo badala ya kazi. Jinsi walivyokwenda kwenye mwendo wa kuabudu ilimaanisha zaidi kwao kuliko walichoamini. Hapo kukaibuka mifumo miwili tofauti sana ya kuabudu kikristo—mmoja Mashariki na mwagine Magharibi. Tambua kukubalika kwa mfumo wakati wajumbe walipota taarifa katika mwaka 1987 BK kwa Vlandimir, Grand Duke wa Kiev, katika imani ya Othodox:

*"Wayunani walituongoza kwenye maadilisho walipoabudu Mungu wao, na hatujui kama tulikuwa mbinguni au duniani. Kwa kuwa duniani hakuna mngh'ao kama huo au uzuri wa namna hiyo, na tumeptea hatuwezi kuielezea. Tunachoju ni kwamba Mungu anakaa pale mionganoni mwa watu, na huduma yao ni ya haki kuliko sherehe za mataifa mengine. Kwa kuwa hatuwezi kusahau uzuri. Kila mtu, baada ya kujaribu kitu kitamu, baada ya hapo hayuko tayari kukubali kilicho kichungu, na kwa hiyo hatuwezi tena kukaa zaidi pale."*

*Msingi wa mambo ya nyakati*

#### C. Mageuzi ya Protestanti

Mzizi wa mageuzi ya Protestantii ilikuwa ni haja ya wanamageuzi kusahihisha msisitizo huu usiotakiwa kwenye mifumo. Walitamani kurudi kwenye kazi za kweli za kanisa. Wanamageuzi walihubiri kwamba wokovu ni kwa imani kwa njia ya kristo—na kwa imani peke yake. Mifumo ya kanisa haikuwa muhimu kama kazi zilivyo. **Tunachoamini** ni muhimu zaidi kuliko **tunavyoabudu**. Yote makanisa ya Katoliki na Othodox walikataa mabishano haya. Vita vilipigwa juu ya swala. Nchi ziliingiliwa. Makafiri wakachinjwa. Makanisa ya eneo yalitesa makanisa mengine ya kikristo. Wapelelezi walikimbilia kudai mabara mapya yaliyogunduliwa kwa ajili ya dini ya "kweli". Kulikuwa na unyanyasaji kila mahali. Kwenye jambo la hali ya juu Urusi, Othodox walipigana na Othodox kwenye mfarakano wa waumini wa zamani wenye nia moja juu ya swala la vidole vingapi vitumike wakati mmoja anapoquivuka mwenywewe. Walikufa kwa mfumo huu hata kama wote walikubaliana kwenye mafundisho ya utatu—kazi! Katikati ya uadui huu, kanisa la Protestantii bila kujali polepole lilitirithi mingi ya mifumo sawa—majengo makubwa ya kifahari, ukuhani wa kitaalamu na mifumo isiyobadilika ya kuhudumu—ambayo Othodox na Katoliki walitumia.

Kiwango ambacho kanisa limeathiriwa na utamaduni wake na wakati uliopita kinategemeana na sehemu kubwa ya uchaguzi ambao viongozi wa kanisa wamefanya.

### IV. UTAMADUNI WA WAKATI HUO NA KANISA

Makanisa Ulaya ya Kati/Mashariki na Muungano wa Zamani wa Urusi zimehangainka leo matokeo ya utamaduni, siasa na historia ya kidini. Kila kanisa la mtaa lina kusanyiko la kipekee na maandalizi. Haiwezekani kuchora picha ambayo inahusika kwa zote. Kiwango ambacho kanisa limeathiriwa na utamaduni wake wa wakati uliopita kunategemeana na sehemu kubwa ya uchaguzi ambao viongozi wa kanisa wamefanya. Maamuzi haya yanaweza kuwa yamefanywa kiuangalifu au bila uangalifu, lakini kwa hakika yalifanywa. Baadhi yake ni thabiti. Mengine yanaweza kurudisha nyuma mfumo wa kanisa la wakati huo wa kufikia walipotea.

Kanuni mbili wazi ziliibuka kutoka kwenye mafunzo ya kanisa la Agano Jipy:

1. Mifumo ya kanisa lazima ibadilike kulingana na hitaji au mabadiliko ya utamaduni
2. Kanisa lazima liwe tayari kubadili mifumo yake ili kwamba isizuie wasioamini au wakristo dhaifu—Lakini ikiepuka dhambi.

Hata hivyo, kanuni hizi mara nyingi zinageuzwa kabisa. Badala ya kufuata mfano wazi wa Biblia, tunachukua moja au yote ya uamzi ufuatao.

### Tunakataa Kubadilika

Makanisa mengi yanakataa kubadilika. Wanaweza wakawa hawajui kabisa kiasi cha "mzigo wa kiutamaduni" waliokusanya zaidi ya miaka 2000 ya historia ya kanisa. Kama wanafahamu, wanaihararisha kama kwamba ni mapokeo ya kale. Mifumo imeletwa mahali pa kazi. Wanafata mwendo wa wakristo Wayahudi na kuegemea kwenye mapokeo yao. Matokeo yake, hawaezi kufikia na kuendana na utamaduni wao.

### B. Tunatarajia Wasioamini Kupatana na Utamaduni Wetu wa Kanisa

Hii ni ya kawaida kukubalika bila swali. Hata hivyo inapingwa kwenye maandiko. Katika Biblia waumini wanatakiwa kuwa yote kwa watu wote. Tunatakiwa kuishi maisha ambayo yanayojilinganisha na wasioamini na kurahisisha kujihusisha kwao kwetu na kusikiliza ujumbe wetu. Tunatakiwa tuwavutie kwa ajili ya mwokozi. Baadhi ya vitu kwenye utamaduni ni dhambi. Lazima vikataliwe. Lakini mara nyingi vinapingana na utamaduni wa kanisa. Hili linapokuwa ndio jambo, kanisa lazima libadilike. Hata Kristo alibadili kabisa utamaduni wake na kuwa mtu ili kuwafikia wenye dhambi—hata hivyo bila kutenda dhambi (Flp 2:7; EBr 4:15).

Katika njia sawa kanisa mara nyingi linatarajia waumini "dhaifu" kwa haraka kuacha vitu ambayo hawako tayari. Lakini upande wa kimaandiko ni kwa waumini wenye nguvu kuachilia haki zao ili kuepukana na kuwawekea kwa nguvu mzigo mzito wakristo dhaifu. Mara ngapi wajumbe wa kanisa wamefanya kama ndugu "dhaifu" na kuwataka wakristo wapya waache utamaduni wao?

Ni kweli kwamba ndugu wenye nguvu wanatakiwa wawafundishe dhaifu. Lakini hili linatendeka baada ya mda wa kutosha. Hatua ya kwanza ni kwa wenye nguvu kuachilia haki zao na kuvumilia upungufu wa ndugu wadhaifu mpaka wanapokua na kukomaa.

### UFUPISHO

Changamoto kwa kanisa leo ni kujua ni wakati gani wa kukabili dhambi kwenye utamaduni unaoizunguka na lini wakati wa kubadilika na kuendana na utamaduni ili kuwapata waliopotea. Haya lazima mara zote yawe katika uwiano. Hili ni jambo gumu kwa kanisa la Ulaya ya Kati/Mashariki na Muungano wa Urusi wa Zamani. Kuna karne za mapokeo na historia yanayolemea wakristo Wayahudi wa kanisa la kwanza. Walikuwa wamejitoa kwa Bwana. Walimoba bila kukoma. Walipendana. Lakini walikuwa na wakati mugumu kuweka pembedi historia ya Wayahudi ya miaka 2000 ili kutimiza Utume Mkuu. Ngoja tubadilike kabla ya mateso mengine kuweza kutawanya wapendwa.

Changamoto kwa kanisa leo ni kujua ni wakati gani wa kukabili dhambi kwenye utamaduni unaoizunguka na lini wakati wa kubadilika na kuendana na utamaduni ili kuwapata waliopotea.

Baadhi ya makanisa leo yatachagua kubadilika na kuwaleta waliopotea, lakini mengi hayatabadilika. Kwa sababu hii kupanda makanisa mapya hata ni muhimu zaidi, na kazi ya mpanda kanisa ni ya dharura. Nguvu ya kiutamaduni ya makanisa mapya inafanana zaidi na kanisa la Antioquia. Waumini wapya wanakuja bila utamaduni wa kidini "mzigo" wa wakristo wa zamani. Wanaweza kujilinganisha kwenye ulimwengu wao na utamaduni kirahisi. Uwezekano wao hauna kikomo. Bila mifumo migumu wako huru kuendana na ibada zao na maisha ili kuwafikia waliopotea.

Hatari ni kwamba waumini wapya wanajua kidogo juu ya utakatifu na mafundisho. Kanisa la Antioquia lilishinda kuja kwa ugumu huo kwa walimu wazuri (Mdo 13:1). Walipokuwa wakiwfundisha watu juu ya yote neema na utakatifu, Mungu aliwatumia kufikia ulimwengu wa siku hizo. Tuwe waminifu hata leo.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni nini baadhi ya dalili za kiutamaduni katika nchi yako au eneo? Vilitoka wapi? Vimetokana na historia, dini, siasa, tabia ya nchi, aina ya maisha au kitu kingine?
- Jinsi gani muumini atofautishe kati ya kitu fulani ambacho ni dhambi na kitu fulani ambacho kinapingana na utamaduni wake wa kidini?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Fanya marudio ya masomo juu ya mfumo na kazi kulingana na somo hili. Orodhesha mifumo na kazi katika kanisa lako.
- Tathimini orodha yako juu kulingana na kile unachokijua sasa kuhusu athari za kihistoria za kiutamaduni kwenye kanisa la kikristo.
- Orodhesha dalili ya matawi mengine ya kihistoria ya ukristo katika nchi yako, kama vile Othodox, Ukatoliki au Uruthelani. Kwa kupinga na kwa maombi tathimini ipi kati ya hizi zimehalarishwa na kansia lako. Zitenganishe kama thabiti au kinyume.

### **VYANZO**

Russian Primary Chronicle: Laurentian Text, Samuel H. Cross. N.p., n.d.

---

## **TABIA YA KIROHO**

---



## Sheria na Injili MAISHA KATIKA ROHO

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuweka wazi ambacho ni cha kawaida kabisa katika siku zetu: Wakristo ambaa ni watunza sheria, lakini ambaa hawakui katika kumpenda Mungu na wengine. Tutajadili mzizi wa tatizo hili; kutumainia sheria ili kuwa watakatifu bila imani inayokua kwenye injili ya Yesu Kristo. Na tutajifunza jinsi mabadiliko ya kweli yanavyozalishwa ndani yetu na kwa wengine.

### ☞ Wazo Kuu

- Kusudi la Mungu kwenye sheria ni katuonyesha hali yetu ya dhambi, utakatifu wake na hitaji letu la Kristo.
- Sheria haiwezi kutufanya watakatifu.
- Utakatifu ni swala la moyo.
- Maisha katika Roho na imani katika injili vinatufungua kutoka katika sheria.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa. . .

- Kuelewa kwamba kusudi la sheria ya Mungu ni katuonyesha hali yetu ya dhambi kinyume na utakatifu wa Mungu, na katuongoza kuona hitaji letu kwa Yesu Kristo kila siku.
- Kujadili kwamba imani inayokua katika injili inatuchukua kutoka kutunza sheria kwenda kwenye upendo wazi kwa Mungu na wengine.
- Kujifunza kumtumikia Mungu katika njia mpya ya Roho na siyo katika njia ya zamani ya muhutiasari ulioandikwa.

### ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Hili ni somo la masaa mawili, mengi ya mawazo katika somo hili yanatoka katika Warumi 7:1-13, Wagalatia 3:1-5 na 3:19-26. Katika kufanya maandalizi ya kufundisha kipindi hiki, uwe na uhakika wa kushukuru vifungu hivi.

## UTANGULIZI

Uhusiano kati ya sheria na injili ni moja ya majadiliano muhimu zaidi ya viongozi wa kanisa. Mara kadhaa katika historia yote ya kanisa, swala hili limechukua hatua ya kati katika mjadala. Mjadala wa kwanza kama huu umeandikwa katika Matendo 15 na katika nyaraka zinazofuata za Warumi na Wagalatia. Swala: kanisa lingesisitiza kushika sheria kama msingi wa njia ya kumtumikia Mungu? Kwa kifupi ilivyoelezwa jibu liilikuwa hapana! (Mdo 15:19-21). Mjadala mwininge kama huo ulikuwa katika karne ya 16 Wakati Mjerumani aliyejitenga aliyeitwa Martin Luther, katikati ya sheria iliyokuwa ya utaratibu wa kidini, aligundua tena mafundisho ya utakaso kwa imani. Luther akaendelea kuhubiri wokovu kama zawadi ya bure mbali na matendo mema na wanamageuzi Waprotestanti wakajiunga na mafundish hayo.

Kufuatia matukio yote haya, Harakati kuu za Mungu zilitokea. Katika Matendo na wakati wa mageuzi ya Waprotestanti, ufalme wa Mungu ukalipuka, watu wakaja kwa Kristo, makanisa yakapandwa, na eneo lote likabadilishwa. Kwa nini hatuoni Mungu akifanya kazi kwa njia hizi za nguvu siku hizi? Nini ni cha lazima kuonja nguvu inayobadilisha ya Yesu Kristo? Pengine sehemu ya jawabu ni ukweli kwamba tunakuwa tunatumia sheria vibaya wakati tunashindwa kutoa injili kwenye huduma zetu.

Tunakuwa tunatumia sheria vibaya wakati tunashindwa kutoa injili kwenye huduma zetu.

Katika somo hili, tutachunguza kwanza kusudi linalokusudiwa la sheria ya Mungu. Pili, tunahitaji kujadili vizuizi nya sheria na kutoweza kwake kuzalisha utakatifu ndani yetu. Na tatu, tutaona njia mpya ya kuishi, ambayo Agano Jipyä linatambulisha kwetu. Hitaji letu ni kujifunza kuishi kwa imani katika injili na katika nguvu za Roho.

## I. KUSUDI LA MUNGU KWENYE SHERIA

### A. Sheria Inatuonyesha Utakatifu wa Mungu

Mungu alitupa sheria ili kwamba pazia lililoficha utukufu wake liweze kuvutwa nyuma na hivyo tuweze kuona kile miyo yetu isicheweza kutambua, utakatifu wa Mungu wa ajabu. Hii ndiyo dhumuni la sheria yake. Haichukui mda kwa anayesoma Biblia kugundua jinsi sheria ya Mungu ilivyo nzito. Sheria ni nzito kwa sababu utakatifu wa Mungu ni mzito. Tunaliona hili katika kila kipengele cha sheria, katika maisha matakatifu inayotutia, katika roho yake isiyobadilika, na katika adhabu yake kali kwa kushindwa. Fikiria adhabu katika kushindwa kutii sheria za Mungu. Tunayaona haya katika Kutoka 21:15-17, 22:20 na Kumbukumbu la Torati 22:20-22. Ukahaba ulihitajika watu wote kupondwa mawe mpaka kufa. Kama kijana anamlaani mzazi kwa kushikwa na hasira kali, alitakiwa kuuawa. Inatisha kufikiri jinsi ambavy wengi wetu wangekuwa wamekuwa kama adhabu hizi zingekuwa zinatushusu.

Tunatakiwa kwa hiyo tuepuke sheria ya Mungu ili kwamba tusiugue kuwa wazi kwetu kwenye utakatifu wake? Siyo, siyo kabisa. Kama hatutamjua Mungu hasa katika ukweli wa utakatifu wake, tutaugua mateso mazito. Kama hili ilivyo gumu, kumjua Mungu katika utakatifu wake ni kwa lazima kwetu kuelewa hitaji letu la kweli kwa Yesu Kristo na ukombozi wake. Bila kuwa na ufahamu unoendelea-kukua wa utakatifu wa Mungu, tutatembea kwa kiburi, tutakuwa tusio na rehema katika uhusiano wetu na wengine, na tutatembea katika ujasiri binafsi na kutokuamini.

Kwa hiyo sheria ni ya lazima, kwanza kwa asiyeamini, kudhihirisha utakatifu wa ajabu wa Mungu ili kumuuongiza kwa Kristo. Sheria vilevile ni ya lazima kwa muumini, kumuuonyesha jinsi utakatifu ulivyo, vilevile kumuuonyesha wapi anafanya makosa na anahitaji kutubu. Tunaweza kusema kwamba sheria ni kueleza dhahili kwa tabia ya Mungu. Kuiga tabia yake, tunahitaji picha inayoonekana.

### B. Sheria Inatuonyesha Dhambi Zetu

Kusudi la pili la sheria ni kutuonyesha dhambi zetu. Katika Warumi 7:7 tumeambiwa jinsi sheria ilivyofanya kazi katika maisha ya mtume Paulo. Kwa amri "usitamani," Paulo alijifunza kwamba kutamani ilikuwa dhambi. Kisha Paulo anatuambia katika mstari wa 8 na 9 kwamba baada ya kujifunza hilo, amri ilifanya kazi kama kioo kinachoonyesha mda wote ambaa angetamani vitu vingine, na aliona jinsi moyo wake ulivyokuwa wa dhambi. "Kwa amri, dhambi ilizaa ndani yangu kutamani kila aina," alisema. Mwishoni, Paulo alivyoona dhambi ilivyokuwa "hai" ndani yake, alikuwa na ufahamu pia wa jinsi alivyokuwa na lawama mbele za Mungu kwa kuwa maneno ya sanamu ya agano yalivytoka nje "na alaaniwe asiyeyaweka imara maneno ya torati hii kwa kuyafanya" (Kum 27:26). Kwa sheria, alijifunza kuwa alikuwa amelaaniwa; alikuwa mtu "mfu".

Kanuni ambayo lazima tuifahamu hapa ni kwamba sheria ni kama mashine ya uchunguzi. Kama ulikisiwa kuwa na kifua kikuu, ungekwenda hospitalini na mashine ya mionzi ingechunguza kifua chako. Kama mashine ilionyesha kuwa ulikuwa na kifua kikuu, ungerudi hospitalini ili mashine ikupatie matibabu uliyohitaji kikitibü? Hapana, wakati mashine ya mionzi ni mashine bora zaidi kugundua tatizo, haiwezi kabisa kufaa kukusaidia matibabu ya kifua kikuu. Hivi ndivyo sheria inavyofanya kazi. Kusudi lake ni kutuonyesha dhambi zetu, lakini haina nguvu ya kuzalisha utakatifu wa kweli ndani yetu.

### C. Sheria Inatuonyesha Hitaji Letu la Kristo

Kama Mungu ni mtakatifu, kama sheria inavyoonyesha, na tu wenye dhambi, kama sheria inavyotuonyesha, kisha nini tufanye? Tunamuhitaji mwokozi! Kusudi la tatu la sheria ni kutuonyesha hitaji letu la Kristo.

Sheria ilikuwa imetolewa kwetu na Mungu "kutuongoza kwa Kristo" (Gal 3:24). Tunaelewa hili lina maana gani? Tunakuja kuona hitaji letu kwa Kristo tunapoona utakatifu wa Mungu, vilevile na kutokuweza kwetu kutunza mahitaji ya sheria. Baada ya kumgeukia Kristo, tunafikiri kuwa sheria inapaswa isifanye kazi jinsi hii? Sheria inapaswa iache kutunyoshea

kwa Kristo baada ya kugeuka kuwa wakristo? Hapana, sheria iko mbele yetu daima katuonyesha kwamba tunamhitaji Kristo, ambaye peke yake anakamilisha kusudio la sheria na kutufanya kustahili kuitwa watoto wa Mungu.

Fikiria maelezo yafuatayo yaliyofanywa na mchungaji mzoefu. Anaelezea: *Ni lazima nikiri kwamba kwa miaka mingi, sikuelewa jinsi ambavyo sheria itaendelea kuninyoshea mimi kwa Kristo mara nilipokuwa mkristo. Tabia hii ilikuwa wazi kwa nanma nilivyoendesha maisha yangu binafsi na huduma. Nilidhani kuwa baada ya kuachana na dhambi zangu za mwanzo, kwamba nilikuwa natunza sheria ya Mungu. Unaweza kuona kwamba nilikuwa na hitaji dogo la neema na injili kwa kuwa nilidhani nilikuwa nikitunza sheria ya Mungu. Sikuweza kuelewa kwa nini wengine hawajafikia kama nilivyofanya kutunza sheria. Nilikuwa nimechanganyikiwa, kwa sababu watu katika kanisa la kwanza nililokuwa mchungaji hawakuonekana kamwe kubadilika hasa. Lakini, kwa huzuni, nilikuwa kipofu kwa ukweli kwamba nilikuwa hata mimi sibadilili, kwa sababu nilikuwa nimeweka ujasiri wangu katika kitu fulani ambacho hakikuwa na nguvu hata kidogo kunibadilisha. Katika yote, nilikuwa nimedhani kuwa nilikuwa natunza sheria, wakati wote nilikuwa mfarisayo! Nilitunza sheria kwa kiwango fulani, lakni wakati huo huo nilikuwa mtakaji kwa nguvu.*

## II. UPUNGUFU WA SHERIA

Kama tulivyoona, sheria ina nafasi yake. Biblia waziwazi inafundisha kuwa sheria ya Mungu ni njema. Warumi 7:12 inasema, "Basi torati ni takatifu na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema." Kwa jinsi hiyo, wakati sheria yenyewe ni haki na njema, haitosherezi kuwa msingi wa kukua katika njia inayompendeza Mungu (Rum 8:3; Gal 3:21). Kama tutakavyoona, kwamba sheria siyo, wala kamwe haikukusudiwa kuwafanya watu watakatifu au kuwa msingi ambao tunajihuisha na Mungu (Gal 3:1-25). Sheria ina kazi nyingine. Haiwezi kutufanya watakatifu kwa sababu ya upungufu ufuatao.

### A. Sheria Haishughuliki na Moyo

Utakatifu kimsingi ni swala la moyo (Kum 6:4,5; Mt 22:37-38). Moyo unapobadilishwa, kila kitu kimebadilishwa. Utakatifu unaotokana na kuangalia ukali wa sheria kawaida unakua kutokana na kuelewa kusiko sahihi kwamba kukomaa kwa ukristo na utakatifu ni swala la tabia. Hili lilikuwa kosa la Mafarisayo (Mt 23:23-28). Walijaribu kupata utakatifu kwa kuangalia ukali wa sheria. Yesu hakika hakuwa amefurahishwa.

Utakatifu kimsingi ni swala la moyo. Moyo unapobadilishwa, kila kitu kimebadilishwa.

Chukua mfano wa mtawala kijana tajiri (Luk 18:18-23). Alikuwa "mtu mzuri" aliyefata sheria. Lakini kutokuwa tayari kwake kuuza mali zake kulidhihirisha moyo wake. Kwa sababu hiyo, Yesu alimkataa. Ingawa alitunza sheria, hakuwa wa kiroho wala mtu mtakatifu. Mtu mtakatifu angemtii Yesu katika hatua hiyo.

Jinsi gani tunafikiri mkristo anakua? Mara kwa mara tunakazania kwenye uhudumu kwenye orodha ya vitu vya kufanya, kama vile kusoma Biblia, kufanya matendo mema, kukutana na kanisa, kushirikisha imani yetu kwa wasioamini, na kuomba. Hivi kwa hakika ni amri na njia ya kukua kwa imani zetu. Lakini tunakosea tunapofikiri shughuli hizi zitazalisha utakatifu ndani yetu. Tunakazia uhudumu wetu wa kazi ya kufanya vitu hivi, tukifikiri kuwa kwa kifupi kufanya vitu hivi tunakuwa watakatifu. Tunakosa kushughurikia swala la miyo yetu na uhalisi wa kazi ya Kristo ndani yetu kama msingi wa kuishi kwa imani.

Kwa kukazania kwenye sheria kama kipimo cha utakatifu, tumepoteza mwelekeo wa mabadiliko ya moyo thabiti ambayo amri mpya inatakiwa kuleta kwa waumini.

Katika makanisa mengi, tunaona ulinganifu kwenye utawala, lakini kukosa haja ya utakatifu katika maeneo yaliyobaki katika maisha. Wakati mwingine kuna utunzaji thabiti wa taratibu, lakini ukosefu wa upendo kwa wengine. Kwa nje, Kunaweza kukawa na ukuaji wa kuthibitisha kwenye mifumo ya "utakatifu." Lakini kwa undani kunaweza kukawa na tabia ya ajabu na ukosefu wa rehema. Huku siyo "kufanana na Kristo." Kinachozalishwa mara kwa mara katika maisha yetu ni "utii" bila upendo, na "kazi za kitakatifu" bila imani.

Mkazo wa Agano Jipywa ni mabadiliko ya awali ya kutoka ndani (Rum 12:2; 2Kor 5:17). Kwa kusisistiza sheria kama kipimo cha utakatifu, tumepoteza mwelekeo wa mabadiliko ya moyo thabiti ambayo amri mpya inatakiwa kuleta kwa waumini. Bado tunapoangalia kwenye kanisa

leo, hatuoni mabadiliko haya. Wakristo wengi ulimwenguni hawana moyo kwa Mungu. Moja ya sababu ya msingi kwa hili ni kwamba tumegeukia kutumainia sheria kama msingi wa maisha na huduma, na matokeo yake, kanisa linachangia udhaifu wa Waisraeli wa Agano la Kale (Rum 9:31-32).

#### B. Sheria Inazaa Hatia

Kama unakubali sheria kama njia ya msingi wa kuhusiana na Mungu, kisha kutokana na hiyo inakuja "laana." "Laana" ni kwamba sheria "ni yote au hakuna kitu." Kama unakwenda kuishi kulingana na sheria, kisha unatakiwa utii YAKE YOTE—MDA WAKE WOTE (Gal 3:10). Lakini hakuna hata mmoja anayeweza kutunza sheria. kwa sababu kama utakatifu wa Mungu ulivyo zaidi ya kipimo, sheria zake ni zaidi tunavyoweza kutunza. Mkazo wa siku zote kwenye sheria kisha unazalisha hali ya kujisikia hatia, kwa sababu huwezi kamwe kuzitunza sheria vizuri vya kutosha. Badala ya kusonga mbele, unahukumiwa na sheria. Inakumalizia furaha, nguvu za Roho, na kurithiwa kwako na Baba wa mbinguni.

Wakati viongozi wa kanisa wanapokazania kuhitaji sheria bila rehema, wanawalemeza watu kwa matakwa ambayo hakuna mtu anayeweza kuyatunza. Badala ya kuwaelekeza watu kwenye jibu linalopatikana katika injili, viongozi hawa, kama Mafarisayo, mara kwa mara wanaunda sheria mpya kuwasaidia watu waweze kutunza sheria za Mungu. Kwa kufanya hivi, kwa kifupi wanachukua sehemu kubwa ya fungu la mzigo, mzigo ambaeo hakuna mtu anayeweza kuubeba.

Katika kitabu cha Dostoyevsk Ujambazi na Adhabu, Dostoyevsky anaelezea upeo wakati mhusika mkuu, Raskulnikov, alikuwa akiendesha gari kuelekea chini kwenye barabara ya kijijini. Safarini mwake, Ruskulnikov alimkuta dereva mwengine njiani ambaye gari lake kubwa la mizigo lilikuwa limekwama kwenye matope. Dreva alianza kumpiga mjeledi punda wake, kujaribu kumulazimisha kuvuta wagon (gari kubwa) kutoka kwenye matope. Punda hakuweza kwa sababu amechoka kwa kujaribu. Lakini dereva alienedelea kumpiga punda, akidhani kuwa mjeledi utampa kichocheo kuvuta wagon nje. Dereva aliishia kumpiga punda mpaka kumuua.

Kwa sababu kama utakatifu wa Mungu ulivyo zaidi ya kipimo, sheria zake ni zaidi tunavyoweza kutunza.

Hivi ndivyo tunavyofanya juma baada ya juma, tunapowaambia watu juu ya matakwa ya sheria bila kuyalinganisha na injili kwa njia ambayo imani katika injili inatupatia uhuru, furaha, na nguvu katika huduma yetu kwa Mungu. Kwa kutumia hatia kama kivutio, tunazalisha "utii" bila upendo, na "shughuli za kitakatifu" bila imani.

#### C. Sheria Inazaa Kiburi

Kuna wengine wanafanya vizuri zaidi kuliko wengine katika kutunza sheria. Watu hawa huwa ni wale wenye tabia nzuri ya kiutawala na kujiheshimu. Mara kwa mara, watu hawa wanatukuzwa kama mtindo wa maisha ya kikristo, siyo kwa sababu ya miyo yao ya upendo lakini kwa sababu ya utii wao wa nje wa taratibu.

Pengine wewe ni mmojawapo wa wale wanaofanya vizuri kuliko kawaida. Unajisikia wakiroho zaidi kwa sababu ya kufanya bidii ya kutunza sheria? Kama unafanya hivyo, ufahamu. Kutunza-sheria na matendo mema, hasa kama matokeo ya kazi ya bidii na utii, mara kwa mara inapelekea matokeo yanayochukiza; majigambo na kiburi (Efe 2:8-9, Flp 3:4ff). Mtu anayetunza sheria kwa juhudi zake mwenyewe kawaida anakuwa na hali ya kiburi juu ya aliyokamilisha (Rum 2:23). Kiburi ni tabia ya mwisho ambayo mtu wa Mungu anatakiwa awe nayo (Flp 2:1-11; Rum 12:3).

Kama Ibrahimu alikuwa na haki kwa Mungu kwa sababu ya kazi zake, kisha alikuwa na kitu cha kujivunia (Rum 4:2). Lakini ilivyotokea, alihesabiwa haki kwa imani na kwa hiyo hakuwa na kitu cha kujivunia. Kinyume chake hakufanya chochote isipokuwa kumwitikia Mungu kwa moyo wa shukurani kwa wema wa Mungu kwake. Kwa njia sawa, mtu wa kiroho hana kiburi juu ya msimamo wake wa kiroho kana kwamba amefika pale kwa juhudi za kazi zake. Badala yake tunajivuna kwa kile Mungu alichotufanya kwa ajili yetu (1Kor 1:29-31; Gal 6:14).


### III. KUISHI KWA SHERIA

Kuishi kulingana na sheria—kiuhalali—kunaweza kuelezewa kama kuishi kwa mtu kana kwamba lazima atii baadhi ya taratibu na utaratibu kupata upendeleo na zawadi kutoka kwa Mungu. Kufata sheria ni muhimu. Kwa hakika mtu mtakatifu au anayetunza na kuheshimu sheria. Lakini kutunza sheria kiuhalali, ili kupata malipo au upendeleo fulani, ni swala jingine.

Hata hivyo, watu wengi wanaelewa vibaya nafasi ya sheria ya Mungu na kiuhalali kuihusisha kwa Mungu. Hili linaonekana katika makanisa ambako kuna mkazo wa kila mara wa kutaka sheria kwa sababu ya kuenea kote kusikia kuwa sheria inatufanya kuwa watakatifu. Kanuni mpya zimeundwa kutuweka kwenye mstari. Vipindi na mazingaombwe vinaandaliwa kutunza baadhi ya muonekano wa utakatifu wa nje. Yote haya yanafanyika kwa matumaini kwamba kwa kutunza sheria hizi na maagizo kutaleta kuachiwa upya chini ya utawala na kuunda utakatifu.

Maisha kufuatana na sheria yanaweza kuelezewa kwa mchoro hapo chini (kielelezo 8.1). Kama maisha yetu yameegemea kwenye sheria kisha, tunapofahamu dhambi katika maisha yetu, tunaitikia kwa upinzani. Tunalaumu wengine au kuikana dhambi. Hii itapelekeea kwenye kiburi au huzuni, kutegemeana na jinsi tunavyochukulia kushughulikia dhambi yetu. Kama tunaishambulia dhambi yetu kwa juhudu zetu—kisha matokeo yake kawaida ni kiburi. Kama dhambi inatushambulia, kisha tunakata tamaa. Lakini katika hali iwayo yote, hakuna furaha. (Tazama swali la Paulo kwa Wagatalia, “*Nini kimetokea kwenye furaha yako?*” (Gal 4:15). Kwa nje, tunapojuhusisha kwenye huduma kwa wengine, kama imehamasishwa kwa sheria kisha juhudu zetu ziko kwenye mstari. Matokeo yake kwa Mara nyingine ni kiburi katika mafanikio ya huduma au kukata tamaa kwa sababu ya kushindwa.

Kielelezo 8.1 Kuishi kwa Sheria—Kama Yatima



### IV. ROHO ANATUWEKA HURU KUTOKA KWENYE SHERIA

Kazi ya Kristo msalabani ilibadili kila kitu kati ya mbinguni na duniani. Kwa kifo chake na ufufuko, Ameishinda sheria na kutupa Makao ya Roho Mtakatifu, kitu chenye nguvu zaidi zaidi sana ya kuishi.

Katika Mathayo 5:17 Yesu, akiwa ameshitakiwa kwa kutoonyesha heshima kwenye sheria ya Agano la Kale, inafanya muonekano ufuatao: “*Msifikiri nalikuja kutangua sheria au unabii; sikuja kuvitangua isipokuwa kuvitimiza.*” Baadhi wanaweza kutumia mstari huu kupendekeza kwamba sheria za Agano la Kale bado zinalazimika kama zilivyokuwa nyakati za Agano la Kale. Kwa jinsi hiyo, neno la Kiyunani kuonyesha “timiza” ni neno “*Plerao*”, likiwa na maana “*kutimiza*” kama kwenye “*kukamilisha*.”

Tambua matumizi ya “*Plerao*” katika vifungu vifuatavyo

- “Alipokuwa amemaliza (*Plerao*) mazungumzo...” (Luk 7:1)

- Baada ya haya yote kulikuwa kumetokea (Plerao)..." (Mdo 19:21)
- Wakati miaka miwili ilipokuwa imepita (Plerao) ..." (Mdo 24:27)

Kwa maneno mengine Mathayo 5:17 inaweza ikatafsiriwa kiurahisi "*Msifikiri nimekuja kuvunja sheria na unabii; sikuja kuivunja lakini kuileta kwenye ukamilifu.*" Hakika, kufikisha mwisho wa sheria ndicho Yesu alichofanya kabisa kabisa, kama vifungu vingine kadhaa vya Agano Jipyaa vinavyoonyesha.

- "Bali sasa, kwa kufia kile kilichotufunga mara, tumetolewa kutoka katika sheria ili kwamba tuweze kutumika katika njia mpya ya Roho, si katika hali ya zamani ya andiko" (Rum 7:6)
- "Kristo alitukomboa kutoka kwenye laana ya sheria kwa kufanyika laana kwa ajili yetu..." (Gal 3:13a)
- "Hivyo sheria imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani. Kwa kuwa sasa imani imekuja, hatuko tena chini ya sheria" (Gal 3:24-24)

Kama mistari hii inavyoonyesha, Kristo ameishinda sheria, kututoa kwenye hukumu yake. Ametimiliza sheria kwa utii wake kamili. Kwa kuwa tumeweka imani zetu ndani ya Kristo, sheria haituhukumu tena! Hatuko chini ya laana yake tena tunaposhindwa kuitii kama tunavyotakiwa. Tuna msamaha wa Kristo uliokamilika na haki kamili, na imani yetu ndani yake inatimiza hitaji la sheria kwetu.

## V. MAISHA KATIKA ROHO NA IMANI KATIKA INJILI

Kama sheria siyo msingi wetu wa kuhusiana na Mungu, ni nini? Na sasa kwamba Kristo ametuweka huru kutoka kwenye sheria, jinsi gani tunakua katika utakatifu? Kama sheria haina nguvu tulizodhani, nini kitawafanya watu kutokuishi kama wasioamini? Wakristo wengi wameishi kwa mda mrefu kwenye mwili na chini ya sheria na kwamba ni vigumu kwao kuweza njia nyininge yoyote ya kukua. Kwa jinsi hiyo, kuna njia mpya ya kuishi maisha ya ukristo wetu na lazima tujifunze kuishi katika njia hii mpya ili kuijua nguvu ya kweli ya kutii na kutumikia katika kuendeleza ufalme.

Badala ya uhalarishaji, Agano Jipyaa linafundisha kwamba Mungu anashughurika nasi kwa neema yake. Kuelewa hili linavyoweza kuwa, tunahitaji kurudia kutazama ulinganifu wa kawaida wa kibiblia ambapo Mungu ni Baba na sisi ni watoto wake. Mtoto ye yote aliye na wazazi wenye upendo anaweza akajihusisha kwenye wazo la neema. Mtoto anayependwa hatumikii njia zake za upendeleo kwa wazazi; anapendwa kwa sababu yupo. Wakati mtoto anapoacha kutii au kuwakatisha tamaa wazazi, anaweza akaadhibiwa, lakini hahitaji kufanya kazi upendeleo tena kwa wazazi wake (kama mwana mpotevu). Haijalishi nini anafanya, anaendelea kuwa mtoto na wakati wote anapendwa bila mashariti.

Kama watoto wa Mungu, tunaweza tukajihusisha kwa Baba yetu **kwa njia yenye nguvu ya injili ya ukombozi, kwa Roho Mtakatifu anayefanya makao**. Haya tuliyapokea tuliporithiwa kama watoto wake (Efe 1:13; Gal 4:6; Rum8:14). Maisha katika Roho na imani katika injili vinapaswa kubadili utu wetu wa maisha ya kiroho vilevile na huduma kwa wengine.

### A. Ukuaji wa Binafsi wa Kiroho katika Roho

#### 1. *Roho anatoa njia mpya ya kutii na kukua katika utakatifu binafsi.*

Tunahitaji kutii, lakini sasa? Swali kama hili alikuwa ameulizwa Yesu: "Ni nini lazima tufanye kuzifanya kazi zile ambazo Mungu anazihitaji?" Jibu la Yesu lilikuwa rahisi: "amini katika yeye aliyenituma" (Yoh 6:28-29). Imani zetu ni za maana katika ukuaji wetu katika utakatifi.

### Jedwali 8.2 Njia Mpya Dhidi ya Njia ya Zamani

<u>Njia Mpya ya Roho</u> <b>Kuhudumu ‘kwa imani katika Injili’</b>	<u>Njia ya Zamani ya Muhitasari Uliaoandikwa</u> <b>Kuhudumu ‘chini ya Sheria’</b>
Kutokana na upendo kwa Mungu kwa mtazamo wa kile Kristo alichonifanyia.	Kutokana na hofu, kujaribu kumtii Mungu vyakutosha ili kukubalika.
Kwa ufahamu wa udhaifu wangu mwenyewe; Ninaweka ujasiri wangu ndani ya Roho Mtakatifu	Kutokana na ujasiri-wa binafsi, juhudzi zangu mwenyewe
Kutoka moyoni mwangu	Kutoka katika utii wa kitumwa
Kutokana na uhuru kutoka kwenye hukumu na kushindwa	Kutokana na matakwa ya kufanikiwa au kuhukumiwa
Kutokana na shukurani ya neema ya Mungu	Kutokana na shukurani ya kujisikia kwa sababu “natunza sheria”

Mtume Paulo anatawanya mwanga zaidi wa njia hii mpya ya kukua katika utakatifu. Katika Warumi 7:1-13 anaelezea kuhudumu “katika njia mpya ya Roho, na siyo katika njia ya zamani ya muhitasari ulioandikwa” (Rum 7:6). Ni nini tofauti kati ya aina hii ya kuishi? Ngoja tuzitazame zikitofautishwa:


Katika Warumi 8:1-4, tunaona kwa mara nyingine tena tofauti kati ya sheria na Roho, na tumeambiwa waziwazi vipingamizi vyakutosha. “Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyo dhaifu, kwa sababu ya mwili, Mungu kwa kumtuma mwanaw...” (Rum 8:3). Sheria haikuweza kuzalisha utakatifu ndani yetu kwa sababu mwili wetu ni dhaifu kuzalisha utakatifu ndani yetu.

Na sasa tunaishi kama wajasiri katika Roho. Sehemu iliyobaki ya Warumi 8 kwa ukamilifu zaidi inaelezea hili. Kwa sababu tumepewa haki na Roho, hatuogopeshwi na hatuko peke yetu kama yatima au watumwa (V.15-17). Kwa sababu ya uhakika wa upendo wa Mungu, hakuna kilicho cha kufisha tena. Roho anatusaidia tunapojuwa dhaifu, na kutuongoza kila siku. Tuna ujasiri wa kuangalia maisha kama tukio, badala ya kazi ya mda mrefu ya kutunza sheria. Tunahama kutoka tukio moja hadi jingine; Kristo ni mfalme mshindi na Roho anatusaidia tunapoendelea. Wakati mwingine Roho atatuongoza katika nafasi za huduma, na kutakuwa na wakati Roho atatuonyesha dhambi zetu. Lakini katika njia hii mpya ya kufikiria, hakuna kinachotisha kwamba hatuwezi kumtumaini Roho kutuongoza katika hilo.

Ni kwa imani katika injili tunapokea Roho, anayetuwezesha kutumika katika njia hii mpya. Fikiria maneno ya Paulo kwa Wagalatia: “Umpokea Roho kwa kutunza sheria, au kwa kuamini ulichosikia? Mungu anakupatia Roho wake na kufanya miujiza mionganii mwenu kwa sababu mnaangalia sheria, au kwa sababu mnaamini mluchosikia?” (Gal 3:2-3; 5).

Mchoro wa kielelezo 8.3 unaelezea maisha katika Roho, Tunapofahamu dhambi katika maisha yetu, kama tumehamasishwa na Roho, tunatubu na kuamini katika msamaha wa Mungu. Hii kwa hakika inapelekea kwenye furaha. Kwa nje tunaitikia kwenye hitaji la huduma kwa kujitoa wenyewe na furaha ndiyo itakuwa matokeo.

### Kielelezo 8.3 Maisha Ndani ya Roho—Kama Mwana



#### 2. *Roho Anatuonyesha Dhambi Yetu*

Tuanapoju, sheria inatuonyesha dhambi yetu, na hivyo hata Roho (Yoh 16:8).

Kama ilivyoelezewa na mduara, kama tunaitikia kwenye kazi ya Roho kama mtoto na kuimiliki, kuitubia, na kuendelea mbele, kisha tunahama kutoka katika toba ya nafsi kwenye furaha iliyobadilishwa. Alama ya toba ya kweli ni kutokuendelea kuhuzuniya lakini furaha iliyorejezwa kwa neema ya Mungu na ukuu wa Kristo ambaye damu yake inatusafisha na kutuweka safi. Kazi ya Roho ni kuendelea kuturudisha kwenye injili.

Tunajuaje kama tunatembea katika Roho? Njia moja ya kujuu ni kutambua jinsi tunavyoitikia kwenye dhambi zetu. Tunaweka sheria na kujitahidi kwa bidii kutumia miili yetu? Kama ni hivyo, tunaishi kulingana na sheria. Tunatibu kwa kuungama udhaifu wetu vilevile na nguvu ya Mungu kutubadilisha?

#### B. *Roho Anatuongoza Kwenye Huduma*

Kama tunatembea katika Roho, kisha maisha ni matukio; ni nafasi ya kufisha ubinafsi na kuchukua kile Roho alichonacho kwa ajili yetu. Mwisho wake, tutakuwa pia na furaha. Kwa jinsi hiyo, kama tunaiishi chini ya sheria na katika mwili, kisha tutaona kuwa nafasi za huduma ni za chini kuliko kujifurahisha. Zinajazwa na hofu ya kushindwa. Na tunapoitikia kwenye nafasi hizi, zinatuacha na kiburi au huzuni, kutegemeana na matokea ya nafasi za huduma yalivyokuwa.

Roho anatupa njia mpya ya kufanya huduma. Kuhudumu kwa imani kunagusa kukua kwetu binafsi katika utakatifu, vilevile na jinsi tunavyowahudumua watu. Jinsi gani tunatafuta kubadilika kwa wengine? Jinsi gani tufanye ili wengine wakue katika utakatifu? Mchungaji Johnny Long, Mmishenari huko Kenya, anaandika jinsi mara nydingi tunavyofanya hili:

*"Sheria inatwaa mahali pa injili katika majumba yetu na tunabakiwa na njia moja tu ya kujibadilisha wenyewe na wengine—kwa kufanya na kulazimisha sheria! Badala ya kumtumainia Roho Mtakatifu, tunatumainia kwenye hatia, majukumu, na uchanga wa kujiamini kufanya mambo kutokea. Kujitegemea wenyewe hasa kunapoza na kusikitisha Roho Mtakatifu na hivyo mambo kuwa mabaya zaidi, na siyo mazuri! Katika, "dunia hii mpya yenye uelevu" mahali ambapo sheria ni mfalme, nimekuja kuamini kuwa sheria yangu, mafundisho yangu, kulazimisha kwangu kwa sheria za Mungu kutaunda vibaya watu wasio kamili ninaolazimika kuishi nao. Ninataka waundike ili wakubalike kwangu na kwa Mungu (katika utaratibu huo). "Kutoka katika Uwana Mwongozo wa Africa, somo—"Sheria Dhidi ya Injili Majumbani na Mahusiano ya Familia" na John Wade Long, Jr.)*

Tunapotafuta mabadiliko (kwa uzuri) katika maisha ya hao tunaowahudumia, kuna maswali matatu muhimu tunayotakiwa kuijuliza wenyewe:

1. *Ni nini LENGO la Huduma Kwa Wengine?*

Ni katika NINI natumaini kuwaona wamebadilika? Kutumia sheria tu katika kuhudumu kwa wengine kunaweza kupelekeea katika uthibitisho wa nje kama kulivyopingwa na utii wa kujisikia moyoni. Chukua, kwa mfano wa mvula mdogo ambaye mama yake alimtaka akae chini kwenye kitu kwa sababu amekosa kutii, na alitaka kumpa baadhi ya ushauri wa malezi. "Mtoto, kaa chini!" aliamuru. Mtoto aliendelea kusimama. "Kaa chini" alisisitiza. Alibakia akiwa amesimama. "Vlandimir, kama hukai chini, nitachukua fimbo na kukutandike!" mwishoni alitishika. Vlandimir alikaa chini, lakini akiwa amemkazia macho mama yake, alisema, "ninaweza nikawa nimekaa chini nje, lakini nikawa nimesimama ndani." Ingawa matendo yake yalikuwa sawa lakini moyo wake ulikuwa bado hauko sawa.

2. *Ni MTINDO GANI WA HUDUMA Nitatumia Kulifiki Lengo hili?*

JINSI GANI ninafikiri mabadiliko haya yatatokea? Mungu hakuunda sheria kubadili moyo wa mtu. Badala yake, ni mfundishaji wa kumvuta katika kujitahidi kusiko na nguvu kwenda kwa Yesu Kristo anayeweza kumbadilisha anapotembea katika Roho kwa kuamini injili. Mwili wetu unakataa wazo la udhaifu wetu na injili pekee inaweza kubadilisha watu, kwa hiyo tunajaribu kubadili tabia kwa kuunda na kulazimisha sheria, na kutoa adhabu. Hatari kuu hapa ni kwamba zoezi hili la sheria linaweza kubadili tabia za watu, lakini tena, moyoni umebadilika kidogo.

3. *Ni kwa jinsi gani mwenyewe NIONYESHE Mabadiliko ninayotafuta*

Ni wajibu upi kubadilika kwa utu WANGU uliko nako katika kuhamasisha wengine kubadilika? Aina ya uongozi tunaofanya kwa wengine katika upandaji wetu kanisa utasema zaidi juu ya kukomaa kwetu kiroho kuliko chochote tunachofundisha. Ni watumishi tunaongoza kwa mfano wetu, ili kwamba watu waseme "Hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa," au tunajaribu kuwalazimisha watu kubadilika tunapowawekea mahitaji? (1Pet 5:3).

Mfano wetu kwenye huduma ni njia ambayo Mungu Baba yetu anatuhudumia, kwa neema. Hivyo huduma yetu inatakiwa iwe na tabia ya neema. Kama maisha yetu na huduma haviendi kuvuka sheria kukazia juu ya nguvu inayokomboya ya injili, kwa Roho Mtakatifu anayefanya makao, kisha tutakuwa vibao vya alama visiviyotumika. Wakati tunaweza tukawa tunawanyoshea watu katika mwelekeo wanaotakiwa kwenda, tutashindwa kuwaongoza kwenye chanzo cha maana ambacho kinawawezesha kuifanya safari.

## SULUHU

Je unaona mabadiliko ya kipeo kati ya sheria na injili? Je unaona tofauti kati ya kutumika kwa "njia mpya ya Roho, na siyo katika njia ya zamani ya miutasari iliyoandikwa?" Hakika, Sheria ya Mungu ina nafasi yake. Inatusaidia kuelewa utakatifu wa Mungu, kuona hali yetu ya kweli ya dhambi. Lakini sheria pia ilitolewa kuntuongoza kwa Yesu Kristo. Hili haliishii tunapokuwa wakristo lakini ni kazi inayoendelea ya sheria katika maisha ya waumini. Ni mpaka tu macho yetu yanapogeuka kwa Yesu, kwa imani, kwamba tunakua kuujua upendo unaotukamilisha kutembea katika upya wa Roho.

Kama kamwe tutaona harakati za upandaji kanisa, injili, na siyo sheria, lazima iwe na sehemu yake sawa kwenye kitovu.

Kama kamwe tutaona harakati za upandaji kanisa, injili, na siyo sheria, lazima iwe na sehemu yake sawa kwenye kitovu. "Kwa kuwa waraka unaua, lakini Roho anatoa uzima." Mungu atupe macho ya kuona ukweli wetu wa kuhitaji injili ya Yesu Kristo na moyo wa kuamini kwamba mahitaji yetu yote yanatimizwa ndani yake.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Mahubiri yako na ushauri wako kwa wengine mara nydingi vinakazia kwenye sheria, kwa sababu unadhani kuwa inawezesha watu kubadilika?
- Ni nini kusudi la sheria na injili katika maisha ya mkristo?
- Kwa nini sheria haina nguvu kuzalisha utakatifu ndani yetu?

- Ni kwa jinsi gani imani katika injili inatuwezesha kuishi katika upya wa Roho?
- Ni nini maana ya kuhalalisha? Unadhani kuwa ni kukataa nguvu ya injili na kuweka matumaini kwenye sheria? Kwa nini na kwa nini siyo?
- Ina maana gani tunakuwa “hatuko chini ya sheria” katika Wagalatia 5:18, ingawa bado tunaitiwa kutii sheria za Mungu?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Fanya marudio ya mchoro 8.2, “Njia Mpya Dhidi ya Njia za Zamani.” Kwa maombi na kwa uaminifu tathimini utii wako mwenyewe kwa Mungu. Matendo yako yanaonyesha kwamba unatumika kwa imani kwenye injili au unatumika chini ya sheria?
- Kwenye karatasi tofauti, jibu maswali yafuatayo:
  1. Ni nini lengo la huduma yangu kwa wengine?
  2. Ni mtindo gani wa huduma nitatumia kukamilisha lengo hili
  3. Ni kwa jinsi gani niwe kielelezo mwenyewe cha mabadiliko ninayotaka kwa wengine? Ni mabadiliko gani ninatakiwa kufanya katika maisha yangu mwenyewe na huduma?

### **VYANZO**

Long, John Wade, Jr. “Lesson 14:Law vs. The Gospel in Family Relationships,” in *Sonship for Africa, Version 1*. Olerand, PA: World Harvest Mission, 1999.



# Toba Kama Njia ya Maisha

- ☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wafunzwa kuelewa jinsi maisha yaliyoelekezwa kwenye injili yanavyotupeleka kwenye aina ya maisha ya toba na imani. Injili inatakiwa ianzishe imani miyoni mwetu ili kwamba tuwe waaminifu kweli kuhusu dhambi zetu, kuweza kuzitoa katika toba mbele za Mungu na kuona furaha ya neema kuu ya Mungun na rehema.
- ☞ **Wazo Kuu**
  - Toba ya kweli ni pamoja na kuwa waaminifu juu ya dhambi zetu badala ya kutoa udhuru juu yake au kuzikataa.
  - Toba ya kweli haina kujionyesha kwa kuwa kujionyesha kunaonyesha ukosefu wa kutumaini katika msamaha wa Mungu.
  - Muumini mtii fu na munyenyekevu anapaswa kutubu chochote Roho Mtakatifu anachodhirisha kuwa dhambi.
- ☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoelewaka, kila mshiriki anatakiwa ...

  - Kuelewa kwamba maisha yanayoelekezwa kwenye neema ya Mungu yanatakiwa yakuongoze kwenye kushughulikia dhambi kwa uaminifu na mwenye furaha, kuendelea, na kujitoa kikamili kwa Bwana..
  - Kukua kuwa na aina ya maisha ambayo yanakua katika ufahamu wa Mungu, kutubu kwa undani juu ya dhambi, na kugundua utajili wa neema ya Mungu inayopatikana katika Yesu Kristo.
  - Uwe mmoja wa wakongwe wa kutubu katika kusanyiko lako na muhudumu wa neema kama mwenyewe ulivyoiona neema kuu ya Mungu.
- ☞ **Ziada**

10A "Sehemu ya Wenye Dhambi" na Stanley Voke
- ☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Tumia mifano ya binafsi na masimulizi kuonyesha jinsi toba ilivyogusa na kuzamisha Maisha yako ya kiroho na jinsi Mungu anavyowaheshimu hao wanaotubu.

## UTANGULIZI

Tumekuwa tukijifunza kurithiwa kwetu na Mungu na jinsi hii inavyoweza kugusa kufikiri kwetu na utendaji kama wana badala ya yatima. Kurithiwa kwetu, ambako kumetuleta katika uhusiano mpya na Mungu, kunatakiwa tena katuongoza kukazia kwenye injili na siyo tu sheria. Kutokana na hili tunajifunza siyo tu tunachotakiwa kufanya kama wakristo, lakini pia tunaona kutiwa hamasa na nguvu ya kukua katika utakatifu wa kweli. Pia tumezungumzia maisha ndani ya Roho na jinsi hii inavyozalisha utakatifu mkubwa sana kuliko tukifungia maisha yetu kwenye sheria, kwa sababu Roho anabadilisha mioyo yetu na siyo tu tabia yetu.

Mabadiliko ya moyo yanatakiwa kwanza kuvunja moyo wa zamani. Hii inatokea katika kutubu ndipo tunapoona wokovu. Na tunachogundua ni kwamba Mungu anaendeleza kazi hii katika utakaso wetu kwa kuvunja moyo yetu ili kuifanya upya. Kama Mithali 6:23 inavyosema, "Na maonyo ya kumwadilisha mtu ni njia ya uzima." Hapa tunagundua njia ya Mungu ya kuhakikisha maisha, ambayo inarekebisha njia ya moyo, kwa kuiitikia kiutu. Hii siyo njia tu inayotutambulisha kwenye maisha ya Mungu anayotupatia katika Kristo, lakini ni njia ya maisha inayotuongozza kwa kuendelea kwenye neema ya Mungu ambayo tena na tena inayofanya upya mioyo yetu.

Ni njia hii ya maisha ambayo sasa tunaifikiria. Kama tungeweza kukamata wazo la kati la somo hili, tunaweza kusema, "Toba ni njia ya maisha."

## I. TABIA ZA TOBA YA KWELI

Sasa kwetu kupata picha ya toba ya kweli ni nini na matunda inayozalisha katika maisha yetu, nenda kwenye Zaburi 51. Hapa tunaona moja ya maelezo ya kukolea ya toba halisi. Hii ni zaburi ya maungamo ya Daudi, kwa moyo wake uliovunjika juu ya dhambi zake. Kutoka katika zaburi hii tunafundishwa dalili za toba ya kweli, sababu kwa nini toba lazima iwe njia ya maisha, na pia baraka za maisha haya ya toba.

### A. Kiri Dhambi Zako

Dalili ya kwanza ya toba ni kukiri kwa unyenyekevu kwa dhambi zako. Daudi anaungama dhambi zake katika mstari wa 3, "Maana nimejua mimi makosa yangu, na dhambi yangu i mbele yangu daima." Moja ya ugonjwa mkuu wa dhambi ni kwamba inafunga na kudanganya moyo. Daudi aliiishi chini ya udanganyifu huu karibu kwa mwaka, mpaka Nathani mtume alipomkabili na dhambi yake kwa masimulizi. Lakini kwa wakati Nathani alipomkaripia Daudi, Daudi alilitikia kwa kutubu kwa unyenyekevu, "Nimefanya dhambi"

#### Mfano

Mara mchungaji anapokuwa na kutokujizuia ambako anaweza kwa kipindi kulipuka hata wakati wa mkutano na viongozi wenzake. Wakati mchungaji huyu alipokiri kwa rafiki yake kwamba alikuwa akiomba Mungu ampe kujilinda, Rafiki yake kihekima alieleza: "Ndugu, unaombea kitu kisicho chenyewe—tatizo lako si kutokujizuia, tatizo lako ni hasira. Kama Mungu angekupa kujilinda usingebadilika hata kidogo kwa sababu ungeitumia katika kuficha dhambi ambayo ni hasira.

Mchungaji huyu alikuwa na tatizo la kukabili dhambi yake na katika hali kama hiyo asingeweza kutubu na kubadilika. Katika Zaburi 32, Daudi anarudia kuhesabu mda alipokuwa ana ufahamu wa dhambi zake lakini akakataa kuikiri (V. 3), na hapa tunaona ufunguo tofauti kati ya kuwa na ufahamu wa dhambi na kuitubia dhambi. Alikataa kukiri kwamba alichofanya kilikuwa makosa. Wakati mwingine, kwa kifupi hatuoni dhambi zetu, lakini mara nyingi tunakuwa tunajua tumetenda dhambi, lakini mioyo yetu inakataa kukubali kuwa tulichofanya ni kosa. Mara kwa mara tunatoa udhuru, kama vile, "Mtu huyu alistahili nilichomfanya." Au "Sikuweza kujizua, nimekosa kustahimili mwenyewe." Kwa udhuru kama huu, tunaepuka kutoka kwenye uaminifu wa kukabili dhambi zetu na kukiri kufanya kwetu makosa. Lakini moyo wa toba unaona na kukubali dhambi iliyo fanyika. Unadaiwa kwenye dhambi, na kukiri kwamba tulichofanya ni makosa kweli.

### B. Tambua "Udhambi wa Dhambi"

Dalili ya pili ya moyo wenge toba ni kwamba unatambua dhambi ni nini hasa. Daudi anakiri katika Zaburi 51:4, "Nimekutenda dhambi wewe peke yako, na kufanya maovu mbele za machoni yako..." Ni wazi, Daudi amefanya dhambi mbele ya watu wengine, lakini moyo wa toba unatambua kwamba machukizo yetu makubwa na hatia yetu kubwa vinapumzika mbele za Mungu, kwa sababu hali ya dhambi zote ni kujiweka wenyewe juu ya Mungu. Dhambi ni kama kumtupa Mungu chini na kukaa wenyewe kwenye kiti chake. Moyo wenge toba ya kweli unanung'unika juu ya tabia kama hiyo ya kiburi.

### Mfano

Katika kambi ya vijana, kijana msichana na mvula walikamatwa katika hali ya dhambi ya zinaa. Wote walijisikia kuaibika na walipochukuliwa kwenye ofisi ya kambi kurudishwa nyumbani, msichana alianza kulia kwa kutojizuia. Baada ya kama dakika kumi ya kusikiliza kilio hiki mshauri alimuuliza, "kwa nini unalia kiasi hiki? Ni kwa sababu umeshikwa na unaogopa wazazi wako watakachosema? Au ni kwa sababu unafahamu ulichofanya ni kinyume na Mungu na unajuta jinsi ulivyomkwaza?" Mara moja, msichana akaacha kulia, kwa sababu aligundua hakuwa amefikiria hata makosa yake mbele za Mungu.

Kwa moyo wenyе toba ya kweli, uvumishi mkuu unatoka katika kufahamu dhambi ni nini hasa. Tunagundua udhambi wa dhambi. Tumeacha kumheshimu Mungu na kujitukuza wenyewe juu yake. Hii ni aibu kuu kwa yule anayejua kuwa Mungu ni muumbaji. Ni aibu kuu pia kwa hao wanaojua upendo wa ajabu mno wa Kristo. Ingawa ni muumbaji wetu, alijinyenyeyezea mwenyewe kwa kufa msalabani kutuokoa viumbe tusio na thamani kama sisi. Kwa kujua upendo wa ajabu wa Mungu, mtu mwenyе kutubu anasagua na kufahamu kwamba amevunja na kunyanyasa upendo huu wa ajabu mno.

Aina hii ya majuto inatupeleka kwenye kuungama kwa Mungu bega kwa bega na Daudi, "umehakikishwa sawa unapoongea na kuhesabiwa haki unapohukumu." Vyovoyote hukumu ya Mungu itakavyokuwa juu ya dhambi zangu, hana lawama na ninastahili kuhukumiwa. Ufahamu kuwa tunastahili hukumu ya haki ya Mungu inatoka katika moyo wenyе toba unaojua dhambi yake ni nini hasa.

Kwa hiyo toba ya kweli inaona na kukiri dhambi. Inaelewa pia udhambi wa dhambi, kama iliyofanywa kinyume na Mungu.

### C. Uvunjike Moyo Dhidi ya Dhambi

Katika toba ya kweli, moyo unavunjika na kuwa na kusikitika. Kunakuwa na kuvunjika juu ya dhambi. Zaburi 51:17 inasema "Dhabihu ya Mungu ni roho iliyovunjika; moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu hutaudharau." Hapa tumeambiwa kuwa Mungu hapendezvi na muonekano wa nje ambao unawenza kuwa uigaji rahisi ambao hauonyeshi tabia ya kweli ya moyo. Katika nyakati za Israeli, kutolewa kwa mnyama kulikuwa kunafanya mara nyingi wakati moyo ukiwa kamwe siyo wa toba ya kweli, na Mungu alikuwa anasimamishwa tena kwa muonekano huu wa nje (Isa 1:10-15).

Mungu hafurahishwi na muonekano wa nje, ambao unaweza kuwa uigaji rahisi ambao hauonyeshi tabia ya kweli ya moyo.

Moyo uliovunjika na kusikitika ni ule ambao umesagua na kuwekwa chini. Hauoni uchungu kwa hali ya juu, haujawi na kiburi. Unachukua sehemu ya chini, nafasi ya mwenyе dhambi, unapolutia kiburi, ambacho hakina msingi, na uasi ambao kimakosa unajitwalia enzi ya Mungu. Yeye peke yake yuko juu ya kila kitu. Ni moyo unaotiisha na kufanya laini kwa majuto ya kushindwa kwetu kumpenda mpendaji mkuu wa mioyo yetu.

### D. Hatari za Ulegevu na Kujiamini

Kila mmoja wetu anajua tunavyohangaika na swala la moyo. Dhambi inatudanganya na hivyo kwa urahisi kuwa watoa habari, na muonekano wetu wa nje ni kopo tupu linalokosa haja za kweli ya mioyo yetu. Ngoja tufahamu kuwa wakati ni rahisi kwetu, upande mmoja, kutohisi ukweli wa "udhambi" wa dhambi. Upande mwininge, ni rahisi kugeuza toba zetu katika kujiamini ambapo tunajaribu kulipa deni za dhambi zetu kwa mateso yetu wenyewe. Zote ni kama kusukumizwa nyuma mbele za macho ya Mungu, kwa sababu zote zimejawa na kiburi cha majivuno. Kuwa ubaridi kwenye dhambi ni kuzifanya rahisi dhambi zetu na kujifikiria wenyewe zaida kuliko tunavyopaswa. Lakini kujaribu kujifanya kustahili msamaha wa Mungu kwa kujiamini kwetu ni kushindwa kukiri kwa unyenyekevu hitaji letu la kweli kwa neema ya Mungu na mwokozi ambaye peke yake alilipa deni ya ajabu ya dhambi

...kujaribu kujifanya kustahili msamaha wa Mungu kwa kujiamini kwetu ni kushindwa kukiri kwa unyenyekevu hitaji letu la kweli kwa neema ya Mungu.

zetu na peke yake anayetoa haki ya kukubalika mbele za macho ya Mungu mtakatifu mkamilifu.

Hatariki kuu kwa mtu wa "dini" ni kudharau ubaridi, lakini siyo kujiamini, kwa sababu haoni kiburi cha majivuno cha kujiamini. Anadhani kuwa anaonyesha kutokufaa kwake, lakini moyo wake uliodanganyika unaonyesha kiburi katika kiwango kibaya zaidi. Anadhani kuwa kuteseka kwake kwa ajili ya dhambi kutamfanya kukubarika na Mungu. Hapa tena anazifanya dhambi zake kuwa kidogo, utakatifu wa Mungu kuwa kidogo, kujitoa kwa Kristo msalabani kuwa kidogo, wakati akijifanya yeye zaidi.

Mtu mwininge anawenza kusema, "Huu, mimi ni mprotestanti. Sijionyeshi kwa ajili ya dhambi zangu." Unafikiri hivyo hasa? Ni kwa mda gani unalia kwa ajili ya dhambi zako na kujipiga mwenyewe kwa ndani kwa makosa uliyofanya? Kwa masaa au kwa siku? Unajisikia mara nydingine kwamba Mungu hawezi kukusamehe kweli kweli, kwa sababu dhambi zako ni mbaya sana? Unajaribu wakati mwininge kufanya kitu fulani kwa ajili ya dhambi zako ukidhani kwamba Mungu sasa anakukubali? Hii ni mifumo ya kujiamini na siyo taba ya kweli, na kama toba yako haizai "matunda" ya toba," inawezekana ni kwa sababu hutubu, lakini kwa kifupi unajiamini.

Katika toba ya kweli, moyo unavunjika na kunyenyekehwa (kuwekwa chini). Lakini kama nafisi zetu zinatuongoza kutawaliwa na dhambi zetu na kutokufaa kwetu, kisha toba yetu inageuka kuwa kujiamini. Mkristo mwenye hekina alikuwa akiwashauri watu, "Kwa kuwa kila mmoja anakuangalia ukichukua dhambi, chukua kumi wakuangalia Kwa Kristo." Huu ni ushauri mzuri hata kwetu pia, kwamba toba yetu inaweza isiwe mazoea ya kujiamini ambayo yanapelekea kwenye aina ya maisha mabaya sana na kuteseka-binafsi kwa ajili ya dhambi zetu.

Toba ya kweli ni njia ya maisha kwa sababu inaunda ndani yetu moyo uliofanya upya kwa ajili ya Mungu tunapoziona dhambi zetu na kuzikiri. Toba ni njia ya maisha kwa sababu mioyo yetu inavunjwa na kunyenyekehwa na kufanya kumpenda Mungu tena. Lakini moyo wa toba una bandia zake, kama vitu vingine vyote ulimwenguni vilivyo. Kwa hiyo, ni lazima turuhusu neno la Mungu kwa mara nydingine tena lituongoze, ili kwamba tusiweze kuangukia kwenye mtego wa kitu kinachoonekana kama toba, lakini hakibebi matunda ya toba ya kweli.

## II. TOBA YA KWELI KAMA NJIA YA MAISHA

Kuishi maisha yenyenye tabia ya toba mawazo yafuatayo yanatakiwa yaeleweke:

### A. Baba Anasubiri Kutusamehe

Watu wengi hawawezi kukiri vya kutosha dhambi zao mpaka wawe na uhakika kuwa wataweza kubeba adhabu. Watoto wanaweza kuficha habari muhimu kutoka kwa zazazi wao kwa kuogopa kuadhibiwa. Tunaweza kuwa sawa kwa Mungu tunapokuwa tuna hatia!

Hatuna kitu cha kuogopa tunapotubu dhambi zetu. Hatuwezi kubeba adhabu kwa ajili ya dhambi zetu. Yesu Kristo ameshafanya! Ili kwamba, "hakuna tena hukumu kwa walio ndani ya Kristo Yesu" (Rum 8:1). Tunaweza tukawa waaminifu juu ya dhambi zetu kwa kuwa tunajua kuwa Mungu anasubiri kutusamehe (1Yoh 1:9, Ebr 4:16).

Mungu anatalialika kwenye visima virefu vya neema yake, ili kwamba tusiogope kumkaribia kwa unyoofu katika utakatifu wake wote. Mungu anajua kuwa uaminifu na uwazi unakua zaidi kwenye udongo wa upendo usiobadilika, na hiki ndicho anachotoa kwetu. Kwa hiyo Mungu ameanzisha agano mpya. Wakristo wametimiza sheria kwamba neema inaweza kutolewa kikamilifu. Mungu ameumba moyo mpya ndani yetu, ili kwamba dhambi isitawale tena. Badala yake dhambi inakuwa ya zamani, mtawala aliayedharauliwa tunapokua kumjua Mungu.

Mungu anajua kuwa uaminifu na uwazi unakua zaidi kwenye udongo wa upendo usiobadilika, na hiki ndicho anachotoa kwetu.

### B. Toba ni Kukubali Kiukweli kwa Tatizo Letu Halisi

Wazo kwamba toba ni njia ya maisha linaonekana la kigeni kwa baadhi ya wakristo, kwa sababu ni rahisi kufikiri hatuko tena, kama Luther alivyoiveka, "halisi, kufaa, wenge dhambi walioiva." Tambua kukubali kwa Daudi anakuja kuwa na moyo wa toba: Tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu, mama yangu alinichukua mimba hatiani" (Zab 51:5). Kwa hakika, haya ni maelezo ya muhimu, ambayo yanaongelea mbegu ya dhambi zinazorithiwa kutoka katika kila kizazi kutoka kwa Adamu na Eva walipofanya dhambi ya kwanza. Lakini Daudi hasumbuliwi na kutupatia maelezo ya theologia ya mwanzo wa dhambi hapa. Badala yake, hii ni kukubali kwa uaminifu kwa tatizo halisi, na sisi tungefanya vilevile kuchukua moyoni kilio chake cha ungamo.

Dhambi siyo tu hali ya tabia iliyotengwa ya kufanya mabaya. Badala, ni...mwendelezo wa sehemu ya tabia kamili ya hali yetu, imani na tabia ilijoengwa kwa undani katika mfarakano kutoka kwa Mungu.

Aina ya maisha ya toba ni sehemu muhimu ya kutembea kwetu kikristo, kwa sababu tatizo letu la dhambi ni halisi na la undani sana. Hata baada ya mtume Paulo kuwa mkristo na kumjua Bwana kwa zaidi ya miaka 20, alikubali kusumbuka kwake na dhambi. Katika Warumi 7:15 anasema, "Sijui nilitendalo. Kwa kuwa ninachotaka kufanya sikifanyi, lakini ninachochukia nakifanya." Dhambi siyo tu hali ya tabia iliyotengwa ya kufanya mabaya. Badala, ni sehemu ya anguko letu la asili sehemu ya tabia kamili ya hali yetu, imani na tabia ilijoengwa kwa undani katika mfarakano kutoka kwa Mungu. Hili linagusa tatizo hasa tulilonalo la dhambi, na kwa hiyo hitaji letu la toba linaloendelea kwa undani, toba ya kuvunjika moyo. Kama tunataka kuona upya unaoendelea katika maisha yetu ya kiroho, ni lazima pia kwa machozi tukubali tatizo letu la dhambi.

### C. Mungu Amejitoa Kufanya Kazi Ndani Yetu

Pale tu tunapoelewa tatizo letu halisi la dhambi ndipo tutatiwa moyo na mstari unaofata katika Zaburi 51: "Tazama wapendezwa na kweli ilio moyoni; Nawe utanujulisha hekima kwa siri" (v.6).

Mungu ameumba moyo ndani ya Daudi ambaa ulijua ukweli tena, kwa kuwa moyo wa Daudi ulikuwa umevunjika kwenye dhambi. Anasema katika Zaburi 32:2 "Amebarikiwa mtu...ambaye ndani mwake hamna hila." Mungu ameondoa hila ya dhambi katika moyo wa Daudi, na toba yake ulikuwa matunda ya kazi ya Mungu.

Utiwe moyo kwamba pamoja na tatizo letu halisi la dhambi, Mungu anafanya kazi kuleta ukweli na hekima ndani yetu. Mda wetu wa toba ya undani hakika ni kazi ya Mungu inayoleta ukweli katika utu wetu wa ndani na hekima katika nafsi zetu. Kwa hiyo tunatakiwa tufungue mioyo yetu kwa Mungu kuweza kufanya kazi hii kwa uhuru ndani yetu. Tunahitaji msaada wake. Kama tuko wanyoofu katika kutembea katika ukweli, kisha tunaweza kuomba kama Daudi alivyoofanya: "Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu, unijaribu uyajue mawazo yangu. Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, ukaniongoze katika njia ya milele" (Zab 139:23-24). Siyo rahisi kutaka kabisa mioyo yetu kuvunjika, lakini ni katika kuvunjika huku kwamba tunatembea katika ukweli na hekima.

### III. BARAKA ZA TOBA YA KWELI

Ukweli katika masomo haya unazingatia katika uhusiano wetu mpya na Mungu kulingana na neema yake, na maisha ya uhuru na nguvu. Mara nyingi tunapofikiria juu ya neema na uhuru tunakuwa na wasiwasi na matunda ambayo katika haya yote "ukombozi" unaweza kuzalisha. Mafundisho ya neema yanaleteleza wakristo kuishi maisha ya juu juu tu? Jibu ni 'hapana' hakuletelezi wakristo kuishi maisha ya juu juu. Kinyume chake, kufundisha neema matokeo yake ni watu wenge upendo na Baba na kwamba wanataka kutii kila amri zake.

Biblia inafundisha baraka za moyo wenye toba. Daudi anauliza kwamba Mungu angejibu kulingana na upendo wake katika kurudisha alichokuwanacho kabla hajatenda dhambi. Daudi anatarajia kwamba angeona neema ya Mungu tena (v.1), kwamba angefutiwa makosa yake yote (v.2), kwamba angemrudishia furaha yake tena (vv. 8,12), kwamba dhambi zake zingefutwa kabisa na Mungu asizione tena (v.9), kwamba awe na moyo safi (v.10,12) na kwamba ampatie Roho wake Mtakatifu (v.11).

Tunaweza kuwa na hakika kwamba Mungu atafanya haya katika 2Wakorintho 1:20, "Maana ahadi zote za Mungu zilizo katika yeye ni ndiyo katika Kristo." Ahadi zote za Mungu ni "ndiyo" kwetu tulio katika Kristo. Katika njia zote ambazo Daudi alizomuuliza Mungu kujibu kwenye toba yake, tunakuta ahadi au kanuni ambazo zinatuhakikishia kwamba hivi ndivyo hakika Mungu atajibu kwenye toba zetu.

Mwishoni, katika mstari wa 17, Daudi anaonyesha mwisho na ukoo wa baraka hizi anaposema kama maelezo ya kweli, lakini Mungu "hataudharau moyo uliovunjika na kupondeka." Tunaweza tukauliza fahari yake katika wakati, lakini Mungu hatageuka kuuacha moyo uliovunjika kwenye dhambi yake. Hii kawaida ni njia ya kurudi kwa Mungu, na mara zote tutapata karibu miyo yetu inapovunjika kwenye dhambi. Anafurahishwa na aina hii ya moyo na atausogeza kwake.

Ukaribu wa Mungu ni zawadi kuu ya maisha ya kutubu. Yesu anamwambia mkristo aliyetubu katika kanisa la Laodikia "nitaingia na kula pamoja naye na yeye pamoja nami" (Uf 3:14-20). Hii inazungumzia ukaribu ambao tutajua miyo yetu inapoendelea kuvunjika kwenye dhambi na kuingia katika undani wa uhusiano na Mungu. Hii inatokea tunapofanya toba kama njia ya maisha.

## SULUHU

Katika somo hili tumekuwa tukimzungumzia Daudi mfalme wa Israel. Ukweli kwamba Daudi alikuwa mfalme siyo kwamba alikuwa ana udhuru katika kutubu. Kinyume chake, nafasi yake ya uongozi ilimaanisha alitakiwa kuwa kielelezo cha toba ya kweli kwa Waisraeli wote. Wachungaji wenyewe hekima na wapanda kanisa wanafundisha kusanyiko lao kutubu. Kwa hakika, viongozi wanatakiwa kuwa mionganoni mwa wa kwanza kukubali mahangaiko yao na dhambi. Zaidi ya hayo, wanapaswa kuwa tayari kutubu dhambi zao kwa wanaowakosea. Wakati kiongozi anapoweza kufanya hivi, kusanyiko au huduma zingine zinazohusiana zinaweza kuwa zaidi na uhusiano na Mungu vilevile.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni nini toba ya kweli?
- Ni nini hatari ya moyo baada ya kuona dhambi zetu?
- Ni nini tofauti kati ya toba na kujiamini? Elezea zote.
- Ni jinsi gani ninaweza kutambua kuwa toba yangu imegeuka kuwa kujiamini?
- Orodhesha orodha ya baraka za toba zilizoombwa na Daudi katika zaburi 51:1-2, 1-17. andika maandiko ya marejeo ambayo yanaelezea ahadi au kanuni ambazo zinafanya baraka hizi kuwa kweli kwetu tulio katika Kristo.
- Unajisikia kuwa Mungu anakukataa unapokuwa umetubu dhambi zako? Kwa nini unajisikia kukataliwa huku?
- Unadhani kuwa unatakiwa kuwa "mtawala" wa kutubu katika kanisa lako? Kwa nini na kwa nini siyo?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Soma "Nafasi ya Wenye Dhambi" na Stanley Voke (Tazama Ziada 10A).



## Nafasi ya Wenye Dhambi NA STANLEY VOKE

*"Sina ninacholeta mikononi mwangu, Isipokuwa nashikilia Msalabani Pake"*

Kitu kigumu kwa yeote ni kuchukua nafasi ya mwenye dhambi. Ni vigumu sana kwa hakika kiasi kwamba wengi hawaichukui kabisa, wakati wengine, wakiwa mara wametolewa kule, hawajari kwenda pale tena. Hakuna hata mmoja kiasili mpenzi wa sehemu ya wenye dhambi. Bado kama hatuendi pale, hatuwezi kumjua kabisa Kristo au kuonja utamu wake wa msamaha wa neema ya Mungu. Kama tunaepuka, tunaweza vilevile kusema "hatuna dhambi" na hivyo kujidanganya wenyewe.

### KUCHUKUA SEHEMU YA WENYE DHAMBI

Sehemu ya wenye dhambi ni mahali tunapokubali bila udhuru kwamba tu wenye dhambi. Tunaweza tukakubali dhambi moja tu kama vile wivu au kiburi; tunaweza kuthibitishiwa kitu fulani kinachoonekana kidogo, lakini kwa kufanya hivyo tumerudi katika nafasi ya wenye dhambi tena—ingawa tunaweza kuwa tumekuwa wakristo kwa miaka mingi. Nyuma ya kila dhambi Mungu anaweza kukuonyesha vitu zaidi bila mzaha mpaka siyo kimoja tu lakini vingi tumevikiri na tumeletwa kwenye kukubali uovu wetu wote wa asili. Mtu Mara alipoungama kuwa ameiba kamba. Aliirudisha. Siku iliyofuata alirudi, wakati huu akimrudisha ng'ombe ambaye amekuwa hayuko tayari kukubali alikuwa amefika mwisho wa kamba yake! Tunapochukua sehemu ya wenye dhambi, tunakubali ukweli kuhusu sisi wenyewe—ukweli wote.

Sehemu ya wenye dhambi ni mahali tunapochukua lawama. Tunaacha kujipa udhuru wenyewe na kusema "sikuwa mimi hasa nilipofanya hivyo." Badala yake tunainamisha vichwa na kusema, "ndiyo, Bwana, nilikuwa mimi; hivyo ndivyo nilivyo hasa. Hatulaumu ufahamu wetu tena kamwe, misukosuko yetu, au watu wengine. Mtu fulani anatakiwa kunyooshea baadhi ya makosa au kutupinga, hata si kwa upole, hatubishi na kujihalalisha wenyewe au kujaribu kuyaelezea mambo kwa mbali. Hata tunaukubali upinzani kwamba kama angelitujua kama kweli tulivyo angepata zaidi ya kupinga. Tunatunza mda usio na mwisho na kupumua tunapokuja kwa haraka kwenye sehemu ya wenye dhambi. Kwa hakika mambo yangetuwa tofauti katika makanisa mengi kama wajumbe wanakutana mara chache pale kwenye sehemu ya wenye dhambi.

Hii ni sehemu ambayo Daudi alichukua kama, wakati Nathani alipomtia changamoto, aliinamisha kichwa chake akisema, "nimetenda dhambi." Hapa Ayubu alisimama na kulia, "Tazama, mimi ni mwovu," na Isaya alisema, "Ole wangu! Kwa maana nimepotea." Hapa watoza ushuru waliomba, "Mungu unirehemu mimi mwenye dhambi"; Hapa Paulo aliangukia miguuni mwa Yesu akisema, "Ondoka kwangu; kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi." Katika sehemu hii, mwana mpotevu aliungama "Baba, nimetenda dhambi na sisitahili tena." Paulo mara nydingi alipiga magoti sehemu ya wenye dhambi na watakatifu wengi wameimwagilia kwa machozi yake. Kama hatujaja hapa, hatujaanza na Mungu (2Sam 12:13, Zab 51:4, Ayu 40:4, Isa 6:5, Lk 18:13, Lk 5:8, Lk 15:18).

Hatutaki sehemu ya wenye dhambi kwa kuwa tunaogopa itaumiza kiburi chetu. Kwa hiyo tunapinga, bisha, kuwaweka wengine kwenye makosa, kujipa udhuru wenyewe, na kwa hakika kufanya chochote badala ya kuchukua sehemu ya wenye dhambi mahali ambapo Mungu anasubiri kusamehe na kutuweka huru.

### KUEPUKA SEHEMU YA WENYE DHAMBI

Mara kwa mara, tunaepuka sehemu hii kwa sababu hatutaita dhambi, dhambi. Tunazungumzia matokeo, kushindwa, udhaifu, ugoigoi, makosa, kutoweza, matamanio; chochote lakini dhambi. Ua la rozi hata kwa jina jingine bado ni zuri tu, na dhambi kwa jina jingine ni kama ubaya tu—kwa Mungu.

Tatizo ni tunafanya tafsiri zetu wenyewe badala ya kukubali ya Mungu. Kwenye maandiko, dhambi ni kitu chochote cha kupungukiwa na utukufu wa Mungu, chochote kinachokosa alama ya ukamilifu wa maadili, au kinachovuka mstari wa mapenzi ya Mungu, chochote kilichopindishwa kutoka kwenye uvutano wa haki ya asili iwe inatoka katika nia, haja, kusudio, siliika, wazo, tabia, mtazamo, neno, starehe au uhusiano. Kama kinafanyika kwa kujificha au kwa kudharau, bado ni dhambi na kuiita kitu kingine tu kunahitaji ama toba ama msamaha ni kuepuka sehemu ya wenyewe dhambi.

Tunaweza kukataa kuiona dhambi kama dhambi. Pengine ni watu watendaji ambao hatuna mda wa kujisumbua na mambo yasiyo na maana sana. Tuna nafasi zetu na vipindi vyetu ya kutunza, Kama Namani, tuko na kazi nydingi na kupata ufahari wetu wakati tunafunika ukoma wetu. Tunakuwa wasemaji kwenye mkutano mkuu wa halmashauri, kuendelea na kazi, kutoa fedha kwa hili na lile—kwa kweli kufanya kila kitu—isipokuwa kuungama ukoma wetu wenyewe wa kiroho unaohitaji kuoshwa na kuwa safi. Tuko kama hao nyakati za Yeremia walioharakishwa kama punda vitani lakini bila kusimama kutubu au kusema, “Nini nilichofanya?” Tuna kazi nydingi sana—kazi nydingi sana kamwe hatutasimama katika sehemu ya wenyewe dhambi. (Yer 8:6).

Tunaweza kuepuka sehemu hii tukijitwalia wajibu wa wakusanya kodi. Kwa mafundisho yetu yaliyofungwa vizuri, ni wanainjili watalaamu wenyewe uhodari wa kuhisi harufu ya kiinjili. Tuanapenda kusahihisha lakini siyo kusahihishwa. Kama Mafarisayo wa zamani tunajiweka nje ya sehemu ya wenyewe dhambi kwa kuwaweka wengine humo. Tumejawa na ufahamu kwamba hatuna nafasi ya moyo uliovunjika na kujuta. Bado hata Henry Martin, mtakatifu mkuu kama alivyokuwa, ameandika katika kitabu chake cha kumbukumbu, “Nimeazimu kamwe kutolaumu mwingine isipokuwa kupata kujua wakati huo huo majuto yasiyo na kifani!” Alikuta anahitaji kuishi kwenye sehemu ya wenyewe dhambi.

Tunaweza kuepuka sehemu hii kwa kujiweka salama ndani ya Kristo hoja isiyo ya kweli kwa wasiotubu. Tumehakikishiwa wokovu wetu, hata hivyo kwa namna fulani hatuwi hatiani na dhambi. Tunafanana na mvulana mdogo ambaye, alipotolewa mezani kwenda kuosha mikono yake, alirudi akiwa na tabasamu kubwa na kusema kwa kushangaza, “Wameosha mikono hivyo wakati huu hatahitaji kamwe kuoshwa tena.”

Kwa imani tu wana wa Mungu na wenyiji wa mbinguni. Lakini bado tu wenyewe dhambi vilevile. Bado tunahitaji kujiosha kwenye “chemicchemi iliyofunguliwa kwa ajili ya dhambi na uchafu” (Zac 13:1). Neema haitatuongoza kwenye dhambi kamwe, lakini daima itatuthibitishia dhambi, na dhambi hivyo iliyofunuliwa mara zote itatuongoza kurudi kwenye neema.

Inawezekana kuepuka sehemu ya wenyewe dhambi kwa kutumia vibaya damu ya Kristo, kiongelea kama “inayofunika” au “inayolinda” kama ilivyofanya damu ya mwana kondoo wa pasaka. Kujitoa kwa Kristo kalvari, kwa jinsi hiyo, ilikuwa kwa ajili ya dhambi. Ni “inayotakasa” siyo tu kwa kifupi *inayolinda*. Kama tunahitaji kwa hiyo, tunafanya hivyo kama mwenye dhambi anayekuja kuoshwa, siyo kama asiye na dhambi anayehitaji tu kuhifadhiwa kutoka kwenye maovu kwa nje yetu. Tunapoongelea tu damu inayotulinda, tunakwepa sehemu ya wenyewe dhambi.

Mwanafunzi wa Spurgeon (mhubiri aliyejulikana vizuri wa kingereza) mara alipohubiri mbele yake kwenye “Silaha zote za Mungu.” Kijana mtukutu, alilgiza ujumbe wake, akijiwekea silaha kipande kwa kipande, mpaka, akiwa amejifunika kote, alipunga silaha ya Roho na kuangua kilio cha shangwe, “Shetani yuko wapi sasa?” Mr. Spurgeon alielekeea mbele na kusema, “kijana, yuko ndani ya hiyo silaha!” Lazima tuwe macho kwamba hatumuruhusu Shetani kuingia kwa kuacha sehemu ya wenyewe dhambi. Miyo yetu ni midanganyifu zaidi ya vitu vingine na, kama maarifa ya theolija ya kigeugeu, tutachukua sura kuficha asili ya kweli. Chini ya usemi wetu kuwa wa kiroho na tunavyojisifia kuwa watu wa kanisa lakini masikini wenyewe dhambi, wanaohitaji kuoshwa kila siku kwenye damu ya Yesu.

### KUTAFUTA NEEMA KATIKA SEHEMU YA WENYE DHAMBI

Siyo kitu cha ajabu kwamba sehemu tunayoepuka sisi wenyewe dhambi ni ile ile aliyochukua Mwokozi asiye na dhambi? Hakika angekuwa mwana wa Mungu kweli angeteremka chini kutoka msalabani! Miujiza, mahubiri yenyewe uwezo, hata ufufuko wenyewe tungemtarajia mtu kama huyo, lakini siyo ubatizo katika mto wa Yorodani na watoza ushuru na Malaya, au wahalifu waliofanya mauaji na wezi! Hata hivyo hapo ndipo alipotoka, kwani uso wake ulikuwa umeelekezwa kuelekea sehemu hii kutoka milele yote.

Pale kwenye ngazi ile ile mwenye dhambi alimkuta pale siku hiyo. Siyo kama msiri huyu aliyekufa akilaumu wengine na kumlaani Mungu, mwizi huyu aliyekuwa anakufa alikubali hatia na kupata msamaha. Amani na paradiso vilimjia alipochukua sehemu ya wenyewe dhambi na kumpata Yesu pale.

Hii ni neema isiyonekana kama ni kweli. Yule anayesitiza yuko sawa atatangazwa kuwa mkosa, wakati anayekiri kuwa na makosa atatangazwa kuwa sahihi. Haki ya Mungu inatolewa kwa hao tu wanaosimama katika sehemu ya wenye dhambi.

Hapa na hapa peke yake ni sehemu ya amani ya kweli, kwani hapa tunakomesha kujitahidi kwetu na kumpata Mungu wetu. Hapa ni mapumziko ya moyo na mlango wa mbinguni. Hapa tunateka hila zetu na kukubali kweli tulivyo. Hapa tunakuja kwa Yesu kuoshwa na damu yake ya thamani. Hapa Roho mtakatifu anatujaza na utakatifu unapatikana. Hapa kuna kuchanua kwa uamsho. Hapa ndipo kanisa lote linatakiwa kuja tena na tena. Ni sehemu ya ukweli na neema na uhuru—sehemu ya wenye dhambi. Lini mara ya mwisho ulikuwa pale? Kwa hakika, uko pale sasa?

---

## **MOAMBI**

---



# Maombi na Kufunga

## ☞ **Kusudi la Somo**

Kutazama upya nafasi ya maombi na kufunga katika utaratibu wa upandaji kanisa.

## ☞ **Wazo Kuu**

- Maombi ni ya lazima kwa ukamilishaji wa kazi ya kiroho ya upandaji kanisa.
- Kufunga ilikuwa njia ya kibiblia ya kuzidisha maombi kote katika Agano la Kale.

## ☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa ...

- Kujua mafundisho ya kibiblia juu ya maombi na kufunga.
- Kuendelea katika utegemezi wake kwa Mungu kupitia maombi na kufunga
- Kuomba na kufunga kwa ajili ya kazi ya upandaji kanisa.

## **UTANGULIZI**

Wapanda kanisa wanapokuwa wanajihusisha na shughuli nyingi muhimu kuona kanisa mpya limepandwa, ni rahisi kutojali malezi ya kiroho. Kama tunajaribu kufanya kazi ya kiroho katika mwili, kukatishwa tamaa kunaweza kuingia kwa kuwa matokeo yanayotarajiwa hayaji. Katika hatua hii mpanda kanisa anahitaji kuacha na kuchukua mtazamo mpya wa nafasi ya maombi na kufunga.

### **I. ASILI MUHIMU YA MAOMBI**

Mungu amejidhihirisha mwenyewe kuwa anayejua yote: Anajua kila kitu. Mungu pia anaweza yote: Anaweza kufanya kila kitu. Kwa nini kisha tuombe? Kama kitu ni mapenzi ya Mungu, hawesi tu kufanya? Au kama hatuombi, hii kwa namna fulani inamzuia Mungu mwenye nguvu-zote kufanya kazi?

#### **A. Mifano ya Aganol a Kale—Mungu Anasubiri Watu Wake Kuomba**

##### a. *Kutoka 3:7*

Waisraeli walikuwa mateka Misri, na Mungu akamtokea Musa na kusema, "...Nimesikia kilio chao...nami nayajua mateso yao. Kwa hiyo nimeshuka kuwaokoa..."

##### b. *Kutoka 32:7-14*

Israeli wamegeuka kinyume na Mungu na kufanya ndama ya kuyeyusha na kuiabudu. Mungu akamwambia Musa, "Sasa niache ili hasira zangu ziwake juu yao niwaangamize. Kisha nitakufanya uwe taifa kuu." Lakini Musa akamuomba Mungu, akimkumbusha ahadi zake. "Na Bwana akaugaili ule uovu aliosema atawatenda watu wake."

##### c. *2Mambo ya Nyakati 7*

Baada ya Solomoni kujenga hekalu, aliomba, akilikabidhi kwa Mungu. Mungu alilitikia kwa kutuma moto kutoka mbinguni kuangamiza sadaka za kuteketezwa na matoleo. Na utukufu wake wote ukajaa hekaluni. Alimwambia Solomoni, "Nimesikia maombi yako na nimechagua sehemu hii kwa ajili yangu mwenyewe kama hekalu la matoleo." Zaidi ya hayo, Aliahidi kwamba, "kama watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha na kuomba na kunitafuta uso na kuacha njia zao mbaya, kisha nitasikia kutoka mbinguni

na kusamehe dhmbi yao na kuiponya nchi yao. Na sasa macho yangu yatafunguka na masikio yangu yatasikia maombi ya watu waombao mahali hapa.”

**B. Mifano ya Agano Jipy—aKuna Uhusiano Kati ya Utendaji Unaochukuliwa Mbinguni na Maombi Yetu**

a. *Yakobo 5:13-18*

Katika kifungu hiki, mtume Yakobo anazungumzia maombi ya imani na ungamo la dhambi. Anasema, “Maombi ya mwenye haki yana nguvu na yanafaa” (v.16). Yakobo anaendelea kunukuru mfano wa Eliya aliyeombea mvua ikosekane kwa miaka mitatu na nusu. Mungu alijibu maombi ya Eliya kwa kuishika mvua. Kisha Eliya akaombea tena mvua na Mungu akaituma.

b. *Luka 6:12-16*

Kabla tu ya uamuzi wa muhimu (wa kuchagua wanafunzi kumi na wawili), Yesu alipanda mlimani kuomba na akaendelea kuomba usiku mzima.

c. *Mathayo 26:36-44*

Yesu alipokaribia kifo chake, aliomba kwa maumivu makuu, “Baba yangu, kama inawezekana, kikombe hiki kiniepuke. Si kama mimi nipendavyo, lakini kama upendavyo.” Mara ya pili Yesu alilia kwa sauti, “Baba yangu, ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisipokunyuwa, mapenzi yako yatimizwe.” Yesu akalia mara ya tatu akiombea kitu kilekile.

d. *Mathayo 6:5-18*

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuomba. Hata “Baba anajua mnachohitaji kabla hamjamuomba yeye,” (v.8). Yesu aliwatia moyo wanafunzi kuomba juu ya mahitaji yao ya kila siku kutimizwa., kuepushwa na majoribu, na kwa mapenzi ya Baba kutimizwa duniani kama ilivyo mbinguni.

e. *Mathayo 7:7-12*

Yesu, akiongea na wanafunzi wake, aliwaambia, “Omben nanyi mtapewa; tafuta mtapata; bisha na mtafunguliwa.” Yesu aliwatia moyo wanafunzi wasiogope kueleza mahitaji yao na haja zao kwa maombi kwa Baba.

**C. Baadhi ya Suluhi Kuhusiana na Asili Muhimu ya Maombi**

Mungu anaweza kufanya chochote anachotaka kufanya, lakini inaonekana kwamba aliamua kusubiri, kuahirisha kazi yake mpaka watu wake wanapoonyesha mapatano yao katika maombi kabla hajatenda. Kutoka kwenye mifano na mafundisho ya maandiko, inaonekana kwamba Mungu amejiunga mwenyewe kwenye maombi yetu, akichagua kukamilisha kusudi lake kupitia maombi haya.

Mungu anaheshimu mapenzi ya mwanandamu na anapenda mwanadamu kufanya kazi mapenzi yake kwa muungano na mapenzi ya Mungu na kwa upinzani wa mapenzi ya Shetani. Maombi ni kuonyesha haja yetu kwenye mapenzi ya Mungu na ni njia moja tunayofanya kazi pamoja na Mungu katika kukamilisha makusudi yake. Maombi siyo mapambano kushawishi na kumshurutisha Mungu kubadili nia yake kuendana na fahari zetu. Badala yake, kupitia maombi tunapambanua mapenzi yake na kisha kuelekeza mapenzi yetu kwenye matakwa ya Mungu na makusudi. Kwa hiyo maombi yana makusudi ya vitu viwili:

- Kuonyesha mawazo yetu na haja zetu kwa Mungu
- Utambuzi wa mapenzi yeke kwetu

**II. WAJIBU WA KUFUNGA**

Kufunga ni kufanya shauri la kuacha baadhi ya vyakula au vyakula vyote au vinywaji kwa kusudi la kuwa na maombi yasiyokatizwa. Pia kunaweza kukawa na mda wa kuacha shughuli na kushiriki pamoja na marafiki kwa ajili ya mda katika utaratibu wa mtu kujitoa kikamilifu kuwa na ushirika na Bwana—kumtafuta yeye na mapenzi yake. **Kufunga ni malezi ya kiroho, siyo amri.** Kwa hiyo, kama mtu ana matatizo ya kiafya au kwa sababu nyininge hawezu kufunga, mtu huyo hatakiwa kujisikia hatia au kuhukumiwa kufanya dhambi. Kufunga kunafanya katika baadhi ya

tamaduni na dini kama kawaida za dini au mapokeo. Kazi ya kufunga kwa kibiblia ni kukazia mwelekeo wa mtu kwa Bwana. Haitakiwa kufanyika kama tu kawaida za dini.

#### A. Mafundisho Ya Kristo

Yesu alifundisha kufunga na kufunga mwenyewe (Mt 4:2). Wanafunzi wake wanaweza kuwa hawakufunga wakati yeye akiwa amefunga wakati akiwa nao (Mk 2:18-19). Kwa jinsi hiyo, hata somo hili waziwazi linaelezea kwamba Yesu alitarajia kwamba wanafunzi *wangefunga baada ya yeye kuchukuliwa mbinguni*. Pia aliwfundisha wanafunzi wake kuhusu Kufunga katika maombi. Katika mandhali ya kufundisha maombi, mara mbili Yesu alisema juu ya kufunga, “Munapofunga...msiwe kama wanafiki...” (Mt 6:16-17). Tambua kuwa alisema “wakati” siyo “kama” kana kwamba haya yalikuwa mazoea ya kawaida ya wanafunzi.

#### B. Mfano wa Kanisa la Kwanza

Katika kitabu cha Matendo, tunaona maombi, kufunga na kupanuka kwa kanisa yote yakienda bega kwa bega. Kanisa lilipomtegemea Mungu, injili ilisonga mbele.

##### 1. Matendo 13:1-3

Viongozi wa kanisa la Antioquia walipohudumu (waliomba) kwa Bwana na kufunga, Roho Mtakatifu aliwajia kwa mafundisho na maelekezo. Kupanuka kwa huduma ya Paulo na kupanuka kwa kanisa kwenye Asia ndogo na Ulaya kulianza kwa maombi na kufunga.

##### 2. Matendo 14:23

Paulo na Barnabas waliwakabidhi wazee wa makanisa mapya chini ya uangalizi wa Bwana kwa maombi na kufunga. Kwa maombi na kufunga, Paulo na Barnabas walipata ujasiri wa kutoa utawala wa viongozi hawa na jinsi ambavyo wangeongoza makanisa yao katika mikono ya Bwana.

#### C. Asili ya Maombi

Kristo alifundisha kwamba kupokea majibu ya mbinguni tunahitaji kuomba, kutafuta na kubisha (Mt 7:7). Kila neno linaonyesha undani zaidi wa kutafuta. Shauri la kufunga linadhahirisha shauku ya haja, mzigo unaoendelea wa moyo ambao ni mzito kuliko haja ya chakula cha kimwili. Mvuto wa kufunga unaonekana kuwa katika makundi mawili. Waumini wanaingia katika kumtafuta Mungu kwa mkazo zaidi wa kumtafuta Mungu kwa makusudi ya:

- kuimashwa kiroho
- Kuendelea kwa ufalme wa Mungu

Kama ilivyoonyeshwa kwenye mafundisho ya Yesu Kristo na mfano wa kanisa la kwanza, kufunga kunatarajiwa na ni kipengele cha maana cha maombi.

#### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Umewahi kutumia mda katika maombi na kufunga? Ilikuwaje ulivyoona? Ulihisi kuimashwa kiroho au kuona Mungu akijibu maombi yako katika njia ya ajabu?

#### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Soma Mathayo 6:16-18
- Elezea jinsi “unafiki” ulivyoonekana walipofunga. Kwa nini walifanya hilo?
- Elezea jinsi mtu anavyotakiwa aonekane anapofunga
- Jinsi gani tunaweza kutunza ufungaji wetu kutokuwa kawaida za dini?
- Panga na kutana na malezi ya kiroho ya kufunga. Chini kuna njia kidogo ambazo baadhi ya wakristo wanafanya hili. Unaweza kuamua kufata moja ya hizi, lakini mfumo ni juu yako.
  - Acha badhi ya vyakula na kunywa kwa mda maalumu
  - Acha vyakula vyote lakini kunywa maji ya matunda na baadhi ya vinywaji kwa mda maalumu.
  - Acha baadhi ya vyakula lakini si vyakula vyote.

- Tenga siku moja kwa juma /mwezi ambayo utafunga.
- Fanya orodha ya vitu maalumu ambavyo utaombea wakati unafunga.
- Andika katika kitabu chako cha kumbukumbu za kiroho ulivyoona wakati wa kufunga kwako. Ulijisikiaje? Nini ulichojifunza juu yako? Juu ya Mungu?

### **VYANZO**

- Duewel, Wesley L., *Touching the World Through Prayer*. Coral Gables, FL: Worldteam, 1986.
- Eastman, Dick, *No Easy Road*. Grand Rapids, MI: Baker Book House, 1971.
- Piper, John, *Hunger for God*. Wheaton, IL: Crossway Books, 1997.



## Kongamano la Maombi

### KUOMBEA KUENEZWA KWA INJILI

#### ☞ **Kusudi la Somo**

Kutoa nafasi kwa wapanda kanisa kuwa na maombi ya muungano kwa wao wenyewe na kwa wapanda makanisa wengine kote Ulaya ya Mashariki na Kati na Muungano wa zamani wa Urusi.

#### ☞ **Wazo Kuu**

Ni muhimu kuombea kuenea kwa injili kupita maeneo yetu.

#### ☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa ...

- Kujua jinsi ya kutumia maombi ya kibiblia vizuri kama kielelezo katika kuomba kwake.
- Kuimariswa kupitia maombi ya wengine.
- Kuomba siyo tu kwa wapanda makanisa ya mtaa, lakini kwa wapanda makanisa wanaofanya kazi katika nchi zingine.

#### ☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Waongoze wafunzwa katika kuomba kwa maombi ya Paulo katika Wakolosai 1:3-14, ukitunza mda wa mafunzo kwa kifupi ili kwamba mda mwangi utumike katika kuomba.

Inashauriwa kwamba wafunzwa wawaombee wafunzwa wapanda kanisa wengine katika nchi zingine wanaopitia katika mafundisho ya aina moja. Nchi ambazo kazi hii iko inafanyika ni Albania, Bulgaria,Czech Republic, Estonia, Hungary, Romania, Urusi, Slovakia, Sebia na Ukraine. Kwa habari za sasa, Wasiliana na Ofisi ya Alliance huko Budapest.

## UTANGULIZI

Moja ya njia nzuri ya kuomba ni kutumia mifano ya kibiblia. Kwa kongamano hili la maombi, fata maombi ya mtume Paulo waliyopewa Wakolosai katika Wakolosai 1:3-14 kama muhutasari wako wa kusifu, kuabudu, na maombi. Tambua kuwa maombi haya yanaanza na kumalizika kwa shukurani kwa Mungu (vf. Kielelezo 6.1). Ukweli kwamba hii ni njia ya kawaida ya kibiblia inakazia umuhimu wa kuomba kwa shukurani. Tutafata mzunguko sawa katika kongamano hili la maombi. Tutaendelea kutoka kutoa shukurani, kwenda kwenye injili, kwenye ufahamu, na kurudi kwenye kutoa shukurani tena.

### I. **MSHUKURU BABA—WAKOLOSAI 1:3-5**

Soma kwa pamoja mistari ya 3-5: “*Twamshukuru Mungu, baba yake Bwana wetu Yesu Kristo, siku zote tukiwaombea; tangu tuliposikia habari ya imani yenu katika Kristo Yesu, na upendo mlizo nao kwa watakatifu wote; kwa sababu ya tumaini mililowekewa akiba mbinguni; ambalo habari zake mlizisikia zamani kwa neno la kweli ya injili.*”

#### A. **Mshukuru Baba kwa Ajili ya Watakatifu**


- katika mafundisho haya (hasa hasa, kwa majina)
- Katika kanisa lako.
- Katika maisha yako: hao amba wamekuwa wa kuigwa kiroho katika maisha yako.

### B. Mshukuru Baba

- Kwa upendo aliokuonyesha
- Kwa imani aliyokupa
- Kwa matumaini uliyonayo katikati ya ulimwengu usio na tumaini.
- Kwamba injili ilikufikia.

Tambua: Uwe maalumu katika maombi yako. Mshukuru na musifu Baba kwa matukio maalumu katika maisha yako ambapo Mungu amekuonyesha upendo, imani, tumaini, na ulipoipokea injili.

### Kielelezo 6.1 Mzunguko wa Maombi



## II. OMBEA INJILI ISIKIKE ULIMWENGINI KOTE—WAKOLOSAI 1:6-7

Soma kwa pamoja mstari wa 6 na 7: "...injili ambayo imewajia. ulimwenguni kote injili hii inazaa matunda na kukua, kama ambavyo imekuwa ikifanya mionganini mwenu tangu siku mlipoisikia ns kuielewa neema ya Mungu katika ukweli wake wote. Uliisikia kutoka kwa Epafura, mtumishi mwenzetu, aliyemuhudumu mwaminifu wa Kristo kwa ajili yenu, na aliyetueleza upendo wenu katika roho.

- A. Ombea kwamba injili izae matunda mengi katika maisha ya watu mliowashuhudia (kuwa maalumu katika maombi yako).
- B. Ombea kwamba injili izae matunda sehemu ambapo wengine wanapanda makanisa. (Wakufunzi watakuwa na orodha ya nchi ambako mafunzo ya wapanda kanisa yanaendelea kwa sasa.)
- C. Ombea wamishenari wengine unaowajua, kwamba huduma yao italeta matunda mengi.
- D. Ombea kwamba Mungu ataita watumishi zaidi waminifu kuichukua injili mpaka miisho ya dunia.

### III. OMBA KWAMBA MUNGU AKUJAZE NA UFAHAMU WA MAPENZI YAKE—WAKOLOSAI 1:9-11

Kimya kimya soma mstari wa 9-11: “Kwa sababu hiyo sisi nasi, tangu siku ile tuliposikia, hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu, ili mijazwe mapenzi ya maarifa yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni; mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu, mkiwezesha kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu wake, mpate kuwa na subira ya kila namna ya uvumilivu...”

- A. Katika sehemu iliyotolewa hapo chini, orodhesha sababu kwa nini Paulo aliomba kwamba waweze kujazwa na ufahamu wa mapenzi yake katika hekima yote na kufahamu. Nini yalikuwa matokeo yaliyotarajiwa? Ya kwanza mawili yamefanyika kwa ajili yako.

1. Kwamba waumini waweze kuishi maisha yaliyojawa na Mungu

2. kwamba waumini waweze kumpendeza Mungu

3. \_\_\_\_\_

4. \_\_\_\_\_

5. \_\_\_\_\_

6. \_\_\_\_\_

- B. Ukitumia orodha uliyokamilisha katika sehemu hapo juu, Ombea vitu hivi kwa washiriki wenzako katika mafundisho haya.

### IV. TOA SHUKURANI KWA BABA—WAKOLOSAI 1:12-14

Soma kwa sauti kwa pamoja mstari wa 12-13: “...Mshukuruni Baba, aliyewastahilisha kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru. Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa mwana wa pendo lake”

- A. Msifu Baba kwa kukuleta katika ufalme wake

- B. Msifu Baba kwamba huishi chini ya ukandamizaji wa shetani

- C. Msifu Baba kwamba umekombolewa

- D. Msifu Baba kwamba dhambi zako zimesamehewa

- E. Msifu Baba kwamba unaweza kumuita “Abba” au “baba.”

---

## **UONGOZI**

---



# Mizunguko ya Uongozi

## ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wafunzwa kutambua wapi wanahitaji kukazania juhudzi za maendeleo ya uongozi wao.

## ☞ Wazo Kuu

- Wapanda kanisa wanahitaji kufanya mafunzo ya viongozi wa vipao mbele zaidi.
- Mafunzo ya ufanisi ya uongozi yanahitaji kwamba mpanda kanisa kutumia mda zaidi na juhudzi na hao watakao kuwa viongozi na kuongezeka katika huduma.

## ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoelewaka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kushawishika kwamba mafunzo ya uongozi yanatakiwa yaye kipao mbele kwa mda wake na juhudzi.
- Kujua jinsi ya kutumia wazo la ‘Mzunguko wa uongozi’ kusaidia kupanda juhudzi za mafunzo ya uongozi.

## UTANGULIZI

Moja ya maamuzi magumu ambayo viongozi wanakutana nayo ni jinsi ya kutumia mda wao. Mahitaji hayaishi. Hakuna kamwe mda wa kuweza kufanya kila kitu. Nini kifanyike, na nini kisubiri? Jibu siyo rahisi, lakini kuna kanuni za jumla. Moja ya mipaka muhimuni kwamba viongozi wapya lazima wafundishwe ili kwa aina yoyote ya huduma kukua na kupanuka. Hili ni kweli hasa katika upandaji makanisa. Bila maendeleo yanayoendelea ya viongozi wapya, utaratibu utadumaa na kufa.

Kila mpanda kanisa lazima ahusike katika maendeleo ya viongozi wapya. Lakini hata hivyo, kuna mahitaji yaliyo kama aina fulani ya maelekezo kuhusu ni nani kiongozi wa kufundisha, na ni mda kiasi gani wa kuwekeza kwa kila mmoja. Yesu ni mfano mzuri wa jinsi ya kutunza uwiano huu.

## I. MIFANO WA YESU

Yesu alikuja duniani ili kulipia dhambi zetu, na kuanzisha kanisa lake. Kanisa hili litakuwa nyenzo yake ya kuhubiri injili kwa mataifa yote. Kwa kufikiri kazi kubwa iliyomkabiri Yesu, inashangaza kweli kweli kwamba alichagua kutumia mda kama alivyofanya. Angekuwa aliweza kufanya miujiza ya ajabu kila siku, na kutumia mda wake kuhubiri kwenye umati uliokuja kuwaona.

Hakika, Yesu alifanya miujiza mingi, lakini siyo kila siku, na siyo mingi kama ambavyo angeweza kufanya. Zaidi ya hayo, wazi wazi alichagua kutumia karibu mda wake mwingu kuwafundisha watu kumi na mbili kuliko umati mkubwa. Badala ya kuwafikia watu wengi iwezekanavyo, Yesu alifundisha viongozi wa kujaa kiganja wa kuwafikia wengine.


Badala ya kuwafikia watu wengi iwezekanavyo, Yesu alifundisha viongozi wa kujaa kiganja wa kuwafikia wengine.

Matokeo yake yalikuwa ya ajabu. . Ingawa falme yenye nguvu ya Urumi kwa ukali sana ilitesa makanisa machanga, mapya, yaliponea chupuchupu na kukua mpaka mtawala wa falme Constantine mwenyewe alipogeuka kuwa mkristo. Wazi wazi njia ya Yesu isiyo ya kawaida inafanya kazi.

Mtazamo wa karibu wa huduma ya Yesu unaonyesha kwamba anaonekana kuwa alishughulikia makundi manne tofauti ya watu. Makundi haya yalikuwa:

- *Watatu*—Yesu kwa kujirudia alimchukua Petro, yakobo, na Yohana mbali na wanafunzi wengine na kuwaonyesha zaidi kuhusu asili yake na kusudi lake. Mifano ni pamoja na Mathayo 17:1, Marko 5:37, Marko 13:3, na Marko 14:33. Tunapoangalia kwenye kitabu cha Matendo, tunaona kwamba hawa watatu walishika nafasi zaidi ya kuonekana katika maendeleo ya kanisa kuliko walivyofanya wanafunzi wengine.
- *Kumi na wawili*—Mitume kumi na wawili walifurahia uhusiano wa pekee na Yesu. Walikuwa wamechaguliwa kwa heshima hiyo kutoka mionganini mwa wafuasi wengi walimfuata (Lk 6:13). Ingawa wanafunzi wengine wangeshika nafasi muhimu katika kanisa jipya, kumi na wawili (kasoro Yuda) wangetoa uongozi. Walikuwa kwa hiyo vipao mbele kwa mda wa Kristo na juhudhi.
- *Wanafunzi*—Kama tulivoona hapo juu, kulikuwa na kundi kubwa la ‘wanafunzi’ ambao hawakuchaguliwa kuwa mionganini mwa kumi na wawili. Kundi hili pia liliacha miji yao na aina ya maisha ili kumfuata yeye (Lk 14:27). Jumala ya idadi ilibadirika mara kwa mara ilivyoonekana. Katika tukio moja, wengi kati yao walimwacha Yesu (Yoh 6:66). Katika Luka 10:1, kundi lilikuwa kubwa vyatya kwa Yesu kuchagua sabini na-wawili kati yao kwa ajili ya huduma maalumu. Baada ya ufufuko wake, alionekana kwa zaidi ya 500 (1Kor 15:6). Na kiini cha kundi la 120 walijitoa wenyewe kwenye maombi wakiwa wamesubiri Roho Mtakatifu waliveahidiwa (Mdo 1:15).
- *Umati*—idadi kubwa ya watu walimfuata Yesu, wakisikiliza mafundisho yake na kusubiri kuona mijizaji (Mt 4:25; 13:2). Tunajua kuwa walifikia idadi ya 5000, kwa kuhesabu tu wanaume (Lk 9:14). Baadhi yao waliamini, na wengine hawakuamini. Watu waliokuwa pamoja walikuwa kuanzia mitume na mafarisayo waliotaka kumkamata Yesu kwenye baadhi ya makosa.

**Kielelezo 3.1 Mzunguko wa Uongozi wa Yesu**




Kielelezo 3.1 kinaelezea makundi haya mbalimbali yaliomfata Yesu kama mfuatano wa mzunguko. Mkazo wa mahusiano unaongezeka tunaposogea kutoka kwenye umati kwenye duara la nje kuelekea kwenye duara la ndani lililo na Petro, Yakobo, na Yohana.

Tunapoangalia katika huduma ya Yesu, Anaonekana kuweka vipaombele vya juu katika kutokea kwa mzunguko karibu sana na katikati. Tunaposogea kutoka nje kwenda mduara wa ndani, Alitumia mda mwangi, akidhirisha ukweli zaidi na akitarajia mengi kama matokeo.

## II. MZUNGUKO WA UPANDAJI KANISA WA UONGOZI

Wapanda kanisa pia wanatakiwa kufata mfano wa Yesu wa kukazia juhud zao za mafunzo yao ya uongozi kwa watu wanaofaa. Kama ungetakiwa kuchora mduara wako wa mahusiano, ungeweza kuonekana kama kitu fulani katika kielelezo 3.2. Kwa 'nje' lingekuwa kundi kwa ujumla ambao unawahudumia—ikiwemo waumini wote na wasio waumini. Ngazi inayofuata ndani lingeweza kuwa ni pamoja na hao waumini wanaonekana kuwa maarufu kama viongozi wa mbeleni. Ndani zaidi linaweza kuwa timu ya upandaji kanisa—hao ambao unafanya nao kazi kupanda kanisa na ambao wameshahusika kwenye huduma. Katikati anaweza kuwa mtu (au pengine watu 2-3) ambao unafanya nao kazi kijuhudi zaidi kuwaandaa kwa ajili ya uongozi.

Kielelezo 3.2 Mzunguko wa Uongozi wa Wapanda Kanisa



Unapoangalia kielelezo 3.2, kuna aina mbalimbali za mawazo ya ufunguo ambayo unatakiwa uyatambue:

- Mtu alivyo karibu zaidi na katikati, ndivyo unavyotakiwa kutumia mda mwangi na juhudi kuwaendeleza kwa ajili ya uongozi.
- Uangetakiwa uwe unafanya kazi kwa kiwango fulani na kila mmoja katika mzunguko wako, kwa kuwa huwezi kuwa na uhakika nani atakuwa kiongozi mzuri au hatakuwa mbeleni.
- Kimawazo, hao walio kwenye mzunguko wa nje wataendelea kuhamia kwenye ule wa ndani wanapokua na kukomaa, na viongozi wanafunzi wanapotolewa kwenye huduma.

- Kwa sababu umetumia karibu mda wako mwingu na mzunguko wa ndani, watu wengine unaofanya nao kazi wanahitaji kushikilia huduma kwenda kwenye mzunguko wa ‘njie’ ili kwamba isiwe kama wameachwa. Utakuwa ‘mwandaaji’ na watakuwa ‘wahudumu.’ Mtindo huu ni wa kibiblia (Efe 4:11-12).
- Viongozi wanafunzi zaidi watakuwa wajumbe wa timu ya upandaji kanisa wanaofanya mzunguko mwinguine. Hii ni sawasawa na Petro, Yakobo, na Yohana waliokuwa ndani ya watatu, lakini walikuwa wajumbe wa kumi na wawili.


### III. MZUNGUKO WAKO WA UONGOZI

Vipi kuhusu hali yako? Nani atafaa kwenye mzunguko wako? Chukua dakika chache na jaza kwenye kielelezo 3.3 kwa majina ya watu pekee na vikundi amba unawahudumia amba wataelezewa zaidi na kila moja ya mzunguko wa uongozi.

Unaweza kuwa timu ya kawaida ya upandaji kanisa, na unaweza usiwe. Hali halisi inaweza kuwa kuanza kanisa mpya kama kikundi, kwa sababu iliyokwisha elezewa katika mafunsdisho haya. Hata hivyo, halisi huwa haiwezekani wakati wote. Kama umeshakuwa na timu, mzunguko unatakiwa uwe rahisi kwako wewe kujaza. Kama siyo, fikiria mawazo yafuatayo na jaza vizuri uwezavyo:

- Kama huna timu ya upandaji kanisa ya ‘kawaida’, pengine una moja ‘isiyo ya kawaida’. Kuna kundi dogo la waliojitoa unaofanya nao kazi kwa karibu mkiwa na lengo la upandaji kanisa mpya? Wanafanya kama timu yako, hata kama siyo ‘kiofisi.’ Lakini unapowaongoza ukitumia kanuni katika nyenzo hii, unaweza ukataka kujadili uwezekano wa kuunda timu iliyoshikamana hivi karibuni.
- Wakati mwinguine unatakiwa uanze kazi mwenyewe, kama vile katika eneo mpya pasipokuwa hata mmoja anayeamin. Kama hii ni hali yako, unaweza kufaa kwenye mzunguko wa njie, lakini unatakiwa kuanza kupanga sasa jinsi utakavyofundisha waumini wapya na kuwasogezza kwenye hatua mapema iwezekanavyo. Hali yako ni mbali kutoka halisi, na inatia mashaka kwamba utafanikiwa sana katika upandaji kanisa mpya labda kama unaweza kuanza kutafuta watu kwa ajili ya mzunguko wa ndani.

#### Kielelezo 3.3 Mzunguko Wako wa Uongozi



- Kama una mashaka kuwa watu wangekuwa kwenye mzunguko wa 'juu', andika majina yao ambayo yanatengwa na mistari mingine. Hii itakukumbusha kutumia mda wa maana kuwatathimini watu hawa, na kuanzisha shughuli za kujifunzia kuona kama kweli ni waminifu. Kama unakuta kwamba siyo, unaweza kisha kuwaondoaa kutoka kwenye mzunguko huo.
- Usiwe na wasiwasi kuwa na watu wengi kwenye mzunguko wa ndani. Yesu aliweza kukazia wafuasi watatu tu—Petro, Yakobo na Yohana. Usiwe na mahangaiko kama huwezi kukamilisha zaidi kuliko Bwana. Kuwa na mwanafunzi kiongozi ni bora kuliko kutokuwa na hata mmoja. Na ni vizuri zaidi kuwa na mmoja tu na kumfundisha, kuliko kufundisha kadhaa kidhaifu.
- Kama huwezi ukafikiria hata mmoja ambaye anaweza kuwa katika mzunguko wa ndani, unatakiwa kuanza bila mzaha, maalumu, kwa mkazo kuomba kwamba Mungu atatoa viongozi kutoka ndani ya kanisa mpya.

Na sasa kwamba umejaza mzunguko wako, fikiria jinsi unavyotumia mda wako na nguvu. Kama una watu katika kila ngazi, unatakiwa uwe unakazania mda wako karibu na katikati. Unafanya hivyo? Ni mda gani mwininge zaidi unaotumia na hao walio kwenye mzunguko wa ndani kuliko wa nje? Ni aina gani ya shughuli unayofanya nao? Uhaendeleza uongozi kwa uangalifu na ujuzi wa huduma kwao?

Kwa kudhani kwamba unatumia mda wa kutosha na viongozi mashuhuri, mzunguko wa nje umeachwa? Hutakuwa na mda wa kutosha na nguvu kuwahudumia peke yako na bado uwaendeleze viongozi. Ni lazima kwamba unajifunza kugawa huduma kwa hao wanaofanya kazi nawe. Unatakiwa kuwa mwandaaji na mtu wa chanzo kwa hao wanaofanya huduma hiyo. Jinsi gani unafanya katika hilo?

#### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni mda gani itachukua kwa muumini mpya kuhama kwenye mizunguko kwenda mzunguko wa ndani? Hii itachukua mda gani kuanzisha kanisa. Huu ni mda unaokubalika?
- Jinsi gani ya juu kufundisha uongozi ni kipao mbele machoni pa wachungaji wengi katika eneo lako? Jinsi gani hili litasaidia au kukwamisha kukua kwa kanisa na upandaji wa makanisa mapya?

#### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Tumia kielelezo chako 3.3 kilichomalizika kuanzisha mpango kuwasaidia hao katika kila mzunguko kuendelea kama viongozi. Kisha kiujuzi tathimini mpango wako kuona kama inawezekana kwako kuuweka. Utakuwa na mda wa kutosha kutumia mzunguko wa 'ndani'? Kiasi gani? Mwingine atahudumia kwenye mzunguko wa 'nje'? nani? Lini? Jinsi gani? Fanya marekebisho yoyote yanayohitajika kwenye mpango wako, na kisha ujadili na mshauri wako. Kisha fanya.



# Utangulizi Kwenye Kazi ya Timu

## KUFANYA KAZI NA WENGINE

### ☞ **Kusudi la Somo**

Somo hili linaelezea jinsi kufanya kazi na wengine katika kupanda kanisa kunaweza kuongeza ufanisi wa mpanda kanisa kwa kujalizia uwezo wake.

### ☞ **Wazo Kuu**

- Kazi ya timu ina ufanisi kuliko kufanya peke yako.
- Kazi ya timu inahusisha kundi kufanya kazi pamoja kwenye kazi ya pamoja.

### ☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati somo hili linapoelewaka, kila mushiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa faida za kuhusisha wengine katika huduma kushinda kufanya peke yako.
- Kuelewa misingi ya kibiblia ya kazi ya timu
- Kujitoa kwenye kazi ya timu kwa ufanisi wa upandaji kanisa.

### ☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili kuhusu kazi ya timu linaendana na yote timu ya upandaji kanisa wa kawaida, na vile vile kwa vikundi visivyo vya kawaida zaidi vya waumini wanaofanya kazi pamoja kupanda kanisa mpya. Inaweza ikasaidia kuuliza kama kuna mmoja wa wafunzwa anafanya katika vikundi vya kawaida, na kisha kuamua ni timu ipi ya kazi inaweza kuwa ya kusaidia zaidi kukazia wafunzwa wako.

## **UTANGULIZI**

Kiongozi hasa wa kanisa anaweza kukuta kusanyiko lake likiranda randa bila madhumuni, hata akiwa na mwelekeo wake wazi. Anaweza kujambia, "Siwezi kufanya kusanyiko kusogea, hata kama natumia kila kipimo cha nguvu nilichonacho. Ninatakiwa kuwasukuma watu wakati wote kwamba tunakwenda sasa ili vitu kukaa vikiwa vimefanyika. Kama nikiacha kusukuma, kanisa letu kwa kifupi litalegea." Jinsi gani inasikitisha maneno haya kwa makanisa mengi. Mwelekeo wenye nguvu kutoka kwenye uongozi wenye nguvu unaekuwa, kwa miaka mingi umeongoza makusanyiko mengi kusinzia. Wanaanza kusogea wakati wanaposukumwa, na kufanya kwa kiwango walichoelekezwa kufanya (Imerithiwa kutoka kwa Kilinski, uk. 159, 160).

Kiongozi "anayefanya kazi peke yake", kama aliyelezewa hapo juu, anaamini njia pekee ya kuongoza ni kutumia muguso wa binafsi na uwezo wa kuvutia, kusukuma na kushawishi wengi. Kwa yule anayechukua njia hii, mafanikio ni pungufu kwenye idadi ya watu ambaa wanaweza kumuiga na kiwango cha uwezo wake binafsi na ubunifu.

### **I. NINI MAANA YA KAZI YA TIMU?**

Kazi ya Timu inahusu kufanya kazi pamoja na wengine kwenye kazi (kama vile kujenga kanisa), Badala ya kufanya peke yako. Kazi ya timu inahitaji kukubaliana juu ya-lengo ambalo kikundi kinalifanyia kazi kulikamilisha. Kwa kufanya kazi pamoja, wajumbe wa kikundi (au timu) wanatumia vipawa vinavyotofautiana vya kila mijumbe, vilevile na mda ulioongezeka na juhudhi ambazo kila mmoja anaweza kuchangia kwenye kazi.

Kazi ya timu inaweza kuchukua mfumo wa huduma ya kawaida ya timu, ikiwa na mkazo wa kuanzisha kanisa mpya. Katika hali hii, kikawaida kutakuwa na timu ya viongozi wanaokubalika, na pengine aina fulani ya mapatano ya kiofisi yanayotaja kazi na majukumu ya kila mjambe. Aina hii ya mpangilio ina faida nydingi. Nafasi zinazelezewa kiwaziwazi, hivyo hata lengo. Kawaida kuna utaratibu wenye nguvu wa kuwajibika ambao unamfanya kila mjambe wa timu kuchangia kwa ufanisi kwenye lengo la pamoja. Kwa jinsi hiyo, kazi ya timu haitakiwi ipungue kwa aina hiyo tu ya hali ya kawaida.

Kazi ya inahusu kufanya kazi pamoja na wengine kwenye kazi, badala ya kufanya peke yako.

Hata wakati 'timu' ya kawaida inapokuwa haipo, au wakati maswala ya kicutamaduni yanaporudisha nyuma kuanzishwa kwa timu, timu ya kazi inaweza na inatakiwa itumike. Karibu kila kazi ngumu ni rahisi wakati kikundi kikiifanyia kazi kwa pamoja. Hii hasa ni kweli wakati kazi inapokuwa kupanda kanisa jipya, ambapo masaa yasyiohesabika ya mtu yanapohitajika kuinjilisha, kufuasa, na kuadilisha wajumbe wa kanisa. Mtu mmoja anayearibu kazi hiyo kawaida anatoa njia ya kuchanganyikiwa na kuchoka, badala ya njia ya kuwafikia umati. Kazi ya timu ni njia nzuri.

Karibu kila kazi ngumu ni rahisi wakati kikundi kikiifanyia kazi kwa pamoja.

Hata vikundi visivyo vya kawaida vinavyofanya kazi pamoja kupanda kanisa vitafanya kazi kiulaini kama kuna mtu mmoja anayekubarika kama 'kiongozi'. Kwa matumaini, kiongozi huyo atakuwa anafanya kama kiongozi-mtumishi, anayewajenga wajumbe wengine, badala ya "kulundikia" kikundi. Somo hili linakazia kwa "kiongozi" na jinsi anavyoweza kuunda anga ambalo linakuza wajumbe. Kuna tabia mbalimbali zinazochangiwa na yote timu ya kazi ya kawaida na isiyo ya kawaida:

- Maono ya huduma (lengo) yanaonyeshwa na kikundi.
- Uamzi unafanywa na kikundi.
- Matatizo yanamilikiwa na kikundi.
- Wajumbe wa kikundi wote pamoja wanawajibika mmoja kwa mwengine.
- Kila mjambe anatumia uwezo wake kuchangia kwenye mafanikio ya ukamilishaji wa kazi.
- Mmoja anakubalika kama 'kiongozi'
- Kikundi kinakamilisha zaidi ya ambacho mmoja angefanya peke yake.

## II. MISINGI YA KIBIBLIA KWA KAZI YA TIMU

### A. Tuliumbwaa Kuwa 'Pamoja'

Mungu anawaita watoto wake kufanya kazi pamoja. Tunaiona kanuni hii mwanzoni kwenye Biblia kama uumbaji wenye. Mungu kwanza alimuumba Adamu lakini mapema alitangaza "Syo vizuri mtu awe peke yake." Kisha Mungu akamuumba Eva "wa kufaa" kuwa msaidizi mwenzi anayefaa kwake."

Solomoni, katika hekima yake yote, vilevile alielewa kwamba tunahitajiana.

*"Afadhalii kuwa wawili kuliko kuwa mmoja; maana wapata ijara njema kwa kazi yao.*

*Maana wakianguka mmoja wao atamwinua mwenzake; lakini ole wake aliye peke yake aangukapo, wala hana mwengine wa kumwinua! Tena wawili wakilala pamoja, hapo watapata moto; lakini mmoja aliye peke yake tu auezaje kuona moto? Hata ikiwa mtu aweza kumshinda yule aliye peke yake, wawili watampinga; wala kamba ya nyuzi tatu haikatiki upesi (Wimbo ulio Bora 4:9-12)*

### B. Viongozi Wanatakiwa Wasifanye Kazi Peke Yao

Musa alikuwa na majukumu makubwa kupita kiasi kama kiongozi wa Israeli wakisafiri kwenda nchi ya ahadi. Musa alikamilisha ya kutosha na alikuwa mwaminifu kama kiongozi, hata hivyo, kama tukiangalia makosa yake, tunatambua kwamba alifanya kazi peke yake sana. Tunamuona Yoshua mara chake na Aroni pembeni mwake, lakini mara kwa mara tunamuona Musa akifanya kama mtu mmoja anaye wajibika kwa umati. Kulikuwa na nyakati ambapo hili lilikuwa zaidi sana kwa Musa na aliondoka mwenyewe kuwa mwathirika wa watu (Kut 17:4); Hes 11:10-14).

Wakati Musa alipoungana tena na baba mkwe wake Yethro katika Kutoka 18, Tunaona kwamba Yethro alikuwa amechomwa na yote Mungu aliyofanya kuititia Musa (Kut 18:1-12). Lakini Yethro alipogundua kuwa Musa alikuwa mwamzi peke yake na kiongozi wa watu wote, mara alimwambia Musa kwamba alichokuwa anafanya "hakikuwa kizuri." Musa kwa kadiri iwezekanavyo alidhani kuwa kuwatumikia watu peke yake kwa njia hii ilikuwa inasitahiki. Lakini alihitaji msaada kuangaza kiasi cha kazi na kuhakikisha kwamba kazi ilikuwa imefanyika kikamilifu. Kwa hiyo Yethro aliunda mpango ambao Musa angechangia majukumu haya na wengine (Kut 18:17-26). Badaye katika hali inayofanana, Wakati Musa alipokuwa amechukia juu ya kuasi kwa watu, Mungu aliona kwamba Musa alihitaji msaada na akaanzisha wazee 70 wa kusaidia 'kuchukua mzigo' (Hes 11:16-17).

Musa akiwatumikia  
watu akiwa peke yake  
"haikuwa vizuri."

### C. Kufanya Kazi Pamoja ni Kipande cha Kawaida katia Huduma ya Agano Jipyä

Tunaona timu ya kazi tena katika mawazo tofauti tofauti. Yesu aliwaita wanafunzi na kufanya nao kazi kama timu. Wakati Yesu alipowatambulisha kwenye huduma, alizidisha juhudzi zao kwa kuwapeleka nje 'wawili kwa wawili' (Mk 6:7; Lk 10:1). Petro alikwenda na wakristo wengine kuinjilisha Kaisaria (Mdo 10:23). Roho Mtakatifu alimtenga Paulo na Barnabas kama timu ya kwanza ya kimishenari (Mdo 13:2). Baada ya safari ya kwanza ya kimishenari, timu iliongezeka kuwa mara mbili (Mdo 15:36-41). Paulo alikuwa na mlango wazi kwa ajili ya huduma, hata hivyo alijitoa kutochukua nafasi kwa sababu alikuwa peke yake mda huo (2Kor 2:12-13). Wakati viongozi walipoteuliwa katika kanisa la kwanza, kikawaida kundi la wazee walichaguliwa kuongoza kila kanisa (Mdo 14:23).

Sababu ya Msisitizo wa kibiblia wa kazi ya timu ni dhahiri: Katika uzidishaji wa washauri kuna hekima kubwa (Mit 15:22), na hakuna mtu mmoja aliye na vipawa vyote (Efe 4, 1Kor 12). Tunahitajiana. Huduma leo inatakiwa ifaidike kutoka katika kazi ya timu. Watu wachache kama 2-5 wanaofanya kazi pamoja kwa kishindo inaweza kuongeza ukuaji wa kanisa jipyä. Katika kupanda kwako kanisa, angalia hao wanaonekana kuwa na maono kama yako, na waombe kucombea juu ya kuijunga nawe kwenye huduma.

Timu ya kazi ghafla  
inaweza kuongeza  
ukuaji wa kanisa jipyä.

## III. TABIA ZA KAZI YA TIMU YENYE UFANISI

### A. Maono ya Wote na Kuielewa Kazi

Kundi la watu haliwezi kwenda pamoja kama haliendi kwenye mwelekeo mmoja. Kazi ya timu inahitaji kwamba kila mjjumbe kujua lengo ambalo kundi linalifanya kazi. Baadhi ya timu za kawaida wana maelezo ya kusudi, ambayo katika sentensi moja yanaelezea kwa nini wanafanya kazi pamoja. Katika zingine, maelezo ya kusudi la kanisa inanweza kuwa maono ya wote ambayo yanaifanya timu ya upandaji kanisa kufanya kazi pamoja.

Kama hujachukua mda kujadili na kukubaliana juu ya lengo na hao unaofanya nao kazi, fanya hivyo upesi iwezekanavyo. Utaratibu huu wenyewe unaweza kuwa uzoefu wenyewe thamani sana. Mnapoongelea juu ya kusudi la kikundi chenu, shauku ya mtu, haja na mapendeleo ya kila mjjumbe yanaweza kuwa ya uwazi. Haja hizi vinginevyo zisingejulikana. Kama shauku na haja ya kipekee ya wajumbe wa timu vinajulikana, fikiria jinsi vinavyoweza kushirikishwa kwenye maono kwa ujumla. Mara kwa mara utakuta kwamba Mungu ameleta pamoja "mchanganyiko" sawa wa vipawa na uwezo ili kuwawezesha kukamilisha kazi.

Shirikisha shauku na haja  
za wajumbe wa kikundi  
katika maono kwa ujumla.

Kwa jinsi hiyo, wakati watu wanapofanya kazi pamoja wana njia inayotofautiana na lengo linalopingana, kufanya kazi pamoja siyo rahisi mara nyangi. Katika hali kama hii, wajumbe wanatakiwa waachie haja fulani, au waunde kikundi tofauti, kama Paulo na Barnabas walivyofanya katika Matendo 15:36-41.

Fanya marudio ya Lengo lenu moja mara kwa mara na kikundi chako. Usidhani kuwa kila mjjumbe anaelielewa.(au kulikumbuka!), ili kwamba lirudiwe tena.

Hapa ni baadhi ya maelezo ya kusudi:

- Timu yetu ipo kwa ajili ya upandaji kanisa hai na linaloongezeka \_\_\_\_\_.

- Kundi letu lipo kuhudumu kwa walevi katika\_\_\_\_\_ katika namna kwamba wapate wokovu kutoka dhambini mwao na uhuru kutoka kwenye uzoevu wao.
- Tunafanya kazi pamoja kuwezesha kuzaliwa na maendeleo ya harakati za kueneza upandaji kanisa katika\_\_\_\_\_.
- Kundi letu lipo kupanga na kuongoza ibada yeny<sup>e</sup> kuleta maana wakati waumini wanapokusanyika katika\_\_\_\_\_.

#### **B. Mda Uliotumika Kwa Pamoja Kuomba na Kupanga**

Kushiriki kwa kikundi cha wajumbe ni kwa thamani wakati watu wanapojuia kinachotokea na kwa utoshelevu kuweza kuwasilisha maoni yao. Hili linaweza kukamilika kwa kukutana pamoja kila wiki (au mara nyingi zaidi) na kufanya mambo yafuatayo:

##### **1. Kuomba Pamoja**

Hakuna kitu kinachowaunganisha watu pamoja katika umoja kama maombi yaliivyo. Wapanda kanisa wanaofanikiwa na vikundi vya upandaji kanisa wanajitoa kwenye maombi. Wanaomba kwa pamoja kwa ajili ya mahitaji binafsi, lengo la huduma na pia walipotea amba<sup>o</sup> wamewasiliana nao.

##### **2. Kujadili Huduma Binafsi**

Timu ya kazi inahitaji kuchukua mda kusikiliza anachofanya mjumbe pekee. Kusikia upya jinsi wajumbe wengine wanavyochangia kunaweza kusaidia kikundi kukua kwa karibu, kujenga moyo na kufundisha ujuzi wa huduma.

##### **3. Pang<sup>a</sup> Pamoja**

Kupanga pamoja kunaweza kuwa uzoefu weny<sup>e</sup> thamani. Baadhi ya viongozi wanafanya mipango na kisha kuwaambia kikundi wanachotakiwa kufanya. Wakati wajumbe wanapokuwa hawana uzoefu au hawajakomaa, wanaweza kuhitaji kiongozi kufanya hilo kwa mda. Lakini mara kwa mara zaidi, kiongozi anatakiwa kuwashirikisha hao anaofanya nao kazi katika utaratibu wa kupanga. Watu wanajitoa zaidi kwenye vitu ambavyo wenywewe wameshawahi kuhusika katika kuanzisha.

Kiongozi anatakiwa kuwashirikisha hao anaofanya nao kazi katika utaratibu wa kupanga.

Kupanga kunakuza uwezekano wa timu ya kazi. Upangaji huu unaweza kuhusisha: 1) kuangalia kazi ya wote, 2) kuonyesha nini kikundi kinahitaji ili kuweza kulifiki lengo lake 3) kufahamu rasilimali za huduma 4) kuendeleza mikakati ya kufikia lengo.

##### **4. Kuadilisha na Kuandaa (kadiri Inavyohitajika)**

Kiongozi mzuri atawezesha maendeleo ya ujuzi wa huduma wa kila mjumbe kama kikundi chake. Ataweka mda wa kuwasaidia ili kuwa wafanisi zaidi katika kuhubiri, kuinjilisha, au kutunza wagonjwa. Kufanya marudio ya huduma iliyopita karibuni inaweza kutoa mda wa kuweza kufundishika wakati mtu fulani anapokuwa tayari kujifunza.

Kama kundi unaloongoza halina mikutano ya mara moja moja, kisha fikiria kuanzisha kulingana na mfano wa mtindo hapo juu.

#### **C. Mahusiano Yeny<sup>e</sup> Tabia ya Upendo**

Timu ya kazi wanakubali utayari wa kupatana na kufanya kazi pamoja. Wajumbe wa kikundi wanahitaji kuwa na utayari wa kuwa wazi kuhusu wao wenywewe. Kwa hiyo, kuheshimiana wao kwa wao, kuelewa, na kutiana moyo na msisitizo wa kutumikiana ni ufunguo asili kwenye kazi ya timu

Wajumbe wa kikundi wanahitaji kuwa na utayari wa kuwa wazi kuhusu wao wenywewe.

Ili kuweza kupata aina hii ya ukaribu, uhusiano mionganoni mwa wajumbe wa kikundi unatakiwa utokane na aina maalumu ya upendo—upendo wa Mungu. Upendo huu haumpendi mwinge kwa sababu ya utu wake, muonekano, uwezo au ufahamu. Unachangiwa na upendo wa Mungu usio na mwisho na usio na mashariti kwetu. Tunapotumia aina hii ya upendo tunatiana moyo na kujengana kama Paulo anavyosema kwa Wathesalonike (1The 5:11). Yesu Kristo ni mfano kwa kiongozi anayetaka kujifunza “Kuwafikiria wengine zaidi kuliko wanavyojiona” (Flp 2:1-8).

Moja ya jaribio la upendo ni jinsi ya kuchukulia migogoro. Migogoro ni ya kawaida, lakini kunapokuwepo kutokupatana, kunatakiwa kuwe na kukubaliana na kujadiliana. Makundi yanayopendana yana ujasiri wa kujadili hata vitu ambavyo hawakubaliani. Wanatambua kuwa kila mjudumbe ni muhimu kwenye kikundi na hataruhusu kutokubaliana kuvunja mahusiano yao.

#### D. Majukumu Wazi na Utofauti

Watu wengi kwenye huduma wanawaangalia watu kama wao wenyele wa kuungana nao katika upandaji kanisa. Hili ni kosa kubwa, na linadharau ukweli kwamba tu mwili wa Kristo wenye viungo vingi, na vipawa vingi tofauti (1Kor12:12-31). Watu mbalimbali wanaweza kukamilisha zaidi kazi inayotatanisha. Kwa mfano, kikundi kinachopanda kanisa jipya kwa pamoja kinaweza kuhitaji watu wanaowajibika kwa yafuatayo:

Watu mbalimbali  
wanaweza  
kukamilisha zaidi  
kazi inayotatanisha.

- Uinjilisti
- Ufuasishaji
- Kuabudu
- Fedha,misaada
- Kuwafanya wajumbe kitu kimoja
- Huduma ya kikundi kiini
- Mafunzo ya huduma
- Kuwatunza wagojwa
- Ukarimu

Timu ya kazi inataka kwamba wajumbe wanafahamiana uwezo wa kila mmoja. Kama wajumbe hawajui nani anayewajibika katika eneo fulani, kisha kiwango cha kuchanganyikiwa kinaelekeea kupanda, na huduma itaumia. Kama hakuna mmoja anayesimamia kuabudu, kikundi kinaweza kujikuta kikitambaa kwenye kila mda wa kuabudu, kwa kuwa kunakuwa hakuna anayejua mpango wa ibada. Kunapokuwa hakuna mmoja anayesimamia fedha, wajumbe wanaweza wasiwe na fungu la kutosha kununulia maandishi ya kiuinjilisti yanapokuwa yanahitajika.

Kazi ya timu inakuwa ya mafanikio zaidi wakati kila mjudumbe anapojuwa majukumu yake na kuwekwa katika hali ambayo imejengwa kwenye uwezo wake. Wakati hili linapotoka, matokeo ya juhudhi za kikundi zinaongezeka, kwa sababu kila mjudumbe anafanya kazi kwa kiwango chao kinachowezekana. Jukumu la msingi la kiongozi wa kikundi ni kuona kwamba hili linatokea.

Kazi ya timu inakuwa ya mafanikio zaidi wakati kila mjudumbe anapowe kwa katika hali ambayo imejengwa kwenye uwezo wake.

#### E. Ukweli na Mawasiliano ya Uwazi Kati ya Wajumbe

Kizuizi kikubwa kwenye mawasiliano mazuri ni mazoea ya kutathimini na kuhukumu bila kusikiliza hasa. Wakati kikundi kinapokuwa kinashiriki kazi ya timu, wanatafuta kuwaelewa wengine kabla ya kutoa ushauri au kushirikisha maoni yao. Aina hii ya mawasiliano inaonyesha upendo na heshima kwa mtu mwingine.

Aina hii ya mawasiliano inatokea tu tunapochukua mda kuelewa matatizo kabla ya kutoa suluhu. Moja ya utawala wa kidole gumba mara nydingi ni kuelezea tena matatizo au maoni ya mwingine kabla ya kujibu. Kuelezea tena kunatoa nafasi ya matokeo na masahihisho. Inaonyesha pia kuelewana na heshima.

Wakati matatizo ya mawasiliano yanapotokea mionganoni mwa wajumbe wa kikundi chako, kumbuka yafuatayo:

- Uliza maswali kuweka wazi mawazo, hisia au maoni ya wengine.
- Kutambua na kukubali mahitaji yako binafsi, orodha ya mambo unayotaka kufanya na kusudio.
- Kutunza kukubaliwa kusiko na mashariti hata unapokuwa hukubaliani.

Kama migogoro ni ya mtu na mtu, kumbuka,:

- Kuongea na waliohusika pekee kwenye hali au swala (Mt 18:15).
- Usijiingize kwenye maneno au masingizio (2Kor 12:20).
- Angalia maneno yako (Yak 2:1-12).
- Bariki, na usilaani (Rum 12:14).

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni faida gani zipo kwa wapanda kanisa kufanya kazi pamoja na wengine, badala ya kufanya peke yako? Ni nini Baadhi ya hasara za njia hii?
- Kazi ya timu inahitaji maoni ya pamoja. Ni mambo gani matatu unaweza kufanya kama kiongozi kusaidia hao wanafanya kazi na wewe kuunda na kukumbuka maoni ya pamoja?
- Wakati mwengine mikutano inaonekana kama kitu cha “kutia uvivu” na “kupoteza mda.” Ni aina gani ya mikutano inaweza kuwa ya kupoteza mda, na ni mikutano ipi inaweza kuwa ya faida kwenye kundi linalofanya kazi pamoja kupanda kanisa?
- Katika mandhali yako maalumu, ni majukumu yapi ni muhimu kuanzisha kanisa jipya (mf. Mwinjilisti, mfuasishaji, n.k.)? Ni muhimu kuwa na majukumu yote kuwepo kabla hujaanzisha kanisa?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Orodhesha kazi nne za ufunguo zitakazokamilishwa katika kazi yako ya upandaji kanisa. Fikiria kwa nani unaweza kukabidhi majukumu kwa kila kazi, kulingana na vipawa walivyonyavyo na uwezo wa waumini wengine ambao wanaweza kuwa wako tayari kusaidia. Kisha amua jinsi unavyoweza kuandaa na kumfundisha mtu kwa kazi hiyo. Kisha ifanye.

### **VYANZO**

- Engel, James F., Jane Overstreet, and Terry Sparks. *Leadership: Making Human Strength Productive*. St. Davids, PA: *The Center For Organizational Excellence*, Eastern College, 1996.
- Kilinski, Kenneth K., and Jerry C. Wofford. *Organization and Leadership in the Local Church*. Grand Rapids: Zondervan, 1973.
- Robinson, Martin and David Spriggs. *Church Planting, The Training Manual*. Oxford, England: Lynx Communications, 1995.



## Maendeleo ya Timu

- ☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuelezea jinsi kiongozi wa kikristo anavyoweza kuunda timu ya upandaji kanisa na kuendeleza tabia na uwezo wa wajumbe.
- ☞ **Wazo Kuu**
  - Ufunguo wa kuanza kwa timu ni kujitoa kwenye kazi ya pamoja, kama vile upandaji kanisa mpya.
  - Jukumu la kwanza la kiongozi ni kuendeleza silika na uwezo wa timu.
  - Kazi ya timu haitoeki tu—inapitia hatua nne.
- ☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

  - Kujua hatua za msingi za kuanzisha timu ya upandaji kanisa.
  - Kuelewa kwamba nafasi ya kiongozi wa timu ni kuendeleza tabia na ujuzi wa kila mjumbe.
- ☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Ingawa nyenzo ya somo hili inahusika na kuwaendeleza wajumbe wa timu ya upandaji kanisa, inatumika na kwa kiongozi wa kikundi kiini, ambaye pia lazima ajitahidi kuendeleza wajumbe wake wa kikundi kiini katika njia zinazofanana. Ni ya thamani pia kwa mchungaji anayetafuta kuwaendeleza wajumbe na viongozi wengine katika kanisa lake.

### UTANGULIZI

Faida za upandaji kanisa kama kikundi zimejadiliwa katika masomo yaliyopita. Pengine umeshakuwa na kundi. Labda huna, lakini ungependa kuwa na moja. Unaweza kuwa hujaaamua na ungependa kujua zaidi jinsi timu itakavyofanya kazi. Somo hili linasaidia kugusa maswala hayo.

Katika njia nyingi, mafanikio ya timu ya upandaji kanisa yanaunganishwa kwa kiongozi. Mara kwa mara, ni wajibu wa kiongozi kuwaandaa wajumbe wa timu. Na wakati timu ya upandaji kanisa inatakiwa ifanye kazi pamoja kufanya maamuzi juu ya maono, kazi na kusudi, lazima bado kuwe na mtu mmoja, kiongozi, ambaye anawajibika kuwasaidia kujitahidi kwenye maono yao na kufikia malengo waliyoyaweka. Somo hili linajitwalia kuwa wewe ni mtu huyo ambaye ataunda na kuongoza timu katika mafanikio ya upandaji kanisa.

### I. KUUNDA TIMU YAKO

Hata kama umeshakuwa na kundi la watu wanaofanya kazi na wewe kupanda kanisa jipya, unaweza au usiweze kuwa na timu. Mengi yameandikwa juu ya nafasi ya timu. Pia kuna kiasi cha utafiti cha ajabu juu ya jinsi ya kuongoza timu. Mengi ya utafiti huu ni ya kiserikali, na wakati huo yakitoa mawazo yanayosaidia, hayatosherezi kwenye timu nzuri ya upandaji kanisa. Unapokusanya timu kwenye kazi ya kiroho ya upandaji kanisa, utahitaji kutafuta mmoja mmoja mweye tabia tatu za msingi:

- Mwenye kujitoa kwenye lengo la upandaji kanisa.
- Mwenye tabia ya kimungu.
- Makubaliano ya kukuza uwezo na kwa nafasi wazi.

Inapendeza, lakini siyo lazima, kwamba uwezekano wa wajumbe wa timu wana sifa zote hizi. Kama wanakosa baadhi ya dalili, wanaweza kukua kwenye maeneo hayo wakati wa utaratibu wa upandaji kanisa. Nafasi yako kama kiongozi itakuwa ya maana katika hali hizi. Unahitaji kufahamu udhaifu na kutia moyo ukuaji wa mara kwa mara. Kama unafanikiwa, timu yako inaweza kuwa mfano kwa ukweli kwamba waumini wote wanakua na kukomaa—hakuna mmoja wetu aliye mkamilifu. Hii inaweza kuwafanya wajumbe wa timu kuweza kuwa makini kwenye mawasiliano mapya ambayo utatafuta kuyashinda.

Kwa upande mwingine, upandaji kanisa mpya ni shughuli isiyu ya mzaha. Kunaweza kukawa hakuna mda au nguvu za kutosha kuchambua kujua udhaifu kwenye timu mnapokuwa mnafanya kazi kuwainjilisha waliopotea na kuwafanya wanafunzi. Yesu hakuchukua watu kamili kama wanafunzi wake, lakini pia alitumia miaka mitatu na nusu akibadili maisha yao kabla hawajawa tayari. Ni mda kiasi gani unao? Kuwepo kwa wajumbe ambao hawajakomaa kwenye timu kunaweza kukaleta madhara makubwa kwa kufanya matendo yasiyo ya kimungu au tabia. Kwa hiyo, utahitaji kutathimini yote uwezo na udhaifu wa kila mjumbe aliyepo kwa uangalifu na kwa maombi kabla ya kufanya uamzi.

Kama bado unaunda timu, tathimini hali hizi katika kila mjumbe aliyeko kwa uangalifu. Kama umeshakuwa na timu ambayo ni pamoja na wajumbe ambao ni dhaifu katika sifa tatu zilizoorodheshwa, unatakiwa kuifanya kipao mbele kwa kuanza kuwasaidia kuweza kuushinda udhaifu. Kushindwa hili, utahitaji kufikiria kuwaauliza kuiacha timu.

#### A. Kujitoa Kwenye Lengo la Upandaji Kanisa

Umuhimu wa lengo la pamoja linaweza kuwa gumu kulieleza. Hili linaonekana kuwa na maana. Katika ulimwengu wa michezo, kwa mfano, timu ‘inayofanikiwa’mara nyinyi ina watu ambao siyo lazima wawe wanaelekeana katika hali zingine zote. Kwa hakika, wanaweza hata wasipendane. Lakini kujitoa kwa nguvu kwenye lengo la kushinda mchezo kunaweza kukawasaidia kushinda tofauti zao na kufanya kazi/kucheza pamoja.

Kama kundi la wasioamini wanaweza kuonyesha ushirikiano huo na kujitoa kwa ajili ya mpira, inaweza ikawa kwa ukubwa kiasi gani matokeo yake ya juhudu za upandaji kanisa? kama kila mjumbe wa timu yako ya upandaji kanisa anatunza kujitoa kwa nguvu na kwa maana kuona kanisa limepandwa, kutakuwa na kuelewana zaidi na uhuru katika uhusiano wao wa huduma. Kujitoa huku kwa nguvu kunaweza kukawa kumeshakuwepo, au unaweza kuwasaidia kuanzisha maono hayo. Njia yoyote, utawasaidia pia kuendelea kutunza kujitoa.

#### B. Tabia ya Kimungu

Fikiria kwa mda wanafunzi Yesu aliowachagua. Hawakuwa wameelimika au kundi lenye’kuweza’. Yesu kwa kuonekana aliangalia sifa zingine. Unatakiwa ufanye sawa. Nini ziliikuwa ni sifa? Wakati gani wanafunzi walipokabiliwa na kuchagua watu wa kuwasaidia, waliangalia watu “waliojaa Roho Mtakatifu na wenye hekima” (Mdo 6:3). Wazi wazi hawakujali juu ya elimu, umri, uwezo, uzoefu, au tabia zingine ambazo tunaweza kudhani kuwa muhimu. Badala yake, walithamini tabia ya kimungu.

Paulo alimwambia Timotheo kuchagua watu “waaminifu” (GK. *Pistos*)<sup>2</sup> (2Tim 2:2). Katika mstari huo huo, anasema “wataweza” kuwafundisha wengine. Neno “weza” au “uwezo” ni tafsiri ya neno la Kigiriki *ikanos*<sup>3</sup>. tafsiri hii imepelekea baadhi kusisitizia elimu au uwezo, kinyume na Matendo 6. Mafunzo ya matumizi ya *ikanos* inaonyesha kwamba tafsiri nzuri ingekuwa “kustahili.” Fikiria juu ya neno sawa katika Matendo 3:11—“Ambaye sifai kuvichukua viatu vyake (*ikanos*).” Unadhani kuwa Yohana hakuwa “anaweza” kubeba viatu, au “hakustahili?” Katika Mathayo, *ikanos* imetafsiriwa kama “kustahili.”

Hii ina maana kwamba Paulo anakubaliana na mitume kwamba tabia ya Kimungu ndilo swala la muhimu zaidi. Bila tabia ya kimungu, “hatufai” kumtumikia Bwana. Inatakiwa iwe hadhi ya msingi ambayo unayoiangalia kwa wajumbe wa timu. Mungu atabariki uchaguzi kama huo. Hata kama wajumbe wa timu yako ni wanaume, wanawake, au wote, kanuni ile ile ya kibiblia itaonekana kufaa. Hii haimanishi kwamba mafundisho, uwezo, au uzoefu hauna thamani. Lakini haya ni ya juu kwa maisha ya kimungu yaliyojawa na Roho.

Tabia ya kimungu ndilo  
swala la muhimu zaidi.


### C. Mapatano ya Kukuza Uwezo kuitia Majukumu Wazi

Timu ya upandaji kanisa inatakiwa iwakirishe kanisa inalotaka kupanda. Mtindo wa kibiblia ni mwili, katika mapana yake kufanya kazi pamoja katika umoja (1Kor 12). Kivuli hiki cha mwili kinaleza faida ya wajumbe tofauti wa timu wenye uwezo wa kukamilisha vipawa vya kiroho. Timu nzuri ya upandaji kanisa itakuwa na mapana haya. Kunaweza kukawa na mwinjilisti, mshauri, mchungaji, mwali muo, mmoja wa kuonyesha rehema, n.k. Kila kimoja ni muhimu. Kunaweza pia kukawa na mapana ya jinsia, umri, na hadhi. Uwiano hasa utategemeana na hitaji la hali yako na wajumbe waliopo. Tazama mapana kama faida badala ya udhaifu.

Kama vile mwili, mapana haya yana thamani tu yanapoelekezwa kwenye lengo la wote. Lazima yawe na kichwa. Katika njia sawa, timu lazima iwe na kichwa, au kiongozi—pengine wewe. Msisitizo ni juu ya kuwaelekeza wajumbe kwenye huduma, badala ya “kuwalundikia wao.” Huu ‘ukichwa’ unatakiwa uwe wa *kiutendaji badala ya kinafasi*. Hakikisha timu inakubaliana kuongozwa.

## II. KUONGOZA TIMU YAKO

Majukumu maalumu ya kiongozi yatahusiana na kusudi la timu anayoiongoza. Makusudi yafuatayo yanaonyesha majukumu ya kiongozi katika mandhali ya kuanzisha kanisa mpya. Unapokuwa unaongoza timu yako, kazania kufanya kila moja ya shughuli zifuatazo.



### A. Endeleta Uhushiano wa Wajumbe wa Timu Yako na Mungu

Uwe mchungaji kwenye timu yako. Toa msaada wa kiroho wanapokuwa katika mahitaji kiroho. Hii inaonyesha kwamba unamjua kila mjumbe wa timu vya kutosha kujua lini wanapokuwa na mahitaji ya kiroho. Tumia mda pamoja nao, na usiogope kuwa uliza “maswali magamu” juu ya kutembea kwao na Bwana na mahangaiko wanayoweza kuwa nayo.

Afya ya kiroho na ukuaji wa kila mjumbe wa timu yako moja kwa moja utaelekezwa kwenye kuelewa kwao kwa neno la Mungu na uwezo wao wa kuweka ukweli wa kibiblia katika matendo kwenye huduma na katika maisha yao ya kila siku. Ombea afya yao ya kiroho na kukua. Kama hawajawahi kuwa na moja tayari, wasaidie wajumbe wa timu kuendeleza malezi binafsi ya kujifunza Biblia na maombi. Omba kwamba watagundua na kuendeleza vipawa vyao vya kiroho, na kisha bila kuchelewa kutazama njia za kuwapa nafasi za kufanya hivyo.

### B. Endeleta Uhushiano wa Wajumbe wa Timu Yako na Wao kwa Wao

Kazi ya timu inahitaji kwamba wajumbe wa timu wanaelewana na kuaminiana. Kama kuna matatizo ya kimahusiano katika timu yako, huduma itaugua. Utahitaji kusaidia wajumbe wa timu kuendeleza na kutegemea uaminifu na upendo kwa mmoja kwa mwengine. Weka malego yafuatayo kichwani unapokuwa unafanya haya.

Kama kuna matatizo ya kimahusiano katika timu yako, huduma itaugua.

- Kuwasaidia wajumbe wa timu kujua vishawishi vyao.
- Kuwasaidia wajumbe wa timu kujua uwezo wao wa mahusiano na udhaifu.
- Kuwasaidia wajumbe wa timu kuendeleza tabia bayana kwenye tofauti zao.
- Kugundua maeneo yenye wasiwasi wa kimahusiano.

#### C. Kuendeleza Maono ya Wajumbe wa Timu Kwenye Huduma

Hali nyingi za upandaji kanisa ni ngumu. Katika hali hizi, timu yako inahitaji kuona maendeleo vinginevyo watakatishwa tamaa. Hii hasa ni kweli kwenye hatua za mwanzoni, wakati msingi unapokuwa umewekwa, na baadaye kidogo, kunapokuwa kuna waliokata shauri wachache. Kiongozi anapokuwa anaangalia njia za kuwasaidia kuona picha kubwa, maono (Z!), ili kwamba waweze kuvutiwa kujitoa zaidi kwenye kazi (Gal 6:9).

Usidhani tu kwamba maono ya malengo yameeleweka na kila mjambe wa timu. Watu katika timu nyingi wanapoteza mwelekeo wa maono kama hawakumbushwi mara kwa mara na kiongozi. Weka maono mbele, na kila inapowezekana tia changamoto timu kufikiri zaidi kidogo, ili kwamba wasijikute wanatosheka na kidogo kuliko Mungu anachokusudia kwa ajili yao.

#### D. Endeleva Ujuzi wa Wajumbe wa Timu Yako

Watu wengi wanaepuka huduma kama hawana ujuzi unaohitajika kuifanya kazi. Watu wengi hawainjilishi au kujifunza Biblia kwa sababu wanajisikia kana kwamba hawajui jinsi gani wafanye. Uwe tayari kuchukua mda kukuza ujuzi wa huduma ambaa timu yako itahitaji kupanda kanisa mpya. Fanyia mazoezi njia ya kujifunza Bublia kwa kufata neno pamoja. Zungumzia juu ya na onyesha njia kadhaa tofauti za kuendeleza uinjilisti.

Uwe tayari kuchukua mda kukuza ujuzi wa huduma wa hao wanaofanya kazi na wewe kupanda kanisa mpya.

Unapowafundisha watu kwa ajili ya huduma, usidhani tu mfano mzuri na maelekezo kwa ujumla yanatosha. Baadhi ya watu wanahitaji mawasiliano ya moja kwa moja na ya binafsi (1The 5:14). Unapokuwa unafundisha ujuzi wa huduma kumbuka yafuatayo:

##### 1. *Andaa moyo wako na akili kabla ya kushauri*

Tumia mda katika maombi, ukimuuiliza Mungu kukupa hekima katika kufanya kazi pengine na timu yote, au na mjambe mmoja. Weka pamoja mpango imara wa ujuzi gani unaotaka kufundisha, na njia tofauti ambazo unazoweza kufanya hili. Fikiria ni mini kilikuwa msaada kwako ulipojua mara ya kwanza jinsi ya kufanya aina ya huduma tofauti.

##### 2. *Angalia nyakati za kufundishika (Mit 25:11 "Neno linenwalo wakati wa kufaa")*

Wakati wa kuelekeza ni wakati:

- Watu hawatishiki.
- Huna hasira ua kuchanganyikiwa.
- Mtu mwingine anatambua hitaji lake la msaada au kusaidiwa.

### III. KUIELEWA TIMU YAKO

Timu yako haitawenza mara moja au ghafla kufanya kazi kwa njia unayopenda. Kila timu inapitia katika utaratibu wa kukua na kukomaa. Mchoro katika jedwali 5.2 unaelezea hatua nne za kawaida ambazo kawaida timu inapitia inapokuwa na kukomaa pamoja. Ni lazima kwa kiongozi kuweza kutambua wapi timu yake ilipo kufuatana na uongozi, mahusiano, majukumu, uhuru, mawasiliano na maisha ya kiroho. Kila moja ya maeneo haya yanawakilisha kipengele muhimu cha afya na ukomavu kwa ujumla wa timu ya upandaji kanisa.

**Jedwali 5.2 Hatua Nne za Maendeleo ya Timu**

	<b>1. TIMU AMBAYO HAIJAKOMAA <i>Kiongozi-anayejijali</i></b>	<b>2. TIMU CHANGA <i>Watu-wanaojijali</i></b>	<b>3. TIMU INAYOJIFUNZA <i>Utaratubu wa-ubinasi</i></b>	<b>4. TIMU INAYOKUA <i>Kusudi la -ubinasi</i></b>
<b>Uongozi</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Viongozi wanafanya mengi ya maamuzi</li> <li>• Mtindo wa (kutoa) maelekezo</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Maamuzi bado yanafanya na viongozi laskini mchango unatolewa, uchaguzi mwangi unafikiriwa</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ushiriki unakuwa mwangi zaidi kadiri wajumbe wanavyofanya kazi kuelekea kwenye kusudi.</li> <li>• Maamuzi yanafanya na timu kwa kufaa na kwa ufanisi</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kiongozi ana uhuru katika mtindo, unaoendana na kwenye hali</li> <li>• Baadhi ya uongozi unavutwa na –kazi, kwa hiyo hao wenye ujuzi wanajitwalia nafasi za uongozi wa mda</li> <li>• Kazi zinagawiwa</li> </ul>
<b>Kusudi la pamoja</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Hakuna kuelewa kunakochangwa kwa nini kinahitaji kufanyika</li> <li>• Kusudi lililochanganya</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Timu bado inakosa umoja wa kusudi lakini wanakuwa na ufahamu wa ukosefu</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kusudi linajadiliwa na kuwekwa wazi kwenye akili ya wajumbe wa timu</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ufanisi unakuwa ndiyo mtazamo</li> <li>• Maendeleo yanakuwa ya kufungamana</li> <li>• Kuweka kwa undani</li> </ul>
<b>Mahusiano</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuelewa kidogo au kutowaelewa wengine...uwezo wao, udhaifu, n.k.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mkazo unakuwa ni kwenye kutaka kuwajua na kuwaelewa wengine, uwezo wao, udhaifu wao n.k.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Upendo na utii mionganini mwa wajumbe unakua</li> <li>• Wajumbe wamekuwa si wapinzani kidogo na wazi zaidi kwenye kuchangia</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kiburi kwenye uanachama</li> <li>• Udhafi unakubalika na kuhesabika</li> <li>• Kujitoa kuwasaidia wengine kufikia kiwango chao cha juu</li> </ul>
<b>Majukumu yaliyowekwa wazi</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuelezeka-vizuri kwa misingi ya mmoja mmoja</li> <li>• Haijawa wazi jinsi nafasi zinavyofaa na majukumu</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuoanisha uwezo na hali kumejadiliwa lakini machache yamefanyika</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Majukumu yanawekwa wazi—uwezo uanaoishwa kwenye hali</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mgawanyo wa kazi ni dhahiri lakini kwa fikira za kazi yote</li> </ul>
<b>Taratibu za kunyumbulika</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Sheria, jinsi na utaratibu uliowekwa kutoka juu au kutoka nje</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Matatizo yanakabilwa zaidi kwa uwazi</li> <li>• Maswala ya hatari yanajadiliwa</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Timu inapeleleza njia tofauti na njia za kupochezana</li> <li>• Mkazo ni kwenye mafanikio</li> <li>• Kuna mapana juu ya jinsi mambo yatakavyofanyika</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Uanzilishi binafsi unatiwa moyo</li> <li>• Uhuru unageuka kuwa sauti kwa yote mikakati na njia</li> </ul>
<b>Mawasiliano</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ufanisi kidogo wa mawasiliano</li> <li>• Upinzani</li> <li>• Makosa yanafunikwa</li> <li>• Kujifikiria mwenyewe</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mawasiliano ni wazi kidogo na ya ufanisi</li> <li>• Kujifikiria mwenyewe</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Uwazi, kazi-kuendana</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mawasiliano yanatabia ya kuamini, uwazi, uaminifu, ushirikiano na kukabili</li> </ul>
<b>Nguvu ya Maisha ya Kiroho</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Maombi ni desturi</li> <li>• Kutembea kwa imani hakumilikiwa kama usoefu wa timu</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Timu inakutana kila mara kuombea mahitaji ya pamoja</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mahusiano yanayohusu mtu yanapimwa dhidi ya maandiko</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Maombi ni kitu cha kawaida, mwitikio wa kwanza kwenye tatizo jipya</li> <li>• Imani ya utiifu inavutiwa</li> <li>• Vita vyatiro kiroho vinaingizwa na timu</li> </ul>

Katika hali ya ndani, timu ya wakristo wanaofanya kazi pamoja wanaweza kuwa katika ngazi sawa katika maeneo yote. Kwa jinsi hiyo, katika hali halisi, wanaweza kuwa hawajakomaa sana katika hali ya uongozi na majukumu maalumu, lakini waliokomaa zaidi kwenye maeneo ya mahusiano na mawasiliano. Hili lina uwezekano wa kutarajiwa.

Mchoro huu una makusudi mawili. Moja, unaweza kutumiwa na kiongozi kusaidia kugundua wapi timu yake ilipo katika misingi ya maendeleo na ukomavu. Pili, inaweza kutumika kumsaidia kiongozi kuona jinsi timu inavyohitaji kukua zaidi, na jinsi ya kuweza kusema wanapokuwa wamefikia ngazi ya juu ya maendeleo.

Kiongozi anatakiwa afahamu wapi timu yake ilipo katika hali ya maendeleo na ukomavu.

Kwa mfano, katika eneo la uongozi, timu inaweza kumuacha kiongozi kufanya maamuzi yote na kuwaambia nini la kufanya. Kwa kutumia mchoro, kiongozi anaona kwamba wajumbe wa timu wanahitaji kushiriki zaidi kwenye kufanya maamuzi. Anaweza kwa hiyo akafikiria njia kadhaa za kuuliza mchango, kuwaomba wengine kusaidia, n.k. Ili kuisaidia timu kukua na kukomaa. Utaratibu huu unaweza na unatakiwa urudiwe kwenye maeneo yote yaliyooodheshwa.

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Jinsi gani kuwa kiongozi wa timu ambayo inapanda kanisa kunatofautiana na kuwa kiongozi kwa ujumla?
- Majukumu ya kiongozi yanakazia kwenye maendeleo ya tabia, maono na ujuzi wa huduma kwa wajumbe wa timu yake. Kwa nini kujisumbua na yote hayo wakati kuna kazi inayotakiwa kufanyika (hii ni kupanda kanisa)?
- Kwa maneno yako mwenyewe, elezea majukumu ya kiongozi yanavyohusiana na kazi inayotakiwa kukamilishwa na wajumbe wa timu ya upandaji kanisa?
- Nini kinaweza kutokea kwenye timu inayokomaa kwenye baadhi ya maeneo na kubakia kutokomaa kwenye maeneo mengine?
- Kiongozi anaweza kusaidia timu yake kuendelea na kukua, au kwa kifupi huu ni utaratibu wa "kawaida" ambao utatokea kwenye timu yoyote inayotumia mda wa kutosha pamoja?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Kwa kutumia mchoro katika jedwali 5.2, "Hatua nne za maendeleo ya timu." Onyesha ni katika hatua ipi timu yako kwa sasa ilipo kwenye maeneo yaliyooodheshwa. Katika kipande cha karatasi kinachojitegemea, tengeneza orodha ya kila eneo (uongozi, kusudi, mahusiano, n.k.) na andika wapi timu yako ilipo kwenye (hatua 1, 2, 3, au 4).
- Angalia kwenye mchoro kuona nini zitakuwa baadhi ya tabia za timu ambazo zimeendelezwa zaidi katika kila moja ya maeneo haya. Kwa kila eneo lilioorodheshwa kwenye karatasi yako, andika angalau matatu yanayoonekana, vitu vinayopimika ambavyo unaweza kufanya ili kuisaidia timu yako kuendelea na kukomaa katika eneo hili.
- Anza kuweka mawazo yako, na baada ya miezi miwili, utazame upya mchoro huu na rudia zoezi hili. Ni katika maeneo gani timu yako imekua? Ni katika maeneo gani imeendele kuwa karibu sawa? Ni njia gani zingine unaweza kujaribu kusaidia timu yako kuendelea kukua na kuendelea kukomaa katika maeneo haya ya "kutojongea"? Fanya marudio ya mawazo yako na ufahamu pamoja na mshauri wako.

### **VYANZO**

- Engel, James F., Jane Overstreet, and Terry Sparks. *Leadership: Making Human Strength Productive*. St. Davids, PA: The Center For Organizational Excellence, Eastern College, 1996.
- Kilinski, Kenneth K., and Jerry C. Wofford. *Organization and Leadership in the Local Church*. Grand Rapids: Zondervan, 1973.

---

---

**VIKUNDI KIINI**

---

---

VIKUNDI KIINI

7

SOMO LA

# Nguvu ya Majadiliano ya Kikundi Kiini

## ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuandaa kiongozi wa kikundi kiini na ujuzi unaohitajika kuongaza nyakati zenye maana za majadiliano kwenye kikundi.

## ☞ Wazo Kuu

- Lengo la majadiliano ya kikundi kiini ni kuwahusisha wajumbe wa kikundi.
- Kiongozi anatakiwa afahamu matatizo ya kawaida kwenye majadiliano.

## ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa ujuzi wa mawasiliano ambao unahitajika kwa kiongozi wa kikundi kiini.
- Kujua kanuni za kuendeleza maswali mazuri ya majadiliano.
- Kufanya mazoezi kugundua na kutatua matatizo ambayo yanatokea wakati wa mda wa majadiliano ya kikundi kiini.

## ☞ Ziada

7A Kikundi Kiini: Mfano wa Maswali ya Majadiliano

## ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Ingawa kusudi la somo hili ni kumwandaa kiongozi wa kikundi kiini kuongoza mda mzuri wa majadiliano, majadiliano yenye siyo lengo la mwisho kwenye kikundi kiini. Mda wa majadiliano yenye maana kati ya wajumbe wa kikundi yanatia moyo ushirikiano, yanaimarisha mahusiano, na kutoa njia ya kujifunza na kutumia ukweli wa kibibia. Kwa kujifunza jinsi ya kuongoza majadiliano vizuri na kuepuka mataizo ya mawasiliano, kiongozi wa kikundi kiini atawea kujenga uaminifu na kujitoa kati ya wajumbe wa kikundi na kukivutia kikundi kutimiza makusudi yake.

Tambua kuwa Somo la 8 la Uongozi "Mitindo ya Kuchochearna" katika mwongozo wa 4 unatimiliza somo hili kwenye eneo la jinsi ya kuwasiliana vizuri na wengine kwenye kikundi kiini.

Panga kutumia angalau dakika 20 za mda wa darasa kwa ajili ya "Kushughulikia Matatizo ya Majadiliano" zoezi mwisho wa somo hili.

## I. KUONGOZA MAJADILIANO KWENYE KIKUNDI KIINI

Thamani ya mda mzuri wa majadiliano kwenye kikundi kiini hauwezi kusisitizwa vya kutosha. Ni kwa majadiliano kwamba wajumbe wanajifunza zaidi juu ya kila mmoja na kukua kwa kuwa pamoja mmoja kwa mwingine katika upendo wa kikristo. Majadiliano ya Biblia ni sehemu nyeti katika utaratibu wa ufuasishaji na ukuaji katika maisha ya muumini. Vikundi kiini vinaongeza nguvu ya majadiliano ya mwingiliano ambao unakosekana katika mikutano ya vikundi vikubwa. Roho Mtakatifu anatumia majadiliano haya kati ya waumini ili kuweza kuwavuta watu karibu na Yesu.

Kiongozi wa kikundi kiini anawezesha majadiliano yenye maana na kuwa kielelezo kwa wajumbe wa kikundi jinsi ya kusikiliza, kuuliza maswali mazuri, na kuepuka matatizo.

Majukumu ya kiongozi wa kikundi kiini ni kuwezesha majadiliano yenye maana na kuwa kielelezo kwa wajumbe wa kikundi jinsi ya kusikiliza, kuuliza maswali mazuri, na kuepuka matatizo

yanayoweza kutokea. Kwa njia hii, kiongozi anaendelea kuwasaidia wajumbe wa kikundi kiini kukua na kukomaa katika imani zao na katika ujuzi wao wa huduma.

Somo hili limeandaliwa kwa kifupi kufundisha mfumo, au njia, za mda wa kuongoza majadiliano kwenye kikundi kiini. Uaminifu, Kujitoa na mahisiano yenye nguvu yanatakiwa yawe matokeo ya majadiliano ya kikundi, siyo uwezo wa kiongozi wa "kuweka maonyesho mazuri." Kila mfunzwa anatakiwa afikirie juu ya mawasiliano ya kikundi na mwingiliano kulingana na utamaduni wake mwenyewe, na kisha kutumia ujuzi unaofaa ambaa utajenga uaminifu kati ya wajumbe wa kikundi kini. Funguo zifuatazo kwenye mawasiliano mazuri ni nyepesi na rahisi kutumia:

#### A. Kusikiliza

Moja ya ujuzi muhimu wa kiongozi kwenye majadiliano ni **kusikiliza**. Kusikiliza kunahusu yote kimwili na kihisia ukikazia kwa mtu anayezungumza. Kumbuka kwamba lugha ya mwili wako inaongea kwa sauti, pengine, kuliko maneno yako. Tunza mawasiliano mazuri ya jicho, na usiwe umetekwa na vitu vingine wakati mtu mwagine anapokuwa anazungumza.

#### B. Uliza

Mara kwa mara, watu ambaa ni wazungumzaji sana wanafanya mazungumzo yote kwenye kikundi kiini. Kama hili linatoka, Uliza wengine kwenye kikundi mawazo yao na mchango wao. Usiruhusu mmoja au watu wawili kutawala mazungumzo.



#### C. Changanua

Wakati mwagine utahitajika kuchanganua kitu fulani ambacho kimesemwa. "Max, una maana gani ulipotumia neno 'kuokolewa'?" Usichukulie unaelewa ambacho mtu amesema, bila kurudia ambacho unadhani amesema kwa maneno yako mwenyewe. Au, muulize kurudia kusema mawazo yake kwa njia tofauti. "Lena, Nimechanganyikiwa kidogo—unaweza kueleza hilo tofauti?

#### D. Hakikisha

Inaweza kusaidia kuwauliza watu kuhakikisha michango yao. Uliza kwa nini wanajisikia hivyo, wapi wanapata wazo kwenye kifungu cha maandiko kilichosomwa, n.k. "Vlandimir, Sifiki kwenye mwisho sawa kama ulivyofanya kwenye mistari hii ya maandiko. Unaweza kutusaidia kuelewa zaidi wazo lako unaloona.

#### E. Zidisha

Wakati mwagine utahitaji kuzidisha majadiliano kwa kuuliza kama kuna mtu ana la kuongeza zaidi, au kwa kuuliza jinsi gani kilichosemwa kinahusiana na mawazo ya nyuma.

#### F. Elekeza Upya

Wakati mtu kwenye kikundi anapomzungumzia kiongozi tu, elekeza swali lake au mchango wake kwa wengine kwenye kikundi. "Bob, ninaelewa kwa nini unajisikia hivyo. Laura, Nini mvuto wako kwenye ushauri wa Bob?" Kama majadiliano kawaida yanakuwa kati ya kiongozi na yeye mmoja tu badala ya mtu kwenye kikundi, watu wallobaki hawana cha kuchangia na kujisikia kuachwa nje. Mawasiliano kwenye kikundi yanatakiwa yaende mbele na nyuma kati ya wajumbe wa kikundi, na siyo njia moja tu kutoka kwa kiongozi kwenda kwa kila mjjumbe wa kikundi.

#### G. Ufupisho

Katika hatua fulani kwenye majadiliano, inaweza kusaidia kusimama na kufupisha kilichosemwa. Toa mawazo makuu au michango ambayo kila mmoja ametoa. Hii itasaidia kutunza mkazo wa majadiliano kwenye somo kuu, na kutoa hisia za ukamilishaji kwa wajumbe wa kikundi.

#### H. Thibitisha

Kumbuka kuwathibitisha wajumbe wa kikundi kwa kutambua na kushukuru kile ambacho kila mtu anasema. Washukuru kwa Mchango wao kwenye majadiliano. "Lisa, ninapenda ujue kwamba ninashukuru kwamba umechangia mawazo yako kwenye hili pamoja nasi." Hata kama mchango ambaa mtu ametoa unahitaji masahihisho, mzungumzaji ni muhimu na anatakiwa ashukuriwe kwa utayari wao wa kuchangia kwenye majadiliano.

## II. KUENDELEZA MASWALI MAZURI

Maswali unayouliza katika kikundi kiini chako yanaweza kwa upana yakakuza mahusiano kati ya wajumbe na kuwezesha ugunduzi wa ukweli wa neno la Mungu. Swali ambalo limefikiriwa vizuri litawatia moyo watu kuchangia kuhusu wao wenyewe, mawazo yao na wanavyojisikia.

### A. Maswali ya Ushirika

Maswali ni muhimu katika kujenga uhusiano binafsi kati ya wajumbe kwenye kikundi. Ziada 7A, "Mfano wa Maswali ya Majadiliano," kuna mifano ya maswali ambayo yatasaidia wajumbe wa kundi lako kuweza kujuana vizuri zaidi. Ni muhimu kwamba unajifunza jinsi ya kuunda maswali yako mwenyewe yanayohusiana na maisha yako na kwenye maisha ya watu kwenye kikundi chako. Uliza maswali ambayo yatawezesha wajumbe kuchangia juu ya wao wenyewe vitu ambavyo isingekuwa rahisi kuonwa na watu wengine: "*Ni kitu gani ulicho na mashaka nacho?*" *Ni badiliko lipi moja linalokuja kwako wakati wa mbeleni? Unajisikiaje juu yake?*" Aina hii ya maswali yanatia watu moyo kuzungumzia mawazo yao ya ndani na fikira, ambazo zinajenga hali ya kujaliana na usaidizi katika kikundi.

Ni muhimu kwamba unajifunza jinsi ya kuunda maswali yako mwenyewe yanayohusiana na maisha yako na kwenye maisha ya watu kwenye kikundi chako.

Uliza maswali ambayo yanaweza kujibiwa kwenye dakika 2-3: "*Unaweza tafadhali kushirikisha eneo moja la mahangaiko unalofanyia kazi wiki hii?*" Katika hatua za mwanzoni za kikundi, mara chache uliza maswali ambayo yatafanya wajumbe wa kikundi kuthibitishana: "*Ni kitu gani kimoja unaweza kuzungumzia angalau juu ya mtu mmoja kwenye kikundi chetu?*"

Maswali ya ushirika ni rahisi lakini hata hivyo yanaimarisha uhusiano kwenye kikundi. Hayahitaji majibu ya kukana (mf. Usiulize, "*Ni nini kosa lako baya zaidi?*"). Kila mmoja kwenye kikundi anaweza kujibu maswali la ushirika, na yanasaidia wajumbe kuweza kujuana na kupendana. Aina hii ya maswali yanawauliza watu kuchangia kutoka miyoni mwao, siyo kutoa maoni kwenye maswala.

### B. Maswali ya Majadiliano ya Biblia

Maswali unayouliza wakati wa mda wa majadiliano ya Biblia yatakuwa na tofauti ndogo kutoa kwa yale unayouliza wakati wa ushirika. Utahitaji kuendeleza maswali ambayo yataongoza kikundi kwenye mafunzo ya kufata neno ya kipande cha maandiko. Wakati kikundi kiini chako kinapokuwa bado kipyta, maswali yako yatakuwa mfano kwao wa jinsi ya kujifunza kwa kufata neno.

Kadiri kundi linavyokua na kukoamaa, utawataka waanze kuuliza maswali ambayo yatawapa ufahamu kwenye neno la Mungu. Unaweza kufanya hili kikawaida kwa kumtaka mmoja wa wajumbe kuongoza mafunzo katika moja ya mikutano. Au, unaweza kufanya hili kinyume, kwa kifupi kwa kuwaauliza wajumbe mawazo munapokuwa mnaptita kifungu cha maandiko pamoja. Unaweza kuuliza vitu kama, "*Nini tunaweza kuuliza juu ya mistari hii ili kuchunguza kiuangalifu ambacho kimeandikwa?*" au, "*Ni aina gani ya maswali ya matumizi unayoweza kufikiri kuhusisha fungu hili kwenye maisha yetu ya kila siku?*"

Kumbuka, mkazo wakati wa mda wa majadiliano ya Biblia siyo tu ufahamu wa Biblia, lakini kugundua ukweli kwenye neno la Mungu ambako kutapelekea maisha yaliyobadilishwa.

Moj ya uwezekano ni kuchukua moja au mbili ya mikutano na kuendeleza somo la majadiliano ya Biblia kama kikundi. Siyo tu hili litawenza kufundisha wajumbe wa kikundi jinsi ya kuendeleza maswali mazuri. Lakini litasaidia kusogeza kuwaandaa wao kwenye huduma itakayokuja, hasa hao watakao kuwa viongozi wa vikundi kiini wao wenyewe.

Wakati kiongozi wa kikundi kiini anapotumia maswali mazuri ya majadiliano ya Biblia, anakuwa kielelezo kwenye kikundi jinsi ya kuongoza mda wa majadiliano ya Biblia. Masomo haya yanatoa mipaka na majaribio ya kuongoza mda wa kuongoza majadiliano kwenye kikundi kiini. Kumbuka, mkazo wakati wa mda wa majadiliano ya Biblia siyo tu ufahamu wa Biblia, lakini kugundua ukweli kwenye neno la Mungu ambako kutapelekea maisha yaliyobadilishwa.

### III. MATATIZO YA MAJADILIANO

Kila kikundi kitakuwa na baadhi ya wajumbe wanaopenda kuongea na wengine ambao ni wakimya zaidi. Baadhi ya watu wanaweza kwenda nje ya njia na kuzungumzia kitu chochote nje kuliko jambo linalozungumziwa. Wengine wanapenda kubishana ili kuhakikisha wazo lao. Kama kiongozi wa kikundi, mara moja utakuta kwamba matatizo yanaibuka katika mda wa majadiliano. Jinsi unavyoyachukulia matatizo hayo ni muhimu kwenye ukuaji wa kikundi kama jumuia inayojaliana, vilevile na ukuaji wa binafsi wa kila mjumbe wa kikundi.

#### A. Aina ya Matatizo ya Majadiliano

##### 1. *Mmoja anazungumza sana/Mmoja hazungumzi kabisa*

Haya pengine ni moja ya mawili ambayo ni ya kawaida wakati wa mda wa majadiliano. Jinsi gani kimahiri unamuuliza mtu anayezungumza sana kuwa kimya na kumuacha mwingine kuchangia kwenye majadiliano? Wakati mtu anapozungumza sana, thibitisha mchango wa mtu huyo na kisha elekeza majadiliano kwa mtu mwingine kwenye kikundi. "Tom, hili ni wazo zuri. Vipi mtu mwingine ambaye hajachangia bado? Kuna mawazo mengine? Jim, umekuwa kimya jioni ya leo, unafikiria nini?" Kiongozi pia anaweza kuchagua kukaa karibu na mtu muongeaji, ili kwamba aweze kufanya mawasiliano ya macho na wengine kwenye kikundi na kuwatia moyo kuchangia.

Wakati mwinghine njia tu utakayopata watu wenyewe aibu au wakimya kwenye kikundi kuongea (angalau mwanzoni) ni kuwaauliza maswali moja kwa moja. "janeti, Ni nini mawazo yako kwenye mstari huu?" Tena, kiongozi anaweza kukaa pembeni kutoka kwa mtu mkimya kwenye kikundi (kwa kudhani kikundi kimekaa kwenye mduara) ili kwamba aweze kuwatia moyo kuchangia kwa kupitia mawasiliano ya macho na lugha ya mwili.

Unaweza ukawa na mtu kwenye kikundi chako ambaye ameshakuwa mkristo kwa mda, na anayejua majibu kwenye mengi ya maswali wakati wa mda wa majadiliano ya Biblia. Tatizo ni, mtu huyu anatoa majibu yote kabla wengine hawajapata mda wa kufikiria juu yake na kudiriki kutoa majibu yao. Katika hali hii, Inaweza ikasaidia kuzungumza na mtu huyu kisiri na kumtaka msaada wa kusaidia kuweka wajumbe wengine wa kikundi kwenye majadiliano. Pengine mtu huyu ni kiongozi mwanafunzi nyeti ambaye Mungu anakutaka kumshauri.

##### 2. *Muongeaji amekuwa kwa ujumla zaidi au Asiyeeleweka vizuri*

Wakati mwingine inawia vigumu watu kueleza kile hasa wanachotaka kusema. Unaweza kuwasaidia kukazia wazo lao au wazo lao kuu kwa kuuliza ufanuzi. "Unaweza ukatupa mfano wa wazo hilo? Wazo lako la ujumla ni zuri, lakini nashangaa kama tunaweza tukaliweka kwenye mkazo mwangavu. Kuna yeote anajua mfano wa kitu kama hiki?" Au unaweza kuhitaji kulisoma upya kwa maneno yako ya kile kilichosemwa, ili kulifanya wazi zaidi na la kueleweka.

##### 3. *Majadiliano yamekwenda nje ya jambo linalozungumziwa*

Kuwaweka wajumbe kwenye njia kunaweza kukawa moja ya kipengele kigumu cha kuongoza majadiliano. Watu wana mvuto wa kuzungumzia wanachojua, hata kama hicho siyo mnachojifunza au kujadiliana. "Kereni, hili ni wazo linalofurahisha, na pengine tunaweza kulizungumzia (au kufanya mafunzo ya Biblia juu yake) kwenye mkutano mwingine." Au, unaweza kusema, "Kereni, hili ni wazo linalofurahisha, lakini halihusiani kabisha na jambo linalozungumziwa leo." Unaweza kisha kuuliza wajumbe wa kikundi swali linalohusiana na jambo linalozungumziwa, ili kuwarudisha kwenye njia.

##### 4. *Kuna swalii ambalo kiongozi na kikundi hawakuweza kulijibu*

Hili linatokea mara nyingi zaidi kuliko unavyoweza kufikiria. Kitu kibaya zaidi kufanya ni kutoa jibu lisiloleweka au la ujumla, na hivyo inaonekana kwamba unajua kitu fulani ambacho hujui. Kundi lako linatakiwa kujua kuwa kiongozi hajui kila kitu. Kama hakuna hata mmoja kwenye kikundi ambaye anaweza kujibu swalii, kisha kama kiongozi, waambie utafanya kila uvezalo kutafuta na kuwajulisha kwenye mkutano unaofata. Jifanyie ukumbusho kufanya hili ili kwamba usisau.

5. *Wajumbe wawili au mmoja wanaingia kwenye mabishano*

Kwanza, mabishano kwenye kikundi chako wakati wote siyo mabaya. Yanaweza kusaidia kuchanganua ambacho kimesemwa, na yanaweza kusaidia kikundi kufikiria kwenye kifungu cha maandiko, au jambo linalozungumziwa. Kwa jinsi hiyo, kuna tofauti kati ya mijadala yenye afya na kukabili kwa hasira. Jukumu lako kama kiongozi ni kumulika kwa uangalifu mazungumzo na kusimamisha kama mambo yanachemshwa sana. "Ivan, Sergei, nafikiri wote tunaelewa wazo lenu mnaloona, lakini tunahitaji kuendelea. Pengine mnawenza mkalijadili zaidi baada ya mukutano wetu."

6. *Mtu fulani wakati wote anachekesha*

Baadhi ya watu wanafurahia kusimulia vichekesho au kuwa wachekeshaji, na katika hali halisi, wanaweza kuwa wa ajabu sana, Mungu anaweza akawa amekipa kikundi chako mtu ambaye ana hisia nzuri za uchekeshaji na uwezo wa kupata kitu fulani cha kuchekesha karibu katika kila hali. Katika mandhali sahihi, watu hawa wanaweza kuwa wa faida kwenye kikundi chako, kwa kuwa wanaweza kusaidia "kuvunja barafu" wakati pengine mambo yanapokuwa siyo ya mzaha sana au ya kuchokesha.

Kwa jinsi hiyo, kama mtu huyu anafanya matani kila wakati na kutaka kuwa wa kutazamwa, mara moja anakuwa tatizo. Mchukue pemberi kisiri na mwambie jinsi unavyoshukuru uwezo wake wa "kusaidia" wakati mambo yanapokuwa ya polepole, au yanapokuwa hayaridhishi, lakini hakikisha unaweka mipaka ya tabia ambayo inafaa na ambayo haifai. Mara kwa mara hatambui kama anasababisha tatizo. Usionyeshe kuwa ye ye ni tatizo, Lakini badala yake kwamba ni vigumu kwa wengine kwenye kikundi kukazia au kushiriki mara nydingi anapokuwa anachekesha.

7. *Mtu fulani pengine hazingatii, au anashughulika na kitu kingine tu*

Kama mtu fulani anaonekana kuchoshwa au kutovutiwa kwenye majadiliano, jaribu kuwafanya kushiriki kwa kuwaliza maswali moja kwa moja. "Bado hatujasikia kutoka kwako, Sharon. Unafikiriaje?" Kama anashughulika na kitu kingine (kufuma, kupurukusha makaratasi, n.k.), jaribu kumfanya kushiriki katika mazungumzo ya wakati huo kwa kumuuliza maswali ya kutosha ili kwamba asiwe na mda wa kufanya chochote kingine anachofanya. Kwa jinsi hiyo, kama hili ndilo analofanya mara zote, unaweza kuhitaji kuzungumza naye kisiri na kumshirikisha jensi tabia yake isivyokuwa ya heshima kwa wengine kwenye kikundi.

Kuna kitu kingine kimoja cha kufikiria katika hali hii. Pengine majadiliano kweli yanachokesha! Kama kuchoshwa kunaonekana kuwa tatizo kwenye kikundi chako, inaweza kuwa hekima kujadili hili na kiongozi wako mwanafunzi, au na mtu mwingine kwenye kikundi unayemwamini, kujifunza ni jambo gani linafaa zaidi kuzungumziwa kwenye kikundi.

8. *Wajumbe wawili kila mara wanakuwa na mazungumzo ya "siri" kati yao*

Kuna njia kadhaa unazoweza kuwafanya kuacha. Moja inaweza kuwa kuwaliza kuchangia walichokuwa wanajadili na kikundi (kwa kudhani wanazungumzia juu ya jambo linalojadiliwa). Lingine linaweza kuwa kuwaliza maswali zaidi moja kwa moja, ili kwamba wasimame kuzungumza ili wazungumze na kikundi. Kama linakuwa tatizo la kila mara, unahitaji kuzungumza na kila mmoja wao tofauti na kisiri juu ya jinsi majadiliano yao yalivyo ya kukatisha kwenye kikundi.

**B. Zoezi:Kuchukulia Matatizo ya Majadiliano**


Wagawanye wafunzwa kwenye makundi mawili, kikundi A na kikundi B. Kikundi A kinachagua mtu mmoja kutoka kwenye kikundi chao "kuongoza" kikundi B. Wakati wanachagua, kikundi B kisiri kinachukua wasiozidi watu 3-4 kuigiza moja ya jukumu lililoordheshwa hapo chini. Kwa mda wa karibu dakika tano, kikundi B kinatakiwa kujadili jambo litakalozungumziwa "Jukumu la Kanisa katika Kukuza Jamii" (au jambo lolote wanilotaka). Kikundi A kinachunguza. Kielelezo 7.1 kinaeleza jinsi ya kupanga makundi mawili.

"Tatizo" watu katika kikundi B wanatakiwa waigize majukumu yao kiulinganifu, na kiongozi kutoka kikundi A anatakiwa ajaribu kutatta matatizo yanapotokea. Kumbuka, watu wa "kawaida" wanatakiwa pia wachangie kwenye mazungumzo, na siyo tu "matatizo" ya watu! Mwishoni mwa dakika tano, kikundi A kinaweza kubuni mtu gani amecheza nafasi zipi.

Makundi yote yanatakiwa yatathimini jinsi kiongozi alivyojaribu kuchukulia matatizo yaliyotoka.

Kikundi B sasa kinachagua mtu wa kuongoza kikundi A, wakati kikundi A kisiri kinachagua watu 3-4 kuigiza tatizo la nafasi, n.k. Shughuli zinaendelea kadiri mda unavyoruhusu.

**Kielelezo 7.1 Zoezi la kujadiliana**



**Nasasi ya matatizo:**

- Mtu mwenye aibu asiyeongea
- "Mchekeshaji" ambaye mara zote anakuwa kichekesho
- Msemaji anayeongea mda wote
- Mtu ambaye anakalia kufanya mambo mengine tofauti
- Marafiki wawili wanaoendesha mazungumzo yao ya faragha
- Marafiki wawili wanaofikia katika mabishano yaliyochemka
- Mtu ambaye kila mara anapenda kuzungumzia kitu kingine tofauti
- Mtu ambaye mara zote haeleweki sana na hayuko wazi
- Mtu anayetoa mahubiri badara ya jibu fupi kwenye swali jepesi

**MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni ujuzi gani wa mawasiliano unaofikiria kuwa muhimu zaidi kwa kiongozi wa kikundi kiini? Kwa nini?
- Ni aina gani za maswali ya majadiliano yangefaa kwa kikundi kipyaa, au kwa mtu mpya aliyejuka kwenye kikundi kilichopo? Ni aina gani ya maswali yanaweza yasifaae katika hali hizi?
- Wakati wa zoezi la "kushughulikia matatizo", ni kwa njia zipi "kiongozi" ameshughulika na matatizo vizuri? Ni kwa njia zipi "kiongozi" ametatua matatizo vibaya zaidi?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Tumia mda fulani ukiandaa maswali ya mfano ya kutumia kwenye kikundi kiini kipy. Ni nini ungefanya kusaidia wajumbe wapya kuweza kujuana?
- Inayofata, Andaa baadhi ya maswali ambayo ungetumia kusaidia kikundi kukua kwa undani kwenye mahusiano yao. Ni jambo gani la kuzungumzia au maeneo ya maisha unayoweza kuzungumzia?
- Mwishoni, andaa maswali ambayo yanaweza kutia moyo kikundi kufikia nje kwa watu walio kwenye mzunguko wao wa mahusiano ya Oikos. Nini ungeweza kuuliza ambacho kingeweza kuwatia moyo kujenga mahusiano na kushirikisha Kristo?



# Vikundi Kiini: Mfano wa Maswali ya Majadiliano

Maswali haya ya majadiliano yanafaa zaidi kwa matumizi wakati wa mda wa ushirika wa mkutano wa kikundi kiini. Yanatofautiana kutoka kwenye maswali ya "kivunja barafu" kwenye Kikundi Kiini Ziada 2A (Mwongozo 2) katika hayo yaliandaliwa kwenda kwa undani katika kujielewa kwa mtu na kuelewa wengine kwenye kikundi. Yanafaa kwa matumizi kwenye kikundi kiini mahali ambapo wajumbe wamesharidhika na mmoja kwa mwagine na mahali ambapo kuna kiwango cha kuaminiana.

Swali limeundwa katika maeneo manne, likiwakilisha aina nne za mahusiano mtu anayoweza kuwa nayo katika maisha yake.

## MAHUSIANO MANNE:

### I. UHUSIANO KWA MUNGU

1. Ni lini mara ya kwanza ulipokuwa macho kwamba Mungu anakupenda?
2. Ni mvuto gani ulio nao wenye nguvu kwa Mungu?
3. Ni nini unafikiri ni kitu kimoja Mungu anajaribu kukuambia?
4. Ni kitu gani kimoja ungetaka zaidi Mungu kukusikia ukisema kwake?
5. Ni swali gani peke yake ungetaka zaidi Mungu kulijibu kwa ajili yako?
6. Elezea mtu unayemjua kwamba anamjua Mungu kiundani wa mahusiano.

### II. UHUSIANO WA MWENYEWE

1. Chora shungi au mkono wa koti kama unavyokuelezea vizuri, na ulezee kwenye kikundi
2. Nini ambacho ungefanya kama ungejua kuwa usingeshindwa
3. Ni nini unapenda kufanya zaidi miaka mitano ijayo kama kusingekuwa vizuizi?
4. Ni mtu yupi anafurahisha zaidi ambaye umewahi kukutana naye? Ni nini ulipenda juu yake?
5. Ni nini ulichokamilisha kinachotoshereza zaidi? Katika maisha yako ya mwanzoni? Katika miaka ya hivi karibuni?
6. Shirikisha mawazo yako makuu matatu
7. Ni nini ukumbusho wako wa kufurahisha zaidi (katika hatua tofauti tofauti)?
8. Elezea tukio lenye maana zaidi katika maisha yako
9. Elezea tabia za "mtu mashuhuri" kwenye kikundi.
10. Nani, mbali na wazazi wako, amekuwa wa kuigwa katika maisha yako?
11. Ni kipawa gani kingeweza kukubariki zaidi?
12. Ni nani unataka idhini yake zaidi?
13. Ni katika uwepo wa nani unafarijika zaidi? Kwa nini?
14. Kama ungekuwa na ulichotaka hasa katika maisha, Nini ungekuwa nacho?
15. Kwa kifupi orodhesha shabaha-ndefu na fupi ya malengo yako.
16. Elezea kichochezi zaidi, mtu mbunifufifi uliyewahi kukutana naye.

17. Ni nini watu watasema juu yako baada ya kuwa umekufa?
18. Orodhesha baadhi ya ubunifu, njia zinazosaidia kuianza siku na kuimaliza.
19. Ni katika nini unatumainia zaidi?
20. Ni nani amebadili maisha yako zaidi?
21. Ni vitabu gani bora zaidi umewahi kusoma (tofauti na Biblia)?
22. Jinsi gani unapenda kutumia mda wako wa ziada?
23. Ni nini kinakufanya zaidi kujisikia kupendezwa?
- 24. Ni nini kinakufanya kuwa na mashaka zaidi, kuwa na wasiwasi, au kuogopa?**

### **III. MAHUSIANO NA WENGINE**

1. Elezea mtu anayemaanisha zaidi kwako, na sema kwa nini.
2. Ni mtu gani wa kwanza aliyekuelewa zaidi?
3. Ni mtu wa aina gani unajikuta mwenyewe ukimwamini zaidi?
4. Ni nini kinamfanya mtu kuwa msikilizaji mzuri?
5. Uko aina ya mtu ambaye wengine wanaweka matumaini yao kwake? Kwa nini?
6. Unajisikiaje kundi hili limekusikiliza (kiushirikiano na kipekee)?
7. Nini kinafanya ndoa nzuri?

### **IV. UHUSIANO KWA ULIMWENGU**

1. Ni nini ungetaka zaidi kujulikana na ulimwengu unaokuzunguka?
2. Ni nini kinahitajika zaidi kwenye jamii yetu?
3. Elezea unavyojisikia juu ya kutokuwa na usawa kwenye jamii yetu. Ni nini kinakufanya kusikitika zaidi?
4. Ni kitu gani muhimu unachowenza kufanya juu ya huko kutokuwa na usawa?
5. Ni nini hitaji dhahiri zaidi kwenye jamii?
6. Nini utafanya kubadili kanisa lako, jumuia yako, au kazi yako kwa ajili ya uzuri?

VIKUNDI KIINI

8

SOMO LA

# Kuwatunza Watu Kwenye Kikundi Kiini

## ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kumwezesha kiongozi wa kikundi kiini na wajumbe wa kikundi kiini kuweza kufahamu na kwa wema kutunza mahitaji ya watu

## ☞ Wazo Kuu

- Mahusiano ni ufunguo kwenye kutekeleza mahitaji.
- Kutekeleza mahitaji ni sehemu muhimu ya maisha ya kikundi kiini.

## ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoelewaka. Kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa yaliyomo kwenye kujenga mahusiano: upendo, maombi na mda unaotumiwa pamoja.
- Kujua jinsi ya kutambua mahitaji ya wajumbe kwenye kikundi.
- Kujifunza jinsi ya kutunza mahitaji ya hao walio kwenye kikundi au watu ambaa kikundi kinawafikia nje.

## ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Panga angalau kutumia dakika 10 kwenye mda wa darasa kwenye zoezi la "Kutunza Watu" mwishoni mwa somo hili. Tambua kuwa hakuna majibu "sahihii" na "yasiyo sahihi" kwenye hali iliyoolewa. Lengo la zoezi ni kuwasaidia wafunzwa kuelewa upendo unaojionyesha wenyewe kuititia matendo wakati mahitaji yanapotokea kwenye kikundi kiini. Kwa kufikiria kwenye baadhi ya hali zilizotolewa, wafunzwa watakuwa wameandaliiwa vizuri kubeba hali zinazofanana kwenye vikundi kiini vyao.

## I. KUJENGA MAHUSIANO

Natalie amekuwa akihudhuria kikundi kiini chake kwa miezi. Anawapenda watu kwenye kikundi, ingawa hakujua mmoja wao vizuri sana, alifurahia kwenda kwenye mikutano mara moja kwa wiki. Mme wa Natalie, ambaye hakuja kwenye kikundi, hivi karibuni amepoteza kazi yake. Pesa zao ziliikuwa zinakwisha, na Natalie alikuwa amehofu sana juu ya nini watafanya kama familia. Alitaka kusema kitu kwenye kikundi, lakini alikuwa anajisikia vibaya na hakutaka kuwasumbua kwa matatizo yake. Mara baada ya hilo, aliacha kuwa anakuja kwenye mikutano ya kikundi, na wajumbe wakati mwingine walishangaa kwa mshangao, "Chochote ambacho kimemtokea?"

Ni nini kibaya katika hali hii? Pengine Natalie angekuwa amezungumza na angalau kuomba kikundi kiini chake kuomba kwa ajili ya familia yake. Lakini tatizo hasa ni kukosekana kwa uhushiano dhahiri kwenye kikundi kini. Hakuwajua watu vizuri kwenye kikundi chake, na hawakumjua. Moja ya kusudi la kikundi kiini ni kutoa ushirikiano, kulisha neno na kutiana moyo ambako wakristo wanatakiwa watoe kwa mmoja kwa mwingine. Lakini bila uhushiano wa kutunzana, hili halitatokea.

Kikundi kiini kinatoa mpangilio bora kwenye mahusiano kukua na kuendelea. Itachukua mda na juhudi kuweza kuwajua hasa wajumbe wa kikundi chako, lakini huduma ya "watu" yenye mafanikio inahitaji mahusiano. Mpaka hapo unapoengesha uaminifu kati yako mwenyewe na watu wa kikundi chako, huwezi ukahudumia kwenye mahitaji yao kikweli mahitaji yao ya ndani.

Huduma ya "watu" yenye mafanikio inahitaji mahusiano.

Katika njia sawa, unataka wajumbe wa kikundi kiini chako kuendeleza mahusiano kati yao wenyewe. Unahitaji kutoa mfano wa utaratibu wa kujenga mahusiano, vilevile na kutoa nafasi kwa hili kutokea katika kikundi kiini chako. Ili mahusiano kukua na kuendelea kwenye kikundi kiini, mambo matatu yaliyomo ni lazima: upendo, maombi na kutumia mda pamoja.

#### A. Kupendana Mmoja kwa Mwingine

Mahusiano na waumini wenzako yanatakiwa yatokane na upendo wa "kweli" wa 1Wakorintho 13. Aina hii ya upendo haupendi mtu mwininge kutokana na utu wake, muonekano au akili. Upendo unaendelea kupenda, hata kama hakuna kurudishiwa kuonyeshwa upendo. Upendo unavutwa na kutokuwa na mwisho kwa Mungu na upendo usio wa mashariti kwetu. Biblia inasema, "Tunapenda kwa sababu alitupenda kwanza... Na ametupatia amri hii: Kila anayempenda Mungu pia anampenda ndugu yake" (1Yoh 4:19; 21).

Jinsi gani upendo unaonyeshwa kwenye kikundi kiini? Watu wanajisikia kupendwa wanapokuwa wamekubarika na wanahisi kuhusika kwenye kikundi. Upendo unakuwepo wakati wajumbe wanapojisikia kuwa watu wanawajali. Upendo unaonyeshwa wakati mtu anapokuwa na matatizo na kikundi (au watu pekee kwenye kikundi) wanamsaidia. Upendo unakuwa wazi wakati wageni wanapokuja na kuona tofauti kwenye mahusiano kati ya waumini kwenye kikundi. Upendo wa kikristo kati ya wajumbe wa kikundi kiini unaonyeshwa kwa matendo, na siyo tu kwa maneno.

#### B. Kuombeana

Uhusiano wa moyoni na waumini wenzako unahitaji maombi, hasa na waumini ambao ni "wagumu" kupenda. Kama kiongozi wa kikundi kiini, unahitaji kuomba na kumuuliza Mungu kukupa upendo na uaminifu kwa kila mjambe wa kikundi kiini. Fikiria juu ya kila mtu na muombee. Ombea uhusiano wako na kila mmoja na uwezo wako wa kuhudumia kila mtu. Ombea ukuaji wa kiroho wa kila mjambe na kwamba kila mjambe atagundua na kutumia vipawa vyake vya kiroho. Ombea kwamba kila mtu atakuwa mshuhudiaji mwenye ufanisi kwa watu katika mtandao wake wa mahusiano. Ombea pia mahitaji binafsi ya kila mjambe na mahangaiko. Unapokuwa unamuombea kila mtu kwenye kikundi, upendo wako kwao utakua na uhusiano wako kwao utakua wa ndani.

Katika njia sawa, Watie moyo kundi lako kuombeana. Panga mda wa kwenye mkutano wa kikundi kiini wakati ambapo watu watashirikisha yote yanayohusiana na matatizo au mahitaji ya binafsi na ya huduma. Kisha tumia mda mkiombeana mmoja kwa mwininge.

#### C. Tumia Mda Pamoja

Inachukua mda kujenga mahusiano. Ni lazima upange kutumia mda na watu katika kikundi kiini chako nje ya mikutano ya kikundi kiini. Unaweza kuwakaribisha kula chakula pamoja kwenye miji yao au kwenye mji wako. Shughuli siyo muhimu kama mda unaotumia pamoja nao. Uaminifu unaendelezwa kwenye uhusiano wakati watu wanapoona kwamba uko dhahiri nao, kwenye familia zao na mapendeleo yao. Wakati matatizo yanapokuja kwenye maisha yao, uaminifu ambao umejengwa kati yako utakuruhusu kuwashudumia. Unaweza pia ukawaruhusu kujua kuwa uko unawafikiria na kuwaombea kwa kuwaita kwenye simu au kuwatumia ujumba wa haraka au barua.

Ni lazima upange kutumia mda na watu katika kikundi kiini chako nje ya mikutano ya kikundi kiini.

Pia inakuwa afya sana kwa kikundi kiini kukaa pamoja mara moja moja kwa matukio maalumu nje ya mikutano ya kikundi kiini. Hii itasaidia kupenyeza na kuimarisha mahusiano kati ya wajumbe wa kikundi. Shughuli hizi zinaweza kuwa si za kawaida sana, kama vile kwenda pikiniki pamoja au kuzunguka nchi kwa kufanya mchezo wa kuteleza. Yanaweza pia kuwa yameundwa, kama vile kufanya kazi pamoja kwenye mradi kumsaidia mmoja wa wajumbe wa kikundi au mtu kutoka kwenye jumuia (Mf. Kufanya marekebisho dari, kusaidia bustani ya mtu mzee, n.k.). Kama wajumbe wa kikundi chako wamekuwa wakiomba na kukutana na wasioamini ambao wasingejisikia kuwa huru kuja kwenye mkutano wa kikundi kiini, haya pia ni matukio mazuri zaidi ambapo wanaweza kukaribishwa. Hii inawapa nafasi ya kukutana na wakristo wengine katika hali ya kufurahisha, pasipo-mazingira ya kutisha.

## II. TAMBUA MAHITAJI YA WATU

Kikundi kiini kinatoa mazingira ya ajabu ambayo ni ya kuhudumia kwenye mahitaji ya watu. Mara kwa mara, kadiri kundi linavyokua na kukomaa, wajumbe watajisikia huru kushirikisha mahitaji na kutafuta msaada. Lakini kutakuwa kawaida na baadhi ya wajumbe ambao hawatashirikisha kiuwazi mahitaji yao, hasa kundi linapokuwa ndipo kwanza limeundwa, au wanapokuwa wapya kwenye kundi. Kama kiongozi wa kikundi kiini, unatakiwa kuwa makini kwa baadhi ya vimuli ambavyo vinaashiria matatizo au mahitaji. Unaweza pia ukasaidia kikundi kujifunza jinsi ya kutambua dalili hizi ili kwamba waweze kuuliza juu ya mahitaji na kuhudumiana mmoja kwa mwingine.



Kuna aina mbalimbali zinazochangia ambazo zitakusaidia kuona kama mahitaji yapo ambayo hayajaelezw. Mara unapomjua mtu fulani, mara kwa mara muonekano wa uso wake au mlio wa sauti unaweza kuonyesha tatizo. Wakati mwingine, mchango wake au majibu yake wakati wa mda wa majadiliano ya Biblia yanaweza kuonyesha matatizo ya kiroho au kihisia. Mtu huyu anajisikiae yeye mwenyewe? Anajisikiae kuhusu Mungu? Hili pia linaweza kuwa linaonekana anapokuwa anaomba.

Wakati mwingine, wakati maombezi yanapokuwa yanatolewa, watu "watadokeza" kwenye tatizo bila hasa kuficha. Kikundi kinatakiwa kimahiri kuuliza kwa undani zaidi, ili kwamba waweze kusaidia kutimiza mahitaji. Wakati mwingine tabia ya mtu isiyofaa wakati wa mkutano wa kikundi itaonyesha kwamba kuna tatizo lililopo. Badala ya kiongozi kumchukua pembeni tu na kumtaka kuacha, kikundi kinaweza kuanza kuuliza maswali na kuchokonoa kuona kama kuna sababu iliyopo kwa tabia yake.

Wakati mwingine tunatingwa na "mambo yote" ya huduma zetu na kusahau kwamba kitu cha muhimu zaidi ni watu ambao tunashughulika nao.

Usimudharau Roho Mtakatifu anapokuwa anakusaidia kutambua mahitaji ya watu. Unapokuwa unaomba na kusoma maandiko peke yako, jifunze kutumainia katika uelekezo wake unapokuwa unatafuta kuhudumia kwa wajumbe wa kundi lako. Usisahau kwamba ili kutambua mahitaji, unahitaji kuyaangalia! Wakati mwingine tunatingwa na "mambo yote" ya huduma zetu na kusahau kwamba kitu cha muhimu zaidi ni watu ambao tunashughulika nao.

## III. KUTUNZA MAHITAJI KWENYE KIKUNDI KIINI CHAKO

Kama kikundi kiini chako kinakwenda kuwa kinachotunza, kulisha neno jumuia ya waumini ambayo Mungu anaiitia kuwa, wajumbe wanatakiwa wajifunze jinsi ya kupendana na "kubebiana mizigo" (Gal 6:2). Kiongozi wa kikundi kiini anahitaji kuonyesha mfano kwa kuwatunza wengine katika njia zinazoonyesha upendo na kujali.

### A. Itikia Kwenye Mahitaji

Wakati mjambe wa kikundi anapokuwa na hitaji au tatizo:

- Kazana kuelewa tatizo na kuiweka katika sehemu yake. "Kama sehemu moja inaugua, kila sehemu inaugua pamoja nayo; kama sehemu moja imetunukiwa, kila sehemu inafurahi pamoja nayo" (1Kor 12:26). Onyesha kwamba unamjali. Chukua mda wa kusikiliza tu kwenye hitaji lake. Fikiria jinsi gani ungejisikia kama ungekuwa katika hali yake.
- Kama kikundi omba juu ya utatuvi. Tunahitaji hekima ya Mungu, siyo yetu. "Kama mmoja wenu anapungukiwa na hekima, anatakiwa amuuilize Mungu, anayetoa kwa ukarimu kwa wote bila kinyongo, na itatolewa kwake" (Yak 1:5). Kwa kufanya hili kama kikundi inasaidia kuimarisha mahusiano na kukipa kikundi kujisikia mshikamano.
- Kama kikundi, tegemea Biblia kwenye majibu. "Kila andiko ni pumzi-ya Mungu, na linafaa kwa mafundisho, kuonya, kusahihisha na kuadilisha katika haki, ili kwamba mtu wa Mungu awe ameandalialiwa vizuri kwa kila kazi njema" (2Tim 3:16-17). Vizuri kikundi chako kinavyojuu Biblia, ndivyo watakavyoandalialiwa zaidi kuhudumia kwenye mahitaji ya watu. Hii pia ni nafasi ya kuonyesha jinsi Biblia inavyotumika kwenye matatizo ya maisha ya kila siku.

- Fikiria nini kikundi kinaweza kufanya kiroho, kihisia, au kimali kusaidia. Wakati mwingine yote yanayoweza kufanyika kwa mtu anayeumia ni kuomba, kutoa faraja na kumfanya kujua kwamba unajari. Kama hitaji la vitu linaweza likatimizwa, kikundi kinatakiwa kuamua nini cha kufanya ili kusaidia.

Kiuwazi mahitaji hayawepo tu kwenye kundi—kama mmoja anakuwa na rafiki mwenye tatizo, kundi linaweza kuamua ni kama na jinsi gani wanaweza kusaidia kutimiza hitaji hilo. Hii ni moja ya njia bora kwa kikundi kufikia nje kwa upendo wa Kristo katika njia inayoonekana.

Wakati mwingine matatizo ni swala la dhambi katika maisha ya mmoja wa kikundi. Kama mmoja kwenye kikundi amefanya dhambi dhidi ya mjmpbe mwingine, Maelekezo ya Yesu katika Mathayo 18:15-17 yanatakiwa yatumike kama njia ya kugusa hali. Kama mmoja kwenye kikundi ameangukia dhambini, kikundi kinahitaji “kumrejeza kwa upole” (Gal 6:1). Kuweka kila mmoja kuwjibika kwenye kutembea kwetu na Kristo ni kipengele muhimu cha ushirika wa waumini kwenye kikundi kiini.

Ni jinsi gani kikundi kinatakiwa kufanya mmoja anapokuwa hakuhuduria kwenye mkutano? Mmoja kutoka kwenye kikundi (siyo lazima awe kiongozi) anahitaji kuwasiliana na mtu huyu siku inayofuata kumfanya kujua kuwa walimkosa. Pengine anaumwa, au ana matatizo mengine. Tena, kundi linaweza kuamua nini lifanye kusaidia. Wakati watu wanapokuwa hawajji kwenye mikutano, lisidharau hilo. Waendeel! Wafanye wajue kuwa kundi linajali!

Kujaliana mmoja kwa mwingine ni agizo ambalo wakristo wote wanalo. Kwa jinsi hiyo, baadhi ya matatizo, hasa matatizo makali ya kihisia, si ya mzaha vya kutosha kiasi kwamba msaada wa kitalamu unatakiwa upatikane. Mtu huyu anapokuwa anashughulikiwa na mtaalamu, kundi linatakiwa kuendelea kumuombea na kumtia moyo.

## B. Zoezi: Kuwatunza Watu

Yafuatayo ni matukio kadhaa ya baadhi ya hali unazoweza kukutana nazo kwenye kikundi kiini chako. Darasani, jadili kila hali na shauri njia ambazo kikundi kiini kinaweza kusaidia. Kunaweza kukawa hakuna jibu “sahihi” au “si sahihi” kwenye hali hizi.

- Katarina: Unapokea simu kutoka kwa Katarina asubuhi baada ya mkutano wako wa hivi karibuni. Anakwambia kwamba hatahuduria mkutano tena, lakini haeleweki sana sababu ni kwa nini. Unapolifkiria, unakumbuka kwamba Katarina alizungumza kidogo wakati wa ushirika au wakati wa majadiliano, na kuondoka bila kuongea na mtu yeote baada ya mkutano kumalizika. Utafanya nini?
- Olga: Wakati wa moja ya mikutano, wajumbe wa kikundi wamekuwa wakishirikisha maombezi binafsi. Inapokuwa zamu ya Olga, anaangalia kwenye sakafu na kusema polepole kila kitu ni sawa, asante. Wakati wa mda wa kuomba, huna uhakika, lakini unahisi kuwa analia. Utafanya nini?
- Andrew na Maria: watu waliooana, Andrew na Maria, wamekuwa wakija kwenye kikundi chako karibu mwaka mzima. Wakati wa mda huo, mahudhurio yao yamekuwa ya hapa na pale, iwezekanavyo. Hivi karibuni, wakati wa mda wa mkutano, ni wazi kwa kikundi kwamba kuna hali dhahiri ya kuhangaika kati yao. Unahisi pengine wana tatizo kwenye ndoa yao, lakini hujisikii kwamba unawafahamu vizuri vya kutosha kuweza kuwaauliza juu yake. Utafanya nini?
- Michael: Hivi karibuni, mmoja wa wajumbe wa kikundi alimkaribisha mmoja wa wafanya kazi wenzake anayeitwa Michael kwenye kikundi. Wakati wa mda wa majadiliano, anauliza maswali mengi na kutaka kujifunza zaidi juu ya Yesu. Kwa jinsi hiyo, Michaeli ana hadhi ya kutotulia, na wakati wote anawachokonoa watu (ionekanavyo bila kulifahamu hilo). Uwepo wake umefarakanisha kile ambacho kilikuwa kikifurahiwa sana mda wa mkutano. Kwa mda wa wiki kadhaa sasa, hajahuduria mkutano, na kuwa mkweli, wengi wa wajumbe wamepata nafuu kwamba hayuko hapo tena. Utafanya nini?

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Katika 1The 2:8, Paulo anaandika, Tumewapenda sana kiasi kwamba tunapendezwa kuwashirikisha siyo tu injili ya Mungu lakini vile vile na maisha yetu, kwa sababu mmekuwa wapendwa sana kwetu." Kwa nini "kushirikisha maisha yao" ilikuwa sehemu muhimu kwenye huduma ya Paulo?
- Fanya marudio ya masimulizi mwanzoni mwa somo hili juu ya Natalie. Nini kingekuwa kimetokea kitofauti kwenye kundi lake, na jinsi gani kundi lake lingekuwa limemsaidia?
- Kikundi kiini kinatakiwa kufanya haraka kusaidia kwenye mahitaji ya kifedha? Kwa nini na kwa nini siyo?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Andika njia mbili au tatu ambazo kikundi kiini chako kinaweza kukua kwenye upendo wao wa mmoja kwa mwingine. Andika shughuli kadhaa ambazo kikundi kiini chako kinaweza kufanya kuombeana zaidi.
- Andika mawazo mawili ya njia ambazo kikundi kiini chako kinaweza kutumia mda pamoja nje ya mkutano wa kawaida. Panga kufanya hili wakati mwingine wakati wa miezi mitatu ijayo.
- Watie moyo wajumbe wa kikundi kiini chako kushirikisha mahitaji, masikitiko na matatizo na kikundi, na angalia njia ambazo kikundi kinaweza kusaidia.

### **VYANZO**

- Mackey, Bob. *All About Cells*, Unpublished materials, 1996.
- Neighbour, Ralph. *The Shepherd's Guidebook*. Houston: Touch Publications, 1992.



# Kuwafundisha Viongozi Wapya wa Kikundi Kiini

- ☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kutoa majaribio ya mipaka kwa kiongozi wa kikundi kiini kilichopo kuwafundisha viongozi wapya.
- ☞ **Wazo Kuu**

Kiongozi mwanafunzi wa kikundi lazima achaguliwe, aandaliwe, na kutolewa.
- ☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

  - Kujua umuhimu wa kuwa na kiongozi mwanafunzi katika kikundi kiini chake, na kujua jinsi ya kuchagua kiongozi mwanafunzi.
  - Kuelewa taratibu za kumuandaa kiongozi mwanafunzi kwa ajili ya uongozi kwa kumuhusisha kwenye maeneo yote ya huduma.
  - Kuelewa taratibu za kumtoa kiongozi mwanafunzi kuongoza kikundi kiini chake.
- ☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Kisha kwenye zoezi la-darasani "Nani wa Kuchagua Wakati Hakuna Uchaguzi Lililo Dhahili" kuna mtiririko wa matukio kadhaa ya viongozi wa kikundi kiini walio na mda mugumu wa kuchagua kiongozi mwanafunzi. Kumbuka kwamba hakuna jibu moja lilio sahihi kwa kila moja ya matukio haya. Kusudi la zoezi ni kusaidia wafunzwa kwa hali ya majaribio ya kuchagua kiongozi mwanafunzi, na kushughulikia hali ambayo inaweza kuwa sawa na yale watakayokutana nayo kwenye vikundi kiini vyao.

Somo la kikundi kiini la 10 kwenye mwongozo ujao linatoa nafasi kwa viongozi wa kikundi kiini kujadili maswali na matatizo waliyonayo kwenye vikundi vyao. Wakumbushe wafunzwa kufanya orodha ya maswali haya na kuyaleta matatizo wanapopokea mwongozo wa nne wa mafunzo.

## I. CHAGUA KIONGOZI MWANAFUNZI

### A. Umuhimu wa Viongozi Wanafunzi

Kiini cha baolojia kwenye mwili wa mwanadamu, kwa asili yake hasa, kitazaliana chenyewe. Tafsiri tuliyochagua kwenye kikundi kiini, ambayo inakitenga mbali na vikundi vingine, ni kwamba kikundi kiini vile vile kinazidisha. Kwa jinsi hiyo, wakati kiini kwenye mwili kinaweza kuongezeka chenyewe, kikundi kiini hakiwezi kuongezeka bila mtu wa kuongoza kiini kipyka kilichotokea.

Falsafa ya jumla ya huduma ya kikundi kiini ni kwamba viini ni matofali ya kujengea, au sehemu ndogo sana, ya mkakati wa huduma kubwa ya kuanzisha makanisa mapya. Kuna njia nyingi na namna ya kutumia vikundi kiini ili kuanzisha makanisa, na makundi yenywewe mara kwa mara ni sehemu ya kiunganishi cha utaratibu wa upandaji kanisa.

Bila viongozi wapya kuanza viini vipyta, ni dhahiri kwamba utaratibu huu unavunjika. Lini unapata viongozi wa kikundi kiini? Kutoka kwenye viini vyenyewe! Moja ya kazi ya kwanza ya kiongozi wa kikundi kiini ni kuchagua na kuendeleza kiongozi mwanafunzi kimaombi. Utaratibu wa ongezeko la kikundi kiini unadhihirika wakati tu viongozi wapya wanapochaguliwa na kufuaswa.

Lini unapata viongozi wa kikundi kiini? Kutoka kwenye viini vyenyewe!

### B. Utaratibu wa Kuchagua Kiongozi Mwanafunzi

Viongozi wa kikundi kiini wanaaminia mafundishio ya Kristo kwa "watu wa kutegemewa watakaokuwa na sifa za kuwafundisha wengine" (2Tim 2:2). Hawa ni watu ambao siyo tu wanaweza kuwa viongozi, lakini ambao pia wanaweza kurudia utaratibu na kuwafundisha viongozi wengine wapya wao wenyewe.

Tuna mifano mingi kutoka kwenye Biblia ya waumini waliokomaa waliotumia mda na kuhudumu na hao walikuwa wamekomaa kidogo katika imani zao na uzoefu wa huduma. Mausia-yanayojulikana sana kutoka kwa Paulo kwenda kwa Timotheo yanaweza kuonekana katika baadhi ya mifano tuliyonayo kwenye Agano Jipya: Yesu na wanafunzi wake, Paulo na Timotheo, Akila na Apolo, Paulo na Sila, n.k.

Nini mahitaji ya kiongozi mwanafunzi wa kikundi kiini? Kila kiongozi wa kikundi kiini aliyekomaa anatakiwa awe na utayari wa aina tatu: tabia, uzoefu, na ujuzi. Utayari huu wa aina tatu, tabia tu ndiyo inayohitajika ili kwa mmoja kuanza utaratibu wa kuendelea kama kiongozi wa kikundi kiini. Uzoefu na ujuzi utakuja kwa mda, kiongozi wa kikundi kiini anapomfuasa kiongozi wake mwanafunzi na kumshirikisha katika maeneo kadhaa ya huduma.

Swala la tabia ni muhimu sana. Kiongozi mwanafunzi anatakiwa awe anakua katika tabia ya kikristo, kama ilivyoordheshwa kwenye sifa za wangalizi na wazee katika 1Timotheo 3:2-12. Kama dalili za tabia hizi zinaonekana, mtu huyu anaweza kufikiriwa "muhitimu" kuwa kiongozi wa kikundi kiini. Lengo la kutafuta kwetu siyo mtu mkamilifu, kwa kuwa mtu kama huyo hayupo. Badala yake, tunataka mtu ambaye kwa uangalifu anakua katika maeneo haya. Tabia ya kiroho imezungumziwa kwa undani katika njia ya tabia za kiroho kwenye kipindi hiki cha mafunzo. Unaweza kuitumia kama kiongozi kwa kutia moyo maendeleo ya tabia yako mwenyewe na ya mwanafunzi kiongozi wako.

Kuwhi kumchagua kiongozi wa kikundi kiini ni muhimu—siyo mapema sana, na siyo kuchelewa sana.

Kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa kutumia mda zaidi katika maombi kabla ya kuchagua kiongozi mwanafunzi. Anatakiwa aombe kwa ajili ya uongozi na hekima kutoka kwa Roho Mtakatifu anapokuwa anafanya uamzi. Kuchagua mmoja kama kiongozi mwanafunzi siyo jambo dogo, na kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa atafute uthibitisho kutoka kwa Roho Mtakatifu juu ya uamzi anaofanya.

Kuwhi kuchagua kiongozi mwanafunzi ni muhimu. Kiongozi wa kikundi kiini hawezu kufanya uamzi mapema sana, wakati pengine anapokuwa hana mda wa kutosha kuchunguza na kupata kujua wajumbe wa kwenye kikundi chake. Kwa upande mwengine, kiongozi mwanafunzi hawezu kuchaguliwa dakika ya mwisho, wakati kiini kinapokuwa tayari kuzidisha na kiongozi kufahamu kuwa anahitaji kiongozi mpya wa kusaidia. Mda wa kutosha unatakiwa utumiwe pamoja na kiongozi mwanafunzi ili kwake aweze kujifunza na kukua katika uzoefu wake na ujuzi kwenye kikundi kiini. Kiongozi wa kikundi kiini lazima kwa maombi aamue lini achague kiongozi wake mwanafunzi na kuanza kuelekeza huduma pamoja naye.

### C. Zoezi: Nani wa Kuchagua Wakati Hakuna Uamzi Dhahiri?

Viongozi wa vikundi kiini mara nyingi wanahangaika na uamzi muhimu wa nani wa kuchagua kuwa kiongozi mwanafunzi. Inasaidia kuchunguza mfano wa mtume Paulo aliposafiri na kuanzisha makanisa mapya. Tunapoangalia katika kitabu cha Matendo, Paulo na Barnabas hawakuweka viongozi kwenye makanisa mapya mpaka safari yao ya pili ya umishenari. Hawakuchagua mara moja wazee kuongoza makanisa haya.

Katika 1Timotheo 3:1 inasema, "Hapa kuna msemo wa kuaminiwa: Kama mtu ye yeyote anaandaa moyo wake wa kuwa mwangalizi, anahitaji kazi njema." Katika 1Petro 5:2, "Uwe mchungaji wa kundi la Mungu ambalo liko chini ya uangalizi wako, ukihudumu kama mwangalizi – siyo kwa sababu ni lazima, lakini kwa sababu u tayari, kama Mungu anavyotaka wewe uwe; siyo kwa ajili ya fedha ya aibu, lakini kwa moyo wa kutumika." Uongozi utachagulisha kwa mtu "anayeuanadaa moyo wake" juu yake na "utayari" na "moyo wa kutumika." Kukomaa kiroho ni sharti kwa uongozi, lakini kiongozi mwanafunzi lazima pia kwa uaminifu awe na haja ya kumtumikia Bwana.

Darasani, Jadili hali zifuatazo:

1. *Mtiririko wa Matukio:* Michael hivi karibuni ameanza kikundi kiini kwenye ujirani wake. Lengo lake ni kuanzisha vikundi kiini vya kutosha vinavyozaliana ili kwamba makanisa kadhaa mapya yaweze kupandwa katika mji wake. Amewaalika marafiki kadhaa na wanafamilia, na kundi limekutana kwa miezi kadhaa tayari. Kila mmoja katika kikundi ni muumini mpya, na hakuna anyeonekana kukomaa vya kutosha kuwa kiongozi mwanafunzi. Michael ameliombea hilo, lakini hana uhakika afanye nini. Anaweza kuchagua muumini mpya kuwa kiongozi wake mwanafunzi? Ungeshauri nini?
2. *Mtiririko wa matukio:* Petro ameanza kikundi kiini kwa msaada wa waumini wengine wawili. Watu wengine hawa wamekuwa wakristo wa miaka kadhaa, lakini hakuna mmoja kati yao aliye na uzoefu wa huduma. Petro anafikiri angesubiri kwa mda mrefu kabla ya kuchagua mmoja wao kuwa kiongozi wake mwanafunzi, ili kwamba wawe na nafasi ya kutosha kumwangalia anapoongoza kikundi kiini. Unafikiria nini juu ya namna hii? Nini ungeshauri?
3. *Mtiririko wa Matukio:* Eugene ameanzisha kikundi kiini kwenye jumuia na watu wengi wasio wafanaya kazi. Kundi linajaribu kuwasaidia watu kwenye jumuia kutafuata kazi, vile vile na kuwatambulisha kwenye Biblia. Eugene aliwaliza wachache waliokuja kuwakaribisha marafiki wengine waliokuwa nje ya kazi. Mwitikio ulikuwa wa kushangaza, na kikundi kilikua kufikia watu 15 kwa mwezi mmoja. Eugene anajua kwamba kundi linatakiwa lionezeke linapokuwa limefikia watu 15, lakini hili ni wazi haliwezi kutokea kwa kuwa hakuna mmoja wa wajumbe ambaye anaamini. Ana wasiwasi kwamba kundi litaendelea kukua, na hajui la kufanya. Ni ushauri gani unaweza kumpa? Unafikiria nini juu ya mkakati wake? Kuna kitu kingine ungekuwa umefanya tofauti?

## II. MWANDAE KIONGOZI WAKO MWANAFUNZI KWA AJILI YA UONGOZI


### A. Muhusishe Kiongozi Wako Mwanafunzi Kwenye Kila Kipengele cha Huduma

Mara unapokuwa umechagua kiongozi wako mwanafunzi, unatakiwa kufanya juhudi za kuwa makini kumuhusisha kiongozi wako mwanafunzi kwenye kila kitu unachofanya kuhusu kikundi kiini. Kila kitu ambacho ulikuwa ukifanya peke yako, ni lazima sasa ujaribu kufanya na kiongozi wako mwanafunzi. Elezea kila kitu, , zaidi ya mara moja, mpaka unapokuwa na uhakika kwamba mwanafunzi wako anaelewa vizuri vya kutosha kuweza kumpatia kiongozi mwingine mpya.

Unatakiwa kufanya juhudi za kuwa makini kumuhusisha kiongozi wako mwanafunzi kwenye kila kitu unachofanya kuhusu kikundi kiini.

Unatakiwa uanze kumuhusisha mwanafunzi wako na maandalizi na uendeshaji wa kila mukutano wa kikundi kiini. Jadili kabla juu ya unachofanya katika kila mukutano, na elezea kwa nini unachukua njia hiyo, Baada ya kila mukutano, jadili kile ambacho wote mmejifunza kutoka kwenye mukutano huo. Kisha panga mukutano ujao kwa pamoja. Jadili matatizo kwenye mukutano, kama vile mmoja anayetawala mazungumzo, na jinsi swala lilivyo (au halikutatuliwa) tatuliwa. Hii inaongeza uhusikaji wa mwanafunzi imeelezewa kwenye kielelezo 9.1.

### Kielelezo 9.1 Kumwendeleza Kiongozi Mwanafunzi



Mara mwanafunzi wako anapokuwa ameridhika na vipengele mbalimbali vya kupanga na kuendesha mukutano wa pekee, unaweza kuanza kumsaidia kuendeleza kuelewa kwa picha kubwa na falsafa ya huduma ya kikundi kiini. Jadili malengo yenu ya upandaji kanisa na elezea jinsi kikundi kiini kilivyo sehemu ya malengo yenu ya upandaji kanisa. Msaidie kufahamu maisha ya mzunguko wa kikundi kiini, na jadili katika hatua ipi kundi lako lipo kwa sasa.

Hakika, utaratibu huu wa kumuhusisha mwanafunzi wako na wewe unahitaji kuwekeza kwa hali ya juu mda wako na juhudhi. Lakini katika utaratibu wa kufuasa, hakuna njia za mkato. Kuwekeza maisha yako kwenye maisha ya mwingine kunahitaji kujitaoa, uvumilivu, na misaada mingi na kutiwa moyo kutoka kwa Roho Mtakatifu.

#### B. Tathimini Mwanafunzi Wako

Kama kiongozi wa kikundi kiini, unajua sana zaidi kwamba una nguvu na udhaifu unapokuwa unaendesha huduma yako. Katika njia sawa, mwanafunzi wako atazidi katika maeneo fulani ya huduma, wakati akifanya makosa au akihangainka katika maeneo mengine ya uongozi wa kikundi kiini.

Ungetakiwa kujadili na mwanafunzi wako vitu ambavyo anafanya vizuri. Hii itatoa faraja na uthibitisho wa wito wake wa kuwa kiongozi. Inafaa zaida pia kuzungumza naye, kwa upendo, juu ya maeneo ambayo anahitaji kukua. Mwanafunzi wa kikundi kiini anaweza kuwa na usoefu mwangi wa huduma na bado akakosa ujuzi mzuri wa huduma. Unapomfuasa mwanafunzi wako, unahitaji kumsaidia kuona ni wapi na jinsi gani anaweza kujitahidi kama kiongozi. Unapoona eneo lenye hitaji, toa njia za kujenga kujitahidi. Kwa maneno mengine, usitaje matatizo tu; toa ushauri wa jinsi gani anaweza kusahihisha maeneo yenye matatizo.

Unapotoa kielelezo cha huduma na mwanafunzi wako, muulize pia kukushirikisha maeneo anayofikiri kuwa unaweza kuwa unahitaji kufanyia marekebisho. Hakuna mmoja wetu aliye kamili, na karibu kila mara tuna mapungufu au udhaifu ambaa hata hatuwezi kuutambua. Uzuri wa uhusiano wa kufuasa ni uwezo wa kusaidiana kufikia kwenye undani wa ukomavu wa kikristo na ukuaji.

Upandaji wa kanisa ni bora ukifanywa kwa timu ya watu wanaoweza kusaidia kufidia uwezo wa mmoja kwa mwininge na udhaifu.

Kwa kujadili na kutathimini pamoja uwezo wenu na udhaifu, unaoonyesha thamani ya kazi ya timu. Upandaji wa kanisa ni bora ukifanywa kwa timu ya watu wanaoweza kusaidia kufidia uwezo wa mmoja kwa mwininge na udhaifu.

### C. Muombee na Ombo Naye Mwanafunzi Wako

Unapomfuasa mwanafunzi wako na kutoa kielelezo cha huduma kwake, chukua mda wa kuombea ukuaji katika tabia yake, uzoefu wake na ujuzi. Ombo kwamba Roho Mtakatifu ataendelea kufariji, kutia moyo na kumuongoza. Ombea pia uwezo wako wa kumfuasa na kuwa mfano wa kiongozi wa kikundi kiini kwake.

Ni muhimu pia kuomba na mwanafunzi wako. Weka mda wa kutumia pamoja naye katika maombi unapokuwa unapanga mikutano na matukio ya kiuinjilisti. Ombo pamoja kuhusu kila mmoja katika kikundi, kuhusu mahitaji yao na kwa watu amba wanawafikia nje. Ombeanenii kuhusu maeneo ya mahangaiko au mahitaji mengine binafsi. Jaribu kupenyeza kwa mwanafunzi wako umuhimu wa ajabu wa maombi katika maeneo yote ya huduma ya kikundi kiini.

## III. MTOE MWANAFUNZI WAKO KWENYE HUDUMA

### A. Mpe Maoni Mwanafunzi Wako

Moja ya hatua muhimu zaidi katika kumtoa mwanafunzi wako kiongozi ni kuendelea kumpatia maono ya kinachoweza kutokea katika maisha yake na huduma. Mafunzo ya ujuzi wa huduma bila maono ni kama kuandaa kwenda safari lakini bila kuwa na mahali pa kuishia kichwani. Mwanafunzi wako anahitaji kuelewa kwamba matokeo ya mwisho nyeti ya huduma yake yanaweza kuwa mengi, makanisa mengi yaliyoanzishwa kupitia huduma yake ya kikundi kiini. Anahitaji kuona jinsi anachojifunza na kufanya wakati huu kinafaa katika "matokeo haya ya mwisho" makubwa ya maono. Utambuzi wa kile Mungu anachoweza kufanya kupitia watu wake wasio wakamilifu kinaweza kuwa kivutio cha ajabu kwa mwanafunzi wako kiongozi. Chukua mda kumuuliza mwanafunzi wako maoni yake ni yapi kwa kazi Mungu anayomuitia kufanya. Tathimini kama unasaidia kuendeleza maono yake. Hakikisha mwanafunzi wako anaelewa kwamba ana nafasi muhimu ya kusaidia kukamilisha Utume Mkuu.

### B. Gawa Huduma kwa Mwanafunzi Wako

Mwanafunzi wako anapokuwa amekua katika kuelewa vipengele kadhaa nya huduma ya kikundi kiini, unahitaji kuanza kugawa madaraka zaidi na zaidi kwake. Kwa ujumla, unatakiwa kuwa kielelezo cha huduma kwa mwanafunzi wako, ukieleza nini ulichofanya na kwa nini. Kisha, fanya huduma pamoja na mwanafunzi wako (kama vile kupanga kwa ajili ya mkutano au kuendesha mda wa majadiliano ya Biblia). Sasa mruhusu mwanafunzi wako kufanya huduma mwenyewe, kwa faraja yako na usimamizi. Kimakusudi, elezea uwezo na udhaifu ulioungundua, na toa ushauri wa kujenga kwenye marekebisho. Mwishoni, mruhusu mwanafunzi wako kufanya huduma bila kujihusisha kwa upande wako. Anapofikia hatua ya kuweza kuendesha mkutano wa kikundi kiini kabisa, unaweza kutaka "kushughulika sana" mda baada ya mda ili kwamba apate ujasiri katika uwezo wake bila kuwepo kwako pale.

Utaratibu huu wa ugawaji unaanza kidogo, lakini hatimaye unataka mwanafunzi wako kuwa na uzoefu mwingu katika kuongoza kikundi kiini bila kuhusika kwako. Ni njia pekee ambayo atakuwa ameandaliwa kikweli kuongoza kikundi mwenyewe, akimtumaini Bwana kumuongoza katika nafasi hiyo ya uongozi.

Tambua kuwa ugawaji madaraka kawaida siyo rahisi kwa kiongozi wa kikundi kiini. Kuachia madaraka na majukumu kwa kikundi chako ni kitu kigumu kufanya. Vipi kama mwanafunzi hatafanya kazi nzuri? Vipi kama anafanya makakosa mengi? Nini kikundi kitafikiria, na jinsi gani watakavyochukulia? Kiongozi wa kikundi kiini lazima ajitokeze kwa imani wakati kiongozi mwanafunzi anapochukua majukumu zaidi na zaidi. Ni lazima ashuke kadiri mwanafunzi anapopanda. Kwa baadhi ya viongozi, inakuwa kama "wamepoteza" kazi yao na sasa hawana ajira. Shirikisha unavyojisikia na mwanafunzi wako wakati wa kipindi hiki, ili kwamba awe tayari kushughulika nalo wakati mda unapokuja kwake kukabidhi kundi lake kwa kiongozi mpya.

### C. Mtoe Mwanafunzi Wako Kuanzisha Kundu Jipy

Kadiri kikundi kiini chako kinavyowafikia nje na kukua, mda utakuja wakati ambao kiko tayari kuzidisha kuwa vikundi kiini viwili. Mda huu unapokaribia, jadili na mwanafunzi wako mkakati wa jumla wa huduma kwenye kikundi chake kipy. Ni nini malengo yake ya kuanzisha kanisa na jinsi gani kiini chake kipy. Kitaingia katika mkakati huu mkubwa wa huduma? Pengine kikundi kiini chake kitakuwa matofali ya kujengea kwenye kanisa hilo hilo kama kikundi chako,

au pengine kikundi chake kitasaidia kanisa tofauti. Sehemu muhimu ni kwamba mwanafunzi kiongozi wako anaewela mkakati mkubwa na wapi kikundi kiini chake kinafaa kwenye mkakati huo.

Mtie moyo mwanafunzi wako kuanzisha timu ya maombi kusaidia kumuombea kabla, wakati na baada ya kuanzisha kikundi kiini kipy. Msaidie kuelewa jinsi ya kuandaa kwa ajili ya mukutano wa kwanza kabisa, kwa kuwa anaweza kuwa hakuwa sehemu ya utaratibu huo wakati kundi lako lilipoanzishwa.

Wakati wa mwezi wa mwisho kabla kikundi kiini chako kuwa tayari kuzidisha, kwa ujumla weka huduma ya kikundi kiini kwa mwanafunzi wako. Katika njia hii, wajumbe wa kikundi kiini watakuwa na ujasiri kwake kama kiongozi mpya wakati makundi mawili yanapokuwa yameundwa kutoka kwenye moja. Mwishoni, Kaa karibu na upatikane kumsaidia mwanafunzi wako na kikundi chake kipy. "Usimuache" kuogelea kwenye maji mrefu mwenyewe. Omnia naye na mshikirie kuwajibika kuchagua mwanafunzi wake mwenyewe kutoka kweye kikundi kipy. Endelea kumtia moyo anapokuwa anaongoza kikundi chake.

(Utaratibu wa kuzidisha kwenye kikundi kiini utazungumziwa kwa undani kwenye somo la 11, "Kuzisha kwa Kikundi Kiini" katika Mwongozo wa 4).

#### D. Anza Utaratibu wa Mwanafunzi Tena

Baada ya kikundi kiini chako kuongezeka, kiongozi wako mwanafunzi aliyepita atakuwa anafanya kazi na baadhi ya watu kutoka kwenye kundi lako la kwanza. Hii ina maana kwamba kundi la kwanza linaweza kuanza tena kwa juhudini kuwafikia na kuwavuta watu wapya. Hii pia ina maana kwamba unahitaji tena kwa maombi kuanza nani atakuwa kiongozi mwanafunzi anayefuata. Utaratibu huu wa kutafuta, kufuasa, na kutoa viongozi ni njia ya ufanisi kuona makundi mapya yameanzishwa, kuona watu wanakuja kwa Bwana, na kutimiza Utume Mkuu kupitia makanisa mapya.

#### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni nini sifa za kiongozi mwanafunzi?
- Kama hakuna mmoja kwenye kikundi chako anayeonekana kufaa kama kiongozi mwanafunzi, Ni nini baadhi ya njia imara ambazo unaweza kuendeleza viongozi kutoka kundini mwako? Nini utahitaji kufanya hili kutokea?
- Nini utafanya kama unachagua kiongozi mwanafunzi kimaombi na anakataa?

#### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Kama bado hujachagua kiongozi mwanafunzi kutoka kundini mwako mwa kikundi kiini, liombee na kisha lifanye. Kama hakuna mmoja nayeonekana kufaa, chagua mtu wa kufuasa na kumwendekeza kwenye uongozi.
- Anza kumuhusisha kiongozi mwanafunzi kwenye huduma na wewe, na kwa juhudini teua huduma zaidi na zaidi kwake.
- Kutoka mda mpaka mda, mtathimini mwanafunzi wako, na muulize mwanafunzi wako kukutathimini kulingana na huduma yako na kikundi.
- Muombee kiongozi wako mwanafunzi.

#### VYANZO

- Neighbour, Ralph. *The Shepherd's Guidebook*. Houston: Touch Publications, 1990.
- Logan, Robert. *Multiplication of Cell Groups*. Old Tappan, NJ: Fleming H. Revell Co., n.d.



---

---

## **UINJILISTI**

---

---



## Uinjilisti wa Kimahusiano

### "UPENDO MKUU SI WA MTU..."

#### ☞ **Kusudi la Somo**

Kukadiria kwa chini hitaji na umuhimu wa kimkakati wa kujenga mahusiano na wasio amini.

#### ☞ **Wazo Kuu**

- Yesu kwa juhudhi alitafuta kuanzisha mahusiano na wenyewe dhambi ili kuwapata.
- Hitaji la Mungu ni kwa wakristo kwenda na kuwatafuta waliopotea kuliko kukutana pamoja na kuwakaribisha waliopotea kuja kwetu.
- Kuna gharama na faida za kufanya urafiki na wasioamini.
- Injili inawakilishwa vizuri tunapokuwa na uhusiano na wasioamini.

#### ☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wanapoelewa yaliyomo kwenye somo hili, washiriki...

- Wataona wafanye urafiki na wasio-wakristo kwa ajili ya ufalme wa Mungu.

#### ☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili la uinjilisti limeandaliwa kukuza mguso wa kihisia wa maandiko ya ufunguo yanayohusiana na uhusiano wetu kwa waliopotea. Ni muhimu kwamba watu wana mda wa kushika fungu la Luka 15 na thamani yake ya wakati huo kwao binafsi. Acha walifikirie kwa ukimya kwa mda na kufikia kwenye majibu yao wenywewe kwenye maswali katika sehemu hii ya 1B.

Kiu yako ya kuwafikia waliopote lazima ioneokane, kibinafsi na kimatendo. Weka na mifano ya jinsi mtu alivyokufikia au jinsi uliviyomleta mtu kwenye imani kupitia mahusiano.

## UTANGULIZI

TAHADHARI! Somo hili lingeweza kubadilisha maisha yako. Kama unaelewa na kutumia ujumbe wake, huduma yako ingekuwa na utajili usiopimika. Wakujaa na kutosheleza zaidi. Ni kweli kwamba pia kama unatumia mafundisho ya somo hili, unaweza kueleweka vibaya kwa marafiki wakristo ambao wanadhani utanajisiwa na ulimwengu, Lakini kumbuka, Yesu mwenywewe aliiwa "rafiki wa wenye dhambi" (Mt 11:19). Itakuwa na thamani hatari kuwa kama yeye.

Kuona harakati za kueneza upandaji kanisa zimeanzishwa katika nchi yako, kueneza uinjilisti wenye maana lazima kutokee. Vipao mbele vyta mkakati lazima vitolewe katika kuwafikia watu... binafsi kwa nyuso na matatizo. Mahusiano yanajenga imani, imani inajenga ushirika, na ushirika unayafikia mataifa!

Endelea kwa tahadhari, lakini enedelea katika imani.

### I. KUFANYA URAFIKI NA WASIO-WAKRISTO

#### A. Mifano Mitatu: Somo Moja—Luka 15


Mafarisayo walikuwa wamechukia kuwa Yesu alitumia mda na wenyewe dhambi. Walijisikia kwamba mtu mwenye haki asingeweza na hataweza kuungana na wenyewe dhambi. Hili lingemtia unajisi mtu mwenye haki. Msimamo wao unaonekana kuwa na ukweli, lakini ilikuwa ni makosa. Katika kuitikia swala hili, Yesu alitoa masimulizi ya vitu viliviyopotea ambavyo vimeandikwa katika Luka 15. Wazo la masimulizi yote matatu ni sawa. Wakati sarafu au mali

zingine zimepotea, tunazitafuta na kufurahi tunapozipata. Lakini Mungu anathamini watu waliopotea hata zaidi ya vitu hivi. Hiyo ndivyo hata sisi tunapaswa.

### B. Ni Somo Gani Tunaweza Kujifunza Kutoka Kwenye Mfano?

- Nini Yesu alizungumzia kwenye mfano huu kulingana na mstari 1 na 2?
- Nini kinasababisha kufurahia huku mbinguni kulingana na mstari wa 9 na 10?
- Nini ni muhimu zaidi kwa Mungu—kundi la watu tisini la waumini wanaomwabudu yeye kwa uaminifu—au toba ya mtu mmoja mwenye dhambi (v. 9,10)?
- Je malalamiko ya kaka mkubwa yalihakikishwa (Ms 29-30)? yalioana na moyo wa Baba?
- Nini kilimfikirisha Yesu zaidi: hakikisho la kidini au wokovu wa waliopotea?
- Unaweza kujichukulia mwenyewe kwenye mfano wa mwana mpotevu? Tabia ipi unayofanana nayo zaidi? Tabia gani unataka kuwa?
- Ni nini tabia ya kunena katika makanisa yetu kwenye kuwafikia waliopotea? Makanisa yetu yanafanana na Baba au na kaka mkubwa zaidi? Uko tayari kuchukua msimamo tofauti, kama ni muhimu kufanya urafiki na kuwafikia waliopotea.
- Ni aina gani ya juhudhi zitakuwa za lazima kuwafikia watu unapoishi.

#### Kielelezo 8.1 Kutafuta Dhidi ya Kualika



### C. Vipi Kuhusu Mistari Mingine ya Kwenye Biblia?


Luka 15 wazi inafundisha kwamba kipao mbele chetu kinatakiwa kiwe kwenda nje na kuwatafuta waliopotea. Yesu wazi alitumia mda “akila na kunywa” na wenye dhambi ili kuwapata. Jinsi gani tunalinganisha ukweli huu na mistari kama:

- 2Kor 6:14 kusiwe na ushirika katika nuru na giza.
- 1Yoh 2:15 Usiupende ulimwengu
- 1 Kor 15:33 Mazungumzo mabaya yanapotosha maadili mema

Hakika ni kweli kwamba ukaribu wa sana wa uhusiano na wasioamini unaweza kupotosha. Marafiki zetu wa karibu wanatakiwa wawe waumini. Kwa mfano, Marafiki wa karibu wa Yesu walikuwa wanafunzi kumi na wawili, Mariamu na Matha, Lazaro na wanafunzi wengine. Wakati huo huo, hata hivyo, Yesu pia alifikia nje kuanzisha uhusiano na wenye dhambi. Alikwenda majumbani mwao na sehemu walipokuwa. “Kuwapenda waliopotea” siyo kitu sawa na kama kuupenda ulimwengu. Na kuhubiri “toba!” siyo kitu sawa kama uhusiano. Paulo wazi wazi aliwaambia Wakorintho kwamba hakukusudia kuwaepuka wenye dhambi (1Kor 5:9-11). Kulingana na Paulo, ni vibaya kuungana na wasio waumini wasio na maadili mema, lakini siyo na wenye maadili wasioamini. Haya ni maelezo ya kushitisha, Lakini hata hivyo, ni kweli.

Hakika tunahitaji hekima kubwa kutambua jinsi karibu uhusiano wetu na wasioamini unavyowenza kuwa. Kwa jinsi hiyo, Mafarisayo walipotoka kwenye upande wa tahadhari iliyozidi, na makanisa mengi na waumini leo wanaonekana kufata mfano wao—badala ya mfano wa Kristo. Ni lazima tuwe na mahusiano na wasioamini wa karibu vya kutosha kuwfanya kutuamini kueleza injili kwao. Suluhu siyo kujiondoa kwa wasioamini—badala yake kuwa waangalifu kutunza haki zetu wenyewe tunapo “kula na kunywa” nao.

#### Kielelezo 8.2 Mitazamo Mtatu ya Mahusiano na wasioamini



## II. KUMFATA KRISTO KWENYE URAFIKI

Yesu hakusimulia masimulizi tu. Alisogeza mbele mifano hii kwa kutoa urafiki wa kweli kwa watu wahitaji. Maandiko yanachangia kwenye asili ya uhusiano wa Yesu.

### A. Warumi 5:6-8

“Unaona, ulipokuwa mda muafaka kabisa, tulipokuwa tungali hatuna nguvu, Kristo alikufa kwa wasio wa kimungu. Mara chache sana mtu atakufa kwa ajili ya mtu mwenye haki, ingawa kwa mtu mzuri mtu anaweza kujaribu kufa. Lakini Mungu anatoa kielelezo kwenye upendo wake kwetu katika hili: Bado tulipokuwa tungali wenyewe dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.”

### B. Yohana 15:13

“Hakuna upendo mkuu kuliko huu, wa mtu kuyatoa maisha yake kwa ajili ya marafiki zake.”

### C. Marko 10:45

“Kwa kuwa mwana wa mtu hakuja kuokolewa, lakini kuokoa, na kutoa maisha yake kama fidia kwa wengi.”

Nini msukumo wa vifungu hivi vitatu vya maandiko? Nini hakikisho la kirafiki Yesu alitoa? Jinsi gani kimvuto tunaweza kuonyesha urafiki na upendo kwa hao walio nje ya mwili wa Kristo.

## III. KUHESABU GHARAMA

### A. Gharama ya Kufanya Urafiki na Wasio-Wakristo

- Itakugharimu mda
- Itakugharimu sifa yako njema “rafiki wa wenyewe dhambi” (Lk 7:34).
- Inaweza ikakugharimu urchungu wa hisia na maumivu.
- Itakugharimu kutokuwa na wasaa.

### B. Faida za Kufanya Urafiki na Wasio-Wakristo

- Unapata rafiki—mmoja mwenye mtazamo tofauti
- Unapanda uwazi kwa ajili ya injili, siyo tu kwa marafiki zako wapya, lakini kwenye mzunguko wake wa marafiki, na kunufaika na wa kwao pia.
- Unapata wakili mionganoni mwa wasioamini kwenye imani yako.
- Unapata tumaini la kaka na dada wapya katika Kristo, wafanya kazi-wenzako wajao katika kazi ya kuifikia jumuia yako na taifa.

### IV. UZOEFU WA MAISHA KUHUSU UINJILISTI WA KIRAFIKA

Tumia mda uliobaki wa somo ukishirikisha vielelezo na mifano binafsi juu ya umuhimu wa urafiki katika uinjilisti kutoka katika maisha yako mwenyewe.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Jinsi gani naweza kuanzisha mawasiliano ya kuungana na wasio wakristo katika jumuia yangu?
- Jinsi gani ya kuanza mahusiano na wasio-wakristo katika jumuia yangu?
- Niko tayari kuhesabu gharama kuondoka na kuwafikia wengine ambao kwa sasa wako nje ya ninakoweza kufika kwa injili?
- Nini kinatokea kwenye harakati za upandaji kanisa kama kukiwa na moyo wenye bidii, uinjilisti unaoendelea unavunjika?
- Jim Elliot, mmishenari mfia dini kwa Waauka wa India wa Ecuador, "Siyo mpumbavu anayetoea ambacho hawezi kutunza kupata ambacho hawezi kupoteza." Alikuwa sawa? Jinsi gani maneno yake yanahusiana na kazi ya kuwaleta watu kwa Kristo?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Ombo kwa ajili ya muguso wa asili kwa wasio-wakristo. Ni kwa njia zipo unaweza kuanza uhusiano na wasio-wakristo katika jumuia yako? Ombo kwa ajili ya ujasiri kutembea katika milango anayofungua. Ombo kwa ajili ya ufahamu wa kuwaona.
- Nitahesabu gharama na kuonyesha imani kufanya urafiki na watano wasio-wakristo kwenye jumuia yangu mwezi huu hatimaye kuwaleta kwa Kristo?
- Ishike siku! Kuwa rafiki na wapate hao marafiki kwa Kristo! Washirikishe katika mafunzo yako ya Biblia, ushirika na huduma ya kuifikia nje. Wafanye kuwa sehemu ya timu!

### VYANZO

- Petersen, Jim. *Living Proof: Sharing the Gospel Naturally*, Colorado Springs: Navpress, 1989.
- Pippert, Rebecca Manley. *Out of the Salt Shaker & Into the World: Evangelism As a Way of Life*. Madison, WI: Intervarsity Press, 1999



---

## **KUFUASA**

---



# Utangulizi Katika Kufuasa

## ☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kutambulisha sehemu ya kimkakati ya kufanya ufuasishaji katika utaratibu mzima wa upandaji kanisa.

## ☞ **Wazo Kuu**

- Kufuasa ni jukumu la kanisa.
- Kufuasa ni moyo wa maisha ya kanisa.
- Kufuasa ni kipimo cha ukuaji wa kanisa.

## ☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoelewaka, kila mshiriki anatakiwa...

- Kuelewa misingi ya kibiblia ya kufuasa kama inavyohusiana na Utume Mkuu.
- Kuwa na maono binafsi makubwa kwa na kujitoa kwenye kufuasa.
- Kuelewa hatima ya kusudi la Mungu na jinsi gani hii inahusiana na kazi ya kufuasa.
- Kuelewa jinsi kufuasa kwa mafanikio kutachangia kwenye mafanikio yake kama mpanda kanisa.

## ☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo la kufuasa kwenye mwongozo waTatu na Nne linaendana pamoja. Imeshauriwa kwamba mkufunzi mmoja aongoze njia yote ya somo la kufuasa. Kama anahitajika mkufunzi zaidi ya mmoja, wakufunzi lazima wawe na ulinganifu wa karibu. Karibia na kuanza mzunguko wa kufundisha wakufunzi wanatakiwa wasome mwendo wote (masomo yote sita, pamoja na utekelezaji wa azimio) kupata uelevu wa njia ya kipekee kwenye yaliyomo.

## **UTANGULIZI**

Kufuasa ni kwa maana katika upandaji wa kanisa na ni jukumu la kanisa la mtaa. Makanisa yanazaa kwa sababu wafiasi wanazaliana wenyewe katika maisha ya wengine kuitia kufanya ufuasishaji. Kama uinjilisti ni ukunga wa kiroho, kufuasa ni uangalizi wa wachanga. Katika utaratibu wa ukuzaji wa watoto, siyo haja yetu kukuza watoto watakaokuwa wategemezi daima na wasiokomaa, kushirikiana na Mungu kwenye utaratibu wa uadilisho na utakaso wa wao kwa wao. Ingawa kufuasa ni kazi ya kanisa la mtaa, inaweza kukamilishwa katika njia tofauti tofauti. Badala ya kupendekeza kipindi kilichoshupaa cha kufanya uinjilisti, mfuatano huu wa masomo utakusaidia kuelewa kazi ya kufuasa katika kazi ya upandaji kanisa na kufikiria katika kukamilisha kwa ufanisi kazi hiyo katika huduma yako ya upandaji kanisa.

### **I. MSINGI WA KIBIBLIA**

Kufuasa ilikuwa kwenye moyo wa huduma ya Yesu wakati alipokuwa duniani. Injili inatoa maelezo wazi ya jinsi Yesu alivyochagua baadhi ya watu kumfuata yeye, na kuwatoa kuendeleza misheni yake. Biblia inawaita watu hawa "wanafunzi", ikiwa na maana wanafunzi wajifunzao, au wanafunzi. Katika Utume Mkuu Yesu anadhihirisha kwamba kufuasa iko kwenye kitovu cha kusudi lake kwa ajili ya kanisa lake mpaka atakaporudi.

"Mamlaka **yote** nimepewa mbinguni na duniani. Kwa hiyo, **kwenda**, **kufanya wanafunzi** wa mataifa **yote**, mkiwabatiza kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, **mkiwafundisha** kushika **yote** ambayo nimewaamuru; nami, nitakuwa pamoja nanyi siku **zote**, mpaka hata mwisho wa vizazi" (Tafsiri ya mwandishi wa Mathayo 28:18-20).

Kufuasa ni moyo hasa wa Utume Mkuu. Neno linalotawala ambalo linaunga kifunga hiki pamoja ni "Yote": mamlaka yote, mataifa yote, vitu vyote (ambavyo nimekuamuru) na siku zote. Katika Kiyunani, "kwenda", "kubatiza" na "kufundisha" ni maneno yenye kuongeza maana. Tenzi tu "fanya wanafunzi" iko kwenye tenzi ya kuamuru. Kwa haya maneno rahisi lakini yenye kina, Yesu analipa kanisa lake yote agizo lake kuu mpaka atakaporudi na ahadi ambayo juu yake mafanikio yamehakikishwa. Katika ukumbusho wa Agano Jipy, hasa katika maandishi ya Paulo, tunaona jinsi kanisa la kwanza lilivyoishi kwa kuonyesha utii kwake kwenye amri hii.

### A. Agizo

Msisitizo mkuu umewekwa kwenye amri ya milele ya "fanya wanafunzi." Tambua kuwa amri ni kufanya wanafunzi, na siyo wakata shauri tu. Vivumishi vitatu vinazovskyendana vinadhihirisha vipengele vitatu muhimu vya utaratibu wa kufanya wanafunzi.

#### 1. Kwenda

Kiyunani cha mwanzo lingetafsiriwa kirahisi 'kama unakwenda' au 'umekwenda.'linatwa kuwa hao wanaotii Utume Mkuu "wanakwenda." Kufuasa ni kuwa sehemu ya asili ya kwenda kwa ajili ya maisha yetu. Yesu hakufanya wanafunzi katika darasa la wasiozaa walitengwa, lakini katika mandhali ya kwenda kwa ajili ya maisha yetu. kufanya kwake wanafunzi kulikuwa kumepanuliwa , kuliko kulikojitenga. Wanafunzi wake watafata mfano wake, kuchukua hatua za mwanzo na siyo kusubiri watu kuja kanisani.

#### 2. Kubatiza

Ubatizo ni ushuhuda wa hadharani ya kwamba mtu ameweke imani yake ndani ya Kristo. Utume Mkuu unaonyesha kwamba ubatizo ni 'kwenye' Utatu. Kutokana na hili tunajifunza kitu fulani cha asili cha utambulisho wa wanafunzi. Moja ya hadhi za ajabu za Utatu ni jumuia ambayo Baba , Mwana na Roho Mtakatifu wanachangia. Katika njia sawa, muumini anabatizwa katika agano la jumuia, jumuia ya waumini wanaochangia aina moja ya umoja kama Utatu (Yoh 17).

#### 3. Mafundisho

Kama wajumbe wa agano la jumuia ya Kristo, kanisa, na hao waliojitoa rehani kwenye ubwana, wakristo lazima wajifunze jinsi ya kuishi kufuatana nao. Tambua kwa uangalifu nini kitafundishwa. Mstari hausemi kuwa lengo ni kufundisha amri, badala, lengo ni **kufundisha utiifu** kwa yote Yesu aliyoamuru. Kuna tofauti ya ajabu kati ya kufundisha amri na kufundisha utii. Kwa kifupi kuwatambulisha watu kwenye mapenzi ya Kristo kwa haikamilishi kusudi la Yesu. Ni lazima tufundishe (na kutia moyo na kuwezesha) watu kutii. Tambua kwamba pia wanatakiwa kufundishwa kutii "yote niliyoyaamuru." Hii ina maana kwamba ni lazima tuwafundishe kutii mapenzi yote ya Kristo, bila kuacha hata moja. Badala, ni lazima tuyachunguze maandiko kila mara, tukijiliza wenyewe, "Tumetii kila kitu kilichoandikwa hapa? Na, "Jinsi gani tunaweza kutii kila amri kwa uaminifu zaidi?"

Mwishoni, tunatakiwa kuvumilia katika mambo haya matatu "mpaka miisho ya vizazi", hii ni mpaka Yesu atakaporudi kwa ajili ya kanisa lake. Kwa maneno haya, Yesu anaonyesha kwamba maelekezo yote haya ni kwa kanisa zima mpaka atakaporudi, siyo tu kwa wafuasi kumi na wawili. Hii inaleta kufanya wafuasi na kupanda kanisa katika ushirika wa maana. Upandaji kanisa unahitaji kufanya wafuasi kukomaza kanisa changa. Kufanya wafuasi kunahitaji upanda kanisaji kuleta waumini wapya katika utaratibu wa kuwa wafuasi.

### B. Ahadi

Agizo lilitolimaliza kuelezewa linaweza kuonekana kulemeza. Kwa jinsi hiyo, tunapokwenda kufanya wanafunzi, kuwabatiza na kujitahidi kuwafundisha yote Yesu aliyoamuru, tunaweza kwenda kwa ujasiri. Tumehakikishwa mafanikio yetu ya mwisho kwa sababu sasa Kristo ana **mamlaka yote** na ameahidi kuwa pamoja nasi **siku zote** mpaka miisho ya vizazi. Yesu

mwenyewe ni hakikisho la mafanikio, tunapokaa ndani yake, tutegemee mamlaka yake na uwepo (cf. Yohana 15:4-17).

Mtume Paulo, akiwa amekaa gerezani, aliandikia kwa uhakika kanisa la Wafilipi (Flp 1:6), "...nikiwa na uhakika na hili, kwamba aliyeanza kazi njema ndani yenu ataichukua mpaka kwenye ukamilishaji mpaka siku ya Kristo Yesu." Kwa sababu aligundua kwamba Mungu alikuwa akifanya kazi na kwamba Roho wa Mungu alikuwa akikaa ndani ya waumini na kwenye ushirika wa waumini, alijua kazi yake haikuwa bure. Hiyo ni habari njema kwetu tunapoingia kwenye majadiliano ya kufanya wanafunzi.

## II. TAFSIRI YA WANAFUNZI NA KUFANYA WANAFUNZI (KUFUASA)

### A. Mwanafunzi

Mwanafunzi anaweza kutafasiriwa kama mmoja aliywewka imani yake ndani ya Kristo na, kwa ubatizo, amejitambulisha mwenyewe kama mwanafunzi wa Kristo na mjambe wa kanisa la Kristo. Kama mjambe wa agano la jumuia ya Kristo, ameweka rehani ya kujitoa kwa Kristo na anayejitahidi kuishi maisha ya utii kwenye mapenzi yote ya Kristo. Utii huu siyo tu uthibitisho wa muonekano wa nje kwenye mapenzi ya Kristo, lakini unachanua kutoka kwenye moyo wa upendo, imani na tumaini. Ukuaji wa wafuasi katika utii ni utaratibu wa maisha yote. Maandiko yanaelezea mwanafunzi kama mmoja ambaye "atajikana mwenyewe na kuchukua msalaba na kufata (Kristo)" (Mt 16:24). Mwanafunzi anasaidia wengine (Mt 20:25-28). Ana upendo mkubwa kwa Kristo (Lk 14:25-27). Watu watajua kuwa ni mwanafunzi wa Kristo kwa upendo wake kwa wengine (Yoh 13:34-35). Maisha yake yatazaa matunda ya Roho (Yoh 15:8).

### B. Kufuasa

Kufuasa kunaweza kutafsiriwa kama utaratibu ambapo kanisa, Kutegemeana na mamlaka na uwepo wa Kristo, linachukua chanzo...

- kuwaongoza watu kwenye imani kwa na kujitoa kwa Kristo
- kuwashirikisha kwa Kristo na jumuia yake ya agano, kanisa, kupitia ubatizo
- kuwaongoza kwenye maisha ya utii kwenye mapenzi yote ya Kristo

Kuwaongoza watu kwenye imani katika na kujitoa kwa Kristo mara nyingi tunamaanisha kama uinjilisti, ambao umejifunza mapepema. Kwa kusudi la sehemu hii ya mafunzo yako, tutadhani pia kuwa wameshashirikishwa kwenye agano la jumuia ya Kristo kwa ubatizo, na ni sehemu ya kanisa lake. Katika sehemu hii ya mafunzo tunarudisha usikivu wetu kuwaongoza kwenye maisha ya utii kwenye mapenzi yote ya Kristo.

## III. WITO WA MUNGU WA KUFUASI

### A. Kumwandaa Bibi Arusi wa Kristo

Tunapoyachunguza maandiko, tunaona kwamba lengo kubwa la Mungu kwenye historia ni kumtukuza Kristo kwa kumfanya kuwa kichwa cha kila kitu. Tunaona kuwa pia Kristo atapewa "bibi arusi" aliyetakaswa na asiyé na lawama, atakayekuwa "mwili wake, ukamilifu wake anayekamilisha kila kitu kwa kila njia" (Ef 1:23). Kristo atatawala enzi, hata hivyo hatafanya mamlaka yake peke yake. Atatawala na bibi arusi wake, kanisa. Katika upandaji kanisa, uinjilisti unakazia kuwaleta watu kuwa sehemu ya Bibi arusi; na kufuasa kunakazia katika kumwandaa Bibi arusi kwenye uhusiano wake na Yesu, Bwana wake.

Kwa hiyo, kanisa ni sehemu ya maana ya mpango wa Mungu wa milele. Yote Mungu anayoyafanya sasa yameandaliwa kufanya jumuia hii takatifu, watu kwa ajili ya kusudi hili—kuwa kweli wamoja pamoja naye na mmoja kwa mwininge, kuwa washiriki kwenye maisha hayo yaliyo na tabia ya Utatu. Mafunuo ya kanisa, na kutolewa kwa mume wake, Kristo, ni la mwisho, tukio la kihali ya hewa lililoandikwa katika Ufunuo. Katika umilele wote Bibi arusi mkamilifu na Mungu kichwa atafurahishwa na kufurahiana. Kanisa hatimaye litaleta kwa Mungu utukufu anaousitahili, unaoashiria tabia yake takatifu na kumwabudu yeye "katika roho na kweli" (Yoh 4:23). Kwa neema yake, Mungu amesimika kanisa kama njia atakayotumia kutimiza kusudi hili. **Kwa ufupisho, amri ya Kristo kufanya wanafunzi ni wito wake**

**kuchukua sehemu katika uumbaji wake wa jumuia takatifu ya Mungu, Bibi arusi mkamilifu na mtakatifu aliyetengwa kwa ajili ya Kristo.**

#### B. Kumfanya Bibi Arusi Kustahiri Kwa Bwana Arusi

Vyovyo tulivyo na yote tunayofanya lazima yatathiminiwe kwa mwanga wa "wito" wa Mungu kuchukua nafasi katika uumbaji wake wa jumuia takatifu ya Mungu, kanisa. Ufanisi wetu katika kufanya wafuasi unapimwa na jinsi tunavyomwanda Bibi arusi vizuri kustahili kwa Kristo. Vitu tunavyofanya sasa vinaandaa anayestahili kwa Kristo? Fikiria maswali haya:

- Tunawaandaa watu kukua katika umoja na Mungu na mmoja kwa mwingine? Tunawaongoza kuishi maisha yanayodhihirisha upendo huo wa kimungu ambao unaonyesha muungano huu?
- Tunawaandaa watu kukua kwa undani katika imani zao na matumaini katika Kristo?
- Tunawaandaa wanafunzi wetu kuhudumu kwa ufanisi kwa wengine, kuwajenga wengine kwa Kristo?
- Tunawaandaa watu kuwa mabalozi wa Yesu, kuwaita wengine kuwa sehemu ya jumuia takatifu ya Mungu na kwa hivyo kupanua Bibi arusi wa Kristo?

#### IV. JINSI KUFUASA KUNAVYOCHANGIA KWENYE UPANDAJI KANISA

Kufuasa kunaegemea kwenye moyo hasa wa upandaji kanisa. Mafanikio yako katika kuanzisha makanisa mapya yatategemea siyo tu kuwapata wakata shauri wapya kwa Kristo, lakini katika kuwafuasa kweli wanaomtii zaidi na zaidi kuti.

**Upandaji makanisa kuko kweye hali halisi ya kuanzisha jumuia ya wanafunzi ambapo hakuna ambaye amewahi kuwepo kabla.** Hatua ya mwanzo ya upandaji kanisa inahusu kuwaongoza watu kwenye imani kwa kujitao kwa Kristo. Kama ambavyo imeonekana kwenye majadiliano juu ya Utume Mkuu, kukata shauri ni hatua ya kwanza katika kufanya wanafunzi.

Ni lazima kila mara ikumbukwe kwamba kukata shauri kwa nia ya kukata shauri hajawahi kuwa lengo. Kukata shauri lazima kueleweke kama hatua ya kwanza tu katika utaratibu wa maisha marefu. Kufanya wanafunzi kunawaongoza hawa waliokata shauri wapya kwenye kuelewa kwa ndani ambako hakujawahi kuwepo kwa mapenzi ya Kristo kwao na kuwajenga katika njia kwamba wanatii zaidi na zaidi kwa utimilifu. Kuelewa huku kwa undani na utii kunatoka kwenye moyo wa upendo ambao unakua katika umoja na Kristo na mmoja kwa mwingine. Kwa maneno mengine, "jumuia" ya kweli inaanzishwa wakati kufuasa kunapokuwa kumefanywa kikamilifu. Kama upandaji kanisa unahusika na kuanzisha "jumuia" mpya za wanafunzi, kisha kufanya wanafunzi, tunavyokuelewa hapa, kwa hakika ni kwa lazima.

Kipengele kingine cha maana cha kuwezesha wakata shauri wako wapya kumtii Kristo ni kuwaandaa kwa ajili ya huduma. Kufanya wanafunzi ni pamoja na kuwawezesha wakata shauri wako kuzaa matunda kwa kuhudumia wengine, kutumia vipawa vyta kiroho Mungu alivyowapa. Kwa hiyo, kufanya wanafunzi kunapelekea kwenye ongezeko la haraka la wafanyakazi wenzio kwenye huduma. Miiongoni mwa wafanya kazi hawa wenzio kutakuwa na hao watakaojiunga kwenye kazi ya upandaji kanisa. Ongezeko hili la haraka la wafanya kazi wenzio ni moja ya michango katika kuanzisha harakati za upandaji kanisa.

#### V. KUANZA NA MWISHO AKILINI

Unapokuwa unaweka pamoja mpango mpana wa kufanya wanafunzi kwenye juhudini zako za upandaji kanisa, unahitaji kufanya kazi katika hatua hizi nyeti:

- Elewa lengo lako la kufanya wanafunzi.
- Elewa hali ya kiroho ya watu wako iliyopo kwa wakati huo.
- Anzisdha mpango jinsi ya kusaidia watu wako kukua kutoka walipo sasa kuelekea kwenye lengo lako la kufuasa.

Fikira zako hapa ni kuainisha nini lengo lako la kufanya wafuasi na kuruhusu lengo kuunda unachofanya sasa. Mungu ndiye anayeonyesha lengo. Jukumu letu ni kuelewa wazi nini Mungu anatuitia kuwa na kufanya na kisha kuitikia kwa imani na utii. Mpango wowote tunaofanya si zaidi

ya utii wetu kwa kuitikia kusudi la Mungu lililodhihirishwa. Tunapanga kwa sababu tunataka kumtii Mungu kwa miyo yetu yote na akili zetu zote. Tunapanga kwa sababu tunatarajia kutii na kuweka kwenye utaratibu maisha yetu kiulinganifu. Mpango kama huo mara nyingi unafanyika kwa kumtegemea Mungu kwa kuelewa. Unazaliwa na kutunzwa kwa maombi.

Kuhusu kufanya wanafunzi, lengo lako ni maisha ya utii kwenye mapenzi yote ya Kristo. Kianzio chako ni hali ya kiroho iliyopo ya watu unaowafusa. Mwishoni, ni lazima uendeleze mkakati wa jinsi unavyokwenda kusaidia watu wako kukua kutoka walipo sasa kufikia lengo la utii kwenye mapenzi yote ya Kristo. Ni lazima utafute njia za kimatendo kuwasaidia kuelewa zaidi kwa undani ina maana gani kuishi kama wajumbe wa agano la jumuia ya Kristo na kuwawezesha kuishi kulingana na hilo, hii ina maana kuishi kwa kutii mapenzi yote ya Kristo. Kufanya wanafunzi kunatokea katika sehemu ambayo haikuandaliwa au mda. Ni mapana, ya utaratibu wa pande kadhaa na kunaweza kukamilishwa kwa mchanganyiko wa mpangilio wa watu. (Rejea Somo 5, (Mifumo ya Kufanya Wanafunzi.)

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Nini kinapungua kwa uinjilisti usio na ufuasishaji?
- Nini tofauti ambayo huduma ya kufuasa kwa ufanisi kunafanya kwenye kanisa jipya?...katika kuanzisha harakati za upandaji kanisa?
- Inawezekana kupanda kanisa bila msisitizo mzuri wa kufuasa? Kwa nini na kwa nini siyo?
- Ni katika mandhali gani tofauti/ taratibu kanisa linaweza kufanya kazi kuelekea kufuasa?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Elezea nini aina za malengo ya kufanya wafuasi kanisa lako kwa sasa linazo.
- Orodhesha malengo ya kufanya unayodhani unatakiwa kuwa nayo.



# Wajibu Kufuasa

## FUNGUO KATIKA KUFANIKIWA KUFUASA

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kufanya marudio ya funguo za kutafakari katika kufanikiwa kufuasa.

### ☞ Wazo Kuu

- Mfuasishaji anayefanikiwa ni yule anayeendelea kukua mwenyewe katika imani, tumaini, na upendo.
- Mfuasishaji anayefanikiwa ni anayetoa kielelezo cha imani, tumaini, na upendo kwa wengine.
- Mfanya wanafunzi anayefanikiwa anakazia katika kitovu muhimu cha imani, tumaini na upendo.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoelewaka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa kwa nini ukuaji wake mwenyewe wa kiroho unaoendelea ni wa lazima katika kufanya wanafunzi.
- Awe ameshawishika kikamilifu juu ya umuhimu wa kimikakati wa kujitoa mwenyewe katika maombi na maandalizi na katika mda wa thamani wa kuwasiliana na waumini katika maendeleo yao kama wanafunzi.
- Kuelewa hitaji la kukazia kwenye mnaendeleo ya watu, siyo ukamilishaji wa vipindi, na kuwa kielelezo na kushawishi ubunifi na uhuru katika kufanya wanafunzi.
- Kuelewa uwezekano wa ajabu wa matokeo ya kulenga kwa mda mrefu kwa kufanya wanafunzi wake wa sasa katika shirika zinazoongezeka na kizazi cha waumini.

### ☞ Ziada

2A Tabia za Upendo Wa Kikristo

## I. KUA KIROHO

Maelekezo ya usalama wa ndege yanatuambia kwamba, katika tukio la dharura, watu wazima wanatakiwa kuvala vifaa vya usalama vinavyohitajika kabla ya kuwasaidia wengine wanaohitaji msaada. Hii ni kwa sababu kama tumeishiwa uwezo kutohana na kutojali wenyewe, hatutawenza kuwasaidia wengine walio katika hitaji. Maelekezo haya siyo ya kiuchoyo lakini ni kwa ajili ya matokeo. Yanatumika pia katika ulimwengu wa kufuasa.

Ukuaji wako mwenyewe wa kiroho kwa hakika ni muhimu kama utakuwa mfanya wanafunzi mwenye mafanikio. Unachojifunza katika mafunzo haya ni mwanzo tu mdogo. Kukuza kwa maisha yako mwenyewe ya kiroho ni lazima iwe kipao mbele chako cha kwanza.

### A. Kuendeleza Utambuzi wa Kiroho

Mwishoni, uwezo wako wa kutambua hali ya kiroho ya watu wako kutategemeana na kiwango chako mwenyewe cha ukomavu wa kiroho. Hakuna kipindi cha mafuzo au kitabu kinachowenza kuwa badala ya hilo. Kadiri unavyokuwa umekomaa, ndivyo undani wako wa usoefu binafsi na uelevu wa imani, tumaini, na upendo, utakavyoweza wazi kutambua kwa undani uwepo wao au kutokuwepo kwa wengine. Kwa undani ulivyokua, ndivyo utaweza kuelewa wazi nini ulimwengu wa kiroho katika maisha ya wanafunzi wako, kutoka katika mtazamo wa Mungu.

Utambuzi wa kiroho unatoka katika kuwa na moyo wako, roho, na akili zilizohakikishwa kwa Mungu. Hii ina maana unaanza kuangalia kwa njia sawa na Mungu anavyofanya. Kile Mungu anachokipenda unakipenda. Kile Mungu anachokataa, unakikataa. Kinachomfanya Mungu kufurahia kinakufurahisha. Kinachomfanya Mungu kuomboleza kinakufanya kuomboleza. Kinachomusababisha Mungu ndicho kinachokusababisha. Malengo yake ni malengo yako. Thamani yake ni thamani yako. Utambuzi wa kiroho unatokana na kushirikishana ushirika wa ndani na Mungu unapokuwa unashirikisha vitu vyote hivi kwake kwa maombi.

Kukua katika utambuzi wa kiroho kunaleta kiu ya kukua katika ufahamu na uelevu kwa Mungu. Utataka kuwa wazi na mkweli kwa Mungu, siyo kuficha kitu chochote kutoka kwake. Utataka kumpa Mungu vyote ulivyo navyo. Utafurahia kila nafasi ya kumtumikia. Utaihesabu kuwa furaha na majaliwa kujitaa kwa ajili yake. Hakuna kitu kitakachokuwa zaidi kwako kuliko kutembea na Mungu kwa njia hizi, kukutana na ushirika wake wa karibu.

#### B. Jifunze Nini Kinazalisha Ukomavu Kiroho

Kuelewa kwako kwa nini kinatakiwa kukua kiroho kunategemeana na mahangaiko yako mwenyewe na mafanikio katika maeneo haya. Kama mwenyewe hujakua, kisha huna uzoefu wa vitendo wa nini kinafanya "kazi" na nini hakifanyi. Kadiri ulivyokua kiundani, 1) ndivyo utakavyoelewa wazi nini mwelekeo unahitaji kuchukua ili watu wako waendelee kukua, na 2) Kadiri utakavyoelewa wazi wazi jinsi ya kushughulika na vizuizi vya kiroho katika maisha yao.

#### C. Endeleta Mguso wa Kiroho

Kuonyesha mfano wa ukuaji kiroho katika maisha yako mwenyewe kutakuwa "jicho wazi" moja pekee kubwa kwa wanafunzi wako. Kuelewa kwao kwa mambo haya kutazama wanapokuwa wanakuchunguza, kwa upande mwengine, kama wanaona kwamba unayaongea yote lakini katika hali halisi huendani na unayoyaongea, kwa haraka watapoteza kivutio. Wanaweza pia wakapoteza heshima kwako kama kiongozi wa kiroho, unayeangamiza uwezo wako wa kuigwa nao katika maisha yao. Utaongea, lakini hakuna mmoja atakayesikiliza.

## II. ELELEZA UPENDO WA KRISTO KWA WANAFUNZI WAKO

Hakika ni muhimu kwamba unawapenda wanafunzi wako kwa upendo unaofanana na wa Kristo na kwamba unaonyesha upendo huu kwao kwa njia za vitendo. Kama wanajua kupita mashaka yote kwamba unawapenda sana, kisha watakuwa wazi zidi na wewe, watakuwa wazi zaidi kukuiga, na watakuwa tayari zidi kutokujali udhaifu wako na makosa. Watajifunza ina maana gani kuwapenda wengine kwa jinsi unavyowapenda wao.

#### A. Ina Maana Gani Kuwapenda Wanafunzi Wako?

Hii inatokana na haja yako—nini moyo wako kweli kweli unataka. **Kupendana maana yake ni kuwa na haja na mmoja kwa mwengine.** Unatamani upendo wa kweli wa mmoja kwa mwengine (Ebr 10:24-25). Unataka kutumia mda na mmoja kwa mwengine (Flp4:1, 1The 2:17-18).

Hii inatokana na furaha yako—nini moyo wako unafurahia. **Kupendana mmoja kwa mwengine maana yake ni kufurahiana** (Flp 4:1; 1The 2:19-20; 2Kor 7:14-16).

Haja yako ya kuwa na kaka na dada wengine ili mweze kufurahiana. Mnafurahiana na kufurahi kuwa pamoja. Unafurahi katika kivuli cha mpPENDWA wako Mwokozi, ambacho unaona hata katika unyenyekevu na kuvunjika kwa watu. Unafurahi unapotambua kazi ya Baba katika miyo ya wengine, kama mama anavyofurahia maneno ya kwanza ya mtoto wake mchanga au hatua za kwanza. Unawakubali na kupongeza wengine kwa jinsi walivy. Unagundua na kufurahia hadhi nzuri za wengine na ukamilishaji wao. Unakuwa mvumilivu na wengine katika kutokuwa wakamilifu na kushindwa kwao.

Hii inatokana na kukabilisha moyo wako na akili—kwa yule ambaye moyo wako na akili vinajilinganisha. Kupendana kama Kristo alivyowapenda ina maana kuwa na moyo mmoja na akili moja (Rum 12:10, 15; Flp 1:27; 2:1-5; Ebr 13:3).

Misingi ya kuwa wamoja kwa mwengine ni kuwa wamoja na Kristo. Kama kilicho ndani ya moyo wa Kristo na akilini kiko ndani yako na wengine, kisha unachangia moyo mmoja na akili. Katika Kristo unachangia mtazamo, thamani sawa, kusudio sawa, kuuugua swa na mzigo, n.k.

Kama mko wamoja moyoni na akilini na wengine haufikirii tena katika namna ya "mimi" au "changu." Lakini badala yake, "sisi" na "chetu." Furaha yako ni furaha yao na huzuni yako ni huzuni yao. Hitaji lako ni hitaji lao. Mafanikio yako ni mafanikio yao na kushindwa kwako ni kushindwa kwao. Unapokuwa umebarikiwa, wamebarikiwa. Matatizo yako yanawapa fikira na wanataka kusaidia kwa kila njia wanayoweza kuyakabili au kuyatatura. Malengo yako yanakuwa ya mvuto maalumu kwao. Wanatamani kufanya kila watakaloweza kukusaidia kuyafanikisha. Wanataka kukupa nafasi ya kuwasaidia na wao pia. Wanatamani kukubariki na kubarikiwa na wewe. Wanataka wakujue na kukuelewa zaidi. Na wanatamani uwajue na kuwaelewa zaidi pia.

#### B. Jinsi Upendo Huu Unavyodhahirika Wenyewe Katika Maisha Yako

Biblia imejawa na maelezo ya jinsi upendo huu unatakiwa udhihirike wenyewe katika maisha yako. Wakati aina hii ya upendo ipo, kimusingi itagusa kile unachofanya, kama ilivyoelezwa, kwa mfano, katika 1Wakorintho 13. Angalia kwenye toleo liliopanuliwa la 1Wakorintho 13:4-7 katika Ziada 2A, "Tabia za Upendo wa Kikristo."

Umeamriwa kuwapenda watu wote. Unatakiwa kuonyesha aina hii ya upendo kwa kila mmoja ambaye Mungu anamleta kwako katika mawasiliano kwa kiwango unachowenza. Kwa jinsi hiyo, una upeo. Huna mda au rasilimali kuonyesha kiasi sawa cha upendo kwa wote. Lazima kuwe na vipao mbele. Mungu ni wa kwanza. Kisha Mungu ameweka wengine katika maisha yako ambao utapata nao aina hii ya uhusiano kwa undani zaidi, kama vile familia yako, kaka zako na dada zako katika kanisa lako la mtaa, n.k.

#### C. Baadhi ya Ushauri wa Vitendo wa Kuonyesha Upendo kwa Wanafunzi Wako

- **Tumia mda nao, kuwafurahia na kuonyesha kwamba una moyo mmoja na akili pamoja nao.** Angalia kwenye tabia za upendo kwa wengine ambazo zimeelezewa kwenye Rum 12:10-21; Flp 2:1-8 na 1Kor 13:40-7.
- **Omiba pamoja.** Ombea matatizo yaliyopatikana na majibu kwenye hali. Muulize Mungu akuonyeshe jinsi ya kuonyesha upendo huo kwa watu aliokupa, katika namna kwamba wataitikia na kukua.
- **Jifunze pamoja.** Soma vitabu kwa pamoja na shirikisha vitu unavyojifunza. Jifunze maandiko pamoja, yatumie kwenye matatizo ya kila siku.
- **Uwe mbunifu.** Tumia mda kiubunifu kukamilisha makusudi mengi. Fanya kazi pamoja, cheza pamoja, muwe na chakula pamoja. Washangaze waumini wanaokua kwa ukweli wako, haja yako kuu kwao.
- **Upatikane.** Ni muhimu kwamba wanafunzi wako kujua unapatikana kujibu maswali na kushauri kuhusu mashaka yanayotokea katika maisha ya kila siku.
- **Tafuta ushauri na msaada kutoka kwa wakristo wengine.** Kama uko dhaifu katika eneo hili (yaani la kuonyesha upendo), tafuta msaada unaohitaji ili kufanya maendeleo.

### III. KAZIA KWENYE MAHITAJI HALISI YA KIROHO YA WATU, SIYO KATIKA VIPINDI

#### A. Fanya Mambo Kuwa Rahisi

Tunza mkazo kwenye kiini rahisi, yaani kwenye upendo, imani na tumaini. Yaliyobaki yataturirika kutokana na haya matatu. Kikuu cha msingi ni upendo. Kama wanafunzi wako wanashindwa kutunza upendo wao kwa Mungu na kwa wengine, Roho Mtakatifu atahuzunishwa na kupewa kiu. Hili linapotokea Roho anakuwa hawezi tena kushuhudia kwenye nafsi zao kwamba ni watoto wa Mungu. Wanaweza kuanza kupoteza kiurahisi yote imani na tumaini. Wanaweza kiurahisi kupoteza ujasiri kwamba kweli Mungu anawakubali, na pengine hata kuwa na mashaka kwamba wameokoka. Kama wanafikia hatua hii, maneno yako yote ya faraja hayatasaidia. Ni lazima utambue kazi anayotaka kufanya Roho Mtakatifu katika maisha yao na kushiriki katika kazi hiyo pamoja naye. Masidie mtu kututua kila swala la dhambi. Usitoe faraja ya uongo. Wasaidie kujua hatima ya kusudi la Mungu kwao na jinsi anavyolifanyia kazi katika maisha yao.

### B. Wawezeshe Kutunza Sawa Sawa Vipao Mbele Vyao

Usiwalemeze watu wako kwa vipindi na shughuli. Wape uhuru kutoka kwenye shughuli ambazo zina umuhimu kidogo ili kwamba waweze kutunza vipao mbele vyao na bila kuwa wamefanyishwa kazi nyingi.

### C. Uwe Mvumilivu

Waumini wapya wana mwendo mrefu wa kwenda. Maisha yao yote ya ndani lazima yafanywe upya: jinsi wanavyofikiri, thamani yao, na haja zao (Rum 12:2).

Lazima uendelee kuwapa tumaini wanapoanguka. Mazoea yao ya kawaida yatakuwa kuelekea kukata tamaa. Unahitaji kuwa kama mzazi anayemtia moyo mtoto wake anapokuwa ameshindwa. Wape mda wa kuja kwenye hisia zao. Watie moyo. Usikate tamaa kamwe juu yao. Lazima wajue kuwa unawaamini na kwamba Mungu anaweza na atasamehe. Lazima wajue kuwa hakuna kitu ambacho watafanya kinachowenza kukusimamisha au Mungu kutokuwapenda. Kama unashindwa kuwasilisha mambo haya, watakuwa katika hatari kubwa ya kupoteza tumaini na kuacha.

## IV. DHAMIRIA KUZALIANA NA KUZIDISHA

Bila kujali ni aina gani ya "mfumo" au muundo unaotumia kwa kufanya wanafunzi, unatakiwa kutafuta njia za kuzidisha hao wanaohusika katika kazi ya kufanya wanafunzi. Huwezi mwenyewe ukamfuasa kila mtu. Rasilimali zako zina kikomo na unahitaji kupata wengine kuhusika kwenye kazi kwa ajili ya faida yao na ukuaji. Ni lazima upnge jinsi gani utaongeza wafanya kazi wenzako kwa ajili ya huduma kwenye ngazi ya kikundi kikubwa, kikundi kidogo, mmoja kwa mmoja.

Kwa ujumla, utahitaji kutoa aina ifuatayo ya msaada kwa hao unaowaandaa kwa ajili ya kazi ya kufuasa:

- Nafasi za kuchunguza watu wanaofanya aina ya huduma ambayo wameandaliwa.
- Maelekezo na mafunzo ya vitendo kwenye ujuzi muhimu wa lazima.
- Kama inahitajika, saidia kuendeleza mkakati wa vitendo kufanya kinachohitajika.
- Nafasi zinazofaa kufanya mazoezi wanachojifunza, kwa matokeo yanayosaidia.
- Ushauri wa vitendo na msaada wanapoendeleza ujasiri na ujuzi.

## V. KILA MARA TATHIMINI HUDUMA YAKO NA UWE TAYARI KUFANYA MABADILIKO YANAYOHITAJIKA

Kila mtu anapokea kile kinachohitajika ili kuishi maisha ya upendo, imani na tumaini? Kila mtu anakua katika upendo na umoja na Mungu na mmoja kwa mwingine? Kila mtu ametumiwa kiufanisi na Mungu kuujenga mwili wa Kristo na familia yake? Kila mtu ametumiwa na Mungu kama wakili wake kwa ulimwengu? Ni mabadiliko gani yanatakiwa yafanyike ili kumuwezesha kila mtu kufanya maendeleo halisi katika kila eneo.

Usipoteze mda kutunza vipindi kwa kutafuta kuwa na vipindi tu. Lengo lako ni kwamba kila shughuli za huduma zinatimiza kusudi lililotajwa kwenye aya iliyopita. Mara zote jiulize mwenyewe kama "mifumo" yako kiufanisi inatimiza "kazi."

## VI. JIFUNZE, JIFUNZE, JIFUNZE

Endelea kuweka mwendo kama mwanafunzi. Usiache kuuliza maswali. Gundua kuwa rasilimali zipo kukusaidia kukua na kukusaidia kusaidia wengine kukua katika Kristo. Waulize wengine ni zana gani zinapatikana na zinazosaidia katika kufanya wanafunzi. Kama baadhi ya rasilimali zinahitajika lakini hazipatikani, ziunde na shirikishana na wengine.

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Jinsi gani mawazo haya yanaweza kuhusiana na ukuzaji wa watoto wetu kwa ajili ya Kristo?
- Jadili maelezo yafuatayo: "watu hawajali ni kwa kiasi gani unajua mpaka wanapojuu ni kwa kiasi gani unajali." Kama hili ni kweli, jinsi gani linaweza kugusa njia tunazohudumu kwa wengine?
- Ni zana zipi nzuri zinapatikana katika lugha yetu? Ni zana zipi zinatakiwa kutafsiriwa au kuanzishwa kukidhi mahitaji yako katika kufanya ufuashajiji?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Soma 1Wakorintho 13:1-7 na tafakari juu ya tabia za Upendo wa Kikristo katika Ziada 2A. Chagua hali maalumu tatu mpaka tano ambazo unahitaji kutumia tabia za upendo. Katika Kitabu cha kumbukumbu zako andika jinsi ulivyotumia tabia hizi na matokeo yake.
- Uganisha orodha ya nyenzo zilizopo katika lugha yako au lugha inayolengwa ya watu unaotafuta kuwafikia katika kupanda kwako kanisa.



# Tabia za Upendo Wa Kikristo

## (1 WAKORINTHO 13:4-7)

Unapokuwa unasoma katika orodha hii muulize Munguakuonyeshe hali maalumu ambazo unahitaji kutumia tabia hizi za upendo.

### Upendo huvumilia

- Upendo unastahimili majereha bila kutoa hasira au uchungu au kulipiza maovu
- Upendo unamtumaini Mungu kufanya kazi katika maisha ya ndugu, ukiacha hukumu mikononi mwa Mungu, na bado ukimtamani ndugu aliyepoteza njia yake.

### Upendo hufadhili

- Upendo unaona shauku kuwabariki wengine, ukitamani tu yaliyo mazuri kwa ndugu, kwa huruma ukimwelewa ndugu katika udhaifu wake, na kuitikia kwenye majeraha kwa matendo ya fadhili.
- Upendo wakati wote unadhihirisha roho ya upole na huruma kwa ndugu, bila kujali ndugu huyo amefanya nini, ukijali kwa jithada kwenye mahangaiko na maumivu ya ndugu yake na kufanya kila unachowenza kufanya kumsaidia ndugu yake kuyabeba.

### Upendo hauoni vivu

- Moyo hauna chuki kwamba wengine wamefaidika au faida kwa kile ambacho hana, na hata uko tayari kutoa nafasi yake na kugeuza kwa ajili yao.
- Upendo unafurahia katika mafanikio na maendeleo ya wengine na kuwatia moyo kuendelea, hauangalii wengine kama washindani kwenye nafasi au nguvu, lakini badala yake kama washiriki kwenye injili ili kuokoka. Upendo wakati wote unauliza, "Nini ninachowenza kufanya kuwasaidia kuwa hata zaidi watumishi wa Kristo wanaotumika.

### Upendo haujivuni na hauna kiburi

- Upendo kamwe haujioni kuwa bora zaidi, "mwenye haki zaidi" mwenye hekima au vipawa kuliko wengine, ukitafuta kujijali wenywewe; lakini uko tayari kutoa tumaini, ukisifu na kutoa idhini kwa wengine
- Upendo, unakubali mipaka yake, uko tayari wakati wote kwenye maelekezo ya wengine, utayari wa kusaidiwa na wengine kuwa na uelevu wa ndani wa neno la Mungu na kuishi kwa uaminifu kwenye neno, na kiundani una fikira juu ya matokeo ya maneno yake na matendo ulionayo kwa ndugu.

### Upendo haujitalutii wenywewe

- Upendo hauna fikira za kujipatia, kujihesabia haki au kujiona kustahili, lakini badala yake una fikira kwa mema ya jumuia kwa ujumla, ukiwa tayari kutoa kwa ajili ya uzuri wa wengine hata vitu hivyo ambavyo ni haki yake.
- Wakati kutokuelewa kunapotoka (ambako wazi si swala la dhambi), upendo uko tayari kuangalia mambo kutoka kwenye mitazamo ya watu wengine na kujitoa kwenye mamlaka halisi na mapenzi yaliyoelezwa ya mwili. Upendo hautendi katika njia inayovunja umoja wa mwili. Badala yake, upendo kiunyenyekevu na kiupole unatafuta kuwasiliana juu ya mvuto wake katika njia zinazotunza umoja wa mwili na heshima kwa walio katika uongozi.

### **Upendo hauchochewi**

- Upendo haukwarzwi haraka au kuwa na hasira, inakuwa vigumu kugundua wakati wengine wanapokosea.
- Upendo unapojeruhija, haurudishi, hautafuti kisasi au kutoa vitisho; badala yake, upendo unarudisha mazuri kwa mabaya.

### **Upendo hauhesabu mabaya uliouguia**

- Upendo hauchunguzi njia za dhambi za wengine au kukalia makosa ya wengine.
- Upendo kwa haraka unasamehe kila kosa, kama mkosaji anatubu au la, na unakataa kukalia hayo badaye.

### **Upendo haufurahii udhalimu**

- Upendo haufurahii kutaja au kujadili makosa ya wengine au kuwaambia ndugu katika namna ya kihukumu au njia isiyo ya kiupendo.
- Upendo unalinda hadhi ya ndugu yake, hauenezi uvumi na majungu, lakin unajaribu kuyakataza.

### **Upendo unafurahishwa na ukweli**

- Upendo unaonea shauku ukweli kusimama katika kila hali, hata inapokuwa inaumiza kufanya hivyo, au hata kama hiyo ina maana mmoja amehakikishwa kuwa na makosa.
- Upendo unaonea shauku kujua ukweli, kutembea katika ukweli, kuukumbatia ukweli, kusimaia ukweli wa neno la Mungu, kutamani Mungu ayachunguze maneno yake, matendo na nia ili kwamba yaweweze kudhihirisha kile ambacho hakimpendezi Mungu.

### **Upendo unabeba yote**

- Hakuna dhambi iliyokubwa sana kiasa kwamba upendo hauwezi kusamehe na kujibu kwa upole.

### **Upendo unaamini yote**

- Upendo wakati wote uko tayari kumpa ndugu yake faida za mashaka, wakati wote kutafsiri maneno ya mtu mwingine na matendo katika njia zaidi ya ukarimu, na kufikia uamzi kwamba ndugu yake hakufanya kosa lolote.
- Upendo unapinga kuhukumu nia kwenye maneno na matendo ya ndugu, ukijua kwamba Mungu pekee kiukweli anajua moyo wa ndugu yake.

### **Upendo unatumaini yote**

- Upendo mara zote unatumaini kwa ajili ya mazuri; na bila kudanganywa kirahisi, uko tayari kusamehe na kumpa ndugu nafasi ya pili.
- Upendo wakati wote unatumaini kupona kabisa kwa ndugu aliyeanguka, ukitumaini na kuomba Mungu kuwa mwenye rehema kwake.

### **Upendo unavumilia yote**

- Upendo haufikii kipeo chake, kufikia kwenye "hatua ya kuvunjika"
- Upendo kamwe hausemi "hilo lilikuwa jani kavu la mwisho!"



# Jua Lengo Lako, Jua Watu Wako

- ☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kueleza wazi malengo ya kufuasa na jinsi ya kutambua ukomavu wa kiroho na ufanisi katika huduma ya wanafunzi wa mtu kwa mwanga wa malengo hayo.
- ☞ **Wazo Kuu**
  - Mfuasishaji mzuri anaelewa upambanuzi wa kibiblia wa ukuaji katika utii wa kiroho na ufanisi katika huduma.
  - Mfuasishaji mzuri anatambua hali ya kiroho ya watu wake.
  - Mfuasishaji mzuri ana lengo maalumu akilini kwa ajili ya watu wake.
- ☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoelewaka, kila mshiriki anatakiwa . . .

  - Kujua upambanuzi wa msingi wa kibiblia kwa ukomavu wa kiroho na ufanisi katika huduma.
  - Kushawishika kwamba ni muhimu kukazania moyo, kuliko tabia ya nje tu.
  - Elewa jinsi ya kuelewa kutathimini ukomavu wa kiroho na ufanisi wa huduma wa wafuasi wake kwenye mwanga wa upambanuzi wa kibiblia.
- ☞ **Ziada**

3A Karatasi ya kufanya mazoezi ya Imani, Tumaini na Upendo
- ☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Inasaidia wafunzwa kufanya kazi ziada 3A kabla hujaanza kufundisha somo hili.

## UTANGULIZI

Kama ilivyolezwa kwenye Somo la Kwanza, "Utangulizi kwenye Kufuasa", Kuna hatua tatu za lazima katika kuendeleza kufanya mpango wa kufuasa kwa ajili ya juhudzi zako za upandaji kanisa:

1. Elewa lengo lako la kufanya wanafunzi.
2. Elewa hali iliyopo ya kiroho kwa watu wako.
3. Anzisha mpango jinsi ya kuwasaidia watu wako kukua kutoka mahali walipo kuelekea kwenye lengo lako la kufanya wanafunzi.

## I. ELEWA LENGO LAKO LA KUFUASA

Hatua ya kwanza katika kuanzsisha mpango wa ufanisi wa kufanya wanafunzi ni kuelewa wazi kwenye hatima ya lengo lako. Kama ilivyolezwa katika somo la kwanza, hatima ya lengo lako katika kufuasa ni kuwawezesha watu kuishi maisha ya utii kwenye lengo lote la Kristo. Lakini hii ina maanisha nini katika hali ya kiutendaji?

### A. Upambanuzi wa Kukomaa Kiroho—Imani, Tumaini na Upendo

Tunaposoma Agano Jipy, tunaona kwamba Yesu anafupisha swala zima la utii katika misingi ya "upendo" (Mt 22:36-40). Dhana hii inaendana na mafundisho yake zaidi katika vitabu vyta Injili zote (Mt 5-7) — Mahubiri ya mlimani, Lk 7:36-50. Lk 11:39-46, Yoh 14:21, n.k.)

Baadaye, tunaona kwamba Paulo anafanya hayo hayo (Rum 13:8-10, 1Kor13:1-13; Gal 5:6, n.k.).

Biblia vilevile kwa mfululizo inatoa asili nyingine mbili muhimu za maisha ya utii: imani na tumaini (1Kor13:13). Kwa taarifa zaidi, rejea kwenye Ziada 3A, "Baadhi ya Marejeo ya Agano Jipya kwenye Imani, Tumaini na Upendo." Imani tumaini na upendo ni dalili muhimu za juu za watu wanaoishi maisha ya utii kwenye lengo lote la Kristo. Ndivyo vipimo vya kweli tu vya ukomavu kiroho. Vitu vingine vyote vinafunata haya. Kama wanafunzi wako wana haya, hivi karibuni pia watakuwa na mengine yote ambavyo ungetaka kuona kwao. Zaidi ya kila kitu kingine chote, unataka wanafunzi wako kuwa watu wa imani, tumaini na upendo.

#### B. Upambanuzi wa Mafanikio Katika Huduma

Inapokuja kwenye huduma, upendo pia ni ufunguo (Efe 4:15-16 na 1Kor 12-14). Bila kujali ni aina gani ya huduma uliyonayo, lengo ni kujenga mwili wa Kristo mpaka mwili wote "umepata kipimo chote cha ukamilifu katika Kristo." Kwa hiyo, maisha ya upendo, imani na tumaini itakuwa matokeo ya lazima kwa wengine—wote wanaoamini na wasioamini. Yesu mwenyewe alisema kwamba "...hakuja kutumikiwa..." (Mt 20:28). Tunahitaji kufata katika hatua zake.

Matokeo ni kwamba kanisa litaona yote ukuaji wa kiidadi na kitabia (mt 13:31-32). Ukuaji wa kiidadi ina maana kwamba kanisa litaongezeka katika idadi, wote mtu binafsi na kusanyiko—hii inagusa mwili wote wa Kristo ulimwenguni kote. Ukuaji wa kitabia ina maana kwamba kanisa linakua katika ukomavu unaofanana na Kristo.

## II. ELEWA HALI YA KIROHO ILIYOPO YA WATU WAKO

Mara unapobainisha lengo lako, yaani aina ya wanafunzi unaotaka watu wako kuwa, unatakiwa kuitathimini kufuatana na lengo hilo. Yafuatayo ni baadhi ya maswali yaliyopendekezwa kuanzia. Hatimaye, kwa jinsi hiyo, uwezo wako wa kutambua ukomavu wa watu wako unategemeana na ukomavu wako mwenyewe wa kiroho. Hakuna orodha, kitabu wala kipindi kinachoweza kuwa badala yake. Kadiri ulivyokomaa kiroho, ndivyo utakavyoweza kutambua wazi hali halisi ya kioho katika maisha ya hao unaowasaadia. Kadiri ya uzoefu wako mwenyewe wa undani na kuelewa imani, tumaini na upendo ulivyo, ndivyo utakavyoweza zaidi kwa wazi kutambua kuwepo na kutokuwepe kwa wengine. Kama "moyo" wako wa ufahamu wa neno la Mungu unaongezeka, utaweza kutumia neno na ujuzi zaidi na ufahamu katika kufanya wanafunzi.

#### A. Kazania kwenye Maswala ya Moyo, Siyo Tabia ya Nje

Katika kuona hali ya kiroho ya watu, ni muhimu kukazania zaidi kwenye maswala ya moyo kuliko tabia ya nje. Uwepo na ukuaji wa imani, tumaini na upendo katika moyo wa mtu ni kitu cha msingi ulicho na fikira nacho. Tabia ya nje (maneno na matendo) yanadhirisha kilicho ndani ya moyo (Mt 12:34-35, 15:18-20; Lk 6:43-45, 8:15). Ni kupoteza mda kujaribu kuzalisha tabia ya haja kama kuna tatizo kwenye moyo. Kama moyo umebadilishwa, tabia inayofaa itafata.

Kama unagundua kitu fulani kwenye tabia zao ambacho siyo sawa, jaribu kutambua sababu na nia dhidi ya matendo yao. Kwa mfano, ngoja tuseme mtu fulani hahudhuri ibada ya kanisa tena. Badala ya kukazania kwenye tabia zao na kuweka msukumo kwao wa kuhudhuria, jaribu kutambua kwa nini wameacha kuja na wahudumie katika ngazi hiyo. Kuna maswali matatu ya msingi ya kujuliza mwenyewe:

- Nini tabia inachodhahirisha juu ya wanachoamini au wasichaomini?
- Nini tabia inachodhahirisha juu ya wanachoelewa au wasichoelewa?
- Nini tabia inachodhahirisha juu ya kubadilika au tabia ya miyo yao?

Katika matukio mengi, itakuwa lazima kuongea na mtu ili kuweza kupata hasa nini kinachoendelea ndani yao.

Huduma ya kufuasa ambayo inashindwa kukazania kwenye moyo inaweza kuzalisha watu wanaoweza kuwa wazuri katika udhihirisho wa nje ambacho ndiyo kinatatokea. Kwa wakati huo, ukuaji mdogo wa kiroho utatokea.

**MUHIMU:** Ingawa badiliko la moyo haliwezi kujulikana moja kwa moja, linaweza kupimwa si moja kwa moja kwa maneo ya mtu na matendo. Jifinze kuangalia katika vipande vya tabia ambavyo vinaonyesha msingi wa tabia ya moyo wao kufuatana na maswali yafuatayo.

## B. Tathimini Ukomavu Katika Upendo, Imani na Tumaini

### 1. Jinsi ya Kutathimini Ukomavu katika Upendo

Maswali ya ufunguo ya kuuliza yanayohusu jinsi gani watu wako wamekomaa kwenye eneo la upendo:

#### a) Upendo kwa Mungu

- Wanamtamani Mungu kuliko vitu vingine vyote au mahusiano? Ni namba moja ya kipaombele katika maisha yao? Kama siyo, nini kimechukua nafasi yake katika miyo yao? Nini wanatamaini kuliko yeye?
- Wanamfurahia Mungu kuliko vyote? Wanamfurahia kuliko vingene? Kama siyo, nini wanachofuarahia zaidi yake? Nini kimechukua nafasi yake katika miyo yao?
- Wana moyo mmoja, roho na akili na Mungu? Kama siyo, nini kimechukua nafasi yake katika miyo yao? Kwa nani au nini miyo yao na akili imeelekea? Na nani au nini wanachojilinganisha? Nani uthamani wao unamuonyesha? Uaminifu wao umegawanyika?
- Jinsi gani wanatembea katika upendo huu kwa kuendelea? Wakati gani wanaanguka, jinsi gani wanafanya haraka kutubu na kuanza kutembea na Mungu tena?
- Wanadhihirisha upendo wowote (usiofaa) kwenye ulimwengu huu? Lazima tufahamu uzito wa swala hili. Kwa hakika ni swala la kiibada ya miungu. Kwa nani na kwa nini mtu ametoa moyo wake ni swali la pekee muhimu tunalokutana nalo katika maisha haya. Wengi wataonyesha miyo iliyogawanyika, wakijaribu kumpenda Mungu na ulimwengu wakati huo huo. Wasaidie wanafunzi wako kutambua kutewezezana kwa nafasi hiyo (Mt 6:24, Yak 4:4-5, 1Yoh 2:15-17). Upendo kwa ulimwengu na upendo kwa mungu hauendani. Mmoja au mwengine utashinda mwishoni. Udhihirisho wazi wa kuendelea kupenda ulimwengu unaonyesha kwamba upendo wao kwa Mungu au umekufa au unakufa, bila kujali jinsi gani "kidini" wanaonekana kwa nje. Ukuaji kiroho hauwezekani mpaka hili linaposhughulikiwa. Tazama orodha ambayo Paulo aliandika akieleza matunda ya mwili. Haya ni nyongeza inayoonyesha kwamba kuupenda ulimwengu kupo miyoni mwao (Gal 5:19-21; 1Kor 6:9-10; Rum 1:28-32; Yak 3:14-16).

#### b) Upendo kwa Wengine

- Wanatamani kuwa na ushirika wa kweli na waumini wengine (Ebr 10:24-25) na kutumia mda pamoja nao? (Flp 4:1, 1The 2:17-18).
- Wanawafurahia waumini wengine? Wanafurahishwa na waumini wengine? Efe 1:15-16, Flp 1:3-8, 4:1, 1The 2:19-20, 3:9).
- Wana moyo mmoja na akili na kaka na dada zao katika Kristo? Wanaonyesha kwa njia za vitendo umoja wao na upendo? (Mdo 4:32-35, Rum 12:10-21, 1Kor 13:4-7, Flp 1:27, 2:1-4, Ebr 13:3).
- Wanapenda familia zao? Wanahudumia familia zao kila mara kwa upendo, wakiimarisha umoja wao kama familia na kujenga kila mjambe kwa Kristo? (Efe 2:25-6:4).
- Wana moyo kwa waliopotea? Wanaonyesha kila mara upendo kwa waliopotea? (Gal 6:10).

### 2. Jinsi ya Kutathimini Ukuaji katika Imani

Swali la ufunguo la kuuliza kuhusu jinsi watu wako wamekomaa kwenye eneo la imani:

- a) Wanaelewa imani ni nini?
- b) Wanaelewa neema ya Mungu?
- c) Imani yao imejengwa imara kwenye maandiko? Wanaelewa vyta kutosha ukweli wa kibiblia (Rum 10:17)?

- d) Wana mvuto wa ndani kwamba Mungu anawapenda kuhusu ukweli huu?
  - e) Wana mvuto wa ndani kwamba Mungu anawapenda na amewakubali kikamilifu katika Kristo?
  - f) Wanaishi kwa imani, wakitegemea neema ya Mungu katika kila eneo la maisha yao?
3. *Jinsi ya Kutathimini Ukomavu katika Tumaini*

Maswali ya ufunguo ya kuuliza kuhusu jinsi watu wako walivyokomaa kwenye eneo la tumaini:

- a) Miyo yao imeelekezwa kwa Kristo na wito wake kwao? (1Yoh 3:1-3). Hivi ndivyo hasa wanavyoishi kwa ajili? (Flp 3:7-14).
- b) Wanaelewa ahadi za Mungu kwao? (Rum 4:18-24)
- c) Wana shawishika kuwa Mungu anasababisha mambo yote kufanyika kwa ajili ya mazuri kwao, kuwaandaa kwenye mwisho alio nao kwa ajili yao? (Rum 8:28-30)

### C. Tathimini Ufanisi Katika Huduma ya Wengine

Kadiri wanafunzi wako wanavyokua katika imani, tumaini na upendo, wanatakiwa kuwa zaidi na zaidi wafanisi katika huduma kwa wengine. Swalii la ufunguo la kutafakari ni:

- Ni wafanisi kwa kutumia vipawa vyovoyote walivyonyavyo na uwezo Mungu aliowapa kuwajenga wengine katika upendo, imani na tumaini? (Efe 4:11-13, 15-16).
- Wanawatia moyo na kuwawezesha watu kukua katika umoja na Mungu na mmoja kwa mwengine? Wanawawezesha wengine kuishi maisha ambayo yanadhihirisha upendo huo wa kimungu ambao unawasilisha muungano huu.? Ebr 10:24-25).
- Wanawapa ndugu msaada wa vitendo wanaohitaji ili kushinda ugumu wa kiroho katika maisha yao? (Rejea kwenye Somo la 4 la Kufanya Wanafunzi, "Kuwasaidia Wanafunzi Kukua Kiroho.")
- Wanawakilisha Injili kwa ufanisi kwa waliopotea? (1The 1:8).
- Wanawaoongoza waliopotea kwa ufanisi kwa Kristo na kuwashirikisha kwenye mwili wa Kristo?
- Wametiwa moyo na kuwawezesha wakristo wengine kwa ufanisi kuwasilisha injili kwa waliopotea kwa maneno na matendo?

### III. MIPAKA YA VITENDO KATIKA KUFUASA

- **Tumia mda pamoja nao mara kwa mara.** Wafurahie na waonyeshe kuwa una moyo na akili moja nao. Angalia katika tabia za upendo kwa wengine ambazo zimeelezewa katika Rum 12:10-21, Flp 2:1-8 na 1Kor 13:4-7.
- **Panga mda wenu pamoja.** Ukuaji wa kiroho katika ufuasishaji hautokei kwa kubahatisha. Wanafunzi wanafanya, na siyo kuzaliwa. Kila mwanafunzi ana mahitaji maalumu, na unahitaji kugusa mahitaji haya katika njia iliyoandaliwa.
- **Shirikisha mahangaiko yako.** Kushirikisha mahangaiko yako na kuwa wazi kwenye mahitaji ya kila mmoja kunasaidia kufanya mshikamano kati yenu na wanafunzi wenu.
- **Ombe pamoja.** Ombeeni matatizo yaliyowapata na majibu yaliyotolewa kwenye hali. Muulize Mungu kuwaonyesha jinsi ya kuonyesha upendo kama huo kwa watu aliokupa, kwa njia ambazo wataitikia na kukua.
- **Jifunze pamoja.** Someni vitabu pamoja na shirikisha vitu mnayojifunza. Jifunze maandiko pamoja, mkiyatulia katika matatizo ya kila siku.
- **Muwe wabunifu.** Tumieni mda kiubunifu kukanilisha makusudi mengi. Fanya kazi pamoja, ombe pamoja, muwe na milo pamoja. Washangaze waumini wapya kwa ukweli wako, nia ya hali ya juu kwo.
- **Upatikane.** Ni muhimu kwamba wanafunzi wako wanajua unapatikana kujibu maswali na kushauri kuhusu mashaka yanayotokea katika maisha ya kila siku.

- **Tafuta ushauri na msaada kutoka kwa Wakristo wengine.** Kama ni dhaifu katika maeneo haya (yaani kuonyesha upendo), tafuta msaada unaohitaji ili kufanya maendeleo haya.

#### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Katika mwanga wa hatima ya kusudi la Mungu, Ina maana gani kukomaa kiroho? Ina maana kuwa mfanisi katika huduma?
- Ni kwa kiasi gani unafikiri watu wako wamekomaa, wanapopimwa kwa imani, tumaini na upendo? Ni wapi ukuaji unahitajika sana? (kama bado hujaanza kufanya kazi na yeoyote, tumia maswali haya kwako mwenyewe .)
- Ni kwa ufanisi kiasi gani unafikiri watu wako wanao kwenye huduma kwa wengine katika mwanga wa upambanuzi wa hapo juu? (kama bado hujaanza kufanya kazi na yeoyote, tumia maswali haya kwako mwenyewe .)

#### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Malizia karatasi ya mazoezi iliyo katika Ziada 3A, “ karatasi ya mazoezi ya Imani, Tumaini na Upendo



## Imani, Tumaini na Upendo KARATASI YA MAZOEZI

Chini kuna vifungu vya maandiko kadhaa ambavyo vilikuwa vimegusia kwenye makanisa kadhaa ya Agano Jipy. Tafadhari zungushia kila kutokea kwa neno "imani", "tumaini" na "upendo" katika vifungu hivi, ukitumia rangi tofauti kwa kila neno.

**Warumi 5:1-5** "1Kwa kuwa tumeshahesabiawa haki kutokana na imani, tuna amani na Mungu kuititia Bwana wetu Yesu Kristo, 2ambaye kwa ye ye tumepeata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo tunasimama ndani yake sasa. Na kufurahia katika tumaini la utukufu wa Mungu. 3Siyo hivyo tu, lakini pia tunafurahia dhiki yetu, kwa sababu tunajua kwamba dhiki inazaa saburi; 4saburi uthabiti wa moyo na uthabiti wa moyo, tumaini. 5Na tumaini halitutahayarishi, kwa sababu Mungu amemwaga upendo wake miyoni mwetu kwa Roho Mtakatifu, ambaye ametupa."

**1Wakorintho 13:13** "Na sasa haya matatu yamabakia: imani, tumaini na upendo. Lakini kikubwa kati ya haya ni upendo."

**Wagalatia 5:5-6** "5Lakini kwa imani, tunasubiri kwa kutazamia kuititia Roho haki ambayo tunatumaini. 6Kwa kuwa katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno wala kutotahiriwa hakufai neno. Kitu tu kinachofaa ni imani inayojionyesha kwa upendo.

**Waefeso 1:15-18** "15Kwa ajili hii, tangu niliposikia juu ya imani yenu katika Bwana Yesu na upendo wenu kwa watakatifu wote, 16sijaacha kuwashukuru, nikiwakumbuka katika maombi yangu. 17Ninaendelea kumuuliza Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Mungu wa utukufu, awape roho ya hekima na mufunuo, ili kwamba mmujue zaidi. 18Ninaomba pia kwamba macho ya miyo yenu yafunguliwe ili kwamba muweze kujua tumaini alilowaitia, na utajiri wa urithi wa utukufu wake kwa watakatifu.

**Waefeso 3:14-19** "14kwa ajili hii napiga magoti mbele za Baba, 15 ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa. 16Ninaomba kwamba kutokana na utajiri wa utukufu wake aweze kuwaimarisha kwa nguvu kuititia Roho wake katika utu wenu wa ndani, 17ili kwamba Kristo akae miyoni mwenu kwa njia ya imani. Na ninaomba kwamba msimikwe na kuwekwa katika upendo, 18muwe na nguvu, pamoja na watakatifu wote, jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina upendo wa Yesu, 19na kujua upendo huu unaopita fahamu—ili muweze kujazwa kuwa kipimo cha ukamilifu wote wa Mungu."

**Wakolosai 1:3-5, 22-23** "3Mara zote tunamshukuru Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu kristo, tunapowaombea, 4kwa sababu tunasikia juu ya imani yenu katika Kristo Yesu na upendo mlio nao kwa watakatifu wote—5imani na upendo unaochanua kutoka kwenye tumaini mliyowekewa mbinguni na kwamba mmeshasikia juu ya neno la kweli, injili..." "22Lakini sasa amewapanatanisha kwa mwili wa Kristo kwa kifo chake kuwakabidhi watakatifu machoni, bila doa na huru wasio na lawama—23kama mkidumu katika imani yenu, mumewekwa kwenye msingi na mkawa imara, bila kuhamishwa kutoka katika tumaini lililo katika injili. Hii ndiyo injili mliyosikia na kwamba imehubiriwa kwa kila kiumbe chini ya mbingu, na ambaye mimi, Paulo, nimekuwa mtumishi."

**1Wathesalonike 1:2-3** "2Mara zote tunamshukuru Mungu kwa ajili yenu nyote, tukiwataja katika maombi yetu. 3Tunaendelea kukumbuka mbele za Mungu wetu na Baba kazi yenu iliyozalishwa na imani, na taabu yenu ya upendo, na saburi yenu inayovutwa na tumaini katika Bwana wetu Yesu Kristo."

**1Wathesalonike 3:6** “6Lakini Timotheo alipotujia hivi sasa kutoka kwenu ametuletea habari njema kuhusu imani yenu na upendo. Ametuambia kwamba mna kumbukumbu zetu nzuri na kwamba mnatamani katuona, kama vile nasi tunavyotamani kuwaona.”

**1Wathesalonike 5:8** “lakini sisi tulio wa mchana, tuwe na kiasi, tukijivika imani na upendo, na chepeo yetu iwe tumaini la wokovu.”

**2Wathesalonike 1:3-4** “3Imetupasa kila mara kumshukuru Mungu kwa ajili yenu, ndugu, kama ilivyo wajibu, kwa sababu imani yenu inazidi, na upendo wa kila mtu kwa mwenzake unaongezeka. 4Kwa hiyo, mionganii mwa makanisa ya Mungu tunaona fahari juu yenu kwa ajili ya saburi yenu na imani katika mateso yote na majaribu mnayostahimili.”

**1Timotheo 1:5** “5Lengo la amri hii ni upendo, unaotoka katika moyo safi na dhamiri njema na imani isiyo ya unafiki.”

**2Timotheo 1:13** “13Mlichosikia kutoka kwangu, tunza kama kielelezo cha mafundisho yanayosikika, kwa imani na upendo ulio katika Kristo Yesu.”

**Filimon 4-7** “4Mara zote ninamshukuru Mungu ninapowakumbuka katika maombi yangu, 5kwa sababu ninasikia juu ya imani yenu katika Bwana Yesu na upendo wenu kwa watakatifu wote. 6ninaomba kwamba muwe na bidii katika kushirikisha imani yenu, ili kwamba mpate kuwa na kuelewa kikamilifu kila kitu kizuri tulichonacho katika Kristo. 7 Upendo wako umenipa furaha kubwa na kutiwa moyo, kwa sababu wewe, ndugu, umeburudisha mioyo ya watakatifu.”

**Waebrania 6:10-12** “10Mungi si dharimu, hatasahau kazi zenu na upendo mliomuonyesha kama muliviyowasaida watu wake na kuendelea kuwasaidia. 11Tunataka kila mmoja wenu kuonyesha bidii ile ile mpaka mwisho, ili kufanya tumaini lenu hakika. 12hatutaki muwe wavivu, lakini muwe wafuasi wa hao wazirithio ahadi za Bwana kwa imani na uvumilivu.”

**Waebrania 10:22-24** “...22Ngoja tumkaribie Mungu kwa moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani hali tumenyuyiziwa miyo tuache dhamiri mbaya na miili yetu ikiwa imeoshwa kwa maji safi, 23Na tulishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke, maana aliyahidi ni mwaminifu sana. 24Ngoja tuangalie jinsi tunavyoweza kuhimizana sisi kwa sisi kwa kazi nzuri na upendo.”

**Yakobo 2:5** “5Sikiliza, ndugu wapendwa: Mungu hakuwachagua walio masikini machoni pa ulimwengu kuwa matajiri katika imani na kurithi ufalme aliowaahidia wanaompenda?”

**1Petro 1:3-9, 21-22** “3Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo! Katika rehema zake kuu alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu, 4tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu, nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu uliotayari—kufunuliwa wakati wa mwisho. Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali. 7Illi kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, ionekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo. Naye mwampenda ijapokuwa hamukumuona, ambaye hamumwoni sasa ; mniamwami na kufurahi sana kwa furaha isiyoneneka, yenye utukufu, 9katika kuupokea mwisho wa imani yenu, yaani wokovu wa roho zenu. 21 Ambao kwa ye ye mmekuwa wenye kumwamini Mungu, aliyemfufua katika wafu akampa utukufu; hata imani yenu na tumaini lenu liwe kwa Mungu. 22Mkishakujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo.”



## Kuwasakiya Kukua Kiroho

Wanafunzi

**Kusudi la Somo**

Makusudi mawili ya somo hili ni kumtayarisha mpanda kanisa kutambua vitu ambavyo wakristo wanahitaji (1) Kujua na kufanya ili kuishi maisha ya upendo, imani na tumaini na (2) kuwaandaa kushughurikia kawaida kinachosababisha mahangaiko ya kiroho.

**Wazo Kuu**

- Kila muumini anakutana na mahangaiko ya kiroho
- Msaada unaofaa kwa mda unaofaa unaweza kuzuia kudumaa kiroho na kutia moyo ukuaji.
- "Kujua " na "kufanya" ni vya lazima ili kuishi maisha ya kimungu na kuhudumu kwa wengine.

**Matokeo Yanayotarajiji**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoelewaka, kila mshiriki anatakiwa...

- Kuelewa na kuweza kutambua kawaida kinachisababisha zaidi mahangaiko ya kiroho kwa waumini wapya.
- Kuwa macho kwa njia zinazofaa za kushughulikia vipingamizi hivi ili kuongeza maendeleo ya kiroho.
- Kuweza kutambua vitu vya dharura zaidi waumini wapya wanavyohitaji kujua na kufanya ili kuishi maisha ya upendo, imani na tumaini na kwa ufanisi kuwashudumia wengine.

**Ziada**

4A Ukuaji Kiroho Unahitaji Tathimini

**Ushauri Kwa Wakufunzi**

Kulingana na uzoefu wako mwenyewe, jaza Ziada 4A kabla ya darasa na tayarisha ubao wa kuonyeshea yaliyomo kwenye darasa. Jaribu kulipa darasa wazo zuri la ni nini wanachojaribu kufanya na karatasi hizi za mazoezi.

Sisitizia nyenzo iliyopo katika mchoro 4.1

### UTANGULIZI

Kama wapanda kanisa, sehemu ya kazi yetu ni kuhakikisha kanisa jipya linakua kiroho. Katika kipindi hiki tutajadili baadhi ya kawaida na vizuizi vya mahangaiko ya kiroho katika maisha ya muumini mpya.

#### I. GUNDUA CHANZO CHA KAWAIDA CHA MAHANGAIKO YA KIROHO

Kuna moja zaidi muhimu la kufikiria ambalo lazima ulishughulikie kama utatambua na kushughulikia hali ya kweli ya kiroho ya watu wako. Hiki ni kipingamizi kikubwa cha kiroho katika maisha yao. Ni nini sababu za kawaida za kuhangai kiroho? Nini kinawazuia wasiishi maisha ya upendo, imani na tumaini? Nini kinawazuia kutokuhudumia wengine kwa ufanisi? Ili wanafunzi wako wakue, unatakiwa utafute njia za kuwasaidia kushinda vipingamizi hivi.

Badhi ya kawaida zinazosababisha mahangaiko ya kiroho ni kama ifuatavyo:

#### A. Waumini Wapya Wanakosa Kuelewa

- Wanashindwa kuelewa baadhi ya funguo za ukweli wa kibiblia
- Hawajui jinsi ya kufanya kinachitakiwa. Hawana uhakika na nini la kufanya au jinsi ya kulifanya (kwa mfano: Kushirikisha injili mtu, kutumia mda na Mungu katika maneno yake na maombi, n.k.)
- Hawana uhakika na jinsi gani ya kuweza kuhusika katika huduma kwa wengine.

#### B. Waumini Wapya Wanakosa Utayari Wa Kutii

- Ni wasahafulifu, au wanakatishwa kiurahisi.
- Wanataka kutii, lakini wanasahau tu kufanya wanachotakiwa kufanya. Katika ulimwengu wenye haraka unaowazunguka, wanasahau vipao mbele vyao na kuzingwa na mambo mengine.
- Wanaelewa ukweli, lakini hawauamini kweli kweli.
- Wameruhusu upendo wa dunia kuwazinga au wamekuwa watumwa wa dhambi.
- Wamevunjika moyo na kuachia.
- Wamekatishwa tamaa kwa Mungu au wakristo wengine na sasa wana hasira nao.
- Hofu inawakandamiza nyuma
- Wanakosa hamasa
- Kama wamepoteza hamasa, jaribu kutafuta kwa nini. Sababu kawaida huwa ni moja au zaidi ya matatizo yaliyotajwa hapo juu.

#### Jedwali 4.1 Kushughulikia Vyanzo Vya Mahangaiko ya Kiroho

TATIZO	WANACHOHITAJI
<p>Wanashindwa kuelewa baadhi ya funguo za ukweli wa kibiblia.</p> <p>Pengine mtu anashindwa kwa sababu ama anamjua Mungu ama si kusudi la mungu kwa ajili yake, kwa sababu haelewi imani ya kweli ni nini wala jinsi ya kuishi kwa imani, kwa sababu haelewi tumaini alilonalo katika Kristo. Pengine haelewi utoaji wa Mungu kwa ajili yake katika Kristo na katika mwili wa Kristo, kwa sababu haelewi upendo wa Kristo kwake wala inavyomaanisha kumpenda Mungu kweli kweli na wengine, au kwa sababu haelewi ina maana gani kuwa sehemu ya mwili wa Kristo, n.k.</p>	<ul style="list-style-type: none"><li>• Masahihisho na maelekezo ambayo yanawasilisha wazi wazi ukweli wa kibiblia wanaoshindwa kuelewa na jinsi ya kuutumia kwenye maisha yao.</li><li>• Nafasi ya kujifunza maandiko kwa undani zaidi.</li><li>• Kutiwa moyo kuwa wanafunzi wa neno na maelekezo kwenye ujuzi wa lazima.</li><li>• Nafasi za kuchunguza watu wanaoonyesha maana ya ukweli huo katika maisha yao wenywewe.</li></ul>
<p>Hawajui jinsi ya kufanya kinachotakiwa.</p> <p>Hawana uhakika na nini la kufanya au jinsi ya kulifanya. Pengine jinsi binafsi wanavyotembea na Mungu (kwa mfano, kuomba, kujifunza Biblia, kuwa na mda wa kimya, n.k.). Au, pengine huduma ya vitendo kwa wengine ( kwa mfano, kufundisha, kutia moyo, kuongoza neno kwenye sala ya familia, kutoa ushuhuda binafsi, kushirikisha injili kwa wasioamini, n.k.</p>	<ul style="list-style-type: none"><li>• Kutiwa moyo kutumia wanayojifunza.</li><li>• Nafasi za kuchunguza watu wanaofanya kinachotakiwa.</li><li>• Maelekezo na mafunzo ya vitendo katika ujuzi wao unaohitajika.</li><li>• Kama inahitajika, saidia katika kuendeleza mkakati wa vitendo kufanya kinachohitajika.</li><li>• Nafasi zinazofaa kufanya mazoezi ya kile wanachojifunza, na usaidizi wa kutoa matokeo.</li><li>• Ushauri wa vitendo na msaada wanapoendeleza ujasiri na ujuzi.</li></ul>

TATIZO	WANACHOHITAJI
Hawana uhakika na jinsi gani ya kuweza kuhusika katika huduma kwa wengine.	<ul style="list-style-type: none"><li>Saidia kuona nafasi tofauti tofauti za huduma na ushauri wa kuweza kuhusika.</li><li>Watu wanaoonyesha shukurani za kweli za juhudii zao.</li><li>Wengine waliohayari kuwaruhusu kuwahudumia wakati wakiendelea.</li></ul>
Kwa kifupi wanashahau, au wanakatishwa kiurahisi.  Wanataka kutii, lakini wanashahau tu kufanya wanachotakiwa. Katika ulimwengu wa haraka unaowazunguka, wanashahau vipao mbele vyao na kuzingwa na mambo mengine.	<ul style="list-style-type: none"><li>Ukumbusho unaoendelea wa kufuutilia.</li><li>Kuchocha kunakoendelea na msaada wa kufanya kinachotakiwa. Kwa vitendo.</li></ul>
Wanaelewa baadhi ya ukweli maalumu lakini kweli hawaukubali.	<ul style="list-style-type: none"><li>Onyo la upole kwa kutoamini na shauri kuamini.</li><li>Sababu ya kuamini ukweli maalumu wanaokataa.</li><li>Nafasi za kuchunguza watu wanaotumia ukweli huu kwa miyo yote katika maisha yao wenyewe.</li></ul>
Wameruhusu upendo wa dunia kuwazinga au wamekuwa watumwa wa dhambi.  Hofu ya ulimwengu, udanganyifu wa utajiri, na haja ya vitu vya kidunia kunaweza mara nyingi kuwa kwa kulemeza. Mkristo ambaye hajakomaa, na hata hao waliokomaa zaidi, wanawenza wakawa hawana uwezo wa kupenda kipinga (Gal 5:17; Mt 13:22, 1Tim 6:8-10, Yoh 2:15-17).  Dhambi inaleteleza kufa kiroho. Roho Mtakatifu anazimishwa. Mtu anakosa nguvu ya kukabili dhambi yake. Anapoteza nguvu ya kumfata Kristo. Anakosa nguvu ya haja ya ushirika wa kweli na anashawishika kumuacha Mungu na ndugu wengine. Mtu anageuka kuwa mtumwa wa dhambi na hayuko tayari tena au kuweza kuvunja kuwa huru mwenyewe (Yoh 8:34, Yak 1:14-15, Ebr 3:13).	<ul style="list-style-type: none"><li>Ushauri wa vitendo na msaada wa karibu kushughulikia udhaifu wao maalumu na kuepuka majoribu.</li><li>Kusaidia katika utambuzi wa dhambi zao au sehemu yenye mapungufu.</li><li>Onyo la upole na ukumbusho wa uzito wa dhambi zao.</li><li>Kutiwa moyo kutubu kwa ajili ya dhambi maalumu.</li><li>Ushauri wa vitendo na msaada wa karibu kushinda dhambi.</li><li>Msaada wa karibu katika kuendeleza tabia mpya.</li><li>Baada ya toba, hakikisho la msamaha.</li><li>Msaada wa karibu kuanza kutembea tena katika roho.</li></ul>

TATIZO	WANACHOHITAJI
<p>Wamekatishwa tamaa na au kuwa wenyе hofu.</p> <p>Katika Agano Jipyа kukatishwa tamaa mara nyingi ni matokeo ya mateso (kutokana na kuteswa au kupoeza –Mt 13:20-21, Ebr 12:3). Watu wako wanaweza kukutana na upinzani kutoka kwenye familia, marafiki au watumishi wa kanisa la mtaa. Hofu ya kukataliwa au upotevu inaweza kuwakatisha tamaa kumfata Kristo. Kukatishwa tamaa kunaweza pia kukatokana na matarajio ya uongo wa maisha ya kikristo yatakavyokuwa, ya kile Mungu atakachomfanyia, au kile kanisa au wakristo walivyo.</p> <p>Kukata tamaa kunaweza kutokana na kushindwa kwake mwenyewe kiroho. Matokeo yake, anaanza kuwa na mashaka kama anaweza maisha ya kikristo au kujisikia kwamba Mungu hawezi tena kumkubali. Anaweza hata akaanza kuwa na mashaka juu ya wokovu wake. Mwishoni anaweza kuwa amekatishwa tamaa sana na kwa kifupi kuachia. Kushindwa katika kujaribu huduma inaweza kumsababisha kupoteza mvuto.</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ukumbusho wa ahadi za Mungu.</li> <li>• Uendelevu wa hakikisho la upendo, kukubalika, na msamaha.</li> <li>• Hakikisho kuwa hawako peke yao.</li> <li>• Uendelevu wa kutiwa moyo kuendelea.</li> <li>• Msaada wa vitendo kukabili hofu zao na kufanya linalohitajika bila kujali hilo.</li> <li>• Hakikisho la ulinzi wa Mungu na baraka kwenye uaminifu.</li> <li>• Uendelevu wa Kutia moyo kutumaini katika Mungu.</li> </ul>
<p>Wamekatishwa tamaa kwa Mungu au wakristo wengine na sasa wana hasira nao.</p> <p>Wakati mwininge waumini wapya wana matarajio yasiyo kweli ya jinsi gani maisha ya kikristo yatakavyokuwa. Wakati matarajio yao yanapokuwa hayakutimizwa, wanakuwa na hasira na Mungu. Au, wakristo wengine wanapowaangusha, wanakuwa na hasira na hawataki tena kuwa pamoja nao. Wakati mwininge wanaweza pia kulaumu Mungu kwa kile-kinachoitwa wakristo wamefanya.</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Maelekezo kuleta matarajio yao kwenye mstari na neno la Mungu.</li> <li>• Kutiwa moyo kuona Kusudi kubwa la Mungu katika kuruhusu mambo hayo katika maisha yao.</li> <li>• Onyo la upole siyo kumlaumu Mungu kwa kushindwa kwa wakristo.</li> <li>• Onyo la upole kuwasamehe wengine kama mungu alivyowasamehe.</li> </ul>
<p>Katika maeneo yote hapo juu:</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Wanahitaji kaka/dada waliojitoa kwao kwa upendo (Rum 12:10).</li> <li>• Wanahitaji watu watakaowaombea na kuomba nao.</li> <li>• Wanahitaji watu watakaowakumbatia kuwajibika mbele za Mungu.</li> <li>• Wanahitaji watu watakaoendelea kuwaangalia miyo yao.</li> <li>• Wanahitaji watu watakaofanya lolote linalohitajika kuwasaidia kushinda matatizo yao ya kiroho na kukua.</li> </ul>

## II. ONYESHA MSAADA WAUMINI WANAOHITAJI KUSHINDA VIPINGAMIZI VYA KIROHO

Unapokuwa unafahamu mahangaiko yao makuu ya kiroho, lazima ujiulize mwenyewe: ni aina gani ya msaada watu hawa lazima wapokee ili kuweza kushinda vipingamizi hivyo? Ni aina gani ya msaada lazima wapate ili waendelee kuishi maisha ya upendo, imani na tumaini? Nini wanatakiwa wawe nacho kuweza kuhudumu kwa ufanisi kwa wengine?

Katika hatua hii lazima uwe mkweli kabisa. Kila mmoja wa watu wako wanakutana na matatizo haya. Wachache wao wataweza kushinda vipingamizi hivi wao wenyewe. Kama hawapokei aina ya msaaa unaofaa, maisha yao ya kiroho yatafikia kusimama. Ni jukumu lako kuhakikisha wanapokea msaada wanaohitaji.

Maandiko yanaliweka wazi kabisa kwamba kufundisha na kuhubiri hakutoshi. Ni matatizo mangapi ya kila mara yalioonekana katika jedwali 4.1 yanayoweza kutatuliwa kwa maelekezo peke yake? Machache kati yake. Biblia inazungumzia hunduma nyingine muhimu nyingi katikati ya mwili wa Kristo, kama vile

- kuonya, kutia moyo, kusaidiana sisi kwa sisi (1The 5:14),
- kusahihisha na kuonya (1Tim 4:2),
- kukanusha (Tit 1:9).
- Kugeuzana kutoka kwenye dhambi (Yak 5:19-20),
- kuamnbiana ukweli katika upendo (Efe 4:15),
- Kushauriana (Kol 3:16),
- kutiana moyo na kujengana (1The 5:11),
- kusisimuana kupendana na matendo mema (Ebr 10:24),
- kuimarisha wadhaifu (Ebr 12:12),
- kufariji na kubishana (1The 2:11-12),
- kuimarishana, kubebeana mzigo (Gal 6:1-2),
- kubebana mmoja kwa mwingine (Efe 4:2),
- kusameheana (Kol 3:13),
- Kuombeana (Efe 6:18, Yak 5:16, iYoh 5:16),
- kutubiana dhambi mmoja kwa mwingine (Yak 5:16),
- kuhudumiana (Gal 5:13),
- kukubaliana mmoja kwa mwingine (Rum 15:7),
- kuheshimiana (Rum 12:10),
- kutendeana mema (Gal 6:10).

Kama mwanafunzi wako kweli ameweka moyo wake kumfata Kristo, atakaribisha aina hii ya msaada. Zungumza naye juu ya hili na pata ruhusa yake kumsaidia katika njia hizi. Kwa hiyo, inapokuwa lazima kumsaidia kushughulika na baadhi ya maswala, haitakuja kama kushitusha.

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni nini baadhi ya sababu za kawaida katika kushindwa kiroho kwa waumini wapya?
- Kwa nini wanashindwa kuhudumia wengine kwa ufanisi?
- Nini ukweli muhimu zaidi wanaoshindwa kulelewa au kuamini?
- Ni vitu gani muhimu zaidi wanavyoshindwa kufanya au wasivyojua jinsi ya kuvifanya?
- Ni aina gani ya msaada ni wa muhimu zaidi kwa waumini wapya katika mwanga wa vizuizi vyao zaidi vya kawaida?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Soma kwa karibu jedwali 4.1 “Kushughulikia Vyanzo vya Mahangaiko ya Kiroho.”
- Soma na tafakari Ziada 4A, “Kukua Kiroho Kunahitaji Tathimini.” Malizia fomu ya tathimini na jibu majibu mwenyewe na angalau kwa mmoja wa wanafunzi wako.



## Ukuaji Kiroho Unahitaji Tathimini

(Jina la mtu)

	Sioo tatizo				Tatizo kubwa
	1	2	3	4	5
1. Anashindwa kuelewa baadhi ya funguo za ukweli wa kibiblia					
2. Kutojua kufanya linalotakiwa					
3. Kutokuwa na hakika kwa jinsi ya kuhusika katika huduma kwa wengine					
4. Anajua baadhi ya ukweli maalumu lakini haukubali kabisa					
5. Kwa kifupi anasahau au rahisi kukatishwa					
6. Anaruhusu upendo wa ulimwengu kumshinda au anakuwa mtumwa wa dhambi					
7. Amekatishwa tamaa					
8. Anaogopa					
9. Wamekatishwa tamaa kwa Mungu au wakristo wengine na sasa wana hasira nao.					
10. Wanakosa mvuto					
11. Mengine					

1. Kama wanafunzi wako wanashindwa kuelewa baadhi ya ukweli wa ufunguo wa kibiblia, ni ukweli gani maalumu wanahitaji kujifunza?
  2. Kama hawajui jinsi ya kufanya wanachohitaji kufanya, ni ujuzi gani maalumu wanaohitaji kujifunza?
  3. Kama wanaelewa baadhi ya ukweli maalumu lakini hawaukubali hasa, ni ukweli gani maalumu wanahitajika kuuamini?
  4. Ni mifumo gani ya msaada wanayohitaji wanafunzi wako kwa dharura?



# Mifumo ya Kufuasa

**Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwawezesha wafunzwa kuelewa baadhi ya “mifumo” ya msingi inayoweza kutumika katika kufuasa na kuanza kuandika mpango wa kufuasa ulioandaliwa halisi kwa waumini wapya.

**Wazo Kuu**

- Kufuasa hakuzuiliwi na mtindo wowote; kila mmoja una faida zake na upungufu.
- Jukumu kuu la wapanda kanisa katika kufuasa ni kufuasa viongozi watakaoweza kufuasa wengine.
- Kuanzisha mpango wa kufuasa kwa waumini wapya ni wa maana kwa ukuaji wa kimwili na kiroho kwa kanisa.

**Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoelewaka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa mifumo minne ya msingi katika kuendesha kazi ya kufuasa.
- Kushiriki katika kuandaa mpango wa kutumika kufuasa waumini wengine. . .

**Ziada**

5A Kufanya Mpango wa Kufuasa

**Ushauri kwa Wakufunzi**

Uwe na hakika wafunzwa wanaelewa agizo la “utekelezaji wa azimio” lao. Lazima waje na mipango yao ya kufuasa kwenye mafunzo ya Mwongozo wa Nne. Maliza kabla ya mda nakara yako ya Ziada 5A, “Mpango wa Kufuasa” kama kwa waumini wapya “halisi”. Uandae ili kuonyeshwa kwenye kibao kama mfano kwa darasa.


Wafunzwa washirikishe walichopata kuwa cha ufanisi kutoka kwenye ufuasishaji wao wenyewe na uzoefu wa kufuasa. Waalike wafunzwa kufanya kama hivyo.

## UTANGULIZI

Mpaka sasa tumeweka mkazo wetu kwenye **kazi** za kufuasa. Tumeona kwamba **kazi** muhimu zaidi inahudumia kusudi moja la kati: kuwawezesha watu kuishi maisha ya upendo, imani na tumaini. Hatimaye, maisha kama hayo ni matokeo ya mabadiliko ya ndani ya kiroho, kubadilishwa kwa moyo. Mabadiliko haya ya ndani yanajionyesha yenyewe katika njia mpya ya kufikiri na njia mpya ya tabia. Njiani, ukweli mpya lazima uwe umemezwa na ujuzi mpya lazima uwe umejifunzwa. Katika mda huo huo, msaada wa nguvu unahitajika ili kwamba vipingamizi vyta kiroho viweze kushindwa. Kwa hiyo, **kazi** tatu za kufuasa ambazo ziko miongozni mwa zile muhimu ni “ 1)Mawasiliano na ukweli nyeti, 2) Maendeleo ya ujuzi wa lazima, na 3) kutolewa kwa msaada wa kiroho unaohitajika.

Na sasa tunakabiliana na swalii la **mfumo**. Ni muundo gani na njia tunazotakiwa kurithi ili kuhakikisha kwamba “kazi” ya kufuasa inafanyika kwa ufanisi? Kuna aina nne za mifumo ya msingi inayoweza kutumika katika kufuasa. Mifumo hii inaweza kutumika sambamba na haimaanishi kuwa ya kipekee.

## I. MFUMO 1: UKUAJI WA BINAFSI



**Mfano:** Maombi ya Yesu ya kucombea katika Yohana 17

**Maandalizi:** Mwanafunzi anafanya kazi mwenyewe. Hii ni pamoja na kujisomea mwenyewe vile vile na kufanya mambo mengine mwenyewe, kama vile kushuhudia, kuomba, n.k.

**Ukubwa:** Mtu mmoja

**Mtindoo wa Huduma:** Kujifunza mwenyewe

**Kazi:** 1) Mawasilisho ya ukweli nyeti, yaani kupanuka kwa uelevu wa ukweli uliokwisha gusiwa kwenye mikutano ya kundi kubwa, kundi dogo na mmoja kwa mwagine, ) Maendeleo ya ujuzi wa lazima.


**Faida:**

- Kiasi kikubwa cha ufahamu na uzoefu vinaweza kupatikana rahisi.
- Usomaji unaweza kulenga kwenye hitaji maalumu la mtu.
- Viongozi wanawekwa huru kutoa mda wao na nguvu kwenye mahitaji ya huduma nyingine
- Mwanafunzi anaweza kujifunza kwa mda wake na kuchukua mda wa kutafakari na kutumia.

**Vizuizi:**

- Mpaka ujaribiwe katika baadhi ya njia, hakuna njia ya kujua ni kiasi gani kimeeleweka au kupatikana.
- Hakuna nafasi ya kumchunguza mwanafunzi anapokuwa anajihusisha katika huduma ili kwamba uweze kumpa ushauri unaosaidia.
- Misaada mingine ya kiroho bado inahitajika.
- Njia isiyo ya binafsi inayolekeza ubinafsi na siyo jumuia.

## II. MFUMO 2: UFUASISHAJI WA MMOJA KWA MMOJA



**Mfano:** Tuanweza kuona Yesu anatumia mfumo huu katika mazungumzo yake na Nikodem (Yohana 3) na mwanamke Msamaria Kisimani (Yohana 4)

**Maandalizi:** Kiongozi au mshauri, wanakutana pekee na mtu mmoja mmoja.

**Ukubwa:** Watu 2 kila mkutano

**Mtindoo wa Huduma:** Kushauri

**Kazi:** 1) Mawasilisho ya ukweli nyeti, 2) maendeleo ya ujuzi wa lazima, na utoaji wa msaada wa kiroho unaohitajika.

**Mawasiliano:** Mawasiliano ya njia-mbili. Mshauri anapokea matokeo kutoka kwa mwanafunzi wake.

**Nani Wanahudumu:** zaidi mshauri. Kwa jinsi hii mshauri anatakiwa aipe kipao mbele kuwafundisha na kuwahuishisha wanafunzi wake kwenye huduma kwa wengine.

**Ongezeko:** Kila mshauri anatakiwa kuwa na mwanfunzi kiongozi anayejifunza jinsi ya kufuasa wengine mmoja kwa mwagine kama ilivyoonyeshwa katika mchoro hapo juu. Viongozi hawa wanafunzi watajifunza kwa "kuchunguza" na "kufanya" chini ya usimamizi. Ufundishaji wa semina pia unaweza kutolewa.


**Faida:** Katika hali nyingi, mawasiliano ya mmoja kwa mwagine ni njia ya pekee utakayopata kujua kinachotokea kiroho ndani ya mtu. Wakata shauri wengi wapya watakua tu wakati mkazo wa binafsi utakuwa umetolewa kwao.

- Kuna kiwango cha juu cha nafasi kumpa mtu msaada anaohitaji.
- Kufundisha na kufunza kunaweza kulengwa kwenye mahitaji maalumu ya mtu pekee.
- Kuna kiwango cha juu cha matokeo, kutambua ni kiasi gani kimeelewaka na kupatikana.
- Kuna kiwango cha juu cha kumsaidia kuweka anayojifunza kwenye vitendo na kumsaidia kuweza kuhusika kwenye huduma kwa wengine.
- Kiongozi anaweza kufahamu kirahisi na kuwfundisha hao walio na umuhimu wa kufanya huduma ya mmoja kwa mwagine na wengine.
- Huu ni muundo wa ajabu kwa kufundishia ujuzi.

**Vizuizi:**

- Mtu mmoja hawezi kutimiza mahitaji yote ya kiroho ya mtu binafsi. Kwa jinsi hiyo, hii inaweza kuhesabika na mikutano kadhaa tofauti ya mmoja kwa mwagine.
- Kiongozi anaweza kuwa na huduma ya mmoja kwa mwagine na watu wachache tu. Ongezeko la washauri wapya inakuwa ni lazima.

### III. MFUMO 3 : HUDUMA YA KIKUNDI KIDOGO



**Mfano:** Tunaona Kristo akionyesha mfumo huu kwenye maongezi ya chumba chake cha juu, yanayopatikana katika injili ya Yohana sura ya 13-16.

**Maandalizi:** Vikundi kiini darasa dogo la jumapili, kikundi kidogo cha kujifunza Biblia, kikundi cha maombi, kikundi cha kanisa la kwenye nyumba, mabaraza, n.k.

**Ukubwa:** Chini ya watu 10-15.

**Mtindo wa Huduma:** uweschajji. Lengo la kiongozi ni kuwezesha wengine kwenye kikundi kufanya huduma ya wao kwa wao. Kufundisha siyo mfumo tu wa huduma.

**Kazi:** 1) Kuwasilisha ukweli nyeti ,2) maendeleo ya ujuzi wa lazima, na 3) utoaji wa msaada unaohitajika.

**Mawasiliano:** Mawasiliano ni maelekezo-mengi.

**Nani Wanahudumu:** Kila mmoja kwenye kikundi kidogo.

**Ongezeko:** Kila kiongozi wa kikundi anatakiwa awe na msaidizi ambaye amefundishwa kuwa kiongozi wa kikundi. Msaidizi atajifunza kwa "kuchunguza" na "kufanya" chini ya usimamizi. Mafunzo ya semina yanaweza pia kutolewa.

**Faida:**


- Viongozi wenye ujuzi kidogo wanaweza kutumiwa kuongoza kundi.
- Kila mmoja anaweza kuhusika. Mawasiliano ni maelekezo-mengi. Kila mmoja ana nafasi ya kutumia na kuendeleza vipawa vyake vya huduma.
- Hao walio na vipawa vya kufundisha au vipawa vingine vya uongozi wanaweza kufahamika kirahisi na kuendelezwa. Hii inafanya kuongezeka kwa huduma kirahisi.
- Kuna nafasi kubwa ya matokeo, kutambua ni kiasi gani kimeelewaka na kupatikana.
- Ni rahisi kukazia mafunzo na mafundisho kwenye hitaji halisi la wajumbe wa kikundi. Kuna nafasi kubwa zaidi ya kuelewa undani wa mahitaji ya kiroho ya watu kwenye kikundi na kutoa aina ya msaada wanaohitaji. Kuna nafasi kubwa ya kuwasaidia kuweka wanachosikia kwenye vitendo

**Vizuizi:**

Viongozi wengi wanahitajika kama idadi kubwa ya watu itahusika kwenye vikundi vidogo (Hii inaweza kuwekwa kando kama kundi dogo limetumika kama eneo la kufundishia viongozi wapya.)

- Watu wengi hawatashirikisha mahitaji yao ya kiroho ya ndani, hata mbele ya kundi dogo. Kama kundi limechanganyika (wanaume na wanawake), kunaweza hata kukawa na uwazi mdogo.

**IV. MFUMO 4: HUDUMA YA KIKUNDI KIKUBWA**



**Mfano:** Mfano kutoka katika maisha ya Bwana unaweza kupatikana kutoka katika Mathayo sura ya 5-7, mahubiri ya mlimani. Mahubiri ya Petro kwa Wayahudi wakati wa pentekosti katika Matendo 2 ni mfano mwengine sawa.

**Maandalizi:** Mahubiri wakati wa ibada, darasa la jumapili, mafunzo ya Biblia ya kikundi kikubwa semina, n.k.

**Ukubwa:** 15, 30, hata watu 100 au zaidi.

**Mtindo wa Huduma:** Kingozi zaidi anahutubia.

**Kazi:** Mkazo mkubwa ni mawasiliano ya ukweli huo nyeti unaoendana na watu walio wengi kwenye kikundi.

**Mawasiliano:** Zaidi katika mwelekeo mmoja—kutoka kwa kiongozi kwenda kwa msikilizaji.

**Nani Wanahudumu:** Kiongozi(v). Huduma inatiririka katika mwelekeo mmoja—kutoka kwa kiongozi kwenda kwa waliobaki katika kikundi.

**Ongezeko:** Viongozi kawaida wanatakiwa mara zote wawe wanafundisha watu wapya kwa aina hii ya huduma. Wafunzwa watajifunza kwa “kuchunguza” na “kufanya” chini ya usimamizi. Mafunzo ya semina pia yanaweza kutolewa. Wanaoweza zaidi wanaweza kuchaguliwa kwa mafunzo ya kawaida zaidi.

**Faida:** Viongozi wachache wanaostahili/ wafanyakazi wenzako wanahitajika kufundisha namba kubwa ya watu.

**Vizuizi:**

- Watu wachache mbali na mzungumzaji (wa) mkuu wana nafasi ya kutumia na kuendeleza vipawa vyao vy ya huduma.
- Njia hii haitumiki kuendeleza viongozi wa baadaye. Isipokuwa njia nyingine imepatikana kuendeleza viongozi, itakuwa vigumu kuongeza huduma kwenye harakati za upandaji kanisa.
- Kufanyika vema, kunahitaji mtu aliye na kipawa kama mwalimu/muhubiri. Mara nyingi ni vigumu kupata watu wa kutosha weny sifa.
- Kiongozi mmoja hana vipawa vyote vinavyotakiwa kukidhi mahitaji yote ya kiroho ya kikundi.
- Kuna nafasi ndogo ya matokeo, kwa hiyo ni vigumu kuelewa kiasi gani kimeeleweka na kupatikana.
- Kuna nafasi ndogo ya kuelewa mahitaji ya ndani ya kiroho ya watu kwenye kikundi na kutoa aina ya msaada wanaohitaji. Kuna nafasi ndogo ya kuwasaidia kuweka katika matendo wanayosikiliza.
- Kuna mazoea ya wasikilizaji wengi kuwa wa kutendewa.
- Hakuna mmoja anayehudumu kwa kiongozi (v)
- Kama huu ni mfumo wa msingi wa huduma, kisha watu wengi hawatakomaa kiroho. Kiongozi mara nyingi anachoka kwa kazi nyingi kwa sababu kuna wafanyakazi wenzake wachache.

## **V. UKUMBUSHO**

Kama wapanda kanisa jukumu lenu la msingi katika utaratibu wa kufuasa ni kufahamu na kufuasa viongozi maarufu. Hawa matokeo yake watafuasa wengine (2Tim 2:2). Unapokuwa unafikiria mahitaji ya wanafunzi wako, kumbuka kwamba watu wana mitindo tofauti ya kujifunza. Kwa mfano, baadhi ya watu wanajifunza vizuri kwenye vikundi, wengine ni wazuri kujifunza wenyewe, bado wengine wanahitaji uangalizi wa mmoja kwa mwengine. Sehemu ya mpango wako wa kufuasa unatakiwa uwe kutathimini jinsi kila mtu anavyojifunza vizuri na kutoa ufuasishaji.

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Katika mandhali yako, ni “mifumo” ipi Mara nyingi makanisa yanatumia katika kufuasa watu wao? Ni jinsi gani mifumo hii imekuwa ya ufanisi kutumika kutoa kile wanafunzi wachanga wanachohitaji? Ni mahitaji yapi hayajatimizwa? Mifumo ipi unadhana inayoweza kufaa zaidi katika kutimiza mahitaji haya?
- Ni mifumo ipi unajisikia uhuru nayo zaidi kuitumia? Ni mifumo ipi unajisikia huna huru nayo kuitumia? Kwa nini?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Kwa Kutumia ziada 5A, “Mpango wa Kufuasa”, tayarisha mpango wa kufuasa kipekee kwa kila mtu unayemfuasa katika huduma yako ya upandaji kanisa.

Ni lazima ulete azimio lako lililomalizika kwenye somo lijalo la kufuasa, amblo litafanyika unapoanza mafunzo ya Mwongozo wa Nne.



## Azimio la Kufuasa

Ziada hii inatoa njia ya kukusaidia kuanzisha mpango wa vitendo kuwasaidia wanafunzi wako kukua katika ukomavu wa kiroho. Ukomavu huu wa kiroho unapimwa kwa ukuaji wa ndani wa mtu, ukuaji katika uhusiano na Mungu, na ukuaji katika uhusiano na watu wengine. Pengine, umeshaanza kufikiria juu ya nini ni ukweli muhimu zaidi na ujuzi unaohitaji kuwfundisha watu wako, hasa waumini wapya. Umejadili pia ni aina gani ya msaada unahitajika zaidi na waumini wapya katika mwanga wa mahangaiko yao ya kwaida ya kiroho. Sasa unatakiwa kupanga lini na jinsi gani utafundisha ukweli maalumu na ujuzi wakati wa miezi kumi na miwili ijayo, vile vile na jinsi utakavyotoa msaada unaotakiwa wa kiroho. Utahitaji pia kufikiria juu ya njia za kuongeza huduma.

Unatakiwa kufanya mpango kwa kila mtu unayemfuasa katika kupanda kwako kanisa. Kama inawezekana, hao walioko katika timu moja ya upandaji kanisa wanatakiwa kufanya kazi pamoja kuzalisha mpango huu.

Karatasi mbili za kuendeleza mpango wa kufuasa zimetolewa katika sura zifuatazo. Kamilisha karatasi ya kwanza ya mazoezi, 5A.1 "Nini Waumini wapya Wanachohitaji Kujua na Kufanya" kama mpaka wa jumla wa waumini wapya katika huduma yako ya upandaji kanisa. Karatasi ya pili ya mazoezi, "Mpango wa Pekee wa Kufuasa" utatumika mara moja kwa kila mtu unayemfuusa. Kutakuwa na ukweli maalumu na ujuzi ambao kila mmoja wa wanafunzi wako wanahitaji kujifunza. Tumia karatasi ya mazoezi 5A.2 kuonyesha jinsi ukweli huu na ujuzi utafundishwa, na katika mfululizo wa utaratibu upi.

Katika kujaza karatasi hizi za mazoezi, tunza michango hii kichwani:

- Onyesha ni mfumo gani (kundi kubwa, kundi dogo, mmoja kwa mwingine, mtu pekee) unafaa zaidi kwa ukweli/mawazo/thibitisho au tabia/ujuzi unaotaka kufundisha. Huhitaji kutumia mifumo yote minne ya ufuasishaji.
- Mara nydingi ni hekima kutumia kwa marudio. Hii ina maana mtu atakuwa amewekwa wazi kwenye ukweli unaofanana au ujuzi mara kadhaa katika mifumo kadhaa. Kwa mfano, unaweza kuhubiri juu ya ukweli fulani jumapili asubuhi na kisha kushughulikia matumizi ya mtu binafsi ya ukweli huo katika vikundi vidogo na katika mikutano ya mmoja kwa mwingine.
- Onyesha utaratibu ambao ukweli na ujuzi unatakiwa ufundishwe. Mara kwa mara kuna mfuatano wenye maana ambao utahitaji kufata.
- Maswala ambayo ni nyeti zaidi kwa uponaji wa kiroho wa kila mtu unatakiwa ushughulikiwe mapema, badala ya baadaye.
- Amua ni nyenzo ipi iliyopo ya ufuasishaji, kama kuna yoyote, unayotaka kutumia. Baada ya kuwa umefanya uchaguzi wako, unaweza kuweka somo linalostahili au kichwa cha ukurasa kwenye karatasi yako ya mazoezi. Katika njia sawa, orodhesha nyenzo zitakazotakiwa kwa mafunzo ya kila mmoja.
- Kila safu katika karatasi ya mazoezi 5A.2 inawakilisha mwezi. Unaweza kuorodhesha masomo kadhaa katika kipande kimoja. Kwa mfano, katika mikutano yenu ya mmoja kwa mwingine katika mwezi wa kwanza, unaweza kuorodhesha masomo tofauti ya kukamilishwa kila juma, kama vile: mda wa mtu na Bwana, jinsi ya kuomba na jinsi ya kushughulikia dhambi. Kwa upande mwingine, wakati wa mwezi wa sita, unaweza kuamua kutumia mwezi mzima kwenye somo moja, kama vile, kuendeleza ushuhuda binafsi.

Ukiwa na timu yako ya upandaji kanisa, tumia karatasi zifuatazo za mazoezi, 5A.1 na 5A.2, kufahamu mahitaji na kuanzisha mpango kwa kila mtu unayetaka kufuasa katika upandaji wako wa kanisa. Jaza katika mchoro ukweli na ujuzi ambao utafundishwa.

**Karatasi ya Mazoezi 5A.1 Nini Waumini Wapya Wanahitaji KUJUA na KUFANYA**

**MAELEKEZO:**

- Orodhesha vitu hivyo ambavyo waumini wapya wanavihitaji zaidi kwa dharura KUVIJUA kuweza kufanikiwa kuishi maisha ya upendo, imani na tumaini na kwa ufanisi kuwahudumia wengine kwa kiwango cha ufahamu wa kuelewa kwenye uthibitisho wanaotakiwa kuwa nao.
- Orodhesha vitu hivyo ambavyo waumini wapya wanavihitaji KUFANYA kufanikiwa kuishi maisha ya upendo, imani na tumaini na kwa ufanisi kuhudumia wengine. Vingi kati ya vitu hivi vinahusu tabia wanayotakiwa waendeleze. Vingi pia vitahusu ujuzi watakaohitaji kujifunza.

	<b>Wanachohitaji KUJUA (ukweli au mawazo/thibitisho)</b>	<b>Wanachotakiwa KUFANYA (mazoea/ujuzi)</b>
<b>Kuishi maisha katika upendo na umoja na Mungu</b>		
<b>Kuishi maisha katika upendo na umoja na familia zao na waumini wengine na kuwajenga katika Kristo</b>		

	<b>Wanachohitaji KUJUA (ukweli au mawazo/thibitisho)</b>	<b>Wanachotakiwa KUFANYA (mazoea/ujuzi)</b>
<b>Kuishi maisha ya imani</b>		
<b>Kuishi maisha ya tumaini</b>		
<b>Kuhudumu kwa ufanisi kwa waliopotea</b>		

**Karatasi ya mazoezi 5A.2 – Mpango wa Pekee wa Kufuasa**

Jina la mtu

Mwezi	Binafsi	Mmoja kwa mwingine	Vikundi vidogo	Vikundi vikubwa
1				
2				
3				
4				
5				

<b>Mwezi</b>	<b>Binafsi</b>	<b>Mmoja kwa mwingine</b>	<b>Vikundi vidogo</b>	<b>Vikundi vikubwa</b>
<b>6</b>				
<b>7</b>				
<b>8</b>				
<b>9</b>				
<b>10</b>				

Mwezi	Binafsi	Mmoja kwa mwingine	Vikundi vidogo	Vikundi vikubwa
11				
12				

**Vitu vya kufikiria:**

- Nani atafundisha/kuhubiri katika ngazi ya kundi kubwa?
- Nani ataongoza kundi dogo?
- Nani atafanya kazi na mtu (wa) mmoja kwa mwingine?
- Jinsi gani utawaendeleza viongozi ili kwamba kila moja ya huduma hapo juu iweze kuongezeka?
- Orodhesha ni msaada gani kuliko kufundisha utatolewa (kama vile kutia moyo, maombi, kuwajibika, n.k.). Ni jinsi gani misaada hii itolewe? Nani atafanya hilo?

---

---

**VITA VYA KIROHO**

---

---



# Kuelewa Mtazamo wa Dunia

- ☞ **Kusudi la Somo**

Kuwasaidia wapanda kanisa kuelewa wazo la mtazamo wa dunia na kuonyesha kwa undani jinsi mtazamo wa mmoja unavyoathiri maisha yake mwenyewe ya kikristo, jinsi anavyofanya huduma yake, na jinsi anavyotafsiri hali ya huduma yake.
- ☞ **Wazo Kuu**
  - Kikawaida mtazamo ulio wa dunia unapingana na mtazamo wa kibiblia.
  - Mtazamo wa dunia unaathiri upandaji kanisa.
- ☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoelewaka, kila mshiriki anatakiwa...

  - Kuwa macho kwenye umuhimu wa kuwa na mtazamo sahihi wa dunia.
  - Kujua msingi wa kimaandiko juu ya ulimwengu wa Mungu, malaika, mtu na asili.
  - Mpanda kanisa atawezza kuchunguza hali yake ya huduma kwa mwanga wa mtazamo wa kibiblia.

## UTANGULIZI

Tunaposema mtazamo wa dunia tunaongelea imani ya kitovu na kuelewa ambako aliko nako mtu kuhusu ulimwengu. Kila mtu endapo anajua au hajui, ana imani ndani ya moyo wake ambayo inaonyesha matendo yake na tabia na kumsaidia kuelezea ulimwengu unaomzunguka. Mtazamo wa dunia unasaidia watu kuelewa asili, watu wengine na nguvu ya asili ya dunia. Watu wanapokua, matokeo ya uzoefu wao yanaletea kuibuka kwa mtazamo wa dunia ambao unaweza au usiweze kutafsiri kiusahihii hali halisi.

Tunaposema mtazamo wa dunia wa kibiblia, tunaongelea kile maandiko yanachosema juu ya vitu vyote, nini kilicho halisi, nini ni kweli, nini NI. Kimaana kunaweza kukawa TU na hali halisi moja, ukweli mmoja au maelezo ya nini NI. Tunaamini kwamba maandiko yanatoa maelezo haya ya ulimwengu. Na ni kwa ukweli huu tunatafuta kupima au kuangalia kuelewa kwetu ulimwengu.

Ni muhimu kwamba wapanda kanisa wana mtazamo wa kibiblia wa ulimwengu ili kuweza kutafsiri sawasawa misukosuko ya huduma zao. Hii hasa ni kweli kuhusu vita vya kiroho. Kama mtu hana mtazamo wa kibiblia wa ulimwengu, anaweza asifahamu mashambulizi kutoka kwa Shetani, au anaweza asijue jinsi ya kuitikia kwenye mashambulizi. Katika somo hili tutapeleleza mitazamo ya kawaida ya ulimwengu na jinsi mtazamo wa dunia wa kibiblia ni wa msingi katika kuelewa vita vya kiroho.


### I. MITAZAMO YA KAWAIDA YA ULIMWENGU

Njia moja ya kuelewa mtazamo wa ulimwengu ni kuangalia kwenye vipengele vitatu vya vitu vyote: asili isiyo ya dunia, asili, na ubinadamu. Tutatumia vipengele hivi viwili kuelezea mtazamo wa ulimwengu hapo chini.

Ngoja tuseme mtu anaumwa. Tunatafsirije tukio hilo? Yote yanatokana na mtazamo wa ulimwengu. Kama tunavyoolezea mtazamo wa ulimwengu hapo chini tutaona kila moja inavyoolezea ugonjwa huu.

#### A. Mtazamo wa Ulimwengu wa Kidunia


Katika mtazamo wa ulimwengu wa kidunia, ulimwengu wa asili na anga la ubinadamu vinatawaliwa na "sheria za asili", ambazo pengine muumbaji Mungu alizianzisha, lakini ambazo leo zinatumika bila kuhusisha nguvu yoyote ya asili ya Mungu. Kuwepo kwa ulimwengu usio wa kawaida, ikiwemo Mungu na roho hai, vinaweza kukataliwa kabisa na watu wa kidunia. Au, Kama nguvu isiyo ya kawaida ipo, watu wa kidunia wanatwaa kuwa inatengana na ulimwengu wa asili/ubinadamu. Uwe muunganiko wowote, inaaminika kuwa wa mbali sana.



Wasomi wa kidunia wanakubali chanzo cha kila tukio kina asili au kusababishwa na mwanadamu. Kwa mmoja anayeumwa, wadudu au mbu, au ugonjwa mwininge umeathiri mwili. Kila kimoja kinaweza kuelezeza kisayansi. Mtu anatakiwa atafute matibabu ya uganga kuweza kupata nafuu, kulingana na mtazamo huu wa kidunia.

#### B. Mtazamo wa ulimwengu wa Kizama


Mtazamo wa ulimwengu wa kizama karibu ni tofauti na mtazamo wa ulimwengu wa kidunia. Katika mtazamo huu wa ulimwengu ulimwengu wa kupita asili unakaribiana sana kwenye ule wa asili na wa anga la binadamu. Roho kutoka kwenye anga la nguvu isiyo ya kawaida inaweza kuishi katika vitu vyaa asili na watu na roho hizi hai zina nguvu za kutawala mambo. Kama mtu anafurahisha roho hizi anaweza kupata kustahili, ikiwemo pamoja na ulinzi na uponyaji. Kama roho imekasirika inaweza kusababisha madhara makubwa.



Mtu anayeumwa, kulingana na mtazamo huu wa ulimwengu, amekasirisha roho au amewekewa ulozi. Ili kuwa vema tena mtu huyu atahitaji kufanya kitu fulani kuridhisha roho au kuvunja ulozi. Matibabu katika hali hii inaweza hata kukaidi ufahamu wa kiganga, ambao hauaminiki katika mtazamo wa zama za kale.

#### C. Mtazamo wa Ulimwengu wa Kimaumbile

Mtazamo wa kimaumbile unatokana na imani kwamba mwanadamu hana uwezo wa kuzuia juu ya ulimwengu unaomzunguka. Nguvu isiyo ya kawaida na msukumo wa kawaida inaelekeza mkondo wa historia, na mtu anaishi vema aezavyo katika kanuni hiyo. Mwandishi mmoja wa Shinto anaiweka sawa:"Maisha ni kama jani linaloelea mtoni. Jani linaweza kukwama katika mzingo mdogo wa maji, au linaweza kutiririka pamoja na maji kwa utulivu kwenye mtiririko mtulivu, au linaweza kufikia kwenda haraka, maji yenye msukosuko. Jani halina uwezo wa kuzuia wapi liende. Kwa hiyo wanadamu wametekwa kwenye kanuni za maumbile yao."



Kisha matibabu kwa mtu mgonjwa yanaweza yasifanye kitu. Kunaweza kusiwe na kujaribu kumtibisha vile vile na kujaribu kuchunguza sababu ya ugonjwa.


### II. MTAZAMO WA ULIMWENGU WA KIBIBLIA

Mtazamo wa ulimwengu wa kibiblia, kama tulivyokwisha kusema, unafundisha mtazamo wa ulimwengu ulio sahihi. Mtazo wa ulimwengu ulio sahihi unaona vipengele vitatu kama hasa vinaendana kimoja kwa kingine.

## B. Asili Kupita ya Kawaida

### 1. Mungu Muumbaji

Kitabu cha Mwanzo kinafungua na maneno, "Hapo mwanza Mungu..." Huu ni msingi wetu wa asili wa kujengea mtazamo wa ulimwengu. Mungu mwenyezi aliyepo nje ya mda, wa milele, anayejitoshereza, muumba wa mbingu na dunia, bila wa kuwa sawa wala mshindani, katika enzi yake ya kutawala matokeo ya historia. Kinyume na mtazamo wa ulimwengu wa kidunia, maandiko yanafundisha kwamba Mungu amehusika katika historia. Kwa Mfano:



- Alielekeza historia ya Israeli katika maandalizi ya Masiya.
- Kristo alikuja ulimwenguni na kuishi na wanadamu.
- Kristo alipaa mbinguni na kumtuma Roho Mtakatifu kwenye kanisa lake.

Biblia inathibitisha kazi hai ya Roho Mtakatifu ndani na katika maisha ya muumini. Roho Mtakatifu anatenda leo. Anauthibishia ulimwengu kuhusu dhambi, haki na hukumu (Yoh 16:8-11). Anawapa waumini maisha mapya (Rum 8:11). Anashuhudia kuwa tu watoto wa Mungu (Rum 8:16). Roho mtakatifu anatusaidia kuomba (Rum 8:26) na anafundisha (Yoh 14:26, 1Yoh 2:27), n 14:26, 1Jn 2:27).

Maandiko hayafundishi kuwa Mungu na Shetani wanalingana hata hivyo msukumo tofauti. Kulgingana na mtazamo wa ulimwengu wa kibiblia, Mungu amekuwepo mwenyewe lakini shetani aliumbwaa. Shetani hana nguvu sawa na Mungu. Mungu anamtawala Shetani kama inavyoonekana katika Ayubu sura ya 1. Kabla shetani hajafanya chochote kwa Ayubu, ilibidi apate ruhusa ya Mungu kwanza.

### 2. Roho Hai Zilizoumbwa (Shetani na Malaika)

Masimlizi ya uumbaji yanaendelea. Ingawa hesabu ya Mwanzo haihusishi uumbaji wa malaika, tunasoma katika Wakolosai 1:16 kwamba Mungu (katika Kristo) aliumba vitu vyote, mbinguni na duniani, vinavyoonekana na visivyooonekana. Katika Agano Jipylo lote linaandika kidogo sana juu ya malaika, ni wazi kwamba wanafanya kazi katika ulimwengu wetu leo (Ebr 13:2). Watu wa kiinjili wengi wanaamini kwamba Ufunuo 12:4 unarejea kwenye ukweli kwamba wakati Shetani alipoanguka alichukua moja ya tatu ya malaika pamoja naye. Malaika hawa "wabaya" wanajulikana pia kama mapepo. Tunajua kwamba mapepo pia yanafanya kazi katika ulimwengu wetu (Yak 3:15, 1Tim 4:1). Tena, Hii inatofautiana na mtazamo wa ulimwengu wa kidunia lakini karibu kwenye mtazamo wa ulimwengu wa zama za kale kwa yote kutambua kwamba kuna vita kati ya Mungu na Shetani. Katika mtazamo wa ulimwengu wa zama za kale, ushindi katika vita unategemeana na nani "mungu" wake ana nguvu. Kama makabila mawili yanafanya vita dhidi ya kila moja, kabila lenye mungu mkubwa litakuwa mshindii. Kwa kutofautisha, maandiko yanafundisha kwamba Mungu ni mshindii. Upinzani unaoonekana unapatikana katika Yoshua 7. Pale watu wa Mungu walikuwa wameshindwa katika vita. Uangalifu wa makini katika somo unaonyesha kwamba hii haikuwa kwa sababu baadhi ya miungu au roho zilimshinda Mungu, lakini kwa sababu watu wake waliugua matokeo ya dhambi zao. Mungu hakushindwa. Aliruhusu waisraeli kushundwa kwa sababu ya kutotii kwao.

Fikiria kuelewa kwako mwenyewe kwa malaika na mapepo. Kwa kiwango gani wanaweza kutenda katika shughuli zako za kila siku? Wanazuiliwa kwa kiwango cha ujuzi na akili? Wanaweza kuhusika katika shughuli za kimwili? Tunaweza tukawa na uhakika wa ushindi dhidi ya shetani? Tutajadili mawazo haya zaidi katika undani zaidi kwenye masomo yafuatayo katika vita vya kiroho.

### C. Asili

Hesabu ya uumbaji inaendelea na jinsi Mungu alivyouumba ulimwengu wa vitu. Hapa pia kuna mitazamo tofauti ya ulimwengu au kuchukulia ulimwengu wa vitu. Wengine wanasema hajjarishi—ni muonekano tu (maumbile); baadhi wanajilinganisha na dunia kama “mama asili” na kutunza heshima ya kuheshimu (kizama); wengine wanashikiria ni kitu mtu anatakiwa ashinde na kutawala (kidunia).

Kufuatana na Biblia, uumbaji wa Mungu ulikuwa umekusudiwa kutangaza utukufu wa Mungu (Zaburi 19). Hakuna kilicho cha ajabu, cha kuvutia, au kizuri kuliko ulimwengu wenyewe—milima mirefu, mawimbi yanayovuma, maporomoko ya maji, mapango ya chini, mashamba ya kijani, ukungu uliofunika miti, maua ya mashambani, kuchomoza kwa jua na kuchwa kwa jua; uumbaji wa Mungu unatangaza utukufu wake! Lengo la Shetani ni kuharibu au kuvunja uumbaji wa Mungu. Kama Shetani hawesi kumuhaaribu Mungu kisha atajaribu kuhaaribu hicho kinachomtuka Mungu. Inashangaza kwamba agizo la Mungu kwa Adamu ilikuwa ni kulima na kutunza bustani (Mwa 2:15). Mtazamo wetu wa ulimwengu unatakiwa kuashiria nia ya Mungu katika uumbaji wake—kwamba uweze kumtukuza yeye. Je shughuli zetu katika ulimwengu wa vitu zinamtuka Mungu?

### D. Mwanadamu

Mwishoni, tunakuja kwenye uumbaji wa mtu katika hesabu ya Mwanzo. Mtu alikuwa ameumbwa nje ya asili ya ulimwengu (hii ni, udongo) lakini pia Mungu alipulizia pumzi ya uhai ndani yake na kumuumba mtu katika mfano wake mwenyewe. Hivyo mtu ni kiumbe kilichotengenezwa; ni yote vitu na kiroho. Haya ni mafundisho ya maandiko. Mtu siyo mwili tu—mchanganyiko wa madawa na viini baadhi wanavyoshikiria (kidunia). Mtu siyo kiroho tu, kama baadhi ya mtazamo wa ulimwengu wa waamini maumbile wa mashariki wanavyoshikiria. Mtu ana Roho na mwili (mwanzo 3:7). Sehemu ya maajabu ya mtu ni kwamba ana uchaguzi huru. Mungu hamlazimishi mtu katika tabia au kufikiria au kumjaza kama mashine ya kuendeshwa. Katika kutofautiana na mtazamo wa ulimwengu wa maumbile, mtu hajateguliwa katika baadhi ya “mito” au maisha yanayoitwa maumbile. Ana matakwa na kufanya uamzi. Anaweza akachagua kupenda Mungu, na anaweza kuchagua kumkataa Mungu (Yos 24:15).

## III. MTAZAMO WA ULIMWENGU NA UPANDAJI KANISA

Maandiko yanatuambia kwamba Mungu hayuko anashindana na Shetani. Shetani amesha shindwa (1Yoh 3:8, Col 2:15, Ebr2:14-15). Katika injili zote kama ilivyoelezwa na kanisa, Mungu anatafuta kusuluuhisha mtu kwake, wakati shetani anatafuta kumdanganya mtu (Uf 12:9), kumulaghai (1Pet 5:8), kumjaribu (1The 3:5), na kumsingizia (uf 12:10).

Vita vya kiroho vinatokea kati kati ya anga la mtu. Kama mtume Paulo anavyooleza katika 2Wakorintho10:3-5, vita hivi ni kwa akili zetu—mtazamo wetu wa ulimwengu.

“Ingawa tunaishi katiki ulimwengu, hatufanyi vita kama ulimwengu uanvyofanya. Silaha tunazotumia kupigana naye si siraha za kiulimwengu. Kinyume chake, zina nguvu katika Mungu hata kuangusha ngome. Tunaangusha mawazo na kila kitu kinachoinuka, kijiuuacho juu ya elimu ya Mungu, na kuteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo.

Tambua jinsi mtume Paulo anavyofanya maunganisho kati ya kuangamiza ngome na mawazo na kuteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo. Mwishoni, fikiria Yohana 8:32, “Utajua ukweli na ukweli utakuweka huru.” Kadiri tunavyojua ukweli na kuufanya kazi, ndivyo tutakavyokuwa washindi zaidi. Hili litaelezewa kwa undani katika somo linalofata, “Mahusiano Katika Vita Vya Kiroho.”

Ni muhimu zaidi kwamba sisi kama wapanda kanisa tuna kuelewa kwa ulimwengu hasa kama ulivyo—hii ni, kama ilivyoelezwa katika maandiko. Upandaji kanisa ni vita vya kiroho. Shetani atashambulia katika njia yoyote anayoweza makanisa yanapopandwa. Kama hatuna mtazamo sahihi wa ulimwengu kisha Shetani anaweza kushambulia (kwa mfano, kwa kutumia magonjwa) na tunaweza hata tusilitambue! Mtazamo sahihi wa ulimwengu wa kibiblia unasaidia wapanda kanisa kwa usahihi kutambua nini kinachotokea katika maisha yake na huduma.

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Kama ambavyo umeshawekwa kwenye ukweli wa somo hili, umeshajifananisha na unayofanya mwenyewe katika maisha yako ambayo hayalingani na mtazamo wa ulimwengu wa kibiblia? Vipi juu ya wanayoyafanya hao walio katika eneo lako unalolenga?
- Jinsi gani kutokulingana huku katika maisha yako kunaathiri uhusiano wako na Mungu, na mwenzi wako, watoto wako au waliopotea?
- Kama mpanda kanisa anaugua sana, hii ina maana kwamba Shetani anamshambulia kwa magonjwa? Lini hili linaweza kuwa ni sababu?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Kutana na muumini mwagine na elezea wazo kuu la somo hili. Shirikisha jinsi tabia yako inavyokwenda kubadilika kutokana na ukweli mpya uliojifunza.
- Fikiria juu ya mtazamo wa ulimwengu wa watu walio katika eneo lako unalolenga. Ni katika njia zipo mtazamo wao wa ulimwengu ni sawa na mtazamo wa ulimwengu wa kibiblia? Ni kwa njia zipo ni tofauti? Ni jinsi gani hili litaathiri mkakati wako wa uinjilisti? Jinsi gani na nini utawafundisha waliokata shauri wapya ili kuleta mtazamo wao wa ulimwengu zaidi katika mstari wa mtazamo wa ulimwengu wa kibiblia?

### **SOURCES**

- Warner, Timothy M. Spiritual Warfare: *Victory over the Powers of This Dark World*. Good News Pub. 1991.
- Demon Possession. *Edited by John W. Montgomery*. Minneapolis, MI: Bethany House, 1976.



## Nguvu ya Vita Vya Kiroho

VITA VYA  
KIROHO

2

Somo

### ☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kusaida mpanda kansa kuelewa nguvu ya uhusiano kati ya Mungu, mtu na roho hai katika vita vya kiroho, na nafasi na mamlaka ya muumini dhidi ya Shetani katika Kristo.

### ☞ **Wazo Kuu**

- Kuelewa sahihi kwa uhusiano kati ya Mungu, mtu na roho ni kwa maana katika mafanikio ya vita vya kiroho.
- Mashambulizi katika akili yanashindwa kwa kutumia ukweli wa neno la Mungu kwenye uongo wa Shetani.

### ☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyoma katika somo hili yanapoelewaka, kila mshiriki anatakiwa...

- Kujua kwamba upandaji kanisa ni vita vya kiroho.
- Kuwa imara katika Bwana na katika nguvu zake kwa kujua nafasi yake katika Kristo.
- Kuweza kujitetea mwenyewe dhidi ya mashambulizi ya kipepo.

### ☞ **Ziada**

2A Kujifunza Biblia kwa Kufata neno Waefeso 4:17-5:2

### ☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili lina mawazo ya mafundisho mengi na mistari mingi iliyonakiliwa. Tafadhari isome kwa uangalifu kabla ya kuiwakilisha kwa wafunzwa. Chagua wazo kuu na mistari ambayo unaweza kuwaambia kuiangalia wakati wa mafundisho.

Ikiwemo katika somo hili ni pamoja na mchoro (kielelezo 2.1) kinachoonyesha mahusiano haya. Unaweza kutaka kuweka haya kwenye kibao kusindikiza mafundisho yako.


## UTANGULIZI

Wapanda kanisa walio kwenye utaratibu wa kujenga kusanyiko mpya la waumini wanajikuta wakiingilia ngome ya adui. Shetani, "mfalme wa ulimwengu huu" (Yoh 16:11), hataki mpanda kanisa kufungua macho ya wasioamini ili kwamba watoke katika giza kwenda kwenye nuru na kupata msamaha wa dhambi zao. (Mdo 26:18). Kuna mashambulizi halisi ya kiroho yanayoendelea, na wapanda kanisa wasiogundua hili watajikuta wenyewe kimajonzi bila kujiandaa kushughuliksa na mashambulizi yanayokuja upande wao. Siyo tu kwamba wanatakiwa kibinagsi wawe wamejiandaa kwa vita vya kiroho, lazima wajue pia jinsi ya kuwasaidia waumini wapya na makanisa yanayoibuka kusimama imara dhidi ya adui.

Kila mshindani kwa ujumla anayepanga maarifa yake ya vita anajua mkakati wake, uwezo na udhaifu, vilevile na wa wapinzani wake. Anaelewa jinsi wapinzani wake wanavyofikiri na kutenda. Mpanda kanisa pia lazima ajue uwezo wake na udhaifu, na lazima aelewé mikakati ambayo Shetani atajaribu kutumia kumshambulia. Ili kuweza kushika mapana ya vita vya kiroho ambamo anajikuta mwenyewe, mpanda kanisa anahitaji kuelewa anga la Mungu, anga la mtu, na anga la roho hai katika ulimwengu huu, na jinsi zinavyoingiliana moja kwa nytingine. Ni lazima aelewé na kuamini ukweli wa yeze ni nani katika Kristo, kwa kuwa ukweli utakuwa siraha muhimu zaidi aliyo nayo katika mapigano ya kiroho ambayo atakutana nayo.

Kielezo 2.1 kinaonyesha mahusiano yanayoingiliana kati ya anga la Mungu, roho hai na mtu. Mchoro huu kwa kuona utasaidia kuelezea baadhi ya mawazo yaliyotolewa katika somo hili.

**Kielezo 2.1 Mahusiano katika Vita Vya Kiroho: Anga la Mungu, Roho Hai, na Mtu**



### I. ANGA LA MUNGU

Mungu ni mkuu "NIPO", wa milele, anayejeweza, anayejitoshereza, asiyeumbwa muumba wa vitu vyote na mtawala mkuu wa anga. Ni mwenye uwezo-wote, anayejua yote, aliye kila-mahali, na wakati wote mtakatifu, mwenye haki, mwenye rehema, mkweli na mwaminifu. HANA WA KULINGANISHWA.

Mungu ni mmoja mwenye nafisi tatu, muungano katika mapana. Wajumbe watatu wa Mungu kichwa. Wanatofautiana katika majukumu, lakini hata hayo ni vigumu kuyatofautisha. Kwa mfano, Mungu anasemekana kuwa muumbaji (Kumb32:6). Lakini katika Yohana 1:3, vitu vyote vinasemekana kuwa vimeumbwa kupitia neno (mwana).

#### A. Mungu Baba

Katika mafunzo haya, nafasi muhimu ya Mungu inawekwa kati kwenye ukombozi: Aliupenda ulimwengu na kumtuma mwana kuwa mwokozi (Yoh 3:16; 1Yoh 4:10). Alimfufua Yesu kutoka kwa wafu (Kol 2:12). Ametuopoa kutoka kwenye mamlaka ya giza na kutuleta katika ufalme wa mwanaye anayempenda" (Kol 1:13) na anawalinda watoto wake kwa nguvu za jina lake (Yoh 17:11).

#### B. Mungu Mwana

Wajibu wa Mwana, Yesu Kristo, kimsingi inakazia kwenye uingiaji wake katika mda na nafasi. Alikuwa mmoja na Baba (Yoh 10:30) aliyechangia katika heshima kutoka umilele wote (Yoh 1:1,2). Alikuwa "Mungu mkamilifu katika mfumo wa kimwili" (Kol 2:9). Alikuwa ulimwenguni kuwa "Mungu pamoja nasi" (Mt 1:23). Lakini alipokuja ulimwenguni, alichukua mfano wa mtumishi (Flp 2:6,7). Wakati wote alifanya mapenzi ya Mungu (Yoh 6:38). Alikuwa msalabani kama mtoaji wa dhambi kwa ajili yetu (Rum 8:3) na alifufuliwa siku ya tatu (1Kor 15:4).

Alipaa mbinguni na amekaa mkono wa kuume wa Mungu Baba, anapotuombea (Rum 8:34). Ni mtoaji wa maisha ya milele (Yoh 17:3). Sasa katika utukufu wake (17:24), Ana nguvu zote (mamlaka) mbinguni na duniani (Mt 28:18-20). Ni "kichwa juu ya kila kitu cha kanisa" (Efe 1:22).

Kufuatana na ulimwengu wa roho, ni mkuu kuliko malaika (Ebr 1:5-2:9). Ni kichwa juu ya kila nguvu na mamlaka (Kor 2:10). Kuna wakati, kila goti mbinguni na duniani na chini ya dunia litapigwa mbele zake (Flp 2:10).

#### C. Mungu Roho Mtakatifu

Jukumu la Mungu Roho Mtakatifu limetajwa kimsingi katika uhusiano na waumini. Mara nyingi zaidi anaitwa Roho Mtakatifu, lakini pia Roho wa ukweli (Yoh 16:13), Roho wa uzima (Rum 8:2), na Roho wa walio hai (2Kor 3:3).

Ni ye ye anayewapa maisha mapya waumini wapya (Rum 8:11), anayeshuhudia kuwa tu watoto wa Mungu (Rum 8:16), anayetusaidia kuomba (Rum 8:26-27), na anayeutuhitishia ulimwengu hatia kufuatana na dhambi (Yoh 16:8-11). Ni mshauri wetu/msaidizi (Yoh 14:16), na mwalimu wetu (Yoh 14:26). Anaishi ndani ya watoto wa Mungu (Rum 8:9), anashuhudia kuhusu Yesu (Yoh 15:27), kuleta utukufu kwake. Ni mkuu kuliko "ulimwengu" (1Yoh 4:4).

## II. ANGA LA MTU

Mungu alipomuumba mtu, aliumba mwanaume na mwanamke katika mfano wake: watu wawili tofauti watakaokuwa mmoja, hivyo kuashiria umoja katika mapana ya Mungu kichwa (Mwa 1:26,27). Kufuatana na roho hai, mtu aliumbwa "wa chini kidogo kuliko viumbe hai vya mbinguni" lakini alikuwa "ametuopoa utukufu na heshima" (Zab 8:5). Alitanywa mtawala wa kazi ya mikono ya Mungu, na kila kitu kiliwekwa chini ya miguu yake (Zab 8:6).

Kwa jinsi hiyo, mtu alichagua kusikiliza uongo wa ibiris, akamtenda Mungu dhambi na kuanguka katika dhambi. Kwa hiyo kila binadamu akawa mwenye dhambi (Rum 3:23), kufa katika uhalifu na dhambi (Efe 2:1) na kuhukumiwa kufa (Yoh 3:17;Rum 6:23). Haki ya mtu kutawala ilitwaliwa na ibiris, na sasa anaishi ulimwenguni akitawaliwa na shetani (Mt 4:8,9).

Wakati mtu anapokuwa muumini katika Yesu Kristo, anaendelea kuishi katika ulimwengu lakini siyo wa ulimwengu tena (Yoh 15:19). Amefunguliwa na Kristo kutoka kwenye nguvu za giza na kuhamishiwa katika ufalme wa mwanawe mpendwa (Kol 1:13). Anachukiwa na kuteswa na ulimwengu (16:18-21) na pia na Shetani na mapepo yake (Efe 6:11). Muumini ni sehemu ya vita vya kiroho kati ya Mungu na nguvu zake na Shetani na nguvu zake (2Kor 10:3-5).

### III. ANGA LA ROHO HAI

#### A. Malaika/Roho Zinazohudumia

Ingawa Biblia inazungumzia mara kwa mara juu ya malaika, hakuna utaratimu wa maelezo juu yake. Tunajua kuwa ni viumbe walioumbwa (Zab 148:2,5; Kol 1:16) walio wa chini kwa Mungu (Ebr 1:4), lakini wa juu kwa mwanadamu (Zab 8:5). Wana ufahamu mkuu lakini hawajui yote (1Pet 1:12). Wana nguvu kubwa lakini hawawezi yote (Mdo 12:7-11). Ingawa kawaida hawaonekani, walipoonekana walielezewa kama “kung’aa” na ‘weupe kama barafu” (Ez 1:13,14; Mt 28:3). Ni mawakala wa Mungu (mdo 7:38) ambao “mara nyangi wanafanya mapenzi ya Baba kikamilifu” (Mt 6:10). Kuhusiana na mtu, ni “roho wanaohudumu waliotumwa kuhudumia wale watakaourithi wokovu” (Ebr 1:14).

#### B. Mapepo/Malaika Walioanguka

Ingawa hakuna mahali ambapo imeelezewa dhahiri, inakubaliwa na wana injili kwamba mapepo ni malaika walioanguka (2Pet 2:4). Wana injili wanaamini kwamba Ufunuo 12:7-9 unaongelelea shetani na malaika zake wakiwa wamevulumishwa kutoka mbinguni kuja duniani. Yuda 1:6 inaongelelea malaika ambao hawakutunza nafasi zao za madaraka.

Katika vitabu vyote vya injili tunaona kwamba moja ya siraha zao ni kudhuru watu kwa magonjwa kadhaa kama vile upofu, ububu na ukoma. Shetani ni mtawala wao (Mt 12:24). Wameungana sana katika kusudi lao baya wakati wanafunzi walipotoa habari kwamba wamewatoa nje mapepo, Yesu alisema, “Ninamuona Shetani anaanguka kutoka mbinguni kama radi” (Lk 10:17,18).

#### C. Shetani

Nani ni Shetani? Ni kiumbe kilichoumbwa, pengine malaika aliyeanguka. Ni mtenda dhambi ambaye kazi yake Yesu alikuja kuiharibu (1Yoh 3:8). Anaitwa malkia wa ulimwengu (Yoh 16:11) na mungu wa “ulimwengu” huu (2Kor 4:4). Vyeo vingine alivyopewa ni muuaji na muongo (Yoh 8:44); simba aungurumaye anayezunguka zunguka akitaka kuwanasa watu (1Pet 5:8; 2Tim 4:17); mdanganyaji wa mataifa (Uf 12:9; 20:3,10); mshitaki wa wapendwa (Zak 3”1; Uf 12:10); malaika wa nuru (2Kor 11:14) nyoka wa kale, mwovu, nyoka mwenye magamba (Uf 12:7,9; 20:2); malkia wa mapepo, Belzaberi (Mt 12:24; Lk 11:15).

Nini Shetani anafanya? Anauendesha ulimwengu kwenye upofu (Uf 12:9). Shetani ulimwengu wote uko chini yake (1Yoh 5:19). Anafanya ishara za kuigiza na miujiza (2The 2:9). Anazungukia ulimwengu wote akitafuta mawindo ya kumeza (Ayu 1:7; 1Pet 5:8). Anafanya vita na watu wa Mungu (Uf 12:17). Anashikilia nguvu za kifo (Ebr 2:14).

Ni nini mipaka ya shetani? Hawezi kwenda zaidi ya Mungu alipomuruhusu (Ay 1:12). Ni adui aliyeshindwa! (Uf 12:7-9). Ni nini mwisho wa Shetani? Atakanyagwa na Mungu (Rum 16:20). Mungu atamwangamiza Shetani (Ebr 2:14) na atamtupia katika shimo liwakalo moto wa kiberiti (Uf 20:10).

### IV. ANGA LA VITA

Tulipokuwa wakristo tulihamishwa kutoka katika ufalme wa giza kwenda katika ufalme wa nuru (Kol 1:13). Ingawa tunaendelea kuishi katika ulimwengu wa mwili, kama raia wa ufalme wa Mungu tumekaa na Kristo katika ulimwengu wa Roho (Efe 2:6). Ni wapitaji na wageni katika ulimwengu (1Pet2:11). Matokeo yake, hatuishi kwa kipimo cha ulimwengu (2Kor 10:12). Kwa hiyo, ulimwengu na mtawala wake, Shetani, anatuchukia (Yoh 17:14) na kufanya vita dhidi yetu.

Katika somo lifuatalo la vita vya kiroho, (“Mapigano ya Kiroho” tutaangalia uwanja ambao Shetani anawapiga waumini, hapa tunaangalia uwanja wa msingi; akili.

“Ingawa tunaiishi ulimwenguni, hatupigani vita kama ulimwengu unavyofanya. Siaraha tunazpigana nazo si siraha za ulimwengu. Kwa kutofautiana, zina nguvu katika Mungu kuangusha ngome. Tunaangusha mawazo na kila kijiiuacho dhidi ya ufahamu wa Mungu, na kuteka nyara kila fikira kuzifanya kumtii Kristo” (2Kor 10:3-5).

Tambua kuwa tunatakiwa kutumia nguvu isiyo ya kawaida dhidi ya fikira na mawazo. Uwanja wa kwanza wa Shetani kushambulia ni akili.

Shetani ni mwongo na baba wa uouno (Yoh 8:44). Moja ya mbinu zake dhidi ya waumini ni kuwadanganya kuamini kwamba uongo ni kweli hasa. Uongo unaweza kuwa kinyume na asili ya Mungu na neno kake, kama ilivyokuwa kwa Eva (Mwa 3:1-4; 2Kor 11:13). Yesu mwenyewe ni ukweli (Yoh 14:6). Katika maombi yake kwa Baba katika Yohana 17, aliomba "watakase kwa ukweli. Neno lako ni kweli" (Yoh 17:17). Lazima tusimame imara katika ukweli wa neno la Mungu.

Uongo wa Shetani siku zote ni kutufanya kuamini kwamba hatuko watakatifu waliookoka kwa neema lakini wenyewe dhambi dhaifu kushinda hali yetu ya dhambi. Kinga yetu dhidi ya uongo huu pia ni kweli. Yesu alisema " Na mtaujua ukweli na ukweli utawaweka huru." Wakati Shetani anapotujaribu kufikiria hatuko kitu, hatuna msaada, hatuna nguvu, n.k. Lazima turudishe kwa ukweli. Katika Kristo tuna mamlaka dhidi ya Shetani na mapepo yake. Kanisa, mwili wa Kristo, umeshakuwa na hatima ya ushindi dhidi ya nguvu za giza. Huu ni ukweli ambao wapanda kanisa lazima waishi na kufundisha. Chini kuna mistari inayoeleza muumini ni nani katika Kristo. Kariri mistari hii na Shetani anapokujaribu uamini uongo, tumia ukweli dhidi yake

### Kielelezo 2.1 Mimi ni nani Katika Kristo

#### ***Kama muumini katika Kristo, mimi...***

- **siko chini ya hukumu, lakini nimepita kutoka katika kifo kwenda kwenye uhai (Yoh 3:18, Rum 8:1)**
- **kiumble kipyä (2Kor 5:17)**
- **nimewekwa huru nje na sheria ya dhambi na kifo (Ro 8:2)**
- **aliyechaguliwa na Mungu (Efe 1:4)**
- **aliyerithiwa na Mungu. Yeye ni Baba yangu (Efe 1:5)**
- **aliyekubaliwa na Mungu (Efe 1:6)**
- **aliyekombolewa, aliyenunuliwa, na kuthaminiwa na Mungu (Efe 1:7)**
- **Mrithi pamoja na Kristo (Eph 1:11; Ro 8:17)**
- **kufungiwa pamoja na Roho Mtakatifu (Efe 1:13)**
- **Kiroho aliye hai (Efe 2:1-7)**
- **mpokeaji wa neema ya Mungu (Efe 2:8)**
- **mfanya kazi mwenzake (Efe. 2:10)**
- **aliyekombolewa na Kristo kutoka kwenye nguvu za giza na kuwekwa kwenye ufalme wa mwanae (Kol. 1:13)**
- **hekalu la Mungu aliye hai (2Kor 6:16)**
- **mkamilifu katika yeye (Kol 2:10)**
- **chumvi na mwanga katika ulimwengu (Mt 5:13,14)**
- **anayekwenda kuwa kama Kristo atakaporudi (1Yoh 3:1,2)**

### SULUHU

Mungu katika utatu ni muumbaji na mtawala wa vitu vyote, akiwemo binadamu na roho hai (malaika, Shetani na mapepo). Ni mkuu kuliko vyote alivyoumba. Wakati Mungu alipomfufua "Kristo kutoka kwa wafu, alimkalisha katika mkono wake wa kuume katika anga la mbinguni, mbali na watawala wote na mamlaka, nguvu na milki, na kila cheo chochote kinachoweza kutolewa, siyo tu kwa kizazi kilichopo lakini pia kile kinachokuja. Na Mungu aliweka vitu vyote chini ya miguu yake na kumteua kuwa kichwa cha kila kitu kwa ajili ya kanisa... Na Mungu alitufufua pamoja na Kristo na kutukalisha pamoja naye katika anga la mbingu" (Efe 1:20-22; 2:6).

Sisi ni akina nani katika Kristo ni msingi wa mamlaka yetu juu ya vilivyo katika anga la roho hai (Shetani na mapepo yake). Tu wamiliki wa asili ya kimungu, watakatifu ambao wakati mwininge tunatenda dhambi. Lazima tupinge mashambulizi ya akili zetu na kushikiria kwenye ukweli wa ushindi

ambao umekuwa wetu katika Kristo. Kama wapanda kanisa, lazima tukumbuke kwamba Yesu alisema, "Nitalijenga kanisa langu na milango ya kuzimu haitashinda dhidi yake."

#### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Chukua mda kufanya marudio somo hili na angalia mistari yote iliyotolewa. Nukuru katika kitabu chako cha kumbukumbu za kiroho ukweli wowote mpya ambao umejifunza au mawazo ambayo yamechukua maana ya ndani kwako.
- Soma kwa sauti orodha "Mimi ni nani katika Kristo" na mshukuru Mungu kwa alichofanya kwa ajili yako. Kariri mistari ya maandiko ya wewe ni nani katika Kristo ambayo una mashaka nayo au hofu. Unapokuwa unakariri maandiko haya, Roho Mtakatifu anafanya ukweli huo kuwa halisi katika maisha yako.
- Fanya mafunzo ya Biblia kwa kufata neno ya Waefeso 4:17-5:21 yanayopatikana katika Ziada 2A.

#### **VYANZO**

- Moreau, A. Scott. *Essentials of Spiritual Warfare*. Wheaton, IL: Harold Shaw Publishers, 1997.
- Anderson, Neil T. *Victory over the Darkness*. California: Regal Books, 1990.



# Kujifunza Biblia kwa Kufata Neno: Waefeso 4:17 - 5:21

Mafunzo haya ya Biblia kwa kufata neno ya Waefeso yameshaanzishwa kwa ajili yako. Kwa uangalifu jifunze kile kilichokwisha fanywa. Kisha malizia mafunzo, ukijibu maswali yote, ukiandika ufupisho unapokuwa umeonyeshwa, na kujaza kila mahali palipoachwa wazi. Uwe na uhakika wa kuandika matumizi.

## I. UCHUNGUZI

Jifunze Waefeso 4:17-24. Andika uchunguzi ufuataao"

### A. Elezea jinsi mataifa wanavyoishi (17-19)

- v. 17 uhafifu wa kufikiri kwao
- v. 18. kuelewa kulikotiwa giza
- v. 18 kutengwa kutoka katika maisha ya Mungu
- v. 18 kutokujua kulikotokana na miyo iliyofanywa kuwa migumu
- v. 19 hisia zilizopotea
- v. 19 kujitoa wenyewe kwenye mambo ya mwili
- v. 19 kujitoa kwenye kila aina ya uchafu
- v. 19 tamaa ya kuendelea zaidi (uchafu)

Katika aya fupi, weka kwa kifupi katika maneno yako mwenyewe jinsi mataifa walivyoishi.

### B. Elezea jinsi ulivyo (Waefeso) Kuja kumjua Kristo (20-23)

- v. 21 ulifundishwa katika yeye kulingana na ukweli ulio katika Yesu
- v. 22 kuweka utu wako wa kale kando
- v. 23 kufanywa upya katika tabia ya akili zako
- v. 23 kuweka utu upya ulioumbwa kuwa kama Mungu katika haki ya kweli na utakatifu

Katika aya fupi, fupisha kwa maneno yako mwenyewe jinsi waefeso walivyomjua Kristo.

## II. UFAFANUZI

Jibu maswali yafuatayo ya kiufafanuzi:

- Jinsi gani matendo ya mtu yanawakilishwa na kufikiri kwake (akili)? (vs 17,22,23).
- Ni sehemu ipi ukweli ulisimama katika kubadilisha matendo ya Waefeso? (21).
- Elezea "utu upya" (22). Jinsi gani kiumbe hiki kipyä kinafanana na uumbaji wa kwanza wa Mungu wa mtu? (Linganisha Mwa 1:27).

## III. MATUMIZI

Waefeso 4:25-5:21 ni matumizi ya Paulo. Orodhesha vitu anavyohusisha katika matumizi yake. Kisha andika maelezo yanayosema jinsi utakavyotumia vitu hivi katika maisha yako na huduma.

Mstari	Matumizi
4:25	Weka kando isiyo ya kweli
4:25	
4:26	
4:26	
4:27	Jinsi gani hasira zinampa Ibirisi pa kuwekea mguu?
4:28	
4:28	
4:29	
4:30	Usimuhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu (Jinsi gani tunamuhuzunisha)?
4:31	
4:32	
5:1	
5:2	
5:3	
5:4	
5:5	
5:6	
5:7	
5:8	
5:9	
5:10	
5:11	
5:12	

**Matumizi katika maisha yangu na huduma:**



# Mapambano ya Kiroho

## WAPANDA KANISA CHINI YA MASHAMBULIZI

### ☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wapanda kanisa kutambua na kujilinda dhidi ya mashambulizi ya kishetani na kuweza kuwasaidia watu wanaoteseka kutohana na taabu ya kimapepo.

### ☞ **Wazo Kuu**

- Mashambulizi ya shetani yanaweza kuwa katika mwili, vitu, akili/hisia au anga la kiroho.
- Kujilinda mwenyewe dhidi ya Shetani kunahitaji ufahamu wa maandiko na ukomavu wa kiroho.

### ☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wanaposhika yaliyomo katika somo hili, wafunzwa wata ...

- Jua jinsi ya kutambua wanapokuwa chini ya mashambulizi ya kishetani
- Kuwa imara katika Bwana na nguvu za uwezo wake.
- Anza kujifunza jinsi ya kujilinda dhidi ya mashambulizi ya kishetani na kuchukua hatua katika chuki ya vita.

### ☞ **Ziada**

3A Kujifunza Biblia: Jinsi gani Yesu alishughulika na watu walio na mapepo?

3B Mchanganuo wa mambo ulimwenguni

## UTANGULIZI

Vita vya kiroho ni hali halisi kwa kila muumini katika Kristo, Wakati mtu anapokuwa muumini katika Kristo, uhusiano wake na kila kitu katika anga la kihisia, kiakili, kiroho na kimwili unabadilika. Muumini ni kiumbe kipyta katika Kristo (2Kor 5:17), mkaazi wa mbinguni (Flp 3:20), na mtoto wa Mungu (Yoh 1:12). Kwa sababu ya uhusiano wake mpya na Mungu, muumini anakawa mlengwa wa mashambulizi na maadui wa Mungu—Shetani na nguvu zake wanaompinga mtu wa Mungu, mipango na makusudi yake.

Somo lina habari ambazo ni za kimsingi katika kuelewa jinsi wapanda kanisa wanavyoweza kuwa katika mashambulizi ya kiroho, jinsi ya kujilinda mwenyewe, jinsi ya kuwasaidia wengine waliokwisha dhurika kwa nguvu za kipepo. Katika mapambano yanayoendelea kati ya Shetani na nguvu za Mungu, kila mara kanisa jipya linapokuwa limeanzishwa shetani anafahamu kwamba anapoteza ngome katika ulimwengu anaotaka kutawala. Kwa sababu ya hili, kwa ushindi atashambulia makanisa mapya na waumini wapya, na kufanya kila awezalo kuwaangamiza.

Wapanda kanisa si lazima tu wawe tayari kwenye mapambano ya kiroho wenyewe (yote kiulinzi na kichuki), lakini pia lazima wawafundishe waumini wapya kwenye vikundi kiini na makanisani juu ya mapambano ambayo ni sehemu yao, endapo wawe wanajua au la. Bila kuwa na kuelewa imara kwa kibibilia kwa vita vya kiroho vinavyoendelea kuwazunguka. Makanisa mapya yataathirika zaidi na mashambulizi ya kishetani ambayo yanaweza kudhoofisha hata kuwaangamiza. Wapanda kanisa wana jukumu la kusaidia kuandaa "jeshi" la Mungu la waumini kwa ajili ya mapambano ya kiroho yaliyo mbele yao.

## I. VIWANJA VYA MASHAMBULIZI YA KISHETANI

Shetani na wenyiji wake mapepo wako ulimwenguni, wakipigana dhidi ya mipango ya Mungu na makusudi. Watu wanaweza kupata mashambulizi ya kishetani katika anga la akili, kimwili na kiroho. Katika somo lililopita la Vita vya Kiroho "Nguvu ya Vita vya Kiroho" tumeona kwamba uwanja wa msingi ni ule wa akili. Katika sehemu hii, tutajadili anga nyinginezo. Shetani na mapepo yake yanazoweza kushambulia moja kwa moja, au kutumia wengine.

Mfano wa baadaye ni katika mateso kutoka ulimwenguni. Mashambulizi haya yasiyo ya moja kwa moja kutoka kwa Shetani yanatakiwa yaje pasipo na kushangaa kwa waumini, mtume Paulo alimwandikia Timotheo "...kila mmoja anayetaka kuishi maisha ya kimungu katika Kristo Yesu atateswa" (2Tim 3:12). Petro aliandika waraka wake wa kwanza kuwaambia waumini jinsi ya kuishi chini ya mateso. Yesu alisema ulimwengu utawachukia wafuasi wake (Yoh 15:18-19). Kwa hiyo, waumini wanatakiwa wasishangazwe na mateso, lakini wanatakiwa wafahamu kwamba ni mashambulizi yasiyo ya moja kutoka kwa Shetani.

### A. Mashambulizi katika Uwanja wa Mwili

#### 1. Afya ya mwili

Sio kila ugonjwa ni matokeo ya mashambulizi ya kishetani. Kwa jinsi hiyo, tunaona katika injili kuwa kuna hali ambazo haya yalikuwa kweli (9:32-33; Lk 13:16; Mk 5:1-13). Tazama Ziada 3A, "Jinsi Yesu Alivyoshughulika na watu waliokuwa na mapepo?".

#### 2. Haja za Mwili kama Vile Chakula na Haja ya Mme na Mke

Mungu aliumba wanadamu na mahitaji na haja. Yanapotimizwa kisawasawa haya ni mazuri. Kwa jinsi hiyo, Shetani anapenda kuchukua kilicho kizuri na kumjaribu mtu kukitumia katika njia zenye madhara. Katika jaribio la Adamu na Eva, Shetani alitumia kitu fulani kilichoonekana machoni (chakula) kuwasababisha kufanya dhambi. Dhambi haikuwa kwa sababu walitaka au walihitaji chakula, lakini kwa sababu walitumia vibaya chakula—katika hali hii chakula ambacho kilikuwa kimefichwa na Mungu (Mwa 3:1-6). Kama vile, Baada ya Yesu kuwa anafunga kwa siku arobaini mchana na usiku, Shetani alimjaribu kupoza njaa yake kwa kutumia nguvu ya asili ya kipekee ya Baba yake (Mt 4:2-4).

Shetani anawajaribu watu kutumia vibaya kile ambacho Mungu ameumba kuwa kizuri. Yohana anaelezea kama sehemu ya ulimwengu (inayotawaliwa na Shetani) tamaa ya macho (1Yoh 2:15-16). Masimulizi mengi ya hivi karibuni yanazungumzia juu ya viongozi wa kikristo ulimwenguni walioangukia katika dhambi ya uzinzi. Wapanda kanisa wako "mstari wa mbele" wa huduma na hivyo wanahitaji kujilinda wenyewe kwa uangalifu dhidi ya vishawishi ambavyo Shetani zaidi atavitoa hasa kwao.

### B. Mashambulizi Katika Uwanja wa Vitu

Uwanja mwininge amba Shetani anashambulia ni katika kuanzisha haja zisizo za afya kwa vitu vizuri ambvyo Mungu ametupa. Shetani alimjaribu Yesu katika uwanja huu kwa kumpa yote katika ufalme wa ulimwengu na fahari yake kama angemshujudia. (Mt 4:8).

Lililo karibu na hili ni haja ya mamlaka. Katika Mwanzo 1:28-29, Mungu alimwambia Adamu na Eva kwamba wangetawala juu ya kila kiumbe hai. Lakini matokeo ya dhambi zao ilikuwa kwamba mwanaume angetawala mwanamke (Mwa 3:15). Ndipo kukaanza mahangaiko ya mamlaka juu ya wanadamu wengine.

Wapanda kanisa wanatakiwa kuwa waangalifu kwamba haja zisizokuwa za kiafya za kumiliki na mamlaka haziwfanyi kuondoa macho yao kwa Yesu.

### C. Mashambulizi katika Uwanja wa Akili/Hisia

Majaribu ya kukatishwa tamaa au kukata tamaa yanaweza kuwa mashambulizi ya moja kwa moja kutoka kwa adui. Tazama Mk 5:1-10 na Lk 0:37-42.

### D. Mashambulizi Katika Uwanja wa Kiroho

Leo kuna ongezeko la haja katika siri. Watu wengi wanatafuta mizimu, kuwasiliana na mizimu, waponyaji wa kuona, maaguzi kwa nyota, n.k. Kutokana na ufanyaji wa mafumbo hayo Shetani anaweza kushikiria maisha ya watu.

Wapanda kanisa wanatakiwa kuwa waangalifu kuepuwa mazoea haya ya mafumbo, na lazima wafundishe wengine kwenye vikundi kiini vyao na makanisa hatari zinazo husika katika mazoea haya. Ni kawaida sana kwa waumini wapya kutokuelewa kikamilifu ukali wa mazoea ya mafumbo haya. Wanaweza kuwa wametembelea waambiaji wa bahati, waponyaji wa kiroho, au mtu mwingine yejote anayeshughulika na shughuli za mafumbo kabla ya kuwa waumini, na hawaoni hatari ya kurudi kwao.

## II. JINSI YA KUJUA KAMA TATIZO LINATOKANA NA SABABU ZA ASILI AU NI MASHAMBULIZI YA SHETANI

Sio rahisi mara nydingi kutofautisha chanzo cha tatizo. Kwa mfano, Siyo kawaida kusikia wafanya kazi wa kikristo wakijilinganisha na masimulizi kama haya:

*"Nilikuwa peke yangu chumbani, nikiwa nimesinzia fofoto. Ghafila nilikuwa nimeamshwa bila sababu yoyote. Giza chumbani lillonekana la kukandamiza na nikajikuta moyo wangu unakwenda mbio, pumzi yangu ikitoka kwa shida na mwili wangu ukijawa na jasho. Nikahisi kuwa hili liliwu ni shambulizi la Shetani, nilikaa kitandani, nikawasha taa na kwa sauti kubwa nikaanza kumkiri Yesu kristo kama Bwana na kumuuliza ulinzi kutokana na roho wabaya wowote wanaajaribu kunidhuru. Nilipoomba, mkandamizo ukaondolewa na nikalala chini na kisha nikalala tena fofoto."*

Mtu anayehusika na masimulizi haya alikuwa ameshambuliwa na Shetani na mara akaendelea na kurudisha mashambulizi. Unaweza kuhisi kuwa uko chini ya mashambulizi ya Shetani, Hapa kuna baadhi ya kanuni za kibiblia za kufikiria. Hazikuandikwa kwa utaratibu wowote.

- Zijaribu roho uone kama zinatoka kwa Mungu (1Yoh 4:1-3)
- Tafuta msaada kutoka kwa mtu katika mwili wa Kristo mwenye kipawa cha kutofautisha kati ya roho (1Kor 12:10).
- Majoribu yanaweza yakawa yanatoka kwa Bwana kutufanya kukomaa na wakamilifu (Yak 1:2-4)
- Majoribu yanatoka kwa mwovu; kama tunaruhusu haja zetu wenyewe mbaya kutusababisha kutoa nafasi , matoke yake ni dhambi (Yak 1:13-14).
- Shetani anashambulia kutufanya kutenda dhambi, lakini Mungu analeta mema (Mwa 50:19-20).
- Shetani anatumia vitu katika maisha yetu ambavyo Mungu anatumia kuonyesha nguvu zake katika udhaifu wetu (2Kor 12:7-9).

## III. JINSI YA KUJILINDA MWENYEWE DHIDI YA MASHAMBULIZI YA KISHETANI

### A. Teka Nyara Kila Fikira Ipati Kumtii Kristo (2Kor 10:3-5)

Kukariri na kutafakari maandiko kunaturuhusu kutathimini mawazo na maono yetu yanayokuja katika akili zetu na kukataa hizo ambazo ziko kinyume na ukweli wa maandiko. Kukariri maandiko pia kunasaidia kufundisha namna yetu ya kufikiri ili kwamba tuongozwe katika kufikiri na kutenda zaidi kama Kristo.

### B. Kugeuzwa Akili Zetu

Muombe Mungu kuchunguza mawazo yako na kudhihirisha kwako kila kilicho kiovu au kisicho safi. Yakiri hayo kwa Bwana na yaache (Zab 139:23-24). Fikiria juu ya vitu ambavyo ni vya kweli, ya staha, yaliyo ya haki, yaliyo safi, yenyenye kupendeza, yenyenye sifa njema, au yenyenye kufaa sifa (Flp 4:8).

Uwe makini na gharika ya uongo wa ngono na majoribu ambayo yanaweza kujaza akilini mwako na mawazo "Shetani hana nguvu dhidi yako isipokuwa kila unachompa kwa kushindwa kuteka nyara akili yako na kwa hivyo kudanganywa katika kuamini uongo" (N. Anderson, Ushindi Dhidi ya Giza Uk 169 na 170).

### C. Vaa Siraha Zote za Mungu (Efe 6:10-18)

Fahamu wokovu wako kwa imani katika Kristo, haki yako mbele za Mungu kwa damu ya Kristo, na amani uliyo nayo na Mungu kwa sababu ni mtoto wake. Chukua mda wa kumsifu

Baba kwa ajili ya ushindi wake juu ya mwovu na ukweli kwamba katika Kristo una ushindi dhidi ya mwovu.

Silaha moja ya kujikinga ambayo muumini anayo ni neno la Mungu—"upanga wa Roho" (Efe 6:17). Waumini wanaonywa katika maandiko yote kusimama imara katika ukweli wa neno (yoh 6:32; 1Pet 5:9).

#### D. Kubali Kufunika kwa Damu ya Mwana Kondoo (Uf 12:11)

Msingi pekee wa ushindi dhidi ya mwili, ulimwengu na Shetani ni damu iliyomwagika ya Yesu Kristo msalabani. Kujitoa kwake kulivunja nguvu ya Shetani na kumruhusu mtu kuingia kwenye ushirika na Mungu. Ni muhimu kwamba waumini wanafahamu kwamba hawawezi kumshinda Shetani kwa nguvu zao wenyewe, isipokuwa kwa damu pekee iliyomwagika ya Yesu Kristo.

#### E. Usiruhusu Dhambi Kutawala Juu Yako (Rum 6:12)

Waumini wanaonywa kujiondoa wenyewe kwenye hali ambayo inaweza kuletea kujitoa kwenye dhambi (1Tim 2:22). Vile vile, waumini wanatakiwa, "kuepuka kuonekana kokote kwa uovu" (1The 5:22; Efe 5:3).

### IV. MIPAKA KATIKA KUSHUGHULIKIA MATESO YA KIPEPO

Katika Agano Jipyä lote na mifano kutoka ulimwenguni kote (Tazama Ziada 3B, "Mchanganuo wa Mambo Kutoka Ulimwenguni Kote"), tunaona watu walio na mapepo. Kuwa na mapepo ni dhahiri katika ulimwengu tunaoishi.

Ni wazi pia kutoka katika maandiko kwamba waumini wanaweza kuijiveka wazi wenyewe kwenye kukandamizwa na mapepo, au kuathiriwa na mapepo. Waefeso 4:27 inawaongelea waumini kutompa Shetani "pa kuweka mguu" katika maisha yao. 1Petro 5:8 waliandikiwa waumini na kutuambia kwamba tuna adui anayezunguka zunguka akitafuta wa kuangamiza. Katika 1Wakorintho 2:11 Paulo anatuambia kwamba Shetani ana hila dhidi yetu, na kwamba anatutaka kuangukia katika mtego wake ili kwamba apate haki ya kutudhuru kwa mapepo yake.

Kila mkristo anatakiwa aweze kujilinda mwenyewe kutokana na mashambulizi ya kishetani, kwa kuwa Mungu ametupa mipaka wazi kutoka kwenye maandiko jinsi ya kuishi na jinsi ya kuva siraha zake kama kizuzi. Ni wazi, wasioamini hawajui jinsi ya kujilinda wenyewe, na hawana nguvu za Roho Mtakatifu katika maisha yao kuwapa uwezo wa kufanya hivyo. Hata hivyo, kuna baadhi ya waumini pia ambao kwa sababu tofauti tofauti wanachagua kuijachia wenyewe kwenye kuathiriwa na mapepo katika maisha yao.

Kwa sababu ya hili, hali hasa ya kufanya kazi na watu wanaougua kutokana na ukandamizwaji wa kimapepo na kumilikiwa kukabiliwa ni kwa **kweli**, siyo kukabiliwa na **nguvu**. Baadhi ya wakristo kimakosa wanaamini kuwa Mungu ni mwenye nguvu zaidi kuliko Shetani, kwamba kwa jina la Yesu wanaweza kuondoa kuwepo kote kwa mapepo katika maisha ya yule anyeugua. Wakati Mungu akiwa na nguvu zote na Shetani siyo, Mungu amempa mtu uhuru wa kuchagua kama au la ataruhusu "mfalme wa ulimwengu" (Yoh 16:11) kuwa na nafasi katika maisha yake. Mungu anachagua kudharau vitu hivi na kumruhusu Shetani kuwa na kiasi fulani cha kutawala katika maisha yetu. Katika kutambua ukweli wa haki ya waumini katika Kristo ambako kunampatia kuchagua kutaka shughuli za kidhambi ambazo vinginevyo zingempa Shetani haki ya kuhangaisha.

Mipaka ifuatayo inaweza kutumika kuwahudumia hao wanaoteseka kutokana na badhi ya aina ya kuwepo hali ya kipepo katika maisha yao.

#### A. Omba na Tafuta Hekima Kutoka kwa Roho Mtakatifu

Kushughulikia kuwepo kwa mapepo kunahitaji hekima kubwa ya kiroho na utegemezi kwa Roho Mtakatifu. Shetani ni adui mwenye nguvu na kukabiliana naye au na nguvu zake kunatakiwa kusiingiliwe kiurahisi. Hitaji la kuelekezwa na kuongozwa kutoka kwa Roho Mtakatifu lazima kusisitizwe kupita, kwa kuwa hakuna "utaratibu" wa kufanya kazi na watu wanaoumwa kutokana na shughuli za mapepo katika maisha yao. Kila mtu ni tofauti, kila hali inatofautiana, na ingawa kuna kanuni za jumla zinazohusika, kila hali inahitaji utegemezi katika hekima kutoka kwa Roho Mtakatifu. Mda katika maombi lazima utumiwe kabla huduma ya aina yoyote inayohusiana na madhara ya kimapepo kufanya.

### B. Fanya Kazi na Wengine

Aina hii ya huduma inatakiwa kawaida ifanyike na angalau na mmoja au zaidi ya waumini waliokomaa katia Kristo. Kama inawezekana, fanya watu wawepo wenye vipawa vya utambuzi na ambao wamewahi kuwa na uzoefu na kukandmizwa/kuwa na mapepo. Chukua mda pamoja kama kikundi omba (na funga, kama ni lazima) unapokuwa unashughulika na mtu anayeugua. Kama ikiwezekana kabisa, wapanda kanisa na wafanya kazi wengine wa kikristo wanatakiwa waepuke kufanya aina hii ya huduma wenyewe.

### C. Onyesha Kilichosababisha

Wakati mwagine kujionyesha kwa mapepo kunatokea bila kutarajia katika sehemu za hadharani kama vile kwenye huduma ya ibada, mafunzo ya Biblia, mikutano ya vikundi kiini, au maandalizi mengine ya ushirika. Katika hali hizi viongozi wa kikristo walioipo wanaweza wasiwe na jingine la kufanya isipokuwa kushughulikia mara moja hali, wakitegemea nguvu na uwepo wa Roho Mtakatifu kuwaongoza.

Kwa jinsi hiyo, ni kawaida zaidi kuwepo kwa mapepo kujionyesha kwenyewe kwa kipindi cha mda katika maisha ya mtu, na katika namna kwamba tatizo linaonekana kwao na wengine wanaowazunguka. Katika matukio haya, ni lazima kuandaa mkutano kati ya mtu huyu na hao walio katika kanisa wanaoweza kumsaidia kuwa huru kutokana na mapepo katika maisha yake. Kusudi la mkutano ni kujaribu na kuelewa nini kimetokea katika maisha ya mtu huyu ambacho kinaweza kikawa kimempa Shetani nafasi ya kumdhuru. Ni wakati pia wa kuona kama tatizo ni la kipepo, au kama kuna sababu zingine za asili zilizohusiska.

Kuna njia nyingi ambazo watu wanaweza kuwa wazi wenyewe kwa Shetani na kumpa nafasi ya kuwashambulia, Baadhi ya maeneo mengi zaidi ni mpamoja na:

- Shughuli za siri: uzinzi, dini za mashariki zinajishughulisha (kama vile sala za utambuzi wa kubuni), umiungu, kutoa damu kwa "siri", kushiriki katika ibada za mazoea, unajimu, kuambia bahati, aina fulani ya nguvu inayomfanya mtu kusinzia na kufanya mambo yanayoamriwa katika usingizi, nguvu za uponyaji, uzoefu nye ya mwili.
- Uchawi na ushetani: wimbo au maneno ya kunuia uchawi, kuloga, sala za kishetani, kuwakabidhi watoto kwa Shetani, sala za kunyanyasa, uchawi (mweupe na mweusi).
- Ukaidi, dhambi inayoendelea na ambayo hajatubiwa: madawa, ulevi, hasira, dhambi za zinaa, machukio, na roho isiyosamehe, n.k.

Ni muhimu sana kwamba watu wanaougua kuwa wazi kabisa na waumini wanaotaka kuwasaidia. Wamewahi hivi sasa, au wakati uliopita kujihusisha na kufanya mambo ya mafumbo? Vipi kuhusu wazazi wao au ndugu wengine? Kama ni waumini, wana baadhi ya dhambi "zilizojificha" katika maisha yao ambazo hawataki kukiri? Iwezekanavyo, chunguza kila kitu kinachoweza kuchangia kwenye kuonekana kwa kipepo katika maisha yao.

### D. Shughulikia Swala la Dhambi

Iwapo mtu aliyedhurika ni muumini au la, ni lazima atake kuwa huru kutokana na kuwe na mapepo. Kutokana na kilichokuwa kimejifunzwa kuhusu shughuli za mafumbo yaliyopita au ya sasa, dhambi zisizoonekana n.k., mtu huyu anatakiwa atubu dhambi hizi na shughuli yoyote ambayo inaweza ikawa imempa Shetani kuweka mguu katika maisha yake. Kila kitu kinatakiwa kitubiwe kwa sauti msamaha kuombwa kutoka kwa Mungu. Mtu anatakiwa akane matendo yoyote yaliyopita ya kishetani na ngome ambazo haya yalimpa Shetani katika maisha yake.

Ni muhimu kulelewa kwamba mtu huyu hahitaji kuwa mkristo ili kuweza kuwekwa huru kutokana na nguvu za kipepo katika maisha yake. Kwa jinsi hiyo, bila ulinzi na nafasi ambayo waumini waliyo nayo katika Kristo dhidi ya Shetani, mtu huyu yuko wazi kwa kujirudia kwa mapepo katika maisha yake, wakati mwagine hata kwa nguvu zaidi (angalia Mt 12:43-45). Maswala ya dhambi yanapokuwa yameshughulikiwa, injili lazima itolewe wazi na nafasi kutolewa kwa mtu huyu kumpokea Yesu kama mwokozi.

Bila kujali hali ya kiroho ya mtu, lazima ajue kuwa atakaporudi kwenye matendo ya mafumbo au dhambi ya ukaidi, anajiachilia mwenyewe kwenye shughuli za kishetani katika maisha yake.

#### E. Ukombozi

Katika hatua hii, muumini aliyejhuisika anatakiwa aombe na kumuuliza Roho Mtakatifu kuwaonyesha jinsi anavyota kushughulikia kazi za kipepo katika maisha ya mtu huyu. Hii inaweza kuwa rahisi kama kufukuza pepo (ma) katika jina na mamlaka ya Yesu. Wakati mwininge, maombi ya mda mrefu na kufunga kunawenza kuhitajika kuvunja katika upinzani wa kiroho wa nguvu za kipepo zinazohusika. Wakati mwininge kwenye maswala ambapo mtu aliyeathirika ni muumini, Roho Mtakatifu atawaongoza kufahamu nafasi yao katika Kristo, kutubu dhambi zao ambazo zimeletea kuwa na mapepo, na kumkana shetani wenyewe.

Tambua kuwa katika mda huu wa kumuweka mtu huru kutoka katika ukandamizwaji wa mapepo, ni vizuri kutowasiliana kwa njia yoyote moja kwa moja na pepo (ma) linalohusika. Yohana 8:44 inatuambia kuwa ibirisi ni muongo na baba wa uongo, na hakuna sababu ya mapepo kusema chochote isipokuwa chini ya ukweli. Wakristo wengi katika huduma na watu walioukandamizwa wametambua kwamba kuongea na watu wenyewe mapepo na kuwaliliza kwamba wajionyeshe wenyewe kunasababisha zaidi ubaya, jeuri, kuonyesha ujeuri, kuanzisha fujo sana na kufanya utaratibu wa kuwa huru kuwa mgumu kutokana na pepo lililohusika.

Katika njia sawa kwamba hakuna "utaratibu wa kimujiza" wa kumuondoa mtu kutokana na kuwa na mapepo katika maisha yake, hakuna pia hakikisho la matokeo kutoka mda wa huduma ya kuombea na kufunguliwa.

Wakati mwininge mtu aliyeathirika atafunguliwa kabisa kabisa na kwa jumla kutoka katika shughuli zote za kipepo. Wakati mwininge kunakuwa na kufunguliwa kidogo au hakuna kabisa. Wakati mwininge Roho Mtakatifu anapenda matatizo kadhaa katika maeneo ya maisha ya mtu aliyeathirika yatatuliwe moja baada ya moja kwa kipindi cha mda. Wakati mwininge maombi zaidi na kufunga yanahitajika. Katika maswala, muumini anatakiwa aombe na kuomba kuendelea kuongozwa na kuelekezwa kutoka kwa Roho Mtakatifu.

#### F. Ufuatiliaji

Inawezekana, muumini aliyejomaa kukabidhiwa kama mshauri kwa mtu huyu kujibu maswali anayoweza kuwa nayo na "kumwangalia" kwa miezi kadhaa. Katika nyakati ambapo ufunguzi mkamilifu haukupatikana, mshauri anaweza kuendelea kufanya kazi na mtu huyu kuangalia katika maeneo ya maisha yake ambapo kunawenza kukawa na dhambi ambayo hajaikiri, kufanya mambo ya mfumbo, n.k. Ingawa kuonekana kwa nguvu za kipepo kunawenza kupungua kwa mda baada ya kuombewa au kukemea nje mapepo, maeneo yote yaliyompa Shetani kuweka mguu kwa mara ya kwanza hayajashughulikiwa, mara au baadaye ukandamizaji wa kipepo utaendelea na kujifanya kujulikana tena.

Kama mtu anampokea Kristo kama mwokozi wakati wa kufanyiwa ukombozi, mshauri anaweza pia kusaidia katika kumfanya malezi muumini huyu mpya na kumukumbusha juu ya ukweli wa yeze ni nani katika Kristo. Kama dalili nyingine za shughuli za kipepo zimeonekana, utaratibu wa ukombozi unatakiwa urudiwe, kwa kuangalia "chimbuko" ambalo mtu huyu amempa Shetani katika maisha yake. Hatima ya uhuru itapatikana wakati ngome zote zitakapokuwa zimeachiwa, wakati mtu anapoelewa yeze ni nani katika Kristo, na wakati Kristo anapokuwa amepewa kutawala kabisa juu ya kila eneo la maisha yake.

#### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Katika maisha yako na huduma kama mpanda kanisa, unakutana na chochote ambacho unaweza kufikiri kuwa ni mashambulizi ya moja kwa moja ya mwovu? Kama ni hivyo, Orodhesha njia kutoka katika mafunzo haya zinazonyesha nini unatakiwa kufanya kusimama kinyume na mashambulizi haya. Mshirikishe hili mkristo aliyejomaa atakayeomba nawe.
- Malizia jedwali katika Ziada 3A.
- Soma mchanganuo wa mambo katika Ziada 3B.

**VYANZO**

- Anderson, Neil T. *The Bondage Breaker*. Eugene, Oregon: Harvest House Publishers, 1990,1993.
- Anderson, Neil T. *Victory over the Darkness*. California: Regal Books, 1990.
- Arnold, Clinton. *Power and Magic*. Grand Rapids, MI: Baker Books, 1989,1992.
- Moreau, A. Scott. *Essentials of Spiritual Warfare*. Wheaton, IL: Harold Shaw Publishers, 1997.
- Moody Bible Institute. *Demon Experiences in Many Lands; A Compilation*. Chicago, IL: 1960.



# Mafunzo ya Biblia

## JINSI GANI YESU ALISHUGHULIKA NA WATU WALIFUNGWA NA MAPEPO?

Jedwali zifuatazo zinaordhesha sehemu kwenye vitabu vya injili mahali Yesu aliposhugulika na watu waliofungwa na mapepo. Malizia mchoro, na kisha andika jinsi ukweli huu unavyohusu katika maisha yako na huduma. Baadhi ya kazi imeshafanyika kwa ajili yako.

Marejeo	Hali ya Nyuma na Mtu mwenye mapepo	Jinsi Gani Yesu Alivyoitikia?	Nini Yalikuwa matokeo?	Ufanuzi:
Mt 4:24-25	Kutoka "... katika Siria yote watu waliletwa kwake...walio na mapepo."	Aliwaponya	Umati mkuu ulimfuata.	
Mk 1:21-28	Katika Kapernaumu siku ya sabato. Mtu wa kwenye sinagodi – "Tuna nini nawe Yesu, Yesu wa Nazareti? Umekuja kutuangamiza? Ninakujua ni nani – mtakatifu wa mungu"	Aliliamuru pepo "Nyamanza kimya! Mtoke mtu huyu!"	Roho chafu zikamtingisha mtu huyo kwa mshindo na kutoka nje!	Yesu anatoa amri kwa roho wabaya na wanamtii. Mapepo yanamjua Yesu ni Mungu na ana nguvu ya kuyaangamiza. Alipoongea, mapepo yalitii. Wakati watoto wake wanapoongea chini ya mamlaka yake, mapepo pia yanattii.
Mk 1:32-39 (Lk 4:40 – 41)	Siku hiyo kama hapo juu. Jioni; nyumbani kwa Simoni na Andrea. Watu walileta wenye mapepo kwa Yesu	Akayaamuru nje mapepo mengi lakini hakuyaruhusu kuongea kwa sababu yalimjua alikuwa nani		Yesu hakutaka watu kumfata kama masia kabla ya kumkubali kwanza kama mwokozi.
Mk 3:15; 6:7 (Mt 10:2-4) (Lk 6:14-16)		Yesu alichagua wanafunzi 12; na kuwapa mamlaka ya kuamru mapepo		
Mt 8:16-17		Aliziamuru roho kwa neno		
Mt 8:28-34	Watu 2 waliokuwa na mapepo waliotoka makaburini walikuwa na fujo na kumpigia kelele Yesu "Una nini na sisi, mwana wa Mungu?" ...umekuja kutuadhibu kabla ya mda unaokubalika?"			Yesu atahukumu mapepo Na yatatupwa jehanamu.
	Walimusih Yesu, "kama unatutoa nje, tutupe katika makundi ya nguruwe	Akasema "Nenda"	Mapepo yakawaingia nguruwe; mji wote ukatoka kwenda kukutana na Yesu; wakamuomba kuondoka kwenye eneo lao.	

Marejeo	Hali ya Nyuma na Mtu mwenye mapepo	Jinsi Gani Yesu Alivyoitikia?	Nini Yalikuwa matokeo?	Ufanuzi:
Mk 5:1-17	Mtu mmoja aliyekuwa na pingu za chuma Hakukuwa na mwenye nguvu wa kumfunga Usiku na mchana alipiga kelele na kujikata kata mwenyewe			
	Mapepo yali muomba Yesu asiyaadhibu.	"Mtoke mtu huyu, ninyi roho wabaya"		
	"Ligion, kwa kuwa tu wengi"	Jina lako ni nani?"		
	Yali ombo kupelekwa kwa nguruwe	Aliyapa ruhusa ya kuwaingia nguruwe	Mapepo yakakimbilia ziwani na yakazama	
	Mtu aliomnba aende na Yesu	"Nenda nyumbani kwako na wambie ni kiasi gani Bwana amekufanya na jinsi ambavyo amekuwa na rehema kwako		
Lk 8:26-37	Kwa mda mrefu alikuwa hakuvaa nguo au kuishi kwenye nyumba		Baada ya mapepo kuondolewa, mtu huyo akapewa nguo na kuwa katika akili sawa	
	Yali muomba kwa kurudia asiyaamuru kwenda shimoni.			Mapepo yaligundua kwamba Yesu ana mamlaka ya kuyaamuru kwenda shimoni
Mt 12:22-28	Kiziwi na kipofu	Yesu alimponya mtu huyo ili aweze kuona na kuongea	Watu walishangazwa "Huyu anaweza kuwa mwana wa Daudi?" Mafarisayo: Anafanya haya kwa nguvu ya Belizuberi. Mafundisho ya Yesu yakafuata Mt 12:25-29 Mt 3:23-30 Lk 11:14-26	
Mt 15:21-28	Yesu akatoka kwenda Tiro na Sidoni; Mwanamke mkanaani: Bwana, unirehemu mimi! Binti yangu anaumwa sana kutokana na mapepo"	"Nimetumwa tu kwa kondoo waliopotea wa Israeli."		
Mk 7:24-30	Bwana, nisaidie.	"Si harali kuchukua na kuwatupia mbwa wao."		

**Matumizi katika maisha yangu na huduma:**



## Michanganuo ya Mambo Kutoka Ulimwenguni

Ifuatayo ni michanganuo ya mambo inayoonyesha baadhi ya wamishenari walivyoshughulika na mapepo kwenye huduma. Isipokuwa mmishenari katika mafunzo ya kwanza, majina yote yamebadilishwa. Hii inaweza kukusaida kukutana na hali sawa unayoweza kukabili unapojishughulisha na kuendeleza kanisa.

### I. MCHANGANUO WA KWANZA: DICK HILLS ANASIMULIA MASIMULIZI YAFUATAYO KUTOKA CHINA

Askari kijana alimleta mke wake kwangu kuondoa mapepo, akisema, "mke wangu yuko uani, na ana mapepo. Mara mbili pepo limemwamuru kujiua, ya kwanza kwa kujitundika na nyingine kurukia kwenye handaki. Mara zote alilitii, lakini niliweza kumuokoa."

"Tulikwenda kuungana kuomba kwamba mwanamke afunguliwe. Ninakiri kwamba niliomba kwa mashaka, nikishangaa kama nitahitaji kipawa maalumu cha uponyaji. Tulipoomba, mwanamke aliyekuwa na pepo alikuwa akichukua maneno kutoka katika maombi yetu na kufanya mzaha. Alikuwa akilia kwa nguvu na kufoka na kufanya vichekesho tuliyokuwa tunafanya. Ionekanavyo, maombi yetu hayakuwa na matokeo mazuri."

Hili liliendelea kwa siku tatu. Tulimwambia askari kuharibu aina yoyote ya miungu nyumbani kwao, ambayo alifanya. Lakini bado pepo halikuondoka. Kisha Mungu akamuonyesha mke wangu kwamba tulihitaji kufahamu nafasi zetu katika Kristo na kumwamuru pepo kuondoka. Tulipofanya hilo, mara moja alikuwa amefunguliwa.

Suluhi lake lilikuwa, "Tulijifunza baadaye kwamba haitoshi tu kuomba au kuimba, ingawa naamini kwamba Shetani anachukia yote maombi na nyimbo. Lazima tumpinge ibirisni na kuamuru kwamba anaondoka" (kutoka Uzoefu wa mapepo katika nchi nyingi uk. 37-39).

### II. MCHANGANUO WA PILI: WAMISHENARI MKE NA MME WANAELEZEA MASIMULIZI YAFUATAYO KUTOKA NCHI YA ULAYA KATI/MASHARIKI

Fatima, mama wa watoto wanenye, aliyetoka kwenye familia yenye matatizo mengi, kubwa zaidi ilionekana kuwa na mizizi ya shughuli za kimapepo.

Akiwa na umri wa miaka 15 aliolewa na Husen, kijana ambaye baba yake alikuwa mgonjwa wa akili. Baada ya miaka kadhaa ya ndoa, alipata ugonjwa wa akili pia. Alikuwa akitulizwa tu kwa dawa. Ingawa alikuwa bado mwisilamu, aliomba aombewe kwa jina la Yesu kukombolewa kutokana na laana ya familia yake iliyoomekeea.

Mama mkwe wa Fatima alikuwa amempatia laana "kwamba angekufa kabla ya mda wake." Na sasa akiwa na miaka 39, alikuwa anakufa kwa kansa. Mmishenari aliseama, "Nilipokwenda kumuona, aliniambia kwamba amekuwa na maumivu ya kutisha kwa siku nzima. Maumivu yanapokuwa makali anajiona amekufa na mama mkwe amevalia kama mchawi na kifimbo mkononi." Ingawa sasa ni mkristo, alikuwa ameogopeshwa sana. Mmishenari aliamua angechukua mamlaka katika jina la Yesu, ambalo alifanya. Fatuma alikuwa ameamuriwa kuomba hivyo hivyo. Aliongezeka kiroho, lakini maumivu ya mwili yaliendelea.

Bila kujali maombi, Fatima alikuwa. Katika mazishi yake, kaka yake na Husen alisimamia. Kaka huyu anajishughulisha na kazi za mafumbo (kuambia bahati nasibu, Kufanya hirizi za kiuchawi, n.k.). Aliletta kiongozi wa kiuslamu ambaye kwa namna fulani ni mchawi kufanya matambiko.

Wiki moja baada ya mazishi, mke wa mmishenari alikwenda pamoja na wanawake wengine kutembelea kaburi. Baada ya hapo, alialikwa kwenda kula chakula cha jioni na familia hiyo. Mtoto wa kike mkubwa wa Fatima, muumini, alimuomba aombe kwa sababu ameshaona baadhi ya ndugu wakiweka udongo kutoka kaburini kwenye chakula cha familia. Kufuatana na mapokeo, hii itasababisha aina moja ya laana iliyomwangukia Fatima kuangukia kwenye familia nzima.

Kama ulikuwa mmishenari katika mafunzo haya, ungeisaidaje familia hii walipokuwa wakipita katika misukosuko hiyo?

### III. MCHANGANUO WA TATU: WAMISHENARI MKE NA MME WANAELEZEA MASIMULIZI YAFUATAYO KUTOKA ROMANIA

Mke na mme katika miaka yao ya mwishoni mwa thelathini waliwaambia wamishenari jinsi ambavyo wamewekwa chini ya laana. Walipoanoa, dada yake na mme (mchawi mweupe) alikuwa ameshona karatasi nyepesi ndogo ikiwa na laana kwenye nguo zao. Laana ilikuwa kwamba wasiweze kupata watoto. Ingawa walikuwa wameharibu karatasi zote, bado hawakuwa na watoto. Sasa karibu na miaka ya mwisho wao wa kuweza kuzaa, wakatafuta msaada. Walitoa taarifa kwamba hawakuweza kuwa na uhusiano wa kawaida kwa sababu kila walipojaribu kufanya hivyo walisikia sauti za masimango zikiwambia hawawezi kufanya.

Wamishenari walisoma nao mistari wakiwaonyesha kwamba wanaweza kuwa huru kutokana na laana hii kwa nguvu za Yesu. Kwa kudai mamlaka yao katika jina la Yesu, walikataa kazi na nguvu za Shetani katika maisha yao na kumuuliza Mungu kuwakomboa. . Mara nyingine walipoongea na wamishenari, walisema kuwa wamekuwa wakidai mamlaka haya na hawajasikia sauti zaidi tena. Ndoa yao ilikuwa imara zaidi. Walidhani kuwa mwanamke alikuwa na mimba, ambayo ilidhirisha kutokuwa sawa.

Kama ungekuwa mmishenari katika masimulizi haya, ungefanya chochote tofauti? Ungelikuwa umesema nini walipotoa taarifa kwamba wangeendelea kutokuwa na mtoto?

### IV. MCHANGANUO WA NNE: MMISHENARI MCHANGA AFRICA ALIPATA UZOEFU HUU WA VITA VYA KIROHO.

Katika mwaka 1986, nilikwenda kwenye safari fupi ya umishenari huko Senegal, Africa Magharibi. Usiku wangu wa pili nchini ulitosha kunifundisha kwamba hakika tulikuwa kwenye mapambano ya nguvu za giza.

Nilikuwa nakaa na wamishenari walioishi katika Ouakam, kijiji kinacho julikana kwa nguvu zake za giza Baada ya ibada ya asubuhi, kwenye mji mwingine siku baada ya kufika kwangu, tuliamua kufanya ibada ambayo hajjawahi kutokea huko Ouakami siku hiyo. Ulikuwa mda wa baraka, na baada ya hapo, tulikuwa tukiongea usiku sana. Wengine katika familia wakapanda juu ghorofani kulala, na nikajienda kulala chini.

Nilijitosa na kujigeuza mpaka 9.00 asubuhi, kisha nikaangukia kwenye usingizi mzito. Ilikuwa joto na unyevunyevu na nilikuwa na feni inayopuriza kuzunguka kitanda. Baada ya mda mfupi, nilikuwa na baridi sana. Lakini nilipojaribu kuinuka kuzima feni, sikuweza kusogea. Akili yangu ilikuwa macho sana, lakini mwili wangu ulikuwa umeshikwa na ganzi. Nilijaribu kulia kwa sauti kuomba msaada, lakini ulimi wangu ulikuwa umevimba mdomoni.

Kwa kuwa mda huu ulikuwa wa kufunga wa waislamu Ramadhani, tulikuwa na kelele nje. Wachawi walikuwa wakitupa laana na viongozi wa shaman wakiomba kwa roho wachafu. Ilikuwa inajulikana kuwa nyumba tulioishi ilikuwa imetembelewa na mchawi ambaye alijaribu kuweka laana juu yake kuwafanya wamishenari kuondoka kijijini.

Nilisikia hatua za mtu akitoka ghorofani, lakini hakuna aliyebaribia kona. Niliona kivuli kikieleke kwangu kutoka upande wa mbali wa chumba. Ilionekana kama picha ya mtu aliyeavaa joho jeusi. Kisha nikasikia sauti ya mnyama ikikatakata mwili wa mnyama kwa meno.

Hofu iliyokuwa ikikua moyoni mwangu ilitilizwa na wazo moja: "Hii ni kazi ya mwovu na Yesu ni kinga yangu." Hivyo nikaamua kuliita jina la Yesu kwa nguvu. Nikasema mara moja, mara ya pili, na mara ya tatu, mdomo wangu ulikuwa umeachiwa, kivuli kikapotea, na kelele zikasimama, na nikakaa kitandani huru bila kuonekana kwa nguvu iliyokuwa imenishikilia. Nikarukia kama mshale ghorofani kwa mmishenari mzee na kumwelezea kilichotokea. Aliniuliza kama nilikuwa nikiota. Nilimhakikishia kuwa haikuwa ndoto. Tukaomba kwa dakika 30 kabla sijawa tayari kupumzika.

*Tokea usiku huo na kuendelea, nilikuwa nikihisi ubaya chumbani mara nydingi, lakini nilipokuwa nikiweka silaha za Mungu na kuziambia roho chafu kuondoka katika jina la Yesu na kwa mamlaka yake, nilikuwa nikilala kwa amani.*

*Sasa ninaelewa nguvu za Mungu katika giza. Ninajua tuko katika mapambano ya kiroho kwa ajili ya roho za wanaume na wanawake, lakini ninahakikishiwa kuwa ye ye aliye ndani yetu ni mkuu kuliko kila roho. Yesu ndani yetu ni tumaini la utukufu.*

**Kama uzoefu huu ungekutokea wewe, ungejua mamlaka uliyonayo kukemea mapepo? Hili linasemaje kuhusu nguvu ya maombi?**